

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Hamsini na Tatu – Tarehe 26 Agosti, 2008

(*Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi*)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:-

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa Mwaka 2007/2008 (*The Annual Report and Accounts of the Tanzania Revenue Authority for the Year 2007/2008*).

Hati ya Uhamishaji Fedha Na.1 ya Mwaka 2007/2008 (*Statement of Reallocation Warrant No.1 of 2007/2008*).

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi kwa Mwaka 2006/2007 (*The Annual Report and Accounts of the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) for the Year 2006/2007*).

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za *Consolidated Holding Corporation* kwa Mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2007 (*The Annual Report and Audited Accounts of the Consolidated Holding Corporation for the Year ended 31st December, 2007*).

MASWALI NA MAJIBU

Na. 467

Ahadi ya Mheshimiwa Rais Kufufua Viwanda Mkoa wa Tanga

MHE. SHOKA KHAMIS JUJMA aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwenye kampeni za Uchaguzi za mwaka 2005 aliahidi wananchi wa Tanga kuwa akipata ushindi atafufua viwanda vya Tanga, kuiongezea uwezo Bandari ya Tanga ili itumike zaidi kwa mambo ya kibiashara, kuiboresha hospitali ya Bombo ifikie hadhi ya kuwa hospitali ya rufaa na ahadi nyingine nyingi; na kwa kuwa Mheshimiwa Kikwete alishinda Uchaguzi na sasa ni Rais wetu wa Awamu hii ya Nne:-

Je, ni viwanda vingapi vimeishafufuliwa Mkoani Tanga tangu Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete aingie madarakani hasa ikitiliwa maanani kuwa nusu ya muda wake wa uongozi umeishapita?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangu Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne aingie madarakani mwaka 2005, hadi sasa jumla ya viwanda saba (7) vimeefufuliwa Mkoani Tanga kama alivyoahidi vikiwemo vifuatavyo:-

Tanga Steel Rolling Mills (Sasa Unique Steel Rolling Mills), Tanga Dairies Ltd. (Sasa Tanga International Processors Ltd), Sikh Saw Mill/MASCO (Sasa Ply and Panel (T) Ltd), Girragee Wattle Extract Company (Sasa Lushoto Lion Wattle Company Ltd), Tip Soap (Sasa Tip Soap (2005) Ltd), Mponde Tea Factory na Dindiru Tea Factory. Viwanda hivi kwa pamoja vimeajiri wafanyakazi 856.

Mheshimiwa Spika, pamoja na viwanda hivi vya zamani kufufuliwa, katika kipindi hiki cha uongozi wa Mheshimiwa Rais Kikwete, jitihada za Serikali za kuhamasisha sekta binafsi kujenga na kuendesha viwanda zimevezesha sekta hiyo kuanzisha viwanda vipyta saba (7) Mkoani Tanga, navyo ni:- *Natural Choice Co. Ltd.* cha Maji ya kunywa na Usindikaji wa Matunda, *E.A. Briguette Co. Ltd* cha Utengenezaji wa Mkaa kutokana na mabaki ya mbao, *Tanzania Gypsum Co. Ltd* cha *Ceiling Board*, *Manujee Products* cha *Vipodozi*, *Herkule Tea Factory*, *Kimso Saw Mills* cha *Mazao ya Mabao* na *Ashers Ltd* cha *Vipodozi*. Viwanda hivyo vimeajiri wafanyakazi 770.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, itaendelea na jitihada hizi za kujenga mazingira wezeshi ili viwanda vilivyokufa vifufuliwe na vipyta vianzishwe siyo tu kwa Mji wa Tanga, ila kwa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Shoka kwa kuuliza swali linalohusu Maendeleo ya viwanda vya Tanga wakati yeye ni Mbunge wa Micheweni Zanzibar, hii ni dalili ya wazi kuwa Muungano wetu unazidi kuimarika. (*Makofi*)

SPIKA: Kwa taarifa yako, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Shoka ameoa Tanga! (*Kicheko*)

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina uhakika kuna baadhi ya Viwanda hivyo alivyovitaja havifanyi kazi. Sasa swali langu; kuna baadhi ya wawekezaji ambao huwa hupewa viwanda kwa ajili ya kuviendeleza. Lakini badala ya kuviendeleza wanang'oa mashine wanapeleka sehemu nyingine badala ya kuendeleza ile ile haja yake ya zamani. Lakini wanang'oa mashine, wanapeleka kwingine, wanafanya kazi nyingine, mifano ninayo.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anasemaje kuhusiana na wawekezaji kama hao?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, sitapenda kупingana naye kuhusu hilo analosema na vile vile sitapenda kumwunga mkono kwa sababu mimi sina takwimu kuhusu watu wanaofanya hivyo. Lakini ukweli ni kwamba kama mtu amesaini mkataba na Serikali kwamba ataendesha kiwanda, wajibu wake ni kufanya hivyo hivyo.

Wizara yangu inafanya uperembaji yaani inafanya tathmini ya viwanda vyote, tumeishaanza Ukanda wa Pwani, Dar es salaam, Pwani na Morogoro na tutakapofika Tanga na kwingineko na kukuta kama kuna mwekezaji ambaye amechukua mitambo ya viwanda ambavyo alikabidhiwa, basi huyo tutamnyang'anya na tutachukua hatua nyingine za kisheria kuhakikisha kwamba viwanda vile vinarudi Serikalini na yeye mwenyewe anafikishwa mahakamani. (*Makofi*)

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi nimefarijika kusikia kauli hii, lakini ningependa nimpe mfano halisi wa kiwanda cha ngozi cha Mwanza. Kiwanda hiki kimeng'olewa mashine, yamebaki ni mapango na kimebadilishwa kuwa karakana ya mitambo ya ujenzi wa barabara. Je, Serikali inasema nini juu ya suala hili?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, nitapenda kupata takwimu sahihi za kilichopelekea mpaka mwenye kiwanda hicho akang'oa mitambo. Kama atakuwa mefanya vile kinyume na mkataba na bila kutoa

taarifa Serikalini na Serikali ikatoa kibali, basi atakuwa amefanya kinyume na mkatuba na Serikali itachukua hatua zinazopasa.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni jukumu la Serikali kusimamia mali za nchi hii; na kwa kuwa Waziri anasema hana takwimu sahihi, ndio kusema Waziri anakubali kwamba Wizara yake inafanya uzembe kusimamia rasilimali za Taifa hili ambazo ziko chini ya Wizara yake?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi kubwa sana na viwanda viko kila mahali, yako mashamba kila mahali na kwa maana hiyo, endapo mtu anafanya uhalifu, siwezi nikakiri hapa kwamba Serikali inakuwa inajua moja kwa moja kwamba uhalifu umeishafanyika. (*Makofi*)

Hata kama kuna mtu kafanya kosa kama hilo labda ameng'oa labda mtambo na kama Serikali haina taarifa, haitakuwa jambo la maana kwa Waziri kuja hapa Bungeni na kusema kwamba hilo ni kosa bila kuwa na takwimu sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi tunapenda kurudia kwamba tunaendelea na uperembaji wa kukagua viwanda vyote vya Tanzania, kuangalia wale wote ambao hawajafuata mikataba kama tulivyokubaliana tutawachukulia hatua na wale ambao wanafanya vizuri tutaendelea kujenga mazingira wezeshi ili waweze kuendelea zaidi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana kwa majibu yako ya ukweli Mheshimiwa Naibu Waziri. Illa ni vizuri kwenye mkutano ujao muweze kutoa taarifa. Waheshimiwa Wabunge wanauliza uliza haya, sasa inapokuwa hakuna taarifa mpaka waulize tena, inakuwa ni tatizo. Asante! (*Makofi*)

Na. 468

Vitambulisho vya Uraia

MHE. MHONGA S. RUHWANYA aliuliza:-

Kwa kuwa ni utaratibu wan chi mbali mbali kuwatambua raia wake kwa kuwapa vitambulisho vya uraia:-

- (a) Je, ni lini vitambulisho hivyo vitatolewa kwa Watanzania?
- (b) Je, ni hatua gani imefikiwa mpaka sasa katika zoezi hilo?
- (c) Je, ni kampuni gani imepewa jukumu hilo na ni vigezo gani vimetumika kuwapa tenda hiyo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, naomba kutoa ufanuzi ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, vitambulisho tunavyovizungumzia ni vya Taifa na siyo vya Uraia. Vitambulisho hivi vinatolewa kwa Raia pamoja na wageni Wakaazi wakiwemo Wakimbizi. Ni vizuri Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla wakaelewa hivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya ufanuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati nikijbu swali namba 129 la tarehe 30 Juni, 2008 liloulizwa na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani nililieleza Bunge lako tukufu kwamba ni adhima ya Serikali kuwa itaanza kutoa Vitambulisho vya Taifa ifikapo mwishoni mwa mwaka 2009. Mpaka sasa jengo kwa ajili ya ofisi anzilishi ya Vitambulisho limeishakamilika na kuanza kutumika. Mratibu Mkuu amekwishateuliwa na zabuni ya kumtafuta Mkandarasi imekwishatangazwa na Makampuni yapatayo 54 ya ndani na nje ya nchi yameomba zabuni hiyo na tayari mchakato wa awamu ya kwanza uko katika hatua za mwisho (*shortlisting*). Aidha, Mheshimiwa Rais ameridhia na kusaini *Establishment Instrument* ya kuanzisha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hakuna Kampuni yoyote iliyopewa jukumu la kutengeneza vitambulisho vya Taifa kwani zoezi la uchambuzi wa zabuni bado linaendelea. Naomba pia nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa zoezi zima la kumpata Mkandarasi litafanyika kwa umakini mkubwa na kuweka maslahi ya Taifa mbele pamoja na kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004 (*Public Procurement Act, 2004*).

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante! Naomba tu atuelezee zoezi hilo la uchambuzi litachukua muda gani?

SPIKA: Majibu, kwa swali fupi, zuri la Kibunge!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, hivi tunavyozungumza, Kamati husika inakaa kuchambua na ninahisi kwa utaratibu ambao wamejipangia maana yake hili ni zoezi ambalo, Mheshimiwa Spika, nataka nitamke katika Bunge lako rasmi, tunataka tuwe makini sana na tuwe waangalifu sana kwa sababu. Kwa hiyo, tunataka tufanye kitu cha uhakika tukizingatia sheria na taratibu zote ambazo zimebekwa.

Kwa hiyo, naweza nikasema kwamba leo tarehe 26, kwa hiyo naweza kusema itakapofika tarehe 26 mwezi ujao, nahisi katika kipindi cha mwezi mmoja watakuwa wamemaliza huo utaratibu ili tuweze kuingia katika mchakato mwingine wa kumpata mkandarasi. (*Makofi*)

SPIKA: Nitarhusu wawili tu; Mheshimiwa Selelii halafu Mheshimiwa Zitto!

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Napongeza sana juhudzi za Serikali kuanzisha Vitambulisho vya Taifa. Nina swali moja tu la nyongeza dogo sana.

Kwa kuwa nchi ya Zanzibar tayari ina Vitambulisho vya Taifa la Zanzibar; na kwa kuwa nchi ni moja, Serikali inaonaje ikishakamilika hii ya Taifa, vile vye Zanzibar vikafutwa, vikabaki moja tu vya Tanzania? (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, Vitambulisho ninavyovizungumzia hapa ni Vitambulisho vya Taifa. Vitambulisho vya Zanzibar ni Vitambulisho vya Ukaazi. Kwa hiyo haya ni mambo mawili tofauti. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri ametufahamisha hapa kwamba Rais tayari amesaini *Establishment Order* ya kuanzisha Mamlaka ya Viambulisho vya Taifa. Lakini itafahamika ya kwamba kumekuwa na mjadala na Waziri Mkuu tayari alisema kwamba suala hilo litaangaliwa la jinsi gani ya kutumia uzoefu ambao sasa hivi upo ndani ya *RITA* na ili kuiunganisha *RITA* na *NIDA* kwa sababu Nida, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa itabidi ianzishe Data Base nyingine wakati tayari *RITA* ina *Data Base* na ndiyo inayosajili Vizazi na Vifo! Sasa, Waziri haoni kwamba kuanzisha Mamlaka nyingine ni kuiongezea Taifa mzigo? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, suala la Mheshimiwa Zitto kuhusu kuwekea mzigo Serikali kwa kuleta Mamlaka nyingine ambayo itashughulikia Vitambulisho vya Taifa ni suala ambalo kama alivyosema ni mjadala ambaou upo.

Mheshimiwa Spika, lakini, naomba kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba suala la Vitambulisho vya Taifa la Tanzania limekuwa ni suala la mjadala wa muda mrefu sana. Kwa hiyo, tumeona kwamba hii *exercise* iende na wakati haya mambo mengine yanatizamwa na kwa kuwa Rais kwa mujibu wa Katiba anayo Mamlaka kama hivi ilivyoonyesha ya kuweza kuweka *Establishment* ya kuiweza kuweka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

Pia inawezekana huko mbele ya safari ikawekwa ikawa kitu kimoja. Kwa hiyo, hakuna tatizo hata kidogo. Nakushukuru.

Na. 469

Mradi wa Umeme – Peramiho

MHE. JENISTA J. MHAGAMA aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa kupidisha Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini tarehe 16/7/2007, Waziri alilieleza Bunge kuwa mradi wa kupeleka umeme Peramiho utaingizwa katika Mradi wa Gridi (Makambako – Njombe – Peramiho):-

(a) Je, Serikali iko tayari kuupa mradi huo jina la Makambako – Njombe – Songea – Peramiho, ili kuthibitisha nia hiyo?

(b) Je, mpaka sasa mradi huo umefikia hatua gani?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mbunge wa Peramiho, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli wakati wa majumuisho ya Bajeti ya Wizara yetu kwa mwaka 2007/2008 hapa Bungeni katika Mkutano wa Nane, Kikao cha 24 cha tarehe 16/7/2007, iliezwa kuwa kuna mradi wa kupeleka umeme kutoka Makambako kwenda Songea hadi Mbinga utakaofadhiliwa na Serikali ya Sweden amba o utahusu pia upelekaji umeme katika baadhi ya maeneo yalliyoko ndani ya Jimbo la Peramiho.

Vile vile katika majumuisho ya Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2008/2009 katika Mkutano wa Kumi na Mbili, Kikao cha 20 cha tarehe 9 Julai, 2008 cha Bunge lako Tukufu, maelezo ya hoja iliyohusu jina na utekelezaji wa mradi wa umeme Peramiho yalitolewa pia.

Mheshimiwa Spika, jina rasmi la mradi huo ni Makambako – Songea 132KV Line. Jina ambalo limekuwa likitumika tangu wakati wa ubunifu wa mradi na utekelezaji wa upembuzi yakinifu na ndilo linalotumiwa kwa mawasiliano rasmi pamoja na kwenye makabrasha mbali mbali yanayohusu mradi huo ndani na nje ya nchi.

Hivyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa licha ya Peramiho, Ludewa, Namtumbo na Mbinga kutotajwa katika jina la mradi, mradi huo utafikisha na kusambaza umeme katika maeneo niliyoyataja awali ikiwa ni pamoja na baadhi ya maeneo ya Jimbo la Peramiho.

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu wa mradi huo ulikamilika Juni, 2006 kwa msaada wa Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa la SIDA. Gharama za mradi huo ni Dola za Marekani milioni 70.4 ambazo zitatumika kujenga njia

ya usafirishaji wa umeme wa msongo wa KV 132 kutoka Kituo cha kupoozea umeme cha Makambako hadi Songea. Umeme wa msongo wa KV 132 ukishafika Songea utapozozwa hadi msongo wa kilovolti 33 kwenye Kituo kitakachojengwa Songea chini ya mradi huo na kusambazwa katika Wilaya ya Songea, Namtumbo, Mbinga na Maeneo mengine ikiwemo Peramiho.

(b) Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema katika hotuba yetu ya Bajeti ya mwaka 2008/2009, utekelezaji wa mradi wa Makambako – Songea unatarajiwa kuanza mwezi Septemba mwaka huu wa 2008. Serikali ya Sweden imethibitisha kufadhili mradi huo.

Mheshimiwa Spika, aidha Serikali kupitia *TANESCO* ina mpango wa kufikisha umeme Peramiho ndani ya mwaka huu wa fedha wa 2008/2009 kutoka kwenye njia inayopeleka umeme katika Kambi ya Chabruma iliyoko Kilomita 17 kutoka Pearamiho.

Mheshimiwa Spika, gharama za mradi huo ni shilingi milioni 306 ambazo zitatumika katika ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa *KV 11* yenye urefu wa kilomita 17 na ufungaji wa *transfoma 5*.

Ujenzi wa njia hiyo kutokea eneo la Chabruma umeishaanza kwa kutumia Bajeti ya ndani ya *TANESCO* ambapo maandalizi ya sehemu za kupitisha nguzo za umeme yalianza tarehe 11 Agosti, 2008, kama wiki mbili zilizopita na kazi ya usimamishaji wa nguzo inatarajiwa kuanza mwisho wa mwezi Agosti, 2008. Kwa mwaka huu wa 2008, njia ya umeme yenye urefu wa kilomita 8 na uwekajiwa *transfoma* mbili za *KV 50* kila moja inatarajiwa kujengwa na kilomita 9 zilizobaki pamoja na ufungaji wa transfoma tatu za *KVA 100* kila moja unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2009.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza kabisa nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuwa baada ya hotuba yangu ya Bajeti, kwa kweli Mawaziri hawa wameonyesha umakini mkubwa katika kushughulikia tatizo la umeme huko katika maeneo yangu niliyoyasema.

Mheshimiwa Spika, maswali yangu mawili ni kama ifuatavyo:- Moja, kwa kuwa sasa mwezi wa Tisa tunasaini huo Mkataba na Sweden kwa ajili ya kutoa fedha za mradi huo mkubwa wa Makambako – Songea.

Je, Serikali bado inaendelea kukumbuka ahadi yake ya kujenga *Min-Power Station* katika Kijiji cha Madaba na kuzingatia umeme huo upite katika Kijiji cha Wino ambacho kiko kando kando kidogo? Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa mimi mwenyewe Mbunge na wananchi wangu wa Peramiho tumeishapata wawekezaji wa Kichina ambao kwa mujibu wa Sheria mpya tuliyoipitisha ya Nishati, wako tayari sasa kuwekeza kwenye sekta ya umeme katika Kijiji cha Magagula kwenye maporomoko makubwa sana, Mhanje na Mgazini.

Je, Serikali iko tayari sasa kushirikiana nami pamoja na wananchi wangu kuhakikisha miradi hiyo mingine midogo kama mitatu hivi inafanikiwa ili kuongeza nguvu ya nishati vijijini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, suala la kuweka *Min-Power Station* Madaba lilikuwemo katika utaratibu uliofanyiwa na tathmini iliyokisiwa kwa Mradi wa Makambako – Songea. Kama nilivyosema umeme wa Makambako – Songea unaokuja pale Songea ni umeme mkubwa wa 132 KV na ukifika pale unapozwa na kupelekwa katika maeneo yote ikiwa kama ni kilovoti 33 na matarajio ni kwamba huko kote utakapofika kutakuwa na *Min-Power Stations* zakupokea umeme huo na kuusamabaza kwenye maeneo husika. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba eneo la Madaba lilitengwa kama eneo la kupokea *Min-Power Station* na sijapokea mabadiliko yoyote katika mpango huo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swal la pili, naomba nimpongeze kwa dhati ya moyo wangu kwa sababu kazi ya kubuni miradi ndiyo hasa sababu iliyopelekea kuanzisha *REA*.

Mheshimiwa Spika, *REA* inataraji kwamba sisi kama Wabunge tukiwa huko, tutagundua maeneo ambayo tunaweza kubuni miradi ya nishati na *REA* kazi yao ni kupeleka watalaan na ku-*finance* miradi kama hii.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba tutafanya utafiti wa hayo Maporomoko ya Magagula na tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge na Uongozi wa jimbo la Peramiho kuhakikisha kwamba huu unakuwa ni mfano wa kuigwa na Watanzania wengine wote.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa Jimbo la Tunduru, Wilaya ya Tunduru iko Mkoa wa Ruvuma na mradi huu wa umeme kwa mujibu wa taarifa ya Mheshimiwa Waziri haufiki Tunduru.

Je, Waziri atakuwa tayari ule msongo unaokwenda Namtumbo badala ya kupeleka kilovoti 33, basi uende kilovoti 66 ili votage hiyo iweze kuwafikia wananchi wa Tunduru ili kasi ya Maendeleo ya Wilaya ile iweze kuongezeka? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, hili suala la kupeleka umeme Tunduru kuititia gridi ya Makambako – Songea nadhani tumeongea na Mheshimiwa Mtutura, lakini lina tatizo moja; kwanza, tukubaliane tu kwamba mpaka hivi sasa mradi huu kwa hatua iliyofikia wa Makambako – Songea ndiyo makubaliano ambayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano imefikia na wahisani wa Serikali ya Sweden.

Sasa, labda huo utakuwa ni mradi mpya ambaa tutabuni baada ya kukamilika huu wa kutoa umeme sasa kutoka Namtumbo kwenda Tunduru. Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mtutura pia kwamba tuliwahi kuzungumza kwamba labda tuwape kazi *TANESCO* wafanye tathmni ya ni wapi itakuwa rahisi wao kupokea mradi

kwa sababu uko uwezekano wa Tunduru kupokea mradi kutoka Masasi pale ambapo umeme wa *ARTUMAS* utakuwa umefika Masasi na huenda ikawa ni nafuu zaidi kwa watumiaji.

Na. 470

Mitindo ya Mavazi ya Kisasa na Muziki wa Kizazi Kipyä

MHE. ERNEST G. MABINA (K.N.Y. MHE. JAMES P. MUSALIKA)
aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika kulinda na kuendeleza utamaduni wetu ndani na nje ya nchi:-

Je, Serikali inasema nini juu ya mitindo ya mavazi kwa vijana wa sasa na muziki *wa Bongo Flavour?*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)
(K.n.y. WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa James P. Musalika, Mbunge wa Nyang'wale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la mitindo ya mavazi kwa vijana wa sasa na muziki wa *Bongo Flavour* ni la mpito. Kimsingi, mabadiliko ya aina ya mavazi kwa vijana na aina ya muziki hivi sasa yanatokana na maendeleo ya sayansi na tekinolojia hususan vyombo vya *electronic* na kutopteka na ukweli kwamba Tanzania sio Kisiwa.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo haya ya sayansi na tekinolojia yanakwenda sambamba na suala la utandawazi ambapo vijana wetu wamekuwa wakipata fursa nyingi ya kuona na kujifunza mengi kuitia mtandao wa *Internet* na Televisheni.

Mambo ambayo vijana hawa wamekuwa wakiyaona na kujifunza ni pamoja na mitindo ya mavazi na muziki.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya nyuma itakumbukwa kwamba kulikuwepo na mitindo ya mavazi , mfano nguo fupi na za kubana(vimini) suruali pana (pekos) na

kadhalika; Aidha, kulikuwepo pia na muziki wa mitindo ya *bumping, break dance, twist* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, aina hizi zote za mitindo ya mavazi na muziki hivi sasa hazipo tena pamoja na kwamba baadhi ya watu waliokuwa wanatumia wapo hadi sasa. bila shaka na mitindo hii mipya iliyoibuka ya mavazi na muziki ya bongo *flavor* na itatoweka.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua mabadiliko yaliyopo ya sayansi na teknolojia yanachangiwa na suala la utandawazi, inaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na umuhimu wa kulinda na kuendeleza utamaduni wetu.

Aidha, ni jukumu letu sisi wote kuanzia ngazi ya familia kuhakikisha kwamba watoto wetu na vijana wetu wanalelewa katika misingi ya utamaduni wetu ili waweze kuzingatia maadili mema ya nchi yetu na kuthamini mila, desturi na utamaduni tuliojijengea.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo napenda kuchukua fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuwapongeza vijana wetu hususan wale wanaoimba muziki wa *Bongo flavor* kwa ubunifu wao wa kutengeneza muziki huo ambao asili yake ni Marekani kwa kuweka vionjo vyenye mahadhi ya Kitanzania na hivyo kupendwa na watu wengi ndani na nje ya nchi ambao ni wapenzi wa bongo *flavor*.

Mheshimiwa Spika, Aidha, kutokana na muziki huo vijana wengi sana wamejajiri na hivyo kuondokana na umasikini.

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza;

Kwa sababu Serikali imekiri wazi kwamba hawa vijana sasa hivi wameanza kujinjiri na wamepata ajira, Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuendelea kuwalinda hawa vijana katika shughuli yao ya muziki ambayo inaleta ajira kwa vijana wetu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,(MUUNGANO)
(K.n.y. WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO): Mheshimiwa Spika, kauli hii ya hapa Bungeni kwamba tunawapa moyo ni ishara kwamba tunawaunga mkono moja kwa moja na kwamba tunatoa fursa waendele. Ninayo mifano hapa ya vijana hawa ambao wamefaidika na fursa hii kwa mfano tunao vijana Judith Wambura *Lady J D* ambaye alikwenda Uingereza na Marekani katika sherehe ya birthday ya Bwana Mandela. Tuna Joseph Mbilinyi maarufu kama Mr. Sugu ambaye alialikwa Bolton, na Uingereza. Joseph Haule maarufu kama Profesa J, ambaye amealikwa Marekani na Uhlanzi, Lucas Mkendela maarufu kama Mr. Nice kaalikwa Japan, Marekani na

Uingereza, Bi. Rehema Chalamila *Ray C* kaalikwa Marekani na Uingereza, Ali Kiba ambaye amealikwa Marekani na kadhalika.

Kwa hiyo,, tunawapa fursa waendelee kwa sababu kuna umuhimu wake ni kwamba inatoa ajira, wanakuza lugha yetu na wanatoa burudani kwa wananchi.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini mimi sikubaliani nayo, naomba kumwuliza swali moja.

Kwa kuwa mbali na mitindo na mavazi lakini pia lugha, vionjo na matendo ya mapenzi ya waziwazi katika nyimbo za Bongo fleva zinavyoathiri jamii, Je, nyimbo na matendo hayo yanatoa mafunzo gani kwa jamii hasa kwa watoto?

SPIKA: Kwa maana nyingine Mheshimiwa Faida uwe unaangalia hii. Wewe ni mshabiki? (*Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO) (K.n.y. WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO): Mheshimiwa Spika, wakati Fulani Mheshimiwa Mstaafu Rais Mwinyi, aliwahi kusema kwamba kila zama na vitabu vyake, kwa hivyo sisi wazee na umri kama huu tuwape nafasi vijana wajimwage katika maisha yao, huu ni wakati wao wale ambao hawapendi wasiangalie tu (*Kicheko*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wabunge kwa sababu somo ni hilo mimi nampenda sana Ali Kiba, Bushoke, *K-lin* basi tuendelee na maswali. (*Kicheko*)

Na. 471

Mradi wa Maji Chankorongo Nyakagomba

MHE. KABUZI F. RWILOMBA aliuliza:-

Kwa kuwa mradi wa maji wa Chankorongo- Nyakagomba ni wa muda mrefu tangu mwaka 1976 lakini haujakamilika:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaukamilisha mradi huo.
- (b) Je, katika utekelezaji Serikali inaweza kuunganisha na maeneo ya gereza la Butendwe kijiji cha Chibingo, Nyamigota na Mji wa Katoro ambao ni mkubwa kuliko baadhi ta miji mikuu ya Wilaya;

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mbunge wa Busanda, napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Chankorongo –Nyakagomba ulifanyiwa usanifu na kuanza kujengwa mwaka 1976 kwa lengo la kuvipatia maji vijiji 11 vya Nyakagomba, Chankorongo, Chigunga, Bukondo, Nyakaswa, Kabuguzo na hospitali ya Butundwe.

Kutokana na uhaba wa fedha mradi ulisimama kujengwa mwaka 1988 baada ya kutekeleza asilimia 85 ya mradi mzima. Kwa kuwa mradi huu ulisanifiwa siku nyingi upo umuhimu wa kuutathmini na kuusanifu upya kabla ya kuanza kazi ya kuukarabati na kuukamilisha. Tathmini hiyo itaangalia upya watu na mahitaji yao, uwezo wa chanzo na miundombinu iliyopo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza mradi wa Chankorongo-Nyakagomba Halmashauri ya Wilaya ya Geita imepanga kufanya uchunguzi na usanifu wa mradi huu katika kipindi cha mwaka 2008/2009.

Vijiji vingine vitakavyofanyiwa uchunguzi na usanifu ni vya Nyango'holongo, Chigunga, Nyakamwaga na Nyakagwe katika Jimbo la Busanda. Mchakato wa kupata wataalam washauri watakaohamasishwa wananchi kufanya usanifu wa miradi na kuisimamia umekwishaanza na kuendelea. Mpango uliopo ni kuwa baada ya wataalamu hao kupatikana uchunguzi na usanifu wa mradi wa Chankorongo-Nyakagomba utafanyika na hatimaye kuanza utekelezaji.

(b) Mheshimiwa Spika, mradi wa Chankorongo-Nyakagomba haukulenga kuhudumia gereza na Butundwe, Vijiji vya Chibingo na Nyamigota na mji wa Katoro. Hii ina maana kuwa Miundombinu iliyopo haitaweza kukidhi mahitaji zaidi. Ili kuhudumia gereza la Butendwe, vijiji vya Chibingo, Nyamigota na Mji wa Katoro, Halmashauri ya Wilaya ya Geita inashauriwa kujadiliana na mtaalam mshauri ili maeneo hayo nayo yaweze kuingizwa katika hadidu za rejea za kazi ya usanifu itakayofanywa hivi karibuni.

MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza;

Mheshimiwa Spika, inasikitika mradi huu ulianza enzi za *TANU* na kwenye Bunge lako tukufu tulisharifiwa kwamba maji yaliyochini ya ardhi katika Wilaya ya Geita hayafai kwa matumizi ya binadamu kwa sababu yana madini ambayo yanaleta athari, sasa tangu mwaka 1976 mpaka leo watu wa geita wanaendelea kuathirika.

(a) Je, Serikali inajisikiaje kuanzisha mraidi mingine sehemu zingine na mraidi huu usikamilike.

(b) Kwa kuwa katika majibu inaonesha kuna kujikanganya na nilipokuja Wizarani Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami aje sasa ili tuweze kuangalia huo mradi na aweze kutoa majibu ambayo yanaweza kutusaidia kuondoa tatizo katika Wilaya ya Geita

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza ni kweli kabisa na mimi nasikitika pamoja naye kwamba mradi ni wa siku nyingi lakini ukitazama mradi wa mwaka 1976 uliokumbwa na kugubikwa na matatizo ya utekelezaji, hivi sasa ni bora kabisa na ni muhimu tutumie fursa hii tuliyonayo Wahandisi wetu washauri ambao sasa wanatekeleza mradi uliofadhiwa na *World Bank* kuutazama upyavinginevyo tutakuwa tunafanya kazi ya kurudia rudia maana miundombinu iliyopo ni ya zamani watu wameongezeka, mifugo imeongezeka. Kwa hiyo, naomba akubaliane na mimi kwamba ni bora kabisa tuweze kulifanyia kazi upya tathmini suala la mradi huu wa Chankorongo na Nakagomba na Serikali imejipanga kuhakikisha unakamilika

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji yenyе madini tumeshazungumza na mimi nimekwishasema wakati fulani nikisema kwamba hata bwawa la Nyamalembo nilisema ni marufuku kulitumia kwa sababu lina madini aina ya *mercury* ambayo ni mabaya kwa wananchi, kwa hivyo naomba niseme kwamba nakubaliana sasa na wito wake nitakwenda mimi mwenyewe binafsi kama Waziri na kama mtaalamu na nitaona tufanye nini kuanzia sasa. (*Makofi*)

Na. 472

Kuwapatia Maji wananchi wa Kijiji cha Mlela

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Kijiji cha Mlela Wilaya ya Kigoma Vijijini wanamatatizo ya maji ambapo hutumia maji kutoka katika visima walivyochimba wenyewe; na kwa kuwa chanzo cha maji kilichopo katika kijijini kwao maji yake hupelekewa wananchi wa kijiji jirani cha Kidahwe:-

- (a) Je, kwa nini Serikali isiwachimbie visima virefu na vifupi wananchi hao kwa kuwa chanzo chao cha maji kilipelekwa Kidahwe?
- (b) Je, ikiwa chanzo cha maji kinacho jitiosheleza kwa nini wananchi wa Mlela nao wasitumie maji hayo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mhehsimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhil Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 1979, Serikali ilikamilisha ujenzi wa mradi wa maji kwa ajili ya vijiji vya Mlela na Kidahwe kutoka kwenye chanzo cha mto Mkuti. Kijiji cha Mlela kipo katika ukanda wa juu wa chanzo cha maji wakati kijiji cha Kidahwe kipo katika ukanda wa chini.

Hivyo kutokana na mwinuko mkubwa wa ardhi haikuwezekana kupeleka maji katika kijiji cha Mlela kwa mtiririko (*gravity*) kama ilivyowezekana kupeleka maji hayo hayo Kidahwe ka mtiririko. Ili kuwanufaisha wananchi wa kijiji cha Mlela, mashine ya kusukumia maji ilifungwa katika chanzo hicho cha Mkuti na maji yalifika Kijiji Mlela.

Kwa upande wa kijiji cha Mlela, mradi ulifanya kazi kwa muda wa miaka miwili tu na baadaye ulisimama kutokana na wananchi wa Kijiji hicho kushindwa kuchangia gharama za kuendesha mradi na kutengeneza mashine yao ya kusukuma maji.

Mheshimiwa Spika, baada ya mradi kusimama mwaka 1981 mashine ya mradi ilihifadhiwa kwenye Ofisi ya Serikali ya Kijiji cha Mlela. Kutokana na kukaa kipindi kirefu bila ya kufanya kazi, mashine hiyo imeharibika na baadhi ya vifaa vyake vimepotea.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka utaratibu mzuri wa kupeleka fedha za ruzuku ya Maendeleo katika Halmashauri zote nchini ikiwa ni pamoja na fedha za kuendeleza miundombinu ya maji. Kwa bahati mbaya kwa miaka miwili mfululizo yaani 2006/2007 na 2007/2008, Halmashauri ya Kigoma haikufuzu kupata ruzuku kutokana na kutopata hati safi za ukaguzi wa fedha. Kwa bahati nzuri katika mwaka 2008/2009 Halmashauri hiyo sasa imefuzu kupata fedha za ruzuku kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya maji.

na Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha wananchi wa kijiji cha Mlela kupata maji safi salama katika mwaka wa fedha 2007/2008 Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma inaendelea na utaratibu wa kuchimba kisima kirefu katika kijiji cha Mlela.

Aidha, Halmashauri hiyo imepanga kuboresha visima vifupi vitatu vya asili kwa kuvijengea *Well rings*, na kuvivekea pampu za mkono, kazi hii nayo imekwishaanza kukikamilisha kwa kazi hizi kutawezesha wananchi 1500 kati ya 6000 wa kijiji cha Mlela kupata maji safi na salama.

(b) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mradi wa maji katika vijiji vya Mlela na Kidahwe kutoka kwenye chanzo kimoja haukuathiri upatikanaji wa maji kwa kila kijiji.

Kwa kuwa Kijiji cha Mlela kipo juu ya chanzo (*upstream*) uwezekano pekee kwa kijiji cha Mlela kutumia chanzo hicho ni kwa kusukuma maji hayo kwa mashine na kuyapandisha hadi kijijini Mlela. Wananchi wa Kijiji cha Mlela wanashauriwa kutambua umuhimu wa kuchangia gharama ya uendeshaji wa mradi wa maji ili mradi wao ufanye kazi na kuwa endelevu.

Kuhamasika kwa wananchi wa kijiji cha Mlela kutaiwezesha Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma Vijijini kutenga fedha kwa ajili ya kukarabati miradi kamtika mipango yake.

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

- (a) Kwa kuwa, Serikali imeamua kuwachimbia kisima kimoja kirefu na visima vitatu vifupi wananchi wa Mlela na watakaofaidika na mradi huo ni wananchi 1500 tu, Je, Serikali itawachimbia lini visima hivyo?
- (b) Kwa kuwa, Kijiji cha Mlela kina takribani watu 6000 na Serikali imeamua kuwachimbia visima wananchi 1500. Je, wananchi waliobakia 4500 watafaidikaje na mradi huo, Serikali haioni kuwa sasa imewabagua?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, mwaka huu tumepata fedha za kuchimba visima hivyo ambavyo vitakidhi mahitaji ya watu 1500, hata hivyo mchakato wa kufanya usanifu kwa ajili ya wananchi wengine wote waliobaki unaendelea ili tuweze kuingiza katika utaratibu wetu huu wa kuangalia vijiji vinavyofadhiliwa na mradi wa *World Bank*.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba vijiji vile pia vitapata maji lakini kwa sasa fedha tulizonazo tumeanza na visima. hivyo vichache.

MHE. DR. SAMSONI F. MPANDA: Mheshimiwa Spika nashukuru, kwa kuwa, miradi mingi ya maji wakala wa uchimbaji wa visima ndiyo hutumika zaidi katika uchimbaji wa hivyo visima;

Je, si wakati muafaka sasa hivi kuanzisha Bodi kwa ajili ya wakala wa uchimbaji visima?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Dr. Samson Mpanda kwamba *DDCA* ni wakala wa Serikali, *Government Executive Agency* na kwa mujibu wa sheria ile ya wakala wa Serikali kila wakala inakuwa na bodi ambayo inasimamia shughuli za Maendeleo za Bodi hiyo. Kwa hiyo, anachosema ni sahihi na ninaamini kabisa kwamba bodi ipo, kama bodi imelala kilichobaki ni kuiamsha tu.

Na. 473

Barabara zilizo chini ya ya TANROADS

MHE. LUKA J. SIYAME aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara za *TANROADS* ikiwa ni pamoja na ile ya Msongamano Utambalila na Isanza-Uporoto kwa muda mrefu zimekuwa zikitengewa fedha za matengenezo na kuripotiwa kuwa kwenye hali nzuri wakati hakuna barabara kati ya sehemu hizo.

Je, Serikali inasema nini kuhusu udanganyifu huo na itachukua hatua gani kwa wadanganyifu hao.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Luka Siyame Mbunge wa Mbozi Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara za Igamba- Msongano-Utambalila yenyeye urefu wa kilomita 87.21 ile ya Zelezeta-Isanza-Itaka yenyeye urefu wa kilomita 39.44 ni barabara za Mkoa zinazohudumiwa na Wizara yangu kupitia wakala wa Barabara Mkoa wa Mbeya

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara hizi zimekuwa zikitengewa fedha kila mwaka, fedha hizo zimekuwa zikitengewa kwa ajili ya matengenezo (*maintenance*) ya jumla ya kilomita 93.7 ambazo zinazopitika, wakati wa jumla ya kilomita 33 hazipitikitii.

Hivyo ukiacha eneo hilo lisilopitika maeneo yote yanayopitika yamekuwa yakifanyiwa matengenezo kila mwaka kulingana na fedha zilizotengwa bila ya udanganyifu wowote.

Mheshimiwa Spika, maeneo yasiyopitika ni kutoka Msongano hadi Tindingoma kilomita 225 katika barabara ya Igamba-Msongano-Utambalila na kutoka Hangomba NAFCO hadi Iporoto kilomita 8, katika barabara za Zelezeta-Isanza-Itaka. Maeneo hayo ni ya chepechepe hivyo huhitaji matengenezo makubwa yanayohusisha kunyanya tuta la barabara, kujenga madaraja na kuweka changarawe. gharama za kazi hizo zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 1.8. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kutafuta fedha za maendeleo kwa ajili ya kukarabati vipande hivyo chepechepe ambavyo kwa sasa havipitiki kiurahisi. kwa kuanzia katika mwaka huu wa fedha wa 2008/2009 Serikali imetenga shilingi milioni 120 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa madaraja kati ya Msongano wa Tindingoma na shilingi milioni 87 kwa ajili ya ukarabati wa sehemu ya Hangomba-Iporoto.

MHE. LUKA J. SIYAME: Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, napenda pia niishukuru *TANROADS* mkoani Mbeya kwa juhudii zao wanazofanya sasa hivi katika matengenezo ya barabara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu hayo mazuri napenda kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri ni shahidi wa hali mbaya ya barabara hizo mbili tulizozitaja kwa kuwa yeye mwenyewe mwaka jana alipokuwa ameagizwa kwenda kutembelea shule zinazojengwa kule alishindwa kufika.Je, anaweza akatoa matumaini gani kwa wananchi wa maeneo hayo kwamba barabara hizo sasa zitatengenezwa kwa muda mfupi ujao maana kwa utengaji wa shilingi milioni 207 kati ya bilioni moja na laki nane ni kwamba itachukua miaka si chini ya kumi na sita kutengenezwa.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nikiri kwamba katika barabara hii mimi binafsi niliwahi kukwama wakati tukikagua shule za sekondari kule Mbeya lakini nijibu kwamba kama nilivyoahidi kwamba Serikali imeanza kuchukua hatua, huu utengaji wa fedha kidogo kidogo ni kutokana fedha zinavyopatikana katika Bajeti, lakini nataka tu nimhakikishie kwamba kadri bajeti ya Serikali itakavyozidi kuimarika na sisi tutaendelea kutenga fedha za kutosha kuhakikisha kwamba barabara hii inajengwa kwa kiwango cha kupitika kwa uhakika.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii kuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, Mkoani Mbeya *TANROADS* inapelekewa hela nyingi sana za matengenezo ya barabara na kwa kuwa makandarasi binafsi wanapopewa barabara hizo kuzitengenezahuwa hawatengenezi mifereji wakati wanajua kwamba *enemy number one* ni maji kwa hiyo wanatengeneza mwaka huu, mwaka kesho wanatengeneza na mwakakeshokutwa wanatengeneza; na kwa kuwa sasa hivi *National Service*, mwaka jana imepewa baadhi ya barabara pamoja na barabara yangu ya Mbeya-Chunya - Makongorosi kuikarabati, na wameitengeneza vizuri na kuweka mifereji.

Je, Serikali sasa itakuwa inawapa JKT kuliko wakandarasi binafsi?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, mimi naafiki kabisa kwamba bila kutengeneza mifereji ya uhakika barabara zitakuwa hazitengenezwi kwa kiwango kinachostahili.

Suala la kuwapa ukandarasi JKT kwa sababu wanatengeneza vizuri, ni suala la msingi isipokuwa kwamba wakati wa zoezi hilo la kutoa kandarasi kwa ujenzi wa barabara hizo ni suala la kushirikisha watu wa *TANROADS* na kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe wa kamati ya ushauri ya Mkoa ya barabara Mkoani Mbeya ni suala ambalo ni vizuri tuendelee kushirikiana nao katika kuwaangalia JKT.

MHE. PASCAL COSTANTINE DEREGA aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliahidi kutoa awamu ya pili ya fedha za taasisi za fedha vijijini kwa lengo la kuwafikia wananchi kwa urahisi:-

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani ya utekelezaji wa ahadi hiyo?

(b) Je, fedha hiyo imepelekwa kwenye taasisi zipi Wilayani Kondoa?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU (K.n.y. WAZIRI WA KAZI AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Pascal Costantine Derega, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kabisa kwamba Serikali iliahidi kutekeleza awamu ya pili ya Mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa kutoa mikopo kwa wananchi kupitia Benki na asasi za fedha kwa lengo la kuwafikia wajasiriamali wengine kwa urahisi zaidi hususani wa vijijini ambao hawakuweza kufikiwa na benki za *CRDB* na *NMB* katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa awamu ya pili ya utekelezaji wa mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi ulizinduliwa rasmi tarehe 31 Disemba, 2007 katika kijiji cha Msowero Wilayani Kilosa Mkoa wa Morogoro.

Jumla ya Benki na asasi za fedha 13 zimeteuliwa na Serikali kutoa mikopo kwa wananchi na kusimamia urejeshaji wa mikopo husika katika Wilaya 68 za Tanzania Bara zikiwemo Wilaya 22 ambazo hazikupata kabisa fedha za mikopo pamoja na Wilaya 46 ambazo zilipata fedha za mikopo chini ya kiwango kilichotengwa kwa kila Wilaya.

Benki na Asasi za fedha zilizoteuliwa ni kama ifuatavyo:- *Akiba Commercial Bank*, Benki ya Posta, *Azania Bank*, *Mbinga Community Bank*, *Mwanga Community Bank*, *Kagera Farmers Cooperative Bank Ltd*, *SCULT (1992) Ltd*, *Presedential Trust Fund*, *Commercial Bank*, *Pride (T) Mufindi Community Bank* pamoja na *CRDB Bank* ambao wamekubali kuendelea kwenye awamu ya pili.

(b) Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza ya mpango huu Wilaya ya Kondoa ilipata jumla ya shilingi 41,641,000/= kupitia benki ya *NMB*, Wilaya ya Kondoa ni mojawapo ya Wilaya zilizopata fedha chini ya kiwango kilichopendekezwa kwa kila Wilaya.

Kwa msingi huo katika awamuy ya pili Wilaya ya Kondoa imetengewa shilingi milioni 100 za kukopesha wananchi na zitatolewa kupitia benki ya *CRDB* ambayo itatoa mikopo mara tatu ya fedha zilizotengwa kwa Wilaya hii.

Hii ikimaanisha mikopo yenyе thamani ya jumla ya shilingi milioni 300 itatolewa kwa wajasiriamali wa Wilaya ya Kondoa kupitia *SACCOS* ambazo zitakidhi masharti ya kukopesheka na wanachama kuwa na uwezo wa kurejesha mikopo itakayotolewa. (*Makofi*)

MHE. PASCAL C. DEREKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza; namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa, katika swali la msingi Naibu Waziri amekiri kwamba Wilaya ya Kondoa pesa zake zimepelekwa katika benki ya *CRDB* na kwa kuwa Wilaya ya Kondoa hatuna tawi la benki ya *CRDB* na kwa kuwa wananchi wanashindwa kufuatilia mikopo yao Dodoma kutokana na gharama kubwa:-

Je, Serikali haioni busara kuhamisha hizo pesa kwenda taasisi ama asasi zingine ambazo zinaweza kufika Wilayani Kondoa?

(b) Kwa kuwa *CRDB* haikopeshi watu binafsi inakopesha taasisi (*SACCOS*).

Je, haioni kwamba ni kutokuwatendea haki wananchi wa Wilaya ya Kondoa hasa wale binafsi ambayo ni wajasiriamali binafi ambao wanataka kukopa kwamba wanalazimika ama hawatapata fursa ya kukopa?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU (K.n.y. WAZIRI WA KAZI AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA): Mheshimiwa Spika, nakiri kabisa kwamba *CRDB* haina tawi Kondoa na kwa hiyo upatikanaji wa mikopo kwa wananchi ambao wanaihitaji inakuwa ni matatizo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nimesema katika jibu la msingi hapa kwa vile zipo asasi nyingi ambazo zimejitokeza kukopesha wananchi labda niseme kwamba atuachie tushauriane tuone kama kutakuwa na asasi nyingine ambayo itakuwa tayari kuwakopesha wananchi wa Kondoa kupitia mpango huu ili wananchi wa Kondoa waweze kupata fedha hizi kwa urahisi.

MHE. HERBERT J. MNTANGI aliuliza:-

Kwa kuwa mkodishaji wa shamba la Mpira la Kihuhwi Wilayani Muheza alitoroka bila kulipa mafao ya wafanyakazi kutokana na hukumu iliyotolewa na mahakama kumtaka awalipe wafanyakazi mafao yao, na kwa kuwa iliyokuwa Ofisi ya Rais (mipango na Uwezeshaji), wakati ikijibu swalı langu namba 130 mwaka 2004 kuhusiana na malipo ya wafanyakazi hao ilijibu Serikali itafanya juhudı kupitia vyombo husika ili mkodishaji aliyetoroka arejeshwe nchini ili aweze kutekeleza hukumu ya Mahakama kwa mujibu wa sheria, endapo juhudı hizo zitashindikana Serikali itatafuta utaratibu muafaka wa kuweza kuwasaidia wafanyakazi husika.

Kwa kuwa, tangu mwaka 2004 hadi sasa mwaka 2008 Serikali hajifanikiwa kumrejesha mkodishaji aliyetoroka Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi yake ya kusaidia kuwalipa mafao wafanyakazi hao.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI) alijibu:-

Mhehsimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swalı la Mhehsimiwa Herbert James Mtangi Mbunge wa Jimbo la Muheza kama ifuatavyo:-

Mhehsimiwa Spika, Serikali ilikodisha mashamba ya mpira ya Kihuhwi Wilayani Muheza, Tanga na Kalungwa lililopo Kilombero, Morogoro kwa kampuni ya *Merchantile Rubber Company Limited (Merchantile Freight company Limited)* ya Kenya tarehe 3 Agosti 1996. Kampuni hii ilishindwa kuendesha na kutekeleza masharti ya mkataba wa ukodishaji ikiwemo la kuendeleza ajira ya wafanyakazi wote waliokuwepo na kuwalipa stahili zo zote kwa mujibu wa sheria. (*Makof*)

Mhehsimiwa Spika, mkodishaji aliposhidwa kuendesha mashamba hayo aliondoka na kuyatelekeza bila ya kufuata taratibu. kufuatia hatua hii wafanyakazi walipeleka madai ya stahili zao mahakamani na hukumu ilitolewa kwa kuwapa tuzo dhidi ya mkodishaji.

Mhehsimiwa Spika, bada ya mkodishaji huyu kuondoka na kuyatelekeza mashamba haya; Serikali iliyakodisha kwa mwekezaji mwingine *Jumaan Muhsin El-Ardhi Co. Ltd*, kwa mkataba wa miaka kumi kuanzia Januari, 2001, mkataba ambao ungeisha mwaka 2011.

Hata hivyo, mkodishaji huyu naye pia alishindwa kuyaendesha mashamba haya na Serikali ikayatwaa Julai 2005.

Mhehsimiwa Spika, baada ya matatizo haya ya mara kwa mara toka kwa wawekezaji, Serikali ilitathmini ufanisi wa mpango uliokubaliwa wa uendeshaji wa mashamba haya ya mpira kwa njia ya ukodishaji.

Serikali iliamua kubadilisha mpango wa uendeshaji na uendelezaji wa mashamba haya ya ukodishaji ili yabakie kuwa sehemu ya kampuni ya *General Tyres* kwa ajili ya malighafi ya kutengeneza matairii.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya Serikali kuwa pale kampuni hii itakapoanza kuyaendeleza mashamba haya, baadhi au wafanyakazi wote waliokuwa kwenye ajira za makampuni niliyoyataja yaliyoshindwa kuendesha mashamba haya watarudishwa kazini.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH SOLOMON SUMARI) alijibu:-

Mhehsimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mtangi Mbunge wa Jimbo la Muheza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikodisha mashamba ya mpira ya Kihuhwi Wilayani Muheza, Tanga na Kalungwa lililopo Kilombero, Morogoro kwa kampuni ya *Merchantile Rubber Company Limited (Merchantile Freight company Limited)* ya Kenya tarehe 3 Agosti 1996. Kampuni hii ilishindwa kuendesha na kutekeleza masharti ya mkataba wa ukodishaji ikiwemo la kuendeleza ajira ya wafanyakazi wote waliokuwepo na kuwalipa stahili zo zote kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, mkodishaji aliposhidwa kuendesha mashamba hayo aliondoka na kuyatelekeza bila ya kufuata taratibu. Kufuatia hatua hii wafanyakazi walipeleka madai ya stahili zao mahakamani na hukumu ilitolewa kwa kuwapa tuzo dhidi ya mkodishaji.

Mheshimiwa Spika, bada ya mkodishaji huyu kuondoka na kuyatelekeza mashamba haya; Serikali iliyakodisha kwa mwekezaji mwengine *Jumaan Muhsin El-Ardhi Co. Ltd*, kwa mkataba wa miaka kumi kuanzia Januari, 2001, mkataba ambao ungeisha mwaka 2011. Hata hivyo, mkodishaji huyu naye pia alishindwa kuyaendesha mashamba haya na Serikali ikayatwaa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, baada ya matatizo haya ya mara kwa mara toka kwa wawekezaji, Serikali ilitathmini ufanisi wa mpango uliokubaliwa wa uendeshaji wa mashamba haya ya mpira kwa njia ya ukodishaji.

Serikali iliamua kubadilisha mpango wa uendeshaji na uendelezaji wa mashamba haya ya ukodishaji ili yabakie kuwa sehemu ya kampuni ya *General Tyres* kwa ajili ya malighafi ya kutengeneza matairii.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya Serikali kuwa pale kampuni hii itakapoanza kuyaendeleza mashamba haya, baadhi au wafanyakazi wote waliokuwa kwenye ajira za makampuni niliyoyataja yaliyoshindwa kuendesha mashamba haya watarudishwa kazini.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, swali la msingi hapa siyo ajira kwa wafanyakazi ambao kwa kweli wamekaa kwa zaidi ya miaka 13 bila kupata mafao yao. Suala la msingi ni kupata mafao yao. Sasa kimsingi Mahakama iliona ya kwamba wafanyakazi wale wana haki ya kulipwa. Kama Serikali ndiyo iliyokuwa msimamizi mkuu wa ukodishaji wa mashamba na imekuwa ikipata fedha kutokana na ukodishaji ule.

- (a) Je, ni kwa nini sasa Serikali isichukue wajibu wake wa kuliwapa wafanyakazi hao?
- (b) Mwaka 2004 wakati wa kujibu swali langu hapa Serikali ilisema itamfuatilia mwekezaji huyu. Katika jibu hili sioni taarifa zozote zinazoonyesha kwamba Serikali ilichukua jukumu hilo. Je, Serikali inasema nini kuhusu hatua ambazo ilipaswa kuchukua kumfuatilia mwekezaji huyu, taarifa inasema nini wamemkosa hasa kwa kutumia polisi wa kimataifa? (*Makofit*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kidogo ili tumalize swali la mwisho.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH SOLOMON SUMARI): Mheshimiwa Spika, kwanza ni vizuri tukaelewa kwamba mkataba wa ajira wa hawa ndugu zetu kule Muheza haukuwa kati yao na Serikali ulikuwa kati yao na mkodishaji. Si wajibu wa Serikali kwa hiyo kuwalipa ni wajibu wa yule mkodishaji na ndiyo maana walipokwenda mahakamani hawakuishitaki Serikali ilimshtaki mkodishaji na kwa hiyo Serikali hapa haina wajibu wa kumlipa mfanyakazi yejote wa mashamba haya.

Lakini la pili Serikali ifuatilie mkodishaji ni kweli wakati jibu la msingi la mwaka 2004 likijibiwa Serikali inasema itajitahidi kumtafuta huyu mkodishaji ili aje atimizie matakwa ya hukumu ambayo iliwapa tuzo wale wafanyakazi. Niseme hapa kwamba mpaka sasa hivi toka mwaka huo, ni mwaka wa nne sasa hawa mabwana hawajapatikana na niseme kwamba si rahisi sana katika kesi kama hii ambayo kwa kweli siyo kesi ya jinai kutumia *Interpol* anayosema na kwa hiyo sisi tunaridhika kwamba juhudhi ambazo zimechukuliwa, zimefanywa na Serikali mpaka sasa hivi zinaridhisha na kwamba tutaendelea kufanya hivyo. Lakini nataka kurudia jukumu la kuwalipa hawa wafanyakazi si la Serikali ni la zile kampuni ambazo zilikodishiwa mashamba haya.

Na. 476

Wananchi Kuuziwa Hisa za Benki ya NMB

MHE. FUYA GODWIN KIMBITA aliuliza:-

Kwa kuwa ipo nia ya kuwalinda na kuwajali kiuchumi wananchi wa Tanzania.

Je, ni tahadhari gani zitachukuliwa ili kuhakikisha hisa (*shares*) za Benki ya *NMB* zitakazouzwa zisinunuliwe zote na taasisi kubwa kama jinsi ilivyotokea katika uuzaji wa hisa za kiwanda cha sementi cha *Wazo Hill*?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mbunge wa Jimbo la Hai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kutangaza kujitoa katika ufanyaji wa biashara moja kwa moja, mkakati ulipangwa ni kuwasaidia wananchi katika kufanya biashara kwa kuwawekea mazingira ya kupata mikopo pamoja na kutoa fursa za kumiliki mashirika yanayobinafsishwa kwa ujumla wake au kwa njia ya ubia. Katika kufanya hivyo, tahadhari mbalimbali zimechukuliwa.

Kwa upande wa *NMB*, katika kuhakikisha kuwa wananchi wanafaidika na hisa za Serikali zinazouzwa Serikali kwa kushirikiana na mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (*CMSA*) imeweka tahadhari zifuatazo:-

(i) Mnunuzi wa hisa lazima awe Mtanzania au kampuni ya Watanzania. Mawakala wana jukumu la kuhakikisha wanaouziwa ni Watanzania.

(ii) Kiwango cha chini cha ununuzi wa hisa ni hisa 100.

(iii) Kutoa upendeleo maalum kwa waombaji wadogo iwapo kutakuwa na maombi zaidi ya hisa zinazouzwa (*over subscription*).

(iv) Hisa moja itauzwa kwa shilingi mia sita (600), kiwango hiki kitawezesha wananchi wengi kununua.

(v) Asilimia 21 ya hisa zitauzwa kati ya hizo asilimia 5 zitauzwa kwa wafanyakazi wa *NMB*.

(vi) Asilimia 80 ya ile asilimia 16 itauzwa kwa Mtanzania mmoja mmoja na vikundi vyta wajasiriamali na asilimia 20 iliyosalia itauzwa kwa makampuni ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuweka tahadhari hizo ni kuwalinda na kuwajali kiuchumi wananchi wa Tanzania.

MHE. FUYA GODWIN KIMBITA: Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Serikali hizi asilimia 21 zote isiachie wananchi ili kuweza kuwasaidia kwa wingi zaidi na zile asilimia 5 ziondolewe tena katika zile hisa za Serikali? (*Makofi*)

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kuruhusu wananchi wale Watanzania wenye vipato vidogo ambao wanamiliki hisa zingine katika baadhi ya mashirika ambayo yameshauza kununua hisa kwa maana ya kuweka dhamana zile hisa zao?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nieleze kwamba wafanyakazi wa Benki ya *NMB* ni Watanzania. Pili, sheria namba 23 ya mwaka 2003 imetoa mwongozo kwamba asilimia 21 tu ndizo ambazo zitakazouzwa kwa Watanzania. Ukiungeza hii asilimia 5 kutoka katika zile 30 zilizobakia tutakuwa tumekwenda kinyume na ile sheria.

Lakini la tatu, nataka niseme kwamba bado Watanzania wana nafasi ya kununua hisa za *NMB* kwa sababu Serikali siku za baadaye nazo hizi asilimia 30 itaanza kuzifikiria kuziuza. Kwa hiyo, kwa maana hiyo, naomba bado kuna upeo mzuri tu wa kwamba Watanzania wote wana hiyo, nafasi ya kununua asilimia 21 na hawa wafanyakazi wa *NMB* nao ni Watanzania kwa hiyo, wamo ndani ya ile asilimia 21.

Mheshimiwa Spika, la nne, ni kwamba kinachohitajika hapa kila Mtanzania aweze kununua shares kutoka katika hizi asilimia 21 kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa katika ile *prospectors*. Kwa mtazamo huo ni kwamba kwa hivi sasa haitakuwa rahisi kwa Mtanzania mwenye *shares* katika shirika jingine kutoa dhamana ya shares zile kwa ajili kununuliwa *shares* za *NMB*.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita. Nawafahamisha kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ana ziara ya kikazi Mkoa wa Kilimanjaro na ndio maana hamumuoni hapa asubuhi na kwa hiyo, anatimiza shughuli zake humu Bungeni ni Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais. (*Makofi*)

Ningempa ushauri tu kwamba kwa siku ambazo ye ye anakaimu nafasi hii humu Bungeni si vizuri tena kuja kujibujibu hapa kushika karatasi. Kwa hiyo, pengine badala ya kujibu mambo ya michezo angetulia hapo hapo atuee mwingine tu amsaidie.

Huyu ni ushauri tu maana yake hayo yananoga ukijaa sawa sawa kwamba umo katika viatu vya Waziri Mkuu. Waziri Mkuu ni hadhi kubwa. (*Makofi/Kicheko*)

Wageni: yupo mgeni wa aina ya kipekee wa Mheshimiwa Balozi Hamis Kagasheki Naibu Waziri wetu wa Mambo ya Ndani ya Nchi naye ni bwana David Mtensa kutoka Bukoba yeze ni mmoja wa watu wachache sana walionusurika katika ajali ya MV Bukoba mwaka Mei, 1996, naomba asimame yule pale. Kwa kweli pole na nadhani kumbukumbu za tukio hilo bado ni nzito nzito sana wakati wote. Lakini namshukuru Mwenyezi Mungu aliyekunusuru. Karibu sana Dodoma. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wa Mkao wa Tabora ikiwa ni pamoja nami tunao wageni pale *Speakers gallery* kutoka Umoja wa Wanawake Tanzania, wakiongozwa na ndugu Martha Kanakamfumu Katibu wa UWT Mkao wa Tabora naomba asimame. Amevaa nguo hiyo kwa masikilizano na Waziri Kabuya. (*Makofi/Kicheko*)

Ndugu Ashura Kimwaga Katibu wa UWT Tabora Mjini yule pale, ndugu Chiku Masanja huyu nimuweke mwisho. Subiri hapana haraka wewe utakuja. Ndugu Kaundime Kasesa Katibu wa UWT Nzega. Ndugu Edna Kigulu Katibu wa UWT Uyui. Ndugu Anjela Milembe Katibu wa UWT Igunga. Na mwisho lakini siyo mwisho kwa umuhimu ndugu Chiku Masanja Katibu wa UWT Urambo. (*Makofi/Kicheko*)

Huyu ndiyo anaweka mambo sawa pale. Kura za wanawake sina wasiwasi nazo kule Urambo. Karibuni sana, tunafurahi sana kuja kwenu hapa kujionea wenyewe mambo ya Bunge.

Tunao ujumbe wa wageni ambaa ni Waheshimiwa Wabunge 5 na watendaji wawili kutoka Bunge la Jamhuri ya Namibia nchi rafiki ya Namibia.

Waheshimiwa Wabunge hawa wamekuja kwa ziara ya kikazi ili kubadilishana uzoefu katika nyanja mbalimbali. Tutakuwa hapa Dodoma hadi kesho kutwa ambapo wataelekea Zanzibar kuonana na Viongozi wa Baraza la Wawakilishi. Sasa Waheshimiwa hawa, *Our visitors from Namibia as follows, honourable Pare Mshelenga*, yule pale.

Yeye ni *Chairperson of the Standing Committee and Leader of the Delegation*. Yupo Chief Ankama yule pale, ahsante sana, karibu. Yuko mwingine *Honourable Anodi Jiuhiiko* yule pale. Yupo *Honourable Unisi Jipinge* yule pale. Ahsante sana. Kwa ukakamavu wake nadhani huyu alikuwa katika mapambano ya kupigania uhuru bila shaka. (*Makofi/Kicheko*)

Yuko pia *Honourable Makenyi Venan* yule pale. Naambiwa huyu ndiyo alitoa hoja Bungeni Namibia kuhusu umuhimu wa haki za kumiliki mali (*Mover of the motion on property rights*). (*Makofi*)

Halafu tunaye Dr. Ben Fula yeye ni (*Consultant*) mtaalam. Pia tunaye kiongozi wa jopo ya secretarieti Bi. Theresa Philemon. Yule pale. *Is a great pleasure to receive our brothers and sisters from the friendly Republic of Namibia. We are very closed eyes,*

we continue to maintain them and your visits adds to strengthen our corporation and unit. Thanks very much and sends our regards to Namibia. (Makofi)

Tunaye bwana Veata Dots Mkuu wa Ushirikiano wa Maendeleo katika Ubalozi wa Ufalme wa *Netherlands*, yule pale. *Welcome, it is a pleasure to welcome one of the significant representatives of the Netherlands with whom we have such a long history of very usefully corporation. Thanks very for being in Dodoma. (Makofi)*

Sasa kuna wageni wa Mheshimiwa Charles Keenja amba ni walimu 10 wa shule ya msingi ya *Millennium* ya Tatu iliyoko Kata ya Kimara jimbo la Ubungo ambalo ndiyo jimbo lake la Ubunge. Wanaongozwa na mwalimu Peter Kimang'ano Mwalimu Mkuu na Mwalimu Benedict Malya Mwalimu Mkuu Msaidizi.

Naomba wasimame wale wa kutoka *Millennium Three*. Wale pale. Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa shule hii ina maendeleo mazuri sana kitalaam ilikuwa ya kwanza Mkoani Dar es Salaam mwaka 2005. Ya tatu kimkoa na kwanza Kimkoa Kiwilaya mwaka 2006 na katika mwaka 2007 yaani mwaka jana kati ya watoto 257 waliofanya mtihani wa darasa la saba 210 waliteuliwa kuingia shule za sekondari. Sasa Mheshimiwa Keenja, tugawane kidogo huwezi kuwahamishia hawa wachache wakaja Urambo au! (Makofi)

Walimu 25 kutoka Shule ya Msingi ya Mbezi nao wasimame tafadhali. Hawa wanatoka kata ya Mbezi Luis wanaongozwa na Mwalimu Eveline Mbishe mwalimu Mkuu na Emakulata Ng'itu Mwalimu Mkuu Msaidizi. Ahsante karibuni sana na tunawashukuru kwa kazi nzuri sana mnayofanya na tunawatakia mafanikio. Ila msisikilize maneno maneno yale ya CWT mara kutaka kugoma, hakuna haja ya kugoma. Dunia ya sasa wanajadiliana na kufikia muafaka walimu, hakuna hapana kugomagoma hapa. (Makofi)

Halafu kuna wageni wa Mheshimiwa Ernest Mabina, ni wazee maarifa wa Nyamalembo Geita, Mzee Ramadhan Khamis Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyamalembo yule na wenzake mzee Haruna Kaliango Mzee Martin Eveli. Karibuni sana. (Makofi)

Pia kuna mgeni wa Mheshimiwa Damas Nakei ni ndugu Ezekiel Katibu wa CCM wa Kata ya Mfano Wilayani Babati Vijiji. Yule pale. Halafu kuna wageni wa Mheshimiwa Dr. Lucas Siyame kutoka Mbozi Magharibi Mheshimiwa Alfred Simkoko Diwani wa Kata ya Kitete Jimbo la Mbozi Magharibi. Mheshimiwa Diwani, Ahsante sana. Karibu sana. (Makofi)

Pia tunaye bwana Gerefasi Mhogo ni Msaafuli kati ya Kamsamba. Ahsante sana.

Sasa Waheshimiwa Madiwani msitoke hapa tena mkarukia kugombea Ubunge sasa hivi. Waheshimiwa Wabunge wanaleteeni kwa heshima hapa mnarudi Mbozi mnaanza kutembea tembea tena. (Kicheko)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wote wa Mkoa wa Manyara ndugu Gitu Soni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Manyara yule pale. Ahsante sana na ndugu Solenda Odedra ambaye amefuatana na Mwenyekiti. Yule pale. Ahsante. Karibuni sana kutoka Manyara. Wapo pia wanafunzi 50 na walimu wao kutoka shule ya msingi Mlimwa Dodoma naomba wasimame kama wapo humu ndani ya Ukumbi. Wale pale. Ahsante. Tunawataki mema katika mafunzo. (*Makofi*)

Kuna jumla ya wanafunzi na walimu 40 kutoka shule ya msingi ya Mvumi Dodoma. Wale wanatoka kwa Mzee Malecela. Ahsante sana. Tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Kuna jumla ya wanafunzi 30 na walimu kutoka Seminary ya Hijra hapa Dodoma, wale wanaotoka Seminary ya Hijra baadhi yao wale pale, ahsante sana. Karibuni sana. Baada ya hao nadhani wageni sasa nimekamilisha. (*Makofi*)

Matangazo ya vikao. Mheshimiwa Omar Kwaangw' Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii anaomba leo saa tano asubuhi wajumbe wote wa Kamati ya Huduma za Jamii mkutano saa asubuhi leo ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Job Ndugai Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira anaomba wajumbe wote wa Kamati hiyo saa tano asubuhi wakutane ukumbi 219. Anasisitiza wajumbe wahudhurie bila kukosa.

Kamati tendaji ya *Life Ministry Tanzania* itakuwa na mazungumzo na chakula cha jioni katika ukumbi wa Hotel ya Mtakatifu Gasper saa 1.00 jioni leo. Mada ya leo ni *The African dream achieving leverage in a global economy*. Kamati inawaomba Waheshimiwa Wabunge kuyapa uzito mazungumzo haya kutokana na umuhimu.

Lakini pia kutokana na ukweli kuwa kadi za mialiko zilikwishawasilishwa kwenu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote wenye kadi za mwaliko kuhusu mazungumzoa yanayohusiana na *The African dream achieving leverage in a global economy* ni saa 1.00 leo Ukumbi wa *St. Gasper Hotel*.

Waheshimiwa Wabunge, weekend hii kulikuwa na zoezi la kupiga shabaha kule Makutupora na matokeo yalikuwa kama ifuatavyo: Washindi wa zoezi la kulenga shabaha kwa silaha ya *SMG (Sub Machine Gun)* mita 100 watatu wa Mheshimiwa Ali Juma Haji. Huyo hapa. Wa pili alikuwa Mheshimiwa Said Juma Nkumba. Nakuomba Mheshimiwa usimame na wa kwanza mshindi ni Mheshimiwa Ponsiano Nyami. Bahati mbaya hayupo. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa kwa zoezi la kulenga shabaha kwa silaha ya pistol mita 50 mshindi wa tatu ni Mheshimiwa Issa Kassim Issa. Leo hayupo

WABUNGE FULANI: Kwa yake kaka yake.

SPIKA: Kwa niaba yake kaka yake. Si haba. (*Kicheko*).

Mshindi wa pili, Mheshimiwa Elietta Switi ndiyo mshindi wa pili. Huyu mwanamke anayejua bastola hivi. (*Kicheko*)

Mshindi wa kwanza ni Mheshimiwa Said Juma Nkumba. (*Makofi*)

Hii yote ni kutokana na uwindaji kwenye ile mbuga ya Rungwa. Lakini natumaini Mheshimiwa unayo leseni ya uwindaji.

Waheshimiwa Wabunge, Muswada wa *National Assembly Administration Bill* umekuwa tayari na imeshindikana kuugawa katika *pigeonholes* kwa sababu wengi wetu tunatumia *pigeonholes* kama ghalo. Unaacha kila kitu mpaka siku ya kuondoka. Sasa nyaraka zote za leo haziwezekani. Kwa hiyo, nimeagiza kwa sababu ya umuhimu wa Muswada wenyewe na kwa kuwa utaiva na kuanza kujadiliwa tarehe 28 yaani keshokutwa basi wahudumu walete humu ndani nakala za Miswada ili kuwagawia.

Lakini kuna wengine taasisi mbalimbali zinatoa vielelezo, zawadi sasa kama bado *pigeonhole* zimejaa kabisa utakosa, hivyo. Utakosa kalenda, utakosa *diary*, utakosa vitu vingi tu ambavyo vingewenza kuwekwa pale. Si rahisi kuwatafutieni pote mlipo na siyo utaratibu mzuri kupitapita humu kugawa kalenda nyingine ni pana na kadhalika. Kwa hiyo, ninawasihi sana muende katika eneo la visanduku ili mpunguze vitu mbalimbali vilivyopo pale. Basi baada ya matangazo hayo Katibu tunaendeleaje sasa.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2008/2009 Wizara ya Fedha na Uchumi

(*Majadiliano yanaendelea*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naendelea kuwashukuru wenzangu namshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama aliyenishikia jana wakati tunamsindikiza mgeni wetu Rais wa Comoro. Namshukuru kwa kazi yake njema. Sasa ameniachia habari kwamba wazungumzaji leo ni 11 kwa kuwa, tunaendelea hadi jioni hii haina shida. Kwa hiyo, nitawataja wanne wa kwanza ili waweze kujiandaa. Mheshimiwa Halima J. Mdee wa pili Mheshimiwa Jenista Mhagama, wa tatu Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda na wa nne Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo. Kwa utaratibu huo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Lakini vile naomba nichukue fursa hii japokuwa tumesema kwamba hotuba ya Mheshimiwa Rais hajadiliwi nikupongeze wewe binafsi kwa hotuba yako fupi.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba mtoke kwa utulivu. Tunaendelea sisi wengine tunaosalia humu. Mheshimiwa Halima Mdee endelea.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nichukuie fursa vile vile kukupongeza wewe binafsi kwa hotuba yako fupi uliyoitoa yenyе mantiki sana na ambayo inaelezea uhalisia wa Tanzania. Ni hotuba ya dakika chache lakini ilikuwa ina ujumbe mzito kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nitazungumzia mambo matatu kama muda ukiniruhusu nitazungumzia suala la nne. Suala la kwanza ni udhamini wa Serikali kwa makampuni kwa kupitia udhamana wa *BoT*. Ni suala jema kabisa kama Serikali yetu inajitolea *ku-guarantee* makampuni hasa makampuni haya yanapokuwa yanakwenda kuomba mikopo kwenye asasi binafsi za Serikali.

Lakini kuna tatizo kubwa sana ambalo nadhani ni changamoto kwa Wizara yetu ya Fedha kuweza kuliangalia ili baadaye tuepukane na matatizo ambayo yanajitokeza sasa hivi. Kuna mtindo ambao umetokea sasa hivi, makampuni binafsi yanakopeshwa na Serikali au yanapewa *guarantee* na Serikali kwamba, kwa asilimia 100 na unakuta makampuni haya yanakuwa yana kiburi kweli kurudisha fedha. (*Makofi*)

Sasa tunapokuwa tunabeba mtindo wa aina hii tunalipeleka Taifa letu pabaya mno. Sasa hivi kuna mfano mmoja sitaitaja kampuni kwa sababu nina *interest* kwa mantiki mimi ni Mjumbe wa Kamati, lakini utakuta kampuni moja inaigharimu Serikali Serikali bilioni 117 na tunajua kwamba Serikali inatoa *guarantee* kwa kampuni nyngi sana.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha zaidi Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nayo inaingizwa katika mkumbo huu. Ni utaratibu wa kidunia kwamba mifuko ya hifadhi ya jamii inasaidia katika nyanja mbalimbali za maendeleo. Lakini ni vibaya sana tunapotumia mifuko hii kui-*abuse* kwamba tumekubaliana kipindi fulani mikopo fulani utatolewa ili kuwawezesha wastaifu wetu kupata pesa, lakini unakuta inapigwa danadana.

Kwa hiyo, hili ni tatizo na ninategemea kabisa Waziri wa Fedha atakaponijibu ataniambia kuna mikakati gani basi ya kuhakikisha kwamba hizi *guarantee* zinatolewa na Serikali zinakuwa zinalipwa kwa wakati muafaka kwa mantiki kwamba Serikali inahakikisha kampuni iliyoomba mikopo kwa benki binafsi zinarudisha kwa wakati muafaka na Serikali inakuwa haipati hasara. Kwa sababu hizi, pesa zikitolewa, maana yake kodi za wananchi nazo ndiyo zimekwenda na maji. (*Makofi*)

Vile vile nilikuwa napenda kuishauri Serikali, kwa sababu haingii akilini, unatoa *guarantee* kwa kampuni kwa asilimia 100! Vile vile wewe unakuwa hauna *mechanism* ya kuwa kweli lile eneo unahakikisha kwamba kweli kile kinachozalishwa na pesa inayopatikana inarudi kwa wale wadau. Sasa unakuta mtu anapewa mikopo kwa asilimia 100, Serikali ina-*guarantee* lakini yule mtu anajiendeshea kama anavyotaka. Sasa hili ni tatizo kubwa sana ambalo inabidi Serikali ili-*address* na iliangular tunafanye. Pesa nyngi sana zinapotea katika mianya hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie kuhusiana na vitega uchumi vyta Serikali. Nimepitia ripoti ya CAG nimeona kwamba Serikali inakaribia mashirika 144 ambayo ina hisa asilimia moja. Lakini cha kusikitisha, haya mashirika yanaendeshwa kama makampuni ya watu binafsi. Watu wanajiendeshea jinsi wanavyotaka, wanatumia pesa jinsi wanavyotaka na kuna mashirika mengine tunapiga kelele hapa kila siku tunaona tunayatetea kwamba yana bajeti ndogo kumbe hata hiyo bajeti ndogo wanajigawia wenyewe. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kuna uchafu kwa hali ya juu katika mashirika. Sheria za manunuzi hazifuatwi. Unakuta Wakurugenzi wa Bodi wenyewe wanajilipa vikao vyta siku tatu kwa siku moja. Kuna uhuni wa hali ya juu katika haya mashirika. Mimi nilikuwa shule, nimeingia Kamati kama siku mbili tatu, nimechanganyikiwa, nikasema mimi nikiendelea kukaa kwenye hii Kamati kwa muda wa miaka miwili na nusu kama sitatoka na mvi, basi ni hatari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo lilikuwa linazungumzwa hapa jana kidogo kidogo kuhusiana na suala zima la Bunge kuingia kwenye hizi Bodi za Wakurugenzi. Madudu tunayozungumza hapa na Wabunge wapo ni Wajumbe wa hizi za Wakurugenzi. Sasa unajiuliza, huyu Mbunge ambaye ni Mjumbe katika hii Bodi ya Wakurugenzi na ambaye naye ni mmojawapo wa watu ambao wanajilipa mara tatu tatu katika hizi Bodi za Wakurugenzi *ata-play roll* gani ya kuisimamia Serikali? (*Makofi*)

Mheshimiwa Rais juzi amesema kuhusiana na kuleta hii Sheria ya kuzuia *Conflict of Interest* wameshabikia kweli kusikia wanasiasa wanafanyabiashara wanatenganishwa. Hawajui kwamba huo moto utawawakia na wao! Kwa sababu haiingii akilini, wewe unaismamia Serikali na wakati huo huo ni Mkurugenzi. Kwa sababu ukiwa Mjumbe wa Bodi maana yake na wewe ni sehemu ya Ukurugenzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri watu wawe *alarted* wajue kwamba ikija hiyo Sheria na wao watapunyuliwa. Najua kwamba kama ukiamua kuwa Mbunge, kuwa Mbunge. Sio unakuwa Mbunge halafu tena unataka pia uwe na wewe msimamizi, uwe mtendaji. Sasa vitu kama hivyo inakuwa haviendi. (*Makofi*)

Vile vile miaka 80 ultolewa Waraka kutoka Ikulu, ambao waraka husika ulikuwa unakataza Wabunge kuwa Wajumbe wa Bodi *unless* kama Sheria imesema hivyo. Sasa sijui ule waraka ulipotelea wapi? Kwa hiyo, naomba tu Mheshimiwa Waziri akija atuambie imekuwaje? Kwa sababu sasa hivi Wajumbe wa Bodi wanateuliwa tu kwa vile ni mtoto wa fulani, kwa vile rafiki yake ni fulani. Hakuna *qualifications* maalum. Vile vile aliyekuwa Katibu Kiongozi - Mheshimiwa Paul Rupia, alitoa sifa za Wajumbe wa Bodi wawe akina nani? Naomba tu tuelenze hivi vitu vilikwenda wapi? Wiliishia wapi na sasa hivi tunaelekea wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala zima la matumizi mabovu ya fedha za Serikali. Taarifa za CAG zinaonyesha kwamba kumekuwa na ongezeko kutoka bilioni 844 mwaka 2005/2006 matumizi mabovu mpaka trilioni 1.08. Taarifa zinaonyesha kwamba kada inayonufaika zaidi ni ya Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa kuna matumizi mabovu sana. Unajua na Tanzania na sisi ni wajanja. Mtu anaiba pesa halafu anajua kue-*justify* yale matumizi. Ndiyo hicho kitu unakuta kinasababisha sana mianya hii inashindwa kuonekana ikoje. Ninatoa mfano mmoja. Japokuwa watu wanaweza wakaona kama vile nina lengo baya, lakini inapotokea mtendaji ambaye yuko katika maeneo yenu anafanya vitu vya ajabu ni vizuri kusema ili baadaye tuweze kuchukua hatua na tuweze kusafisha huu uozo uliopo. (*Makofit*)

Kuna utaratibu ambao unaitwa *sister cities* ambao unakuta wanaalikana Madiwani vijana kutoka mji mmoja kwenda mji mwagine. Taarifa zilizopo na ambazo pia ushahidi upo unaonyesha kwamba Meya wa sasa hivi wa Manispaa ya Kinondoni, alitumia hiyo *opportunity* ya Madiwani vijana kumweka mkwe wake kwenye safari kwenda Marekani. Taarifa ambazo zipo zinaonyesha vile vile kwamba Halmashauri ndiyo ilikuwa inahusika katika kulipa hayo malipo. Sasa kwa bahati nzuri wenzetu wa Marekani wako makini. Kwa hiyo, umakini wao ukafanya wagundue hili na walizie. Lakini inavyosemekana ni kwamba karibu shilingi milioni saba zililipwa. Wote wa ndani wanasema hivyo, ushahidi upo unaonyesha kwamba ilionekana Manispaa ndiyo ingegharamia hiyo safari.

Sasa vitu kama hivi, vinakatisha tamaa sana. Huu ni mfano mmoja. Ndiyo maana mimi kuna siku nililiza, huyu ni Mungu? Kinondoni kumeoza! *It is a known fact*, hakuna ubishi. Vitu kama hivi tunakwenda kujiaibisha kwenye mataifa. Unampeleka mkwe wako Marekani kwa kutumia nafasi ya Diwani! Hiyo ni aibu! (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, matatizo kama haya ndiyo yanayosababisha kwamba kila siku ripoti za CAG zinaonyesha matumizi mabovu ya fedha na tusipoziba hii mianya, mwisho wa siku tutajikuta karibu bajeti nzima ambayo tumeipitisha hapa ndiyo CAG anasema zimetumika kwa mantiki hiyo. Kwa hiyo, lazima tujifunze na lazima tujue tunasonga mbele vipi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, naona muda unakwenda. Naomba nimalizie kwenye hili suala la mikopo inayoitwa JK. Kimsingi hii inaonekana kwamba Watanzania wote tunaweza kuwa wajasiriamali. Kwa hiyo, sijui mambo yanakwendaje. Lakini mimi siamini kwamba kila Mtanzania ni mjasiriamali.

Mimi leo ukinipa biashara, sana sana nitachanganyikiwa tu na biashara hiyo itakufa. Lakini taarifa za BoT zinaonyesha kwamba kulikuwa hakuna utaratibu ambao ulikuwa umeandaliwa tayari kuweza kukamilisha hili jambo. Ndiyo maana sisi tulikuwa tunapiga kelele kusema kwamba huu ulikuwa ni uamuvi wa kisiasa ambao matokeo ya sasa hivi yanaanza kuthibitisha hivyo. Hakuna uwiano kabisa katika mgao wa fedha kati ya Mkoa mmoja na mwagine.

Unaweza kukuta Mkoa mmoja kwa mfano Mbeya ina shilingi bilioni sita, wakati huo huo Singida, Kigoma imepata shilingi milioni 500 tu. *It is not an initial population.* Mbeya ina *population* gani ya kupata shilingi bilioni sita ukilinganisha na Dar es Salaam

ambayo inapata shilingi bilioni mbili? Ukilinganisha na Kanda ya Ziwa ambayo imepata pesa ndogo kabisa uki-*compare* na hii, Mbeya ndiyo ina-*lead*. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hapa kuna tatizo na tusipokubali kuli-*address* hili tatizo tutakuwa hatufiki popote. Kumekuwa kuna malalamiko kwamba kuna tatizo la mgawanyo wa majukumu katika ya uongozi wa Wilaya na mabenki kuweza kubainisha watu gani wana sifa ili waweze kupewa mikopo na vile vile katika marejesho. Kwa hiyo, tumetoa pesa na marejesho yenyewe nayo yanakuwa ni hafifu. Ripoti ya *BoT* inaonyesha hivyo. Kwa hiyo, matokeo yake, hizi pesa zitakwenda chini. Sasa nataka tu Mheshimiwa Wazari akija anieleze haya mabilioni ambayo yanaitwa ya JK, mkakati wake kwenda mbele ukoje? Maana haya ndiyo makosa ambayo tumekwishayafanya, pesa zinaweza kuishia chini wachache waaminifu wakarudisha, matokeo yake pesa zinazidi kupotea kila siku pasipo sababu yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia hayo, nashukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Halima Mdee. Msemaji wangu anayefuata ni Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, wakati huo ajiandae Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwanza nakushukuru sana wewe, ila nakupongeza sana kwa jinsi na kwa kweli ulivyomudu kuongoza shughuli za Bunge letu kwa stahili yako ile ambayo ni ya *speed* na viwango vinavyotakiwa. Kwa kweli katika hilo hakuna ubishi kabisa, lile uliloahidi kwetu tunashuhudia kwa macho yetu kwamba kwa kweli linatimia na mimi basi nikuombee inshallah Mwenyezi Mungu azidi kukupa baraka wewe, Naibu Spika na Viongozi wengine wote wa Bunge kushirikiana kwa pamoja kuweza kuliweka Bunge letu katika *standard* ya kimataifa ambayo inatakiwa. Nakushukuru, nakupongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ni kweli kabisa Kanuni Namba 53 haituruhusu kuwashisha shughuli za mbele kwa mujibu wa utaratibu, Kanuni ile ndogo ya kwanza na ya nane. Lakini niseme tu kwamba ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri sana ambayo ilitoa mwelekeo wa masuala muhimu kama Kiongozi wa nchi ametimiza wajibu wake wa kuielekeza nchi namna gani. Anaufahamu wa mambo yanayoendelea. Ila namshukuru sana kwa kutoa maamuzi kwa kuanzishwa kwa *CDF*. Hilo kwa kweli ni lazima niseme, Mheshimiwa Rais ametutendea haki sana wananchi wa Tanzania na amewatendea haki Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini namshukuru pia kwa kukubali kuamua sasa kwa kweli Sheria ya Bunge iletwe Bungeni ili iweze kujadiliwa na kuitishwa. Kwa hiyo, hilo pia ninaomba niseme ninamshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia namshukuru kwa kuamua fedha za *EPA* ziende kwenye sekta ya Kilimo. Hilo lazima niseme. Masuala mengine tutayajadili kwa mtambuka itakapofika wakati muafaka wa kujadili hotuba ile na wewe ulishatupa

mwongozo jana. Kwa hiyo, tunaheshimu mwongozo wako na tunasubiri wakati muafaka utakapofika, basi tutafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa labda nianze kuchangia hotuba yenyewe kwa mtazamo ambao nimeuona. Mimi si Mchumi, sijasomea mambo ya fedha wala ya uchumi lakini nina *interest* sana na mambo ya biashara na nina upeo mdogo wa kuelewa haya mambo ya fedha. Lakini yapo mambo ambayo ninayoguswa nayo na ninadhani ni ya msingi kabisa nikiyasema hapa ndani leo.

Mheshimiwa Spika, taarifa za Mheshimiwa Waziri na taarifa za Wizara yetu ya Fedha na Uchumi tumeambiwa kwamba sasa hivi pato la Taifa limekuwa likikua na tumeambiwa sasa hivi ukuaji wa pato la taifa umefikia kwa takriban asilimia saba. Mimi nasema hiyo *economic growth rate* naipongeza, ninasema kwamba ni hatua. Lakini kinachonipa shida kidogo ni namna gani hii *growth rate* ya uchumi inaendana sambamba na *population growth rate* katika nchi yetu. Kwa sababu ongezeko la idadi ya watu na ukuaji wa uchumi katika nchi yetu, mimi naona kabisa kwamba ni *universal proportional* bado havijawa katika uwiano ule unaotakiwa. Uwiano huo sasa unatuletea athari kubwa sana na hasa katika maendeleo kwa wananchi wanaishi vijiji.

Mheshimiwa Spika, uchumi wetu kwa asilimia hiyo saba, tunasema umeshakuwa kwa asilimia saba umetegemea sana sekta zifuatazo:- sekta ya viwanda, sekta ya ujenzi na sekta ya maliasili. Sekta hizi ndizo sekta ambazo katika nchi yetu sasa hivi zinaonekana zinakua kwa kasi na zina-*boost* kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi katika nchi yetu ya Tanzania. Lakini ninasema hivi, bado asilimia 80 ya pato la Taifa la nchi yetu linategemea katika sekta ya kilimo. Wote tunakubali kwamba sekta ya kilimo ndiyo sekta mama na ni sekta kiongozi katika nchi yetu na sekta ya kilimo ndiyo ni sekta ambayo ikisimamia ukuaji wa uchumi ni sekta endelevu ukilinganisha na hizi sekta nyiningine nilizozitaja.

Hizi sio sekta endelevu sana na sio sekta za kuziamini sana. Lakini sekta ya kilimo ndiyo sekta ambayo tunatakiwa tuiamini. Lakini sekta hii ya kilimo kama wenzetu wa Wizara ya Fedha hawataweka jicho la makusudi kabisa kwa kuthamini kabisa kwamba sekta ya kilimo ndiyo sekta kiongozi na kutoa fedha za kutosha ili sekta hii ya kilimo iendelee kuwa sekta kiongozi, mimi nina wasiwasi ukuaji huu wa uchumi ukilinganisha na ukuaji wa ongezeko la idadi ya watu katika nchi yetu ya Tanzania, huko mbele tunaweza kujikuta tuna uchumi uliokua lakini usiowasaidia wananchi wa Tanzania na kama hatutasimama katika kuhakikisha kwamba sekta ya kilimo inaendelea kuongoza kwa sasa hivi, tuna taarifa ambazo wanatupa tunaambiwa kwamba sekta hii ya kilimo katika kuchangia pato la Taifa imeanza kushuka badala ya kwenda juu, inaanza kupungua kwenda chini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hapo ninaanza kuwa na hofu. Tumejitangazia tunatakiwa tuwe na mapinduzi ya kijani kwa maana ya kusukuma kabisa jitihada zetu katika suala zima la kilimo. Mimi nashauri mambo yafuatayo, ni lazima Wizara ikubali kwamba katika mipango yake katika nchi yetu ya Tanzania na hususan kwenye sekta ya kilimo, hebu waangalie, hivi ni kwa kiasi gani Serikali imeweka nguvu ya ziada kwenye

suala zima la *import and export* ya mazao ambayo yanalinwa katika nchi yetu ya Tanzania? Ni kwa kiasi gani tume-*add value* katika mazao yetu haya tunayolima na hii hatuwezi kufanikiwa kama kweli Wizara ya Mipango haitakuwa makini katika kusimamia suala hili.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba kama tuki-*add value* kwenye mazao ya kilimo *it means* kwamba pato la Taifa litaongezeka na linapoongezeka ina maana kwamba kodi ambazo wenzetu wa *TRA* wanaofanya kazi nzuri sana ya kukusanya mapato katika nchi yetu ya Tanzania wataweza kuwa na vyanzo vingine vingi vya mapato ambavyo ni vya kudumu na vinavyoolewaka. Lakini hapo bado hatujawa makini kabisa, ile *favorable balance of payment* haijaka katika mtizamo ambao kwa kweli ni mtizamo wa kiuchumi, ni mtazamo wa kuiongoza nchi yetu ielekee katika uchumi ambao ume-*stabilize* uchumi ambao ni wenyе tija, uchumi ambao utawakomboa wananchi wa Tanzania na kuwa na maisha bora.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba Wizara hii ya Mipango na Fedha izingatie umuhimu wa kuleta mageuzi ya viwanda. Nchi zilizoendelea tunesema kwamba suala la viwanda ndilo lilopeleke kuwa na maendeleo makubwa sana katika nchi za Ulaya. Sasa ninaomba hebu bajeti ya mwakani na hotuba ya Mipango na Fedha ya mwakani, watuambie wanaoanishaje suala hili la sekta ya kilimo na suala zima la sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, nilisema kwamba ku-*add value* kwenye mazao yetu ni lazima tuwe na viwanda. Wala mimi sizungumzii viwanda vikubwa sana ambayo viro katika nchi yetu, hapana. Tunaweza kuanza na *cottage industries*, tukaanza na vijiwanda vidogo vidogo. Kule wanakolima pamba wakapata viwanda vidogo vidogo. Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake juzi ametuambia kilo mbili za pamba zinaweza kutoa masharti mangapi? Kilo moja, sharti moja. Sasa kama haya masharti tungayatengeneza katika nchi yetu, kwa maana hiyo tungeweza kuongeza *export*, lakini tungkuwa tume-*add value* kwenye mazao yetu na hivyo tungeweza kuongeza pato la Taifa na uchumi wa nchi yetu kupitia sekta ya kilimo ambayo ni sekta mama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumbaku vile vile, hata mahindi tunayolima katika jimbo la Peramiho, kila siku tunayaiza mahindi kama mahindi, lakini tuki-*add value* tukatengeneza unga na mambo mengine kadha wa kadha, mimi nadhani tunaweza tukawa *stable*. Hii tabia ya kuendelea kuuza *raw materials* itatupeleka pabaya, imeshapitwa na wakati. Hebu amueni, Mheshimiwa Waziri wa Fedha wewe ndiye mwenye mipango ya nchi hii, fanya maamuzi baba yangu. Tengeneza mkakati nchi yetu isonge mbele badala ya kuendelea kuwa hapa mahali ambapo ipo.

Mheshimiwa Spika, lakini tunapozungumzia hili la kuoanisha ongezeko na ukuaji wa uchumi ninaomba sana Kitengo cha Takwimu, Kurugenzi yetu *Agency* yetu ya Taifa ipewe nyenzo za kutosha. Wale watu ndiyo wanaohifadhi takwimu zote. Mimi nilicheka sana, wale watu wanajua hata wanaomiliki redio katika nchi ya Tanzania ni wangapi, wanawake ni wangapi, wanaume ni wangapi! Sasa hawa watu ni muhimu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa kweli ndugu zetu wa Takwimu na wanaye Mkurugenzi mzuri sana Mama Chua, namfahamu, yule mama ni kiongozi mahiri, mpambanaji, ana

uchungu na nchi yake ya Tanzania. Hebu wapeni *support* wale watu. Kwa kweli watatuletea takwimu na bila takwimu hatuwezi kwenda mbele, hatuwezi kujipanga.

Mheshimiwa Spika, hata wewe ukitaka kufanya vizuri kwenye familia yako lazima ujue una watoto wangapi, watakula nini, watavaa nini. Ni shilingi ngapi zinatakiwa kuwalisha, jana, kesho, juzi na siku zijazo. Bila kuwa na takwimu, hakuna kitakachofanyika. Wapewe nguvu ndugu zetu wa Takwimu, apewe msaada wa kutosha sana yule mama ili aweze kutusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tudhibiti pia *leakages*. Katika kuingiza pato la Taifa bado kuna mianya mingi sana ambayo inatupoteza mapato. Watu wanapeleka bidhaa kwa njia za panya, wanafoji kabisa masuala yote ya uingizaji na utoaji wa mizigo. Haya ndiyo maeneo ambayo inabidi tuyakamate, Tuyafanyie kazi, lakini mimi nafahamu mwaka 1871 wenzetu wa UK waliwatafsiri *Internal Auditors* kama ni *watchdogs*. Hawa *watchdogs* ndiyo nadhani ni watu muhimu sana katika kutusaidia kuhakikisha sana suala la udhibiti wa mapato linashughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, mimi ninashangaa, hivi inakuwaje haya mamilioni yanapotea kila siku kwenye Halmashauri, kwenye Wilaya na kwenye Mikoa? Hawa *watchdogs* wako wapi? Inawezekana hawajengewa uwezo. Wenzangu jana wamesema sana, wapewe nyenzo, wafanywe nini, nakubali. Nadhani hawa watu ni muhimu, kama wenzetu mwaka 1871 waliwatafsiri hawa ni *watchdogs*, wasimamizi wakuu, wadhibiti, hebu tuwatumie vizuri waweze kutusaidia. Lakini tuseme hawa ni Wakaguzi wa Ndani, ndiyo *Internal Auditors*. Kwa hiyo, nadhani hawa Wakaguzi wa Ndani wapewe uwezo wa kutosha, watasaidia sana kukuza uchumi wa nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nisimalize bila kuzungumzia kero kubwa ya Hazina katika kutekeleza majukumu yao. Mimi nawapongeza Hazina, kweli wanafanya kazi. Lakini pia watu wengine wanaochelewesha maendeleo ya nchi ya Tanzania ni watu wa Hazina, wamekuwa wakifikiri kwa taratibu sana katika kufanya maamuzi ya kutoa fedha ili ziweze kutekeleza mipango mbalimbali. Iko miradi mikubwa sana ya Kitaifa, inatakiwa ipate *Government Guarantee*. Lakini Hazina wamesababisha miradi mingine ikose kupatiwa fedha za misaada *in one hundred percent* kwa sababu ya kuchelewa kutoa *Government Guarantee*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa huko siko tunakotaka kwenda. Wizara ishughulikie mirathi kwa utaratibu mzuri. Jana nilihoji hapa, utaratibu ule wa mikataba ya huduma bora kwa wateja iko wapi? Wananchi wanapata shida kwenye mirathi. Hiso fedha mmeziweka wapi wakati ni za kwao na walikuwa wanachangia? Wapewe watu kulingana na taratibu zilizowekwa. Malipo ya pensheni, bila kulia; nimefika Wizarani, mzee mmoja mpaka ametaka kuzimia kwa sababu ya panda, shuka, nenda rudi, hana hela ya chakula, hana nauli ya daladala. Hebu niwaalize Hazina, hivi ninyi mna miyo ya jiwe namna gani hamuwezi kuona kwamba mnatakiwa kuwa *efficient* katika masuala haya muhimu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninashangaa, hivi ni nini? Ni tatizo gani? Haya mafaili, sasa hivi tuna teknolojia ya kisasa kabisa ya kompyuta. Una-click tu lakini kazi ni

kubwa! Mtu hawezi kupata mirathi, hawezi kupata pensheni bila kumlilia Mungu wake na machozi ya damu yamtoke ndiyo aweze kupata haki yake. Kule kusumbua ili kupatikana kwa haki ya mtu ni dhambi kubwa sana hata mbele ya Mungu. Ninayo malalamiko ya wajane, yaani Mheshimiwa Waziri tunakuamini, hebu fanya mabadiliko katika haya. Mkataba bora wa kutatua haya matatizo, mkataba wako wewe unasema nini, ama wa kwako uko kwenye kabati katika kutatua matatizo haya? Tuambieni, mmekwama mahali, leteni sheria tuibadilishe, wahurumieni hawa watu wanavyopata shida katika kutafuta haki zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, malipo ya wastaaifu ni hivyo hivyo. Ni mlolongo mtupu! Mwisho niseme hivi, hiki kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2008/2009 umetuonyesha mwelekeo wa mwaka 2007/2008, umeeleza vizuri kwa mfano Sekta ya Kilimo hapa tumeelezwa. Tumeambiwa idadi sijui ya vyuo vya wanafunzi kilimo viliongezeka kutoka saba mpaka 11. Ni aibu! Saba mpaka 11! Hapana! Ndiyo, tuko kweli tunaamini kilimo ni sekta kiongozi! Tunachemka! Tunaambiwa kwamba kupanua kilimo cha umwagiliaji tulitoka hekta 268,388 mpaka 283,000 zilizoongezeka ni 81 tu.

Mheshimiwa Spika, tufanye mabadiliko kama tuko *serious*. Nakushukuru kwa kunipa nafasi. Namtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Jenista, kama kawaida mchango wako ni mzito na umezungumza kwa ufasaha mkubwa na umakini na dhati na vizuri sana kutetea wastaaifu kwa sababu umri ndiyo unakwenda kwenda hivyo na baadaye tunazamia Waheshimiwa Wabunge kuingizwa katika mfumo wa Pensheni. Sasa sijui na sisi tutakuwa tunafia kwenye ngazi za Hazina sijui, basi tutayaona huko siku za mbele. Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda atafuatiwa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. (*Makofi*)

MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie kidogo hii hotuba ambayo ipo mbele yetu. Mambo mengi yamezungumzwa na wachangiaji waliotangulia, lakini mimi nitajaribu kuchangia kwa kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kero ambazo aliahidi kuzishughulikia, lakini hadi hivi sasa hazijashughulikiwa na hii ni kuanzia mwaka 2006 mpaka hivi sasa. Nakukumbusha tu na uzuri wenyewe ni kwamba *ni-declare interest* Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu Waziri wote ni marafiki zangu kabisa. Kwa hiyo, nazungumza hii kutoka moyoni mwangu yale ambayo mliahidi, lakini hamkushughulikia.

Mheshimiwa Spika, nianze na huduma za benki. Mwaka 2006 nilajaribu kuelezea matatizo ambayo yanatupata katika Wilaya ya Chunya kutokana na huduma za benki. Hii nilielezea kutokana na hali halisi ya Wilaya ya Chunya jinsi ilivyo. Katika kijiji cha mwisho kiko umbali wa kilomita 270 hadi pale huduma ya benki inapopatikana na kule kuna watumishi, watumishi wanasadifiri kwa muda wa siku tatu kufika pale. Sasa unawenza uka-*imagine* wewe mwenyewe mwalimu ambaye anatakiwa awe darasani kwa wiki nzima, lakini kwa sababu ya utaratibu ambao upo anasadifiri kwa muda wa siku tatu

kwenda na siku tatu kurudi. Kwa hiyo, utakuja kuona kwamba karibuni wiki nzima hayupo darasani. Niliomba kwamba, kama haiwezekani kuwa na benki kule, basi hata *mobile bank* iwepo.

Mheshimiwa Spika, niliahidiwa kwamba wataliangalia na watalishughulikia, hiyo ni kero. Kwa kweli watumishi na watu wengine ambao wanafanya biashara wanapata shida sana katika huduma ya benki. Inaweza pengine ikafikiriwa kwamba labda sisi kule hatuna hela. Hapana! Tuna hela nyingi sana ambazo zinatokana na miradi mbalimbali. Tuna ziwa pale na tunavua samaki, tuna dhahabu, yaani kila kitu kipo kule ambacho kinatokana na fedha ambayo inapatikana. Lakini tunashindwa mahali kwa kwenda kuziweka, badala yake tunaweka kwenye vyungu. Nilikuwa naomba tu Mheshimiwa Waziri, ukumbuke tu, kama mlivyoniahidi, bahati nzuri mliniahidi kwamba mtakuja kule kujaribu kuzungumza na hivi vyombo vya fedha, lakini mpaka hivi sasa bado hamjaja. Nawakumbusheni tu kwamba hiyo ni kero katika Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye huduma za Bima ambayo ni kero vilevile. Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake walishaniahidi kwamba wangeshughulikia, yaani inashangaza bima imeshaiva zaidi ya miaka mitatu hawajapewa fedha. Nilipouliza mwaka 2006, Wizara ilisema waziwazi kwamba ni kweli Wilaya ya Chunya hawakulipwa kwasababu walipokuwa wanalipwa fedha zikaisha na wakaahidi kwamba watajitalidi, lakini mpaka hivi sasa ni miaka mitatu imepita. Nilikuwa naomba na hiyo ni kero, zile ni hela za watu, ni mkataba ambao Wizara au bima iliwekeana na hawa watumishi. Sasa kwanini isitekeleze huo mkataba? Bahati nzuri katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameonyesha mafanikio ya bima jinsi yalivyo, sasa kwanini mpaka hivi sasa hizo bima hazijalipwa? Ni kero mojawapo. Mimi nilisema nitachangia tu kuonyesha kero ambazo ziliahidiwa lakini bado hazijatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, nianze kumpongeza vile vile Mheshimiwa Waziri kwa utaratibu ambao ameubadili hivi sasa wa malipo ya pensheni. Ilikuwa ni shida kweli! Malalamiko yalikuwa nchi nzima, walikuwa wameanza kuandamana katika baadhi ya maeneo. Ule utaratibu wa kulipwa mwezi mmoja mmoja na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri umelitambua hilo, nampongeza tu kwa kurudisha ule utaratibu wa miezi sita sita, itatusaidia sana. Lakini tatizo ni mirathi. Kama mzungumzaji aliyepita alivyosema, nami nimekuletea *note* zaidi ya mbili kukukumbushia kuhusu mirathi ya baadhi ya watu ambao wanadai hayo malipo yao lakini mpaka hivi sasa kutoka mwaka 2006, nakukumbusha tena Mheshimiwa Waziri, rafiki yangu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kero ambayo imejionyesha kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana. Ule mfuko wa JK ambao Mheshimiwa Halima ametamka wazi wazi kwamba Mbeya ilipata bilioni sita. Sasa jambo la kushangaza, kwenye Jimbo langu hata mtu mmoja hakupata. Jamani na ninyi ni marafiki zangu, hivi ni kweli? Suala kama hilo hata mtu mmoja katika Jimbo langu hakupata hizo bilioni sita, zilikwenda wapi? Yaani hawakujua kweli kwamba kule Chunya kuna Jimbo la Songwe? Zile fedha zilipelekwa katika utaratibu ambao tayari walikuwa wameuanzisha wao wenyewe, watu wamejiandikisha, lakini hata mmoja hakupewa! Nikaahidiwa kwamba awamu ya pili basi

wataangaliwa, mpaka hivi sasa hakuna. Ninasikia kuna maeneo mengine tayari hizo fedha zimeshaanza kutolewa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyozungumza, ni kero tu. Sasa nakwenda kwenye kero ya mwisho inayohusu mizani. Sijui kama kweli tunatambua kwamba sasa hivi utaratibu wa mizani ni kero kubwa ambayo inaleta usumbufu mkubwa sana kwa waendesha magari. Hebu tuangalie pale Kibaha, ukipita pale wakati wa jioni magari mpaka darajani, kutoka kule kwenye mizani yenyewe mpaka darajani yamepanga msururu. Hivi kweli hatuwezi tukawa na utaratibu mwingine wa kuweza kujaribu kusawazisha hilo? Kuna wakati fulani nilijibiwa hapa kwamba upo utaratibu wa kujenga mizani kama miwili pale pale upande wa nyuma kule na upande wa mbele, lakini sina uhakika kama kweli hizo shughuli zinafanyika au zitafanyika. Kwa hiyo, naomba tu Wizara iangalie huu utaratibu ni kero kubwa sana. Tungeiangalia tu ili kusudi tutafute mbinu jinsi ambavyo tunaweza kushughulikia hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi sana mimi nilisema kwamba ni kero zinazonihusu mimi, kwa hiyo, sina kitu chochote zaidi. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake, lakini vilevile akumbuke hizo kero kwamba aliahidi mwenyewe. Kwa hiyo, ninategemea kwamba sasa zitashughulikiwa. Nashukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofifi*)

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii muhimu sana. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, ambaye kwa sababu ya muda sifa zake ni nyingi sana. Ameshika nyadhifa mbalimbali katika maeneo nyeti mengi, jana mlisikia ikizungumzwa kwamba aliwahi hata kuwa Msajili wa Hazina. Kwa hiyo, sifa zake ni nyingi.

Naanza na sifa kwa sababu nina sababu, ninakuja na mambo mazito mwisho, najua anayamudu ana uwezo nayo. Nimpongeze pia kwa kuteuliwa kwa nafasi hiyo hiyo Mheshimiwa Sumari ambaye pia kwa historia yake ya nyuma kwa haraka nilivyofanya utafiti ameshashika nyadhifa mbalimbali kwenye maeneo ya *institutions* zinazohusu fedha. Kwa hiyo uwezo anao na hata mabilioni ya JK alikuwa mmoja aliyeshughulikia kwa kasi kubwa sana kwa hiyo, uwezo pia anao.

Nimpongeze pia Mheshimiwa Mzee. Huyu namfahamu. Nilianza kumfahamu akiwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa kweli wanajeshi wengi ambao walikuwa wanadai mafao yao kwa muda mrefu waliweza kulipwa kwa jitihada yake kwa muda mrefu bila usumbufu. Watu waliokuwa wanadai Jeshi, mimi hususan nimeshughulikia watu zaidi ya watatu, ambao wote walipata fedha zao kwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, maana yangu ya kuwapa sifa zote hizi, wanamudu Wizara hii. Nimpongeze pia CAG kwa kazi nzuri sana anayoifanya, kwa kweli katika watu ambao wanani faraja katika nyakati hizi katika nchi hii ni CAG na ofisi yake. Kwa kweli nampongeza sana.

Nimpungeze pia Katibu Mkuu, Manaibu Katibu wakuu wote wa Wizara ya Fedha. Hapa naomba niamtambue pia Bwana Maswi. Bwana Maswi, huwa namtambua sana kwa sababu ye ye ndiye anashughulika na fedha za kupeleka kwetu Wilayani kwenye Halmashauri na Mkurugenzi wake na baadhi ya Watendaji wa Wizara. Nasema baadhi, sio wote. Niseme tu mpaka sasa hivi kazi nzuri mnaifanya, najua magazeti yanawasumbua, wakati mwingine vyombo nya habari, lakini lile ambalo mnaona linasemwa ambalo lina ukweli, basi rekebishi kwa sababu hawa nao wanaturekebisha ili tuweze kurekebisha yale ambayo hayaendi sawa. Lakini kwa yale ambayo mnaona kwa kweli hayana msingi ni kuyaacha na kuendelea mbele. Niwaeleze tu, usipoandikwa kwenye vyombo nya habari, usiposemwa semwa na wananchi, ina maana hufai kitu. Uwepo, usiwepo ni sawa.

Kwa hiyo, mjue kwamba kazi yenu inafanyika na inaonekana ndio maana mnazungumzwa. Habari nyingine mnakuwa mara nyingine mnaziacha zilivyo. Kwa mfano leo asubuhi nimesikia kwenye redio, naomba ninukuu: walisema kwamba: “*Bwana Tibaigana yuko huko kwake Kagera na Masilingi amekwenda mbio mbio na ana hasira sana kwa sababu anahisi Jimbo lake linachukuliwa.*” Masilingi tulikuwa naye jana hapa Mheshimiwa na leo tumekuwa naye. Kwa hiyo, vitu vingine ni katika mambo fulani ya nyakati. Kwa hiyo, ni kuyaacha. Nawapeni chachu mwendelee na kazi yenu.

Mheshimiwa Spika, nasema Wizara ya Fedha ni Utu wa mgongo wa nchi yetu
SPIKA: Pia Masilingi sio Mbunge wa Muleba Kaskazini, ni wa Muleba Kusini.
(*Kicheko*)

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nyongeza hiyo. Kwa hiyo, naona kwamba msisitizo huo kwamba sio yote ambayo ni ya kuyachukulia na kuyafanya kazi, yatawasumbua mshindwe kufanya yale ambayo mnakusudia. Naomba tu niseme matatizo, kwanini nilisema baadhi ya watendaji wa Wizara? Wengine wamezungumzia, lakini naomba nizungumze kwamba kuna tatizo kubwa la ucheleweshaji wa malipo. Hili nadhani mtakumbuka hata Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna kipindi alichangia hoja katika kikao hiki, alizungumza pia na akatoa hoja kwamba Hazina ni lazima kuna kitu cha kuangaliwa. Kwa kweli kuna matatizo. Unakuta bajeti imeandaliwa, imeletwa, imekubalika, imepitishwa, lakini unashangaa vitu vinachelewa.

Nitoe mfano, *OC* ya Kilindi. Unakuta inakaa mwezi unakatika karibu na mwisho wa mwezi unaokuja ndio *OC* inaenda, wakati sisi hatuna mapato yoyote, tunategemea *OC*. Sasa inapotokea dharura Mbunge, ndio anakuwa *OC*, sasa tatizo ni nini? Bado najaribu kuuliza, juzi tumeongelea Malaysia, *OC* haijaenda tangu Aprili ilisitishwa. Imekuja kwenda juzi kidogo na imechelewa, mishahara inachelewa, sijui sehemu nyingine. Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, mimi nina hakika kabisa kwa jinsi ya sifa zenu nilivyozieleza, wanao uwezo wa kuweza kujua tatizo ni nini. Kama ni mfumo, basi mfumo umepitwa na wakati, uangalieni upya mjue tatizo ni nini? Au kama ni watumishi, nadhani kuna watumishi ambao wamekaa muda mrefu sana kwenye madawati kiasi kwamba

wanafanya kazi kwa mazowea na wanaona wao ni wao hakuna mwingine wa kwenda pale, kwa hiyo wanaendelea hivyo hivyo. Au labda kuna wengine wanaogopwa kwa sababu wanajua maslahi ya wakubwa na siri za wakubwa. Nyakati hizo zimepitwa na wakati sasa hivi, kila mtu anajua. Kwa hiyo, mimi nadhani hawa watu ni wa kuondolewa au pia nahisi kuna watendaji wengine pale ambao wamewekwa lakini hawana uwezo na kasi ya kazi wanazozifanya inavyokwenda sasa hivi. Kwa hiyo, naomba mchekeche angalau hata katika Bunge lijalo tuweze kuona mabadiliko yamefanyika, wapelekeni sehemu nyingine za kazi wakaone mazingira mengine wajifunze upya halafu mlete wengine maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kero moja. Kuna kero ambayo mimi kwa kweli inaniuma sana. Niliizungumzia pia hapo awali nikichangia bajeti hii. Nitoe mfano ili niende haraka. Kuna fedha za magari zimetolewa kwa Wilaya kadhaa shilingi milioni 70 kwa ajili ya ununuzi wa magari na Kilindi ikiwa mojawapo ambayo hatuna magari kabisa. Fedha hizi zikaja na maelekezo zipelekwe Miundombinu. Zilipelekwa Miundombinu mwaka jana hadi dakika hii ninapoongea magari hayajatoka. Naambiwa kawaida huwa ukiagiza kama *block*, bei inashuka. Sasa tumepewa shilingi milioni 70, wote tumepeleka kule Miundombinu, wanachochelewesha ni nini? Au kuna kamisheni nyingine inayosubiriwa tena Miundombinu wapunguziwe zaidi? Ninamuomba Mheshimiwa Waziri, hayo magari basi yatoke kabla ya mwisho wa mwezi wa tisa. Mwaka mmoja na ni muda mrefu sana, tupewe sababu ni kwanini inakuwa hivyo?

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile niseme lingine. Kuna Halmashauri changa kama ya Kilindi ambayo mapato yake ni kidogo sana. Sisi tunategemea magulio na msimu wa kilimo, kwa hiyo, kwa kweli hali inakuwa ni ngumu sana. Sasa unakuta kuna hizi fedha, mtatambua wote kwamba leseni za utafiti wa madini hapa Tanzania ni sawa na uchimbaji, ni uchimbaji moja kwa moja, sasa zile fedha zote zinakwenda Serikali Kuu. Hebu jaribuni kubuni kwamba *percent* fulani iende kwenye Halmashauri iweze kutusaidia. Kwa sababu sisi tunaona tu watu wanatafiti, wanatafiti, haina mwisho na madini yanakwisha lakini hela zote zinakwenda Serikali Kuu. Kwa hiyo, nilikuwa naliombea sana hilo.

Mheshimiwa Spika, suala la pensheni ndogo naomba nisilirudie, wenzangu wamelisema sana. Jamani inueni viwango vya pensheni, hamwezi kuelewa umuhimu wake mpaka pale mnapokuwa nyie ni *pensioners* ambao mnategemea pensheni. Kwa hiyo, nami naongeza hapo msisitizo.

Mheshimiwa Spika, hisa za *NMB* Mheshimiwa Naibu Waziri amejaribu kueleza leo asubuhi lakini naomba nieleze tena kwa msisitizo. Hii 21%, 5% wamesema ni wafanyakazi, 16% ni wananchi wote ambao ni milioni 37 *point* na taasisi zake, wananchi wa Kilindi watapata hizi hisa kweli? Au ni kwa watu fulani fulani mpaka zimalizwe huko mijini ukawaelimishe wale watu waelewe ni kitu gani, hisa zimeshakwisha. Mimi naomba, kwa sababu amesema sheria haimruhusu, basi naomba wahimize Serikali iweze kuuza zile asilimia 30 za *share* zilizobaki mapema. Vilevile *NBC* sasa hivi inafanya kazi vizuri, Serikali ni lini mtafkiria kuweza kuuza *share* za *NBC*?

Mheshimiwa Spika, pia niseme hapa, naishukuru sana *NMB*, kwa muda mrefu nimekuwa nikizungumza hapa Bungeni, nikitoa wito, nikibembeleza, hatimaye tunawashukuru ofisi yao inamalizia ukarabati na wakati wowote tutaanza na huduma ya benki ya kwanza Wilaya ya Kilindi ambayo ni *NMB*. Naomba niite na nyingine. Nichukue fursa hii na mimi kama wenzangu, nimpongeze Rais kwa uamuzi wake wa awali. Nasema wa awali kwa sababu najua kuna hatua nyingine zinafuatia kwa ajili ya kuamua hela za *EPA* nyingine ziingie kwenye *consolidated fund* ambayo itakuwa ni ya Serikali na nyingine ziende *TIB*. Sasa mimi nisemee zile za *TIB*.

Huu uamuzi ni mzuri sana, lakini hawa walikuwa wamezoweа *industries*, viwanda na *estates* ndio ilikuwa kazi yao kubwa. Sasa hivi wanaletewa kilimo, kuna haja ya kufungua *window* ya kilimo ambayo kwanza waongezewe uwezo kwa jinsi tunavyofahamu *TIB*, *capacity* yao ni ndogo sana. Kwa hiyo, tunaomba hapa waangaliwe *capacity* yao kwa maana ya watumishi na sio tu watumishi, watumishi wenye uwezo wa kufanya kazi hizo ambazo ni za sekta ya kilimo ambaо wanaelewa wana-deal na watu gani, kwa ajili wakulima mnaelewa uelewa wao.

Kwa hiyo, tupate watu wa aina hiyo na vitendea kazi ambavyo vinaendana na wakati ili angalau tuweze kufikia hilo lengo. Kwa hiyo, hili nilikuwa naliomba sana Mheshimiwa Waziri, aweze kulismamia. Lakini kwa sababu Mheshimiwa Rais alisema pale kuna shilingi bilioni 260 kama nilimnukuu sawa sawa lakini hata kama sio sawa sawa kuna fedha ambazo zipo ambazo zitaingia kwenye *consolidated fund* ambayo inatakiwa muda wote iwe na pesa kama alivyoeleza.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia kwako, kuna mambo mengi ambayo yanahitajika yafanyike na kwa haraka ambayo hayajafanyiwa kazi. La kwanza kabisa, ninaomba niseme Benki ya Posta, kama taasisi nyingine, benki hii imekuwa ikifanya kazi vizuri sana, wote tunaona. Haijaweza kwenda Mikoa yote kwa sababu inajiendesha kwa pesa kidogo sana, lakini wengi mtakubaliana nami kwamba kazi hiyo wanayoifanya ni nzuri sana. Hawa watu hawana mtaji, wamekuwa wakiomba. Huko nyuma tumesikia wakiomba sana mtaji. Wameomba shilingi bilioni 15 sijui shilingi bilioni 20, wala sio fedha nyingi.

Sasa mimi namwomba Mheshimiwa Waziri, ninaamini kwamba analishughulikia suala hili kwa sababu kwa kuchunguza nimesikia wanalishughulikia na kwa kasi yake najua kwamba litakamilika. Wapewe basi hata shilingi bilioni 10 tu ili angalau waweze kumalizia kufungua *branches* kwenye maeneo yaliyobaki wanunue na vitendea kazi ambavyo ni vya teknolojia ya sasa, kompyuta na kadhalika ili waweze kufanya kazi vizuri. Wameaminiwa, wamepewa kazi ya kushughulikia mabilioni ya *JK*, hilo nadhani hawatashindwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni vitambulisho. Kwenye vitambulisho leo Mheshimiwa Naibu Waziri, ameleeza hapa umuhimu na zabuni zimetolewa. Zabuni zimetolewa, hakuna pesa, zabuni ikishapita tunasubiri mpaka *financial year* ijayo ndio kazi ianze. Sasa katika fedha hizo Mheshimiwa Waziri, kwa sababu ya *seriousness on this matter* na upande wa pili wa muungano wanasema kazi ya vitambulisho imefanyika,

ile tunaacha tunasema kwa nchi nzima ya Tanzania, tunaomba basi hilo liweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, nyumba za askari ni kilio cha muda mrefu, wengi ambao tumeeleza tumeshuhudia nyumba imetenganishwa na blanketi, kila mtu alisema hapa aliyoona. Basi tunaomba fedha zipelekwe huko na hususan fedha za magari, Wilaya ya Kilindi yote hakuna gari la Polisi. Ikifika, gari la Mbunge ndio linakuwa gari la Polisi au labda siku moja *DC* ndio aache gari lake litumike na Polisi. Ninaomba sana, huo ni mfano mmoja na mifano ipo mingi. Halmashauri ya Kilindi inajenga jengo la Halmashauri, Mheshimiwa Waziri, limefika mahali pazuri tumefika kwenye lenta, tunahitaji shilingi bilioni moja tu kukamilisha. Vitu vinapanda bei kila siku. Tukingoja mpaka mwakani itakuwa shilingi bilioni mbili, bilioni tatu. Tunaomba basi na sisi tufikiriwe kwenye hela hizo hizo.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Huria waliomba hela pia za kuweza kuwasaidia kuendesha kazi pale. Unakuta mitihani inashindwa kusahihishwa kwa sababu hakuna fedha za kuwalipa wasahihishaji, matokeo yanashindwa kutoka na kadhalika. Hivi ni vitu ambavyo nimeona ni vya muhimu vimejirudia mara kwa mara, tuweze kuvifanyia kazi.

Lakini lingine ninalotaka kusema, kwa kweli wengi tumeungana mkono na Rais kwenye vita hii ya ufisadi, rushwa na ubadhirifu. Kila mtu amechangia kwa nafasi yake, mwananchi wa kawaida mpaka sisi Wabunge. Lakini hapa nataka kusemea moja. Kuna watu ambao wamejitoa mhanga kwenye maneno haya, wamesimama kidete bila uwoga wala kujali maisha yao na familia zao na kusema.

Mheshimiwa Spika, natoa mfano, mmoja ni Mheshimiwa Anne Malecela, lakini baada ya hapo tukashangaa magazeti yanaanza kumkejeli, mara wamwandike *Anne in Anne Out*, mara sijui waandike ooh, sijui huyu tuone atafanya nini, muda umefika alisema hapatatosha! Jamani! Sasa hivi matokeo yametokea, Mheshimiwa Rais wetu ametufundisha subra. Mambo yamefanyika, lakini tupeane moyo, mtu anapoibua jambo kwa maslahi ya nchi yetu na sio binafsi, tupeane moyo, tumuunge mkono, tusaidiane ili nchi hii ifike mahali. Tukianza kukatishana tama, wote tutanyamaza, halafu tatarudi kule kule ambako tumekuwa miaka yote. Hilo niliona niliseme.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho, kabla muda wangu haujawkwisha niseme pia tuna tatizo lingine. *Priorities* zipo, tunaweka vipaumbele vyetu, mipango tunaifanya na Bunge kwa mfano tuliwekewa semina tukakaa tukafanya yote hayo, lakini utashangaa ikija kwenye utekelezaji, miradi haikamiliki kwa wakati, wakati fedha zilishatengwa na zimetolewa. Au zile fedha ikifika katikati zinafanyiwa kitu kingine, mradi haukamiliki au haikamiliki kwa viwango. Nina mifano mingi ambayo inatumia mabilioni, mradi umefika katikati eti ghafla maamuzi yamebadilika, wanaanza kitu kingine cha tofauti. Yale mabilioni yamekwenda pale, tatizo ni nini? Sasa hawa watatu nilianza na sifa zao kwa maana najua wanaweza wakachambua tatizo ni nini kwa kushirikiana na sisi na wengine wengi na wataalamu wa uchumi tulionao ndani ya nchi yetu tukaweza kujua matatizo ni nini na tukaweza kuyatatua, kwa pamoja tutashirikiana.

Mheshimiwa Spika, juzi ulimwambia Rais, mambo yote yanawezekana ndani ya nyumba hii, tuna madaraka ya kufanya mambo mengi. Tuko tayari kuyafanya bila uwoga, bila hofu, kwa hiyo, tunaomba mtutumie na tutashirikiana na ninyi ili kazi iendelee na hatimaye maisha bora kwa kila mtanzania yaweze kufikiwi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante. (*Makofii*)

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Naomba nianze kwa kukubali kwamba mimi sio mtu wa fedha wala sio mchumi. Mimi kwa uweledi wangu ni mtu wa mazingira, masuala ya rasliamali za asili. Kwa hiyo, kwa kweli katika mchango wangu nitajikita kwenye eneo la mipango; *Planning* katika Taifa letu na jinsi linavyohusisha masuala ya mazingira, *development planning and environment*.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ambayo mimi binafsi nimeendelea kuona yanaonyesha udhaifu katika katika utendaji kazi wa Serikali ni katika eneo la mipango pamoja na *planning*. Ninataka nithibitishe hilo kwa kuangalia mlolongo mrefu sana wa michakato mbalimbali ya mipango ambayo tumeijaribu katika kipindi chote tangu wakati wa uhuru. Kwa mfano tangu wakati wa uhuru tulikuwa na mipango ya vipindi, kulikuwa na mipango ya miaka mitatu, miaka mitano, miaka 15 na miaka 20. Tulikuwa na *RIDEPS* (*Rural Intergrated Development Plans*), tulikuwa na *Zonal Physical Plans*, tulikuwa na *Emergency Plans* nyingi sana, tulikuwa na *Rolling Forward and Budgeting Plans* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mipango hii yote imekuwa na matatizo na kasoro mbalimbali na ninataka nitoe mifano michache ambayo inahusiana na mazingira. Kwa ujumla mipango yetu yote na mchakato wa kuandaa mipango ulikuwa *top – down*. Unaanza juu, unashuka chini kutoka kwenye ngazi za Wizara kwenda chini kwenye viji. Mipango yetu ilikuwa inategemea sana wahisani, katika kufikiri na hata katika kutupa fedha za kufanya michakato hii na hiyo ililetu suala la *sustainability*, uendelevu wa mipango hiyo kama itakuwa endelevu au hapana na kwa kweli haikuwa endelevu na mingi ilishindakana tuliiacha. Mipango yetu mingi ilikuwa ni ya kisekta, haikuwa *intergrated*.

Kwa hiyo, kila watu, kila sekta walikuwa wanaangalia kama kwenye *pegion hole* mipango yao wenyewe bila kujali mazingira yanayowazunguka na sekta nyingine zitahusika vipi katika mpango wao. Mipango yote hiyo kwa ujumla ilikuwa haihusishi sana masuala ya mazingira, kwa hiyo, haikuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, naona mambo yameanza kubadilika sasa na Baraza letu la Mawaziri kwa ujumla wamekubaliana kuhusisha masuala ya mazingira kwenye tathmini au kwenye michakato ya kuandaa sheria, kuandaa sera, mikakati na mipango kwa mujibu wa sheria mama ya mazingira ya mwaka 2004 na tumekubali kwamba sheria ile inatutaka katika sekta zetu katika mipango yetu ya kitaifa iwe ya Mkoa, Wilaya, lazima tuhakikishe mipango hiyo imehusisha masuala ya mazingira. Kitu ambacho kwenye *level* hiyo

kinaitwa *strategic environmental assessment* ambayo ina maana tathmini ya kimkakati ya mazingira.

Kwa hiyo, kukubali huko na Baraza la Mawaziri linawawajibisha Mawaziri hawa pamoja na Wizara hii kuhakikisha kwamba masuala ya mipango yanahuisha mambo ya mazingira na hususan kuhusisha *strategic environmental assessment* katika mipango inayoandaliwa. Nafarijika kuona kwa sasa tumenza vizuri, tutakuwa na Tume ya mipango, lakini ombi langu ni kwamba Tume hiyo basi katika timu ile ya wataalamu hawa wa mipango kuwepo na watu wenye utaalamu wa mazingira na hususan wenye uweledi katika masuala ya tathmini ya kimkakati ya mazingira, *strategic environmental assessment*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hii ni muhimu kwa sababu ninachotegemea sio utaratibu wa sasa wa kufanya kwa mfano *environmental assessment* au *strategic environmental assessment* baada ya mipango na sera hizi kuwa zimeandaliwa na baada ya mradi kuwa umeandaliwa utaratibu unatutaka tuainishe masuala ya mazingira, wakati tunafanya mchakato wa mipango hiyo. Hapa kwa sababu nazungumzia mipango, wanasema mpango wowote utakaokuwa *rulled out*, mchakato ule uwe umehusisha masuala ya mazingira humo ndani yake. Kwa hiyo, ni lazima uwe na watu, wataalamu hao kwenye timu hiyo ya watu wanaofanya *planning*.

Utaratibu ni kwamba, kuna kitu kinaitwa *strategic environmental assessment principles* ambazo ndio zinatakiwa zizingatiwe na *principles* ambazo zinatakiwa ziainishwe wakati wa kufanya mchakato wa mpango kama zifuatazo na ni chache tu:-

Kwanza, inatakiwa kuhusisha, mpango uhusishe, uangalie *in broad terms* masuala ya ki-baiolojia, ki-ikolojia, ki-jamii na ki-uchumi. Vyote hivyo viangaliwe kwa pamoja, nadhani ndio timu ikiwa *intergrated* vya kutosha, watakuwa wanavichambua na *ku-disscuss* pamoja wakati wakifanya na kuanda mpango huo.

Pili, wahakikishe kwamba mpango watakaoutoa unakuwa endelevu, ni *principle* nydingine.

Tatu, wazingatie uwajibikaji, kwamba kila mtaalamu atahusika na kitu fulani katika Wizara katika kutekeleza huu mpango utahusika na masuala fulani. Ni lazima Wizara na wataalamu wale wawajibike *at the end of the day* na matokeo yatakayotokana na mpango huo utakapoanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kimoja cha msingi, *planning* hiyo iwe endelevu, ishirikishe wadau katika ngazi zote. Haitatusaidia, tutarudi nyuma kule kule. Mkikaa Wizarani, hata hiyo timu ikikaa peke yake kule na ikatoa mpango au mkakati au sera haitatusaidia, ni lazima ihusishe wadau wa ngazi zote kabla mpango huo haujaidhinishwa au haujakubalika na sisi wote.

Kama tutafanya hivyo tutahusisha au kuwa na wataalamu wenye uweledi wa *strategic environmental assessment* katika *planning* yetu tutaondoa na kuepusha kabisa

wakati mwingine umuhimu wa kufanya *environmental impact assessment* ambazo zinatakiwa ziwe nyingi sana. Kwa sababu kwenye mpango na mkakati mwishoni kunakuwa na miradi kadhaa na kila mradi unatakiwa uwe na *environmental impact assessment*, lakini ukifanya vizuri mpango wako ukaainisha kwenye *level* ile ya ngazi ya juu masuala yote ya mazingira ya kiuchumi ya kijamii yamehusishwa yote, pengine sio lazima sana kufanya *environmental impact assessment* kwenye ngazi ya mradi. Hiyo itatupunguzia sana gharama za utendaji na kuhakikisha kwamba miradi yetu inakuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba, Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake nitataka anithibitishie hilo. Ninachotaka kujua ni kwamba: Je, katika timu hiyo ya mipango wameweka au wataweka wataalamu wenyewe uweledi wa kutosha kwenye mambo ya mazingira na hususan mambo ya *strategic environmental assessment?* Watusaidie kuainisha masuala hayo ya kimazingira, kiuchumi, kijamii, ki-ikolojia kwenye mchakato huo wa mipango ambayo itakuwa inatekelezwa au inaandaliwa kwa faida ya nchi yetu.

Mimi nina uhakika kama tukiendelea kudharau masuala ya mazingira hatutafika mbali. *Resources* zetu nyingi tulizonazo hapa nchini ni zile zinazokwisha, hatutaendelea kuwanazo, hatuwezi kula keki tukabaki nayo, ni lazima tuainishe mambo yote ya kiuchumi, kimazingira na kadhalika, tuhakikishe kwamba kila tutakachojaribu kukifanya hakitatuletea athari ambazo tutashindwa kuzimudu hapo baadaye. Tuhakikishe kwamba chochote tutakachokiibua, mradi au mkakati, sera inakuwa ni endelevu, sisi tutafaidika kiuchumi, lakini watoto wetu wataendelea kuziona raslimali hizo bado zipo wakaendelea nao kuzitumia kwa faida yao hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Naomba niseme kwamba naunga mkono hoja, isipokuwa nitataka huo ufanuzi wakati wa majumuisho nijibiwe hilo. Ahsante sana. (*Makofit*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi. Sasa namwita sasa Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Fred Mpandazoe Tungu ila nashangaa wachangiaji watarajiwa wanne wanaofuata hawamo katika ukumbi, nao ni Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Kilontsi Muhamma Mporogomyi, na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah. Sasa sijui kama wapo karibu au itakuwaje. Lakini hao wawili Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Fred Mpandazoe Tungu.

MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu. Awali ya yote napenda nitamke kwamba mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa hiyo, ninalolifanya sasa ni kusisitiza na kuongeza yale ambayo hayamo katika ripoti ya Kamati ya Fedha na Uchumi iliyowekwa mezani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nianze vile vile sasa kuchangia kwa kuwapa pole wananchi wa Tabora Mjini na kwa habari nilizonazo, pole hizi zifike mpaka

kwa wananchi wa Shinyanga kwa sababu tuna tatizo kubwa sana la umeme kuanzia siku ya Ijumaa usiku mpaka hivi leo na hatujui tatizo hili litakwisha lini. Sasa kwa kupitia Bunge lako Tukufu ningependa Serikali ifahamu, najua inafahamu, lakini ichukue hatua za dharura kuhakikisha kwamba tatizo hili linamalizwa, kwa sababu vinginevyo shughuli zote za kiuchumi ambazo ndiyo msingi wa kodi na mapato ya Serikali katika Mikoa hiyo miwili sasa hivi zimesimama. Matatizo mengine ni pamoja na ukosefu wa maji katika Mji wa Tabora. Bila umeme hakuna maji, kwa hiyo, hii ni dhahiri kwamba jambo hili linahitaji kushughulikiwa kwa dharura.

Mheshimiwa Spika, tunayo jenereta pale katika kituo cha umeme cha Tabora, lakini jambo la kusikitisha ni kwamba jenereta ile ilipaswa kuwa *standby*. Yanapotokea matatizo ya namna hii iweze kuwashwa lakini haiwezi kuwashwa kwa sababu na yenye ni mbovu pamoja na kwamba ni *standby*. Kwa hiyo, hayo ndiyo matatizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niendelee na suala la Tabora. Katika kuhitimisha hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu alitamka kwamba Serikali imesikia kilio cha wananchi wa Tabora mpaka Kigoma kupitia Urambo kuhusu barabara mbaya na kwa hiyo, pamoja na kwamba kulikuwa hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya barabara ya Manyoni, Itigi, Tabora, Urambo na Kigoma, Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema Serikali itatenga Shilingi bilioni 10 kwa kuanzia kwa ajili ya mradi huo. Sasa ningependa kupitia Wizara ya Fedha, nipate maelezo ya uhakika kwamba: Je, Wizara ya Fedha imeshazitenga fedha hizi kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niendelee kwenye suala la ubinafsishwaji wa Benki ya *NMB*. Ubinafsishaji wa Benki ya *NMB* umeleta maneno mengi na Wabunge wamekwishachangia. Mimi ningependa kuchangia kwa kusisitiza yale yaliyokwishesemwa, lakini nirejee kwenye Sheria inayohusika.

Mheshimiwa Spika, Sheria inayohusika ambayo kwa bahati mbaya inaelekea Wizara ya Fedha bado hawajakiangalia kile kipengele cha 6(b) ambacho kinasema, baada ya kuuza asilimia 70 ya Benki hiyo, Sheria hii ina-*cease* ku-*operate*. Kwa maana hiyo, kama kweli Wizara ya Fedha ingekuwa inatusikiliza ingeweza ikuza zile hisa 21% kwa wananchi na Mashirika kama ambavyo imepangwa kwenye Sheria kwa sababu suala la kuwapa wafanyakazi haliko kwenye Sheria. Lakini kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Fedha inaona ni vizuri na mimi nakubali kwamba wafanyakazi wakipata hisa katika Benki ile ni vizuri kwa sababu watakuwa *committed* kama *part owners* wa Benki hii. Sasa kwa maana hiyo na kwa sababu Sheria haiifungi Serikali kuwauzia 5% wafanyakazi, basi wafanye hivyo baada ya kuwa Sheria hii itakapositishwa kutummika. Yaani wakishauza zile asilimia 70 halafu wanaweza wakatenga 5% kutoka kwenye asilimia 30. Kwa hiyo, kusema kwamba Sheria haituruhusu kuuza chochote toka asilimia 30 sio sahihi.

Mheshimiwa Spika, hii hapa ni Sheria na wakitaka waipitie wataona inawapa huo mwanya wa kuwapa wafanyakazi 5% hata 10% au 20% wakitaka lakini wasijifiche nyuma ya pazia kwamba Sheria haituruhusu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, kwenye mabenki, tena hii Benki ya Twiga ni mali ya Serikali haina mtaji wa kutosha, sasa hivi ni Taasisi tu ya fedha, ni mali ya Serikali kwa asilimia 100. Ushauri wa Kamati ni kwamba Serikali iongeze mtaji lakini ushauri wa Kamati uko katika namna kama vile ziongezwe shilingi bilioni 1.2 ili Benki ile ifikie mtaji wa chini kabisa wa shilingi bilioni tano.

Lakini Benki haziendi kwa mtaji wa chini kabisa, kwanza hii ni benki au ni taasisi ya fedha ambayo inaendelea. Katika vitabu vyake tayari ina mikopo mizuri na mibaya. Mikopo mibaya ina tabia ya kuharibika halafu ikaathiri mtaji wa Benki, kwa hiyo tukiwekeea mtaji ule wa shilingi bilioni tano tu, maana yake ni kwamba Benki hii ikifanya hasara ya shilingi milioni 500, 600, 700 au 800 tayari ule mtaji umekwenda chini na benki haiwezi tena kuendelea. Kwa maana hiyo, ushauri ni kwamba tuiwekee mtaji mkubwa, siyo tu ule wa kusema iwe shilingi bilioni tano, basi, hapana! Tuwe na mtaji mkubwa, ikiwezekana hata mara tatu ya shilingi bilioni tano. Ikipata hasara hata kama ndogo isiende chini.

Mheshimiwa Spika, lakini pili benki yoyote uwezo wake wa kutoa mikopo una uhusiano wa moja kwa moja na mtaji wake. Sasa kama una mtaji mdogo wa shilingi bilioni tano tu utakuwa unakosa kutoa mikopo mikubwa kwa sababu wakija wale wateja wazuri, tena wakubwa, unawaambia mtaji wangu hauniruhusu kukukopessa kwa sababu nina shilingi bilioni tano tu.

Sasa kama kweli tumepania kuifanya Benki hii ya Serikali na kwa sura ya Serikali, hebu tuiwezeshe kuwa benki nzuri yenyе mtaji mkubwa na vile vile mtaji wake ndio utakaoweza kuifanya benki ifungue matawi mengi zaidi kwa sababu benki inapata faida kutokana na biashara na huwezi kufanya biashara yenyе matawi mawili au matatu, ukiipa mtaji mkubwa itakuwa na matawi mengi na kutokana na matawi mengi ndivyo utakavyoweza kufanya biashara kubwa. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kulisisitiza hilo.

Mheshimiwa Spika, katika suala la deni la Serikali, katika ukurasa wa 39 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wameeleza kwamba deni la Serikali limedhibitiwa vizuri na linakwenda vizuri na kwamba sasa jitihada zitafanyika ili deni hilo liwe linaendelea kuwa zuri, nakubali. Lakini kwa bahati mbaya kitabu hiki cha Waziri wa Fedha hakijatuambia lolote kuhusu mikakati ya Serikali kuhusiana na suala la dhamana za kitaifa zitakazouzwa kwenye soko la kimatifa kwa maana ya *Sovereign Bonds* ambazo tayari hata Mheshimiwa Rais amekwishatamka hapa katika ukumbi huu kwamba mipango inafanywa tutoe *Sovereign Bonds*, dhamana za kitaifa katika masoko ya mitaji ya kitaifa.

Mimi nilitarajia katika hotuba hii angalau Wizara ingetupa mwanga wa nini kinachofanyika kwa sasa hivi kwa maana ya mpangilio, yaani ratiba ile. Kuna masuala ya *rating*: Je, katika kuifanya nchi yetu tathmini ya kwamba inakopesheka kwa kiasia gani, utaratibu huu umefikia wapi? Kuna suala la kumchagua *Lead Bank* ambaye ndiye atakayeza dhamana hizi katika masoko ya kimataifa, utaratibu huu umefikia wapi? Tuta-raise kiasi gani huko kwenye soko la mitaji la kimataifa? Tunahitaji kukopa kiasi

gani na kwa sababu gani? Sasa mambo haya ni vizuri yakajulikana wakati huu kwa sababu huu ndiyo mpango unaotupeleka katika kutengeneza bajeti ya mwaka utakaokuja.

Kama kitabu hiki hakizungumzii hayo na hili ni jambo muhimu ambalo wengine ndiyo tunajua ni mkombozi wa uchumi wetu kwa maana ya kuwekeza katika eneo la miundombinu katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokuja, ndiyo kusema unaweza kufika mwaka unaokuja unasema mambo yalichelewa kuanza na kadhalika. Basi tujiwekee ratiba ili tujue tunakokwenda na tujue ni miradi ipi hiyo ambayo Serikali inatarajia kuiweka katika utaratibu mzima wa kukopa kutoka katika soko la mitaji la kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ombi na vilevile msukumo kutoka kwa Wabunge kwamba Serikali ianzishe Benki ya Wakulima. Benki ya Wakulima ni muhimu, sasa hivi tunayo *agency* ya Serikali ambayo inaitwa Mfuko wa Pembejeo za Kilimo. Hivi kuna tatizo gani la kubadilisha huu mfuko wa Pembejeo wa Kilimo ukawekwa katika mfumo wa Benki? Ukaongezewa fedha katika utaratibu ule ule amba hata Mheshimiwa Rais amesema zinakwenda *TIB* kwa ajili ya kuongeza katika dirisha la kilimo. Tunayo tayari *agency* inayoshughulika na pembejeo za kilimo, kwa nini tusiibadilishe hii ikawa ndiyo mwanzo wa Benki ya Kilimo? Tayari ina mtandao na watumishi, ni kuibadilisha tu kwa kutumia Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ili iwe Benki kamili. Kwa hiyo, ushauri wangu ni huo.

Mheshimiwa Spika, kuna katazo la Benki Kuu kwamba wanaotaka kununua hisa za *NMB* wasikope, katazo hili mimi nalionna kama batili kisheria kwa sababu katika Sheria za Makampuni kinachokatazwa ni kampuni husika kuwakopesha wanaotaka kununua hisa ndani ya kampuni hiyo hiyo.

Kwa mfano sasa hivi ningelielewa katazo hili kama ingewakataza wafanyakazi wa *NMB* wasikope *NMB* kununua hisa za *NMB*, lakini kama mtu amekopa mahali pengine utamkatazaje kutumia mkopo kununulia hisa *NMB*? Kwa sababu kinachotakiwa *NMB* ni mtaji, ni kuongeza mtaji na siyo kuongeza deni. Kwa hiyo, watu wakikopa mahali pengine wakaja kununua hisa wao wanawekeza kwa sura ya mtaji.

Kwa maana hiyo, suala la kuwakataza watu wasikope na mabenki mengine yasikopeshe kwa ajili ya kununua hisa *NMB*! Mimi nalionna kisheria ni batili na halafu kwanza tunajisumbua bure. Mtawezaje kusimamia kwamba mteja anayekuja kununua hisa *NMB* hakukopa? Nashauri tusijaribu kuweka mambo ambayo hata kuyasimamia hatuyawezhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali hebu ifanye mambo muhimu ambayo ndiyo yanayoweza kusimamiwa kwa sawa sawa kuliko kujiingiza katika shughuli ambazo hata usimamizi wake ni matatizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naendelea na suala la Tume ya Mipango. Tume ya Mipango ni chombo muhimu sana katika kuamsha uchumi wetu kwa maana ile ile ya kwamba sisi hatuwezi kuwa tunapanga pesa bila kujua miradi ipi na

priorities zetu kwa maana ya vipaumbele vyetu vikoje. Tume hii ndiyo itakayotusaaidia. Lakini kwa jinsi ilivyo sasa hivi, imewekwa kama ni chombo kidogo tu cha ushauri.

Hebu tuiangalie tena tuishauri Serikali kupitia Baraza la Mawaziri, imshauri Mheshimiwa Rais kwamba tutengeneze Tume ya Mipango yenyenye uzito wa kuitwa Tume ya Mipango kama jina lenyewe linavyostahili na kwa maana hiyo, itahitaji vilevile awepo Waziri wa Nchi atakayemsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia shughuli za Tume ya Mipango kwa sababu sasa hivi kama ilivyo Tume ya Mipango imewekwa katika Ofisi za Mawaziri wa Nchi waliyopo amba o wao sasa hivi mikono yao imeja kwa sababu ya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hawa Ghasia anashughulikia mambo ya watumishi wa nchi nzima hii, halafu umpelekee Tume ya Mipango, kusema kweli ni kumwongezea mzigo mkubwa. Mheshimiwa Sophia M. Simba anashughulikia mambo ya Utawala Bora na yenyewe ina mambo yake mengi tu. Kwa hiyo, hili kwa uzito wake Baraza la Mawaziri limshauri Mheshimiwa Rais kwamba kuna haja ya kuwa na Waziri wa Nchi Mipango atakayemsaidia Mwenyekiti wa Tume ya Mipango Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, hilo ndiyo nilikuwa nataka niliweke hivyo pamoja na kukubaliana na wenzangu amba o wamelizungumzia katika sura ya kusema kwamba ni vizuri kuwa na Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nakwenda haraka haraka nikidhani muda ungenitupa mkono. Sasa nirudi tu kwenye udhibiti wa fedha haramu. Udhibiti wa fedha haramu pamoja na Sheria iliyopita kama vyombo vinavyohusika kama Benki Kuu na kile kitengo cha Hazina vikiwezeshwa vizuri kwa maana ya raslimali watu na raslimali vifaa vitafanya kazi nzuri na kwa kweli vyombo hivi viwili kama vingelikuwa vinafanya kazi yake sawa sawa hata lile tatizo la *EPA* ambalo mimi naliita kama kengele ya hatari katika eneo hili la fedha haramu, lingeweza kudhibitiwa na lisingekuwa kubwa kiasi hicho. Lakini kwa sababu kulikuwa na upungufu katika utendaji wa usimamizi, ndiyo maana hili jambo likatupitia kama lilivyotupitia. Kwa hiyo, ili lisije likatokea hivyo tena naishauri Wizara kupitia chombo chake kikubwa Benki Kuu wajitazame vizuri na kusimamia vizuri hili eneo la fedha haramu kama vile Sheria ya Fedha Haramu inavyoitaka Serikali ifanye.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsante sana. (*Makofifi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga. Nafarijika kuona baadhi ya wachangiaji niliodhani hawapo, kumbe walikuwa katika utaratibu wa kujianaa tu. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Fred Mpandazoe Tungu, atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo na baada ya hapo ajiandae Mheshimiwa John Paul Lwanji.

Mheshimiwa Fred Mpandazoe Tungu karibu!

MHE. FRED MPENDAZOE TUNGU: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa dhati kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa na kwa dhati napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba aliyoitoa Bungeni hivi karibuni na kwa dhati pia naomba nikupongeze wewe kwa ushauri ulioutoa kwa Mheshimiwa Rais kwa niaba ya Wabunge wote wakati ukitoa shukrani. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwaka 1962 katika kitabu chake cha “Tujisahihishe” alisema kwamba sababu moja inayotuzuia sisi Waafrika kuendelea ni kutoa majibu rahisi kwa matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, ukiivuta kamba itakufuata kokote kule, ukiisukuma haitakwenda kokote.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Nchi yetu ina raslimali nyingi sana na ziko katika maeneo mbalimbali. Kuna maeneo ambayo yana raslimali nyingi, almasi, dhahabu nyingi, mifugo mingi, samaki nyingi kwa sababu yana maziwa au bahari yamepakana nayo.

Mheshimiwa Spika, kila eneo linachangia katika pato la Taifa kutokana utajiri uliyonayo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 katika kuchangia pato la Taifa Mkao wa Dar es Salaam ulikuwa wa kwanza na Mkao wa Shinyanga ulikuwa wa pili. Ni dhahiri kwamba Mkao wa Shinyanga ulikuwa wa pili kutokana na utajiri uliyonayo kwani kuna almasi nyingi pale Mwadui, kuna dhahabu na kuna mifugo mingi katika mkao huo. Lakini katika *report* hiyo ya mwaka 2004/2005 Mkao wa Shinyanga pamoja na utajiri wake ulikuwa wa pili kwa umasikini.

Mheshimiwa Spika, Mkao wa Shinyanga kuwa wa pili kwa umaskini maana yake ni kwamba huduma za jamii, hospitali, maji na afya hazilingani na mahitaji yaliyopo. Hali hii unaweza kuilinganisha na hisani ya mshumaa. Mshumaa unapowaka unaawaangazia waliouzunguka, wanafurahi kwa Mwanga wake, lakini wenywewe unaendelea kuteketea na baadaye utazimika.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mkao wa Shinyanga unaweza ukawafananisha na mshumaa unaowaka, kwa utajiri walionao wanachangia sana pato la Taifa, wa pili katika Mikoa yote 22 Tanzania Bara, lakini hawanufaiki na utajiri huo kutokana na mipango ya maendeleo inayopangwa katika mkao huu kwa sababu Mkao wa Shinyanga ni wa pili tena kwa umaskini hauna huduma nzuri lakini vilevile uko nyuma kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninaamini sana kama Mkao wa Shinyanga utawezeshwa utachangia zaidi kuliko ilivyo sasa, kama umekuwa wa pili katika kuchangia pato la Taifa

na umaskini ulionao nina hakika kama utawezeshwa kwa huduma za barabara, afya na maji unaweza ukachangia vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iweke utaratibu wenyewe uwiano mzuri unaozingatia jinsi maeneo yanavyochangia katika pato la Taifa na vilevile iangalie sehemu nyingine au maeneo mengine yako nyuma kimaendeleo kwa hiyo mipango kama alivyosema Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga Tume ya Mipango ijidhatiti zaidi kuweka mipango ikiangalia uwiano huo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo naomba nichangie ni kuhusu changamoto iliyopo katika mfumo shirikishi wa kushirikisha jamii katika mipango ya maendeleo, mpango huu kwa kiingereza unaitwa *Participatory Planning Approach*. Utaratibu huu ni mzuri sana, unawataka wananchi wenyewe watambue matatizo yao na wayaibue, wakubaliane miradi ya kutekeleza na waisimamie miradi hiyo na Serikali kwa sasa inautumia mradi huo, lakini utaratibu huu hasa ni moja ya masharti wa misaada mnayopata kutoka nchi wahisani na ni masharti kwa *NGOs* nyingi zinazoweka miradi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini katika *report* ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwaka 2006/2007 inaeleza kwamba fedha takribani shilingi bilioni saba katika Halmashauri zetu hazikutumika kwa sababu wananchi walishindwa kuibua miradi na *report* hiyo ya Mkaguzi imeeleza kwamba kiasi cha fedha karibu shilingi bilioni 60 katika Halmashauri hazikutumika au miradi hiyo 60 kwa sababu wananchi hawakuweza kuchangia miradi hiyo kwa sababu wananchi katika utaratibu wa *Participatory Planning Approach* wanatakiwa kuchangia 20.

Mheshimiwa Spika, changamoto ninayoiona mimi kuna Watanzania karibu milioni 20 ambao wanaishi kwa matumizi ya chini ya dola moja kwa siku, yaani ni masikini na kuna na kati ya hao Watanzania karibu milioni 10 hawajui familia zao zitakula nini kesho. Kwa utaratibu wa kukutana na kuibua miradi, kukaa na kutekeleza ndiyo sababu shilingi bilioni saba kwenye Halmashauri hazikutumika kwa sababu walishindwa watapata wapi muda wa kufanya hivyo?

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 60 hazikutumika kwa sababu wananchi walishindwa kuchangia sio kwamba hawataki, lakini watu karibu milioni 10 hawajui familia zao zitaishije kesho. Kwa utaratibu huu wa *Participatory Planning Approach* watawezaje kutekeleza miradi hiyo? Ninasikia kwa mfano miradi ya *ASDP* kuna shilingi trillion 2.7 ambazo wananchi wanatakiwa waibue miradi na itekelezwe na wasipoibua, fedha hizo zinakwenda kwingine. Ina maana mfumo huu utanufaisha sehemu zenye mwamko wa elimu na sehemu ambazo wananchi siyo masikini. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iangalie na ikiwezekana iingilie kati, kuna miradi ambayo imepitishwa na kuidhinishwa na Halmashauri iitekeleze, tukisubiri wananchi waibue, kuna maeneo yataendelea kuachwa nyuma kimaendeleo na maeneo mengine yataendelea sana kuwa na maendeleo jambo ambalo ni hatari na linaweza kuleta upungufu wa amani.

Mheshimiwa Spika, Budha alisema hivi: “Usiamini jambo lolote kwa vile tu mtu mwenye hekima amelisema; usiamini jambo lolote kwa sababu watu wengi wanalikubali jambo hilo; usiamini jambo lolote kwa vile tu vitabu nya kale vimeliandika; usiamini jambo lolote lile.” Tena alinishtua sana Budha aliposema hilo la mwisho akasema: “Usiamini jambo lolote lile kwa vile tu vitabu vitakatifu vimelisema.” Budha anasema: “Amini jambo lile ambalo wewe mwenyewe umelipima na umeliona ni kweli.”

Mheshimiwa Spika, kulingana na Budha alivyosema, napenda kusema na kuishauri Serikali kwamba Serikali isiamini jambo lolote lile kwa vile tu nchi maarufu duniani na zilizoendelea zimelisema. Serikali isiamini ushauri wowote kwa vile tu nchi wahisani zimeshauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali isiamini jambo lolote tu au Sera yoyote kwa vile tu Sera hiyo au ushauri huo umetayarishwa na mashirika ya kimataifa na *NGOs* za kimatifa, Serikali iamini na kutekeleza ushauri au Sera ambayo imeipima na kuiona kwamba inalingana na mazingira ya nchi yetu na ni kwa manufaa ya Watanzania. (*Makofi*)

Huu mfumo wa *Participatory Planning Approach* umesititizwa sana na baadhi ya wafadhili na *NGOs* za kimataifa na mashirika ya kimataifa. Naomba Serikali iangalie changamoto hiyo kwa makini na kwa gharama zote ili iweze kuingilia kati na kuona tutumie mfumo gani.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema jambo moja. Nitoe mfano mmoja, kulikuwa na mtu mmoja alikuwa amepewa achague hukumu tatu, alikuwa mhalifu lakini. Hukumu ya kwanza amuue mkewe, hukumu ya pili amnyweshe sumu mwanaye na hukumu ya tatu anywe pombe. Mtu huyo alichagua kunywa pombe na baada ya kunywa pombe akamuua mkewe na akamnywesha sumu mwanaye.

Mheshimiwa Spika, nchi za Afrika zimepata ushauri mwingi kutoka nchi zilizoendelea na wafadhili, ushauri ambao ulionekana ni mzuri na nafuu ili tuondokane na umaskini na utegemezi lakini baadaye tumeendelea kuwa na utegemezi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka tuwe makini zaidi na ikibidi tuchukue maamuzi magumu kwa sasa ili baadaye tupate manufaa. Kuna msemo wa Kingereza unaosema: “*Where there is no pain there is no gain.*” *No pain, no gain.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nchi yetu ina changamoto nyingi sana, tunapata ushauri mwingi sana, tuupime kwa dhati ushauri huo, sio tu kama unelezwa na nchi maarufu sana duniani na/au tunapewa na nchi wafadhili hapa wanaotufadhili kwa muda mrefu tuupime na tuone kwamba unalingana na mazingira ya nchi yetu na ni wa maslahi kwa Taifa letu. Yule mtu aliambiwa kuchagua hukumu tatu, aliona ile ya mwisho ni rahisi sana akanywa pombe, baada ya kunywa pombe aliyoyahofu akayatenda, akamuua mkewe na kumnywesha sumu mwanaye. Kwa hiyo, naomba sana Serikali izingatie hayo mambo mbalimbali ambayo tunashauri.

Mheshimiwa Spika, naona muda umekwisha, naomba kuunga mkono hoja.
(*Makofî*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mpendazoe na hasa kwa nukuu zako ambazo ni za falsafa ya hali ya juu kabisa. Tunakushukuru kwa hayo na naunga mkono hoja kwamba Serikali yetu isije ikanywa pombe.

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hoja hii muhimu ya Wizara ya Fedha ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu masikini.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia, naomba kwanza nitoe pongezi zangu za dhati kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ambaye pia ni Msemaji Mkuu wa Wizara hii, lakini pia nitoe pongezi kwa Waziri na Manaibu Waziri na watendaji wote ambao kwa kweli kwa kiasi kikubwa wamesimamia sana matumizi ya fedha na hivyo uchumi wetu kuanza kupanda kwa kasi ambayo imeonekana.

Mheshimiwa Spika, naanza kumpongeza Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa sababu mwaka jana tuliongea sana masuala ya fedha zilizopotea hasa za *EPA* na *BOT* lakini wengi walitubeza, tukazomewa, lakini tunashukuru Mungu kwamba, baadaye ukweli umeonekana na ukweli huu umewekwa hadharani na mpPENDWA wetu Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete – Mwenyekiti wa CCM alivyokuja Bungeni juzi na kueleza wazi kwamba fedha zile za *EPA* ni kweli zilipotea na naamini ni wizi na hao wezi lazima wakamatwe pamoja na kwamba Rais amewaongezea muda, samahani kwa kuongea hili, pamoja na kwamba nakiuka kanuni ya 53, lakini kwa jinsi ambavyo niliguswa na hotuba ile nimeona nami niseme.

Mheshimiwa Spika, la msingi zaidi nikupongeze wewe binafsi kwa jinsi ambavyo ulikuwa wazi katika maneno yako ya *vote of thanks* ambayo kwa kweli ingekuwa vigumu sana kwa mtu mwengine kuweza kusema yale mbele ya Mheshimiwa Rais, lakini nakupongeza na hiyo imeonyesha kabisa ni jinsi gani ambavyo una *standards* na *speed*. Pongezi sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye suala zima la Soko la Hisa. Ni kweli kabisa kwamba hili Soko la Hisa litasaidia sana wananchi katika kukuza vipato vyao na hasa tunapozungumzia suala zima la hisa za *NMB*. Ni kweli wametangaza kwamba watauza hisa hizo, lakini nadhani siku ambazo zimetolewa na Wizara ni ndogo sana kwamba *deadline* ni tarehe 8 Septemba, 2008. Nadhani kuna umuhimu wa Wizara kuona kwamba angalau waongeze muda kidogo ili wananchi wengi kidogo waweeze kununua hisa hizo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na suala zima la hisa, kuna uelewa mdogo sana kuhusu suala hilo kwa sababu hakuna elimu ambayo imekuwa ikitolewa. Labda niwapongeze sana *CRDB* na *NICO*, wao wameweza sana kutoa semina kwa wateja wao, lakini bado hawa wengine hawajaanza. Nashauri kwamba kwa sababu suala zima la hisa ni jipya sana kwa wananchi wa Tanzania, kwa hiyo, nashauri kwamba, kuna umuhimu

mkubwa sana wa Serikali au benki husika au wale wanaotoa hisa hizo kuweza kutoa elimu ili wananchi waweze kuelewa.

Mheshimiwa Spika, hata mimi binafsi na nina hakika na Wabunge wengine tumekuwa hatujui vizuri suala hili, ukishanunua hisa unashibiri gawiyo, lakini kumbe kuna utaratibu kwamba ile hisa unaweza kuiuza sehemu nyingine pale ambapo soko lake limepanda. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara au mashirika yanayohusika yaweze kutoa semina kwa wananchi ili waweze kuelewa maana halisi ya hisa ili waweze kuzitumia kwa ajili ya kuongeza vipato vyao.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la *KNCU 1984 Limited*. Wengi wanaotoka Kilimanjaro na zile sehemu zinazolima kahawa walismeshwa kwa kahawa kwa wakati huo na ndiyo maana wengi walifika hapo walipo. Suala langu ni kuhusu benki inayoitwa *Kilimanjaro Cooperative Bank Limited* mwaka 1992/1993, *KNCU 1984 Limited* walichukua zaidi ya shilingi milioni 776 za wakulima na mpaka leo hii wakulima wale hawajarudishiwa zile fedha.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kujua ni jinsi gani wakulima wale wanawenza kurudishiwa fedha zile kwa sababu kwa kweli sasa hivi ukiangalia zao la kahawa limerudi chini sana na kuanzia miaka ile ya 1992 wakulima wengi baada ya kukosa fedha zile waliamua kuondokana na kahawa, wengine wakakata kahawa zao na kuanza kuotesha machungwa na matunda mengine. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujumuisha, atuambie ni kwa nini *KNCU 1984* walichukua fedha zile na mpaka leo hawajazirejesha? Lakini kibaya zaidi, hawakuzitumia kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wa kahawa kule Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu *TRA*. Kwa kweli napenda kuipongeza sana *TRA* kwa jinsi ambavyo wameweza kuendelea kukusanya kwa kiasi kikubwa sana kodi za wananchi na hasa wafanyabiashara. Lakini pamoa na pongozi hizi bado niwaombe waendelee kuvuta soksi kwa sababu kuna maeneo mengi kodi hazikusanywi, lakini vilevile niishauri Serikali, sio tu kwamba *TRA* wanapokusanya fedha nyingi, basi na matumizi yaye makubwa waendelee kutanua, naomba waendelee kudhibiti matumizi ya fedha ili wakulima na wananchi wa kawaida waweze kufaidika na zile kodi ambazo wanazitoa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo hata leo asubuhi ulizungumzia ni suala la Walimu. Kumekuwa na matatizo makubwa sana ya posho za Walimu, lakini wote tunajua kwamba Walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu na wote tuliomo humu ndani na viongozi wakuu hawakufika hapo walipo bila kazi za Walimu. Inasikitisha kuona kwamba ni kundi hili peke yake ndilo ambalo halitendewi haki kwa maana ya kwamba wanawekewa malimbikizo mengi sana na sasa hivi nasikia imefika bilioni zaidi ya 16, ni kwa nini kundi hili la Walimu ambao hawana kitu kingine chochote cha kuweza kujikimu zaidi ya mishahara yao na hizo posho wanashindwa kulipwa? Lakini ndiyo tunaowatumia sana wakati wa kampeni na ndiyo wanaotusaidia sana katika kusimamia uchaguzi lakini ndiyo hawa hawa tumeamua kuwaacha wanalia.

Mheshimiwa Spika, naomba pamoja na kwamba sishabikii migomo, lakini inapofikia haki ya mtu imepuuza kwa siku zote hizo, kweli kuna haja ya kuongea mezani, lakini inapofika kwamba Serikali haioni sababu muhimu za kilio chao, kuna haja ya kugoma. Kwa hiyo, naomba Serikali ione kweli Walimu wanategemea zaidi mishahara yao tofauti na watu wengine. Kwa hiyo, muwaone na muweze kuwasaidia pale ambapo wanastahili haki zao za kimsingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuliongelea ni kuhusu suala la Kitengo cha *Internal Auditors* katika Halmashauri. Kwa kweli kitengo hiki ni muhimu sana na tumeona jinsi gani fedha zinavyopotea. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iimarishe kitengo hiki ili fedha hizo zisiweze kupotea kwa sababu limekuwa ni jambo la kawaida. *Internal Auditor* anakwenda kwa Mkurugenzi kuomba gari, kwa hiyo, unaona hapa suala zima la *professionalism* linaweza kukiukwa. Kwa hiyo, tunaomba kitengo hiki kiwe huru ili waweze kufanya kazi vizuri na hivyo tusiwe na matatizo na nakisi katika mahesabu yetu kule kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kuliongelea ni suala la *Procurement*. Ni kweli kwamba fedha nyangi za bajeti zinakwenda katika manunuzi, lakini manunuzi hayo yamekuwa yakinotafutiana sehemu na sehemu na wengi wameshalizungumzia hilo na tuna ile Sheria ya Manunuzi. Ni wazi kwamba unaweza kukuta kuna maafisa ambao hawafai kununua lakini wanunua. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara ione ni jinsi gani kitengo hiki cha manunuzi kinaboreshwu, lakini vilevile kuwe na sheria kali ili wale maafisa ambao hawaruhusiwi kununua wasinunue.

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala zima, kwa mfano la ununuzi wa vifaa mbalimbali kama vile magari au vinginevyo. Unakuta Wizara, tunazo Wizara nyangi Serikalini lakini unakuta moja labda inahitaji magari kumi na nyngine kumi aina ile ile, lakini utakuta wanatumia wakala tofauti, kwa hiyo, hata lile punguzo linakuwa dogo. Kwa hiyo, nadhani ni vyema kama Serikali inataka kununua magari ya aina moja, basi itumie mnunuzi mmoja ili kuleta faida katika nchi kwa maana ya kwamba lile punguzo linaweza kuwa kubwa sana kama yatanunuliwa kwa mtu mmoja.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la Benki Kuu. Ni kweli kwamba Benki Kuu ni chombo nyeti sana na ndiyo nguzo kuu ya uchumi wetu na ndicho chombo kinachotumika katika kudhibiti, kuratibu na kuhakikisha kwamba mfumuko wa bei au thamani ya fedha zetu haishuki. Lakini nikienda kwenye kitabu chetu cha Kambi ya Upinzani ukurasa wa tano, naomba kunukuu, inaelezwa kwamba: “Taarifa ya ukaguzi wa hesabu ya Benki Kuu uliofanywa mwaka 2006/2007 umebainisha matumizi ya shilingi milioni 551 kwa ajili ya kununua picha zenyenye sura ya Marehemu Daudi Balali ambapo picha hizi waliofanya uchunguzi wamegundua kuwa zingeweza kuwa na thamani ya shilingi milioni 4.76”. *That means* ni mara mia moja.

Mheshimiwa Spika, suala langu la msingi hapa ni kwamba, inawezekanaje chombo kama Benki Kuu ambacho tunakiamini ndicho kinachodhibiti uchumi wetu na ndicho kinachoratibu fedha zetu kiweze kufanya matumizi makubwa ya fedha kiasi hicho, iweje picha kama ilikuwa ni shilingi milioni tano ziwe milioni 551? Kwa kweli

nahitaji majibu. Wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha atuambie, hivi picha hizi zilikuwa zinatengenezwa kwa almasi au kwa *tanzanite* ambayo ni madini ghali au ni kwa madini gani? Kwa sababu haiwezekani picha iliyokuwa iwe shilingi milioni tano, iwe shilingi milioni 551. Kwa hiyo, naomba tuone ni jinsi gani tunaweza kudhibiti matumizi ya fedha zetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu ripoti ya CAG. CAG amesema kabisa kwamba matumizi mabaya ya fedha ameyagundua katika sehemu tatu na moja ni kutofuata Sheria ya Manunuzi. Pili, ni usimamizi dhaifu wa fedha za umma na tatu, kutotekeleza mapendekezo ya ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, ambalo nataka kulizungumzia zaidi ni hilo la manunuvi ambalo nimeshalizungumzia. Kwa hiyo, nilikuwa naomba na nadhani hii inatokana na kwamba bado Serikali haijampa mamlaka kamili, hajawa huru huyu CAG. Kwa hiyo, naona kuna haja ya kuja na Muswada mpya ili tuone ni jinsi gani Mkaguzi Mkuu anaweza kupata meno ya kutosha ili aweze kudhibiti haya mambo ambayo amekuwa anayasema lakini hayatekelezwi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la riba. Ni kweli kwamba riba katika benki zetu imekuwa kubwa sana na inatofautiana na kwamba kutofautiana kwake kunatokana na soko huria. Lakini nashukuru kwamba jana katika TV nilimwona Gavana wa Benki Kuu akisema kwamba sasa hivi wanafuatalia kuona ni jinsi gani taasisi zake za fedha zinatoa riba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani hii ni hatua nzuri na pia kwa utaratibu huo huo kwa sababu ilikuwa ni semina, nadhani pia Gavana ataitoa kwa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu sisi ndio tunaowawakilisha wananchi na tunapokwenda huko Majimboni watatuhoji. Kwa hiyo, itakuwa vyema kama tutakuwa tumeshaelewa ni jinsi gani riba zinatolewa ili wapiga kura wetu waweze kutuelewa na waweze kuelewa ni jinsi gani vilevile wanaweza kuchukua mikopo. Kwa hiyo, naona semina hii ikija kwa Waheshimiwa Wabunge itakuwa ni vizuri.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu hizi ATM. Ni kweli ATM inarahisisha sana kuchukua fedha hasa siku za *weekend* na hata siku za kawaida, lakini imekuwa ni jambo la kawaida kuwa hazifanyi kazi, tena siku za *weekend* unaweza kuwa ndiyo umeshaamua kwenda kuchukua fedha, lakini unakuta hakuna, umeshaamua na familia yako unakwenda mahali unakwenda kuchukua fedha, unakwenda benki moja unakuta hakuna, unakwenda nyingine na nyingine. Sasa naomba kujua hivi, kama kwenye Tawi moja *ATM services* hazipo wanakwambia huduma zimeshitishwa kwa muda, hivi hiyo inakuwa *automatically*? Kwa mfano kama ni NBC imegoma, basi ni zote za Mkoa wa Dar es Salaam hazitoi huduma au ni vipi?

Mheshimiwa Spika, ni vyema kujua ili mtu kama akikosa sehemu moja arudi nyumbani kwa sababu watu wanakuwa hawaelewii. Kwa hiyo, wakitoka kwenye benki moja wanahangaika kwenda nyingine na nyingine. Tunaomba kujua kama *system* ikiwa *collapsed* inakuwa ni kwa benki zote za aina hiyo au ni kwenye matawi machache ili

wananchi wasiwe wanahangaika kuzurura kutoka sehemu moja kwenda nyingine badala yake watafute mbadala mwingine wa kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naomba nirudie kidogo yale ambayo nimeyasema kwa kusema kwamba, naomba sana suala zima la *KNCU 1984 Limited* kule Moshi, tujue kwa nini hizo fedha zilichukuliwa na ziko wapi ili wakulima waweze kufaidika na fedha zile.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba kwamba pamoja na kwamba nimevunja ile kanuni, nikuulize kwa sababu wewe una uzoefu, najua Mheshimiwa Rais alisema kwamba zile fedha za *EPA* ziende kwa wakulima, nadhani ni wazo zuri, lakini najua kwamba jukumu la mgawanyo wa fedha, kwa jinsi gani zitatumika au matumizi ya fedha yanatolewa na Bunge lako Tukufu. Pia fedha kama hazina mwenyewe, basi huwa zinapelekwa kwa Wasii Kabidhi Mkuu wa Serikali. Naomba kujua kama hiyo ni sahihi na kama sivyo, basi inakuwaje? Je, Bunge lina jukumu gani kwa fedha hizi za *EPA*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Kwa kuwa umechomekea suala la kutaka nadhani Spika atoe mwongozo ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge hakuna chochote kilichokosewa kwa Mheshimiwa Rais kuagiza fedha za *EPA* ziende katika Mfuko tena wa kuwasaidia wakulima. Sababu yake ni hivi, tuelewane. Kazi ya Bunge ni kuidhinisha sio kupanga matumizi, tunapoletewa hapa tayari Hazina na Serikali imekwishapanga kwa kila Wizara, tunachofanya hapa ni kuidhinisha.

Sasa zinapotokea fedha nyingine ambazo hatujaidhinisha na wala hii mnaitaja *EPA* kwa sababu ni jambo ambalo limesemwa sana, lakini zipo fedha za wafadhili, kuna *Bill Gate Foundation* na kuna wengine wanazileta fedha hizo kwa wakati ambao bajeti imekwishapitishwa, Serikali haiwezi kuzikataa, kinachofanyika fedha hizo zinaelekezwa kwenye matumizi yanayotatua matatizo ya wananchi mara zinapopatikana halafu taarifa zinakuja kutolewa Bungeni ambayo inaweka sawa mahesabu ya fedha zilizoongezeka. Kwa hiyo, kwa fedha hizi pia ndiyo itakavyokuwa na ni utaratibu sahihi kabisa. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja ya Wizara hii. Kwa mara nyingine niipongeze hotuba ya Mheshimiwa Rais na pia hotuba ya Mheshimiwa Rais Ahmed Sambi aliyyotuhutubia jana. Kwa kweli imetusisimua na imeonyesha urafiki na udugu kati ya hizi nchi mbili.

Mheshimiwa Spika, nikirudi kwenye hoja hii, kuna mwanafalsafa mmoja Mgiriki alipata kusema kwamba, ukweli mara zote ni rahisi kuuelewa pindi unapogundulika, lakini tatizo ni jinsi ya kuugundua.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, siku hizi mnasoma sana falsafa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa endelea hayo nimambo mazuri tu.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, nimemnukuu huyu mwanafalsafa ili Serikali ituambie ukweli kuhusu watumishi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Imekuwa kero kubwa sana. Juzi nilikwenda Jimboni katika shughuli zangu binafsi, lakini Jumapili asubuhi hata sijafikiri kwenda Kanisani nilikuta msururu wa watu na malundo ya barua zao.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka Itigi kulikuwa na karakana moja kubwa ya *East African Road Services*, Makao Makuu yalikuwa Iringa, lakini *second* kwa nchi hii ilikuwa ni Itigi. Sasa baada ya kufa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki watu wengi walibaki pale. Kwa kawaida wafanyakazi wengi huwa wakikaa muda mrefu mahali huamua kufanya makazi yao mahali walipo. Kwa hiyo, hawa watu wamekuwa mzigo kwa Wabunge, nami nikiwa mmojawapo, wanansumbua sana.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi nimewapeleka Wizarani toka Mheshimiwa Mama Zakhia Meghji, lakini wanazungushwa wanarudi hakuna kitu, kuna watu ambao hawakulipwa kabisa, kuna watu ambao wamelipwa lakini wanadai kwamba kuna mafao mengine walihidiwa basi ili mradi ni adha kubwa. Sasa naomba ukweli ni upi hasa juu ya suala hili kwa sababu nadhani kuna ukweli kwa sababu *aliye-breach contract* ya ajira hapa ni nani?

Mheshimiwa Spika, yule gwiji wa mahesabu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Umbrecht aliainisha vizuri sana baada ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuvunjika Januari, 1978, huyu Umbrecht aliteuliwa kutathmini rasilimali na mafao ya watumishi wa *East African Community*, alipokabidhi ripoti yake siku hiyo hiyo alilipwa lakini wafanyakazi wa Tanzania wakaachwa, Kenya na Uganda wakalipwa. *You can imagine* hata Idd Amin pamoa na ukatili wake huo aliona ni afadhali awalipe wastaafu wale. Idd Amin alipenda damu lakini kwenye mali na nini hakupenda, angeweza kuzichukua hizo, lakini aliona umuhimu wa watu wake akawalipa. Lakini sisi hatukufanya hivyo, wakaambiwa waendelee mpaka watakapostaifu, lakini Jumuiya ya Afrika Mashariki ilikuwa na *Executive Board* yake.

Mheshimiwa Spika, hiyo *Executive Board* ilijumuisha Marais wa nchi hizo tatu lakini sasa sijui na za Mwalimu nazo ziliingizwa wapi maana haikuelezwa hizi fedha zilikwenda wapi za upande wa Tanzania maana tutakapojuwa hilo ndipo tutakapojuwa kweli kwa sababu Serikali ndiyo ilikiuka huo mkataba kwa sababu mafao yalikuwepo lakini wafanyakazi hawakulipwa. *This is a breach of contract!* Sasa tumeambiwa yanayowezekana leo mfanye leo, lakini hawakufanyiwa hivyo, ikawa *deferred indefinitely*.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu ilishauriwa na Uingereza kwamba, jamani kama mmeshindwa kulipa tuwasaidie, lakini inavyosemekana hawakukubali kwa maana kwamba hilo ni suala la ndani tunaweza kulimaliza. Lakini mpaka leo hawa watu wanasota. Majibu ya mkato tu tunapata, wengine walilipwa, waliwaingiza wenzao mitini. Kwa hiyo, wa mijini wengine wakaghushi za wenzao wakalipwa, lakini hiyo siyo *solution*, mtu ambaye hakulipwa alipwe, kama ni hasara basi

hiyo ni hasara ya Serikali. Kama watu wa mjini wameghushi wakachukua fedha za wenzao, hiyo iwe ni hasara ya Serikali sio hasara ya mtu.

Mheshimiwa Spika, kama tusivyojali *value for money*, nalionna kabisa kwamba tuna tatizo la kutothamini kazi. Kwa maana ya *value for work*, mtu ametumikia lakini siku anapomaliza basi huyu mtu anaonekana basi yeze siku zake zimekwisha, hastahili. *If you don't value for money or you don't value for work*, kuwazungusha wastaafu hawa ni sehemu ya rushwa na sio rahisi mtu atoke Itigi kwenda kumwona Waziri ofisi kwake. Waziri anaweza kupenda umwone, lakini kuna urasimu hapa katikati. Atamwonaje Waziri? Kwa sababu kuna msururu wa watu kabla ya kumwona Waziri, hiyo nauli, posho, malazi Dar es Salaam watamlipa?

Mheshimiwa Spika, *now, let us be realistic*, atamwona wapi Waziri? Mheshimiwa Waziri ana mikutano, anatakiwa *State House*, anatakiwa kwenda nje, sasa atakaposema njoo kesho au kesho kutwa atakaa anamlisha nani? Kwa sababu watu wote hawakai Dar es Salaam. Naomba suala hili tulipatie ufanuzi kama ni kuunda timu, nilimsikia Mheshimiwa Mbunge wa Maswa jana aliposhauri kwamba sio suala la kukaa ofisini, iundwe timu iwafikie hawa watu, wengi hawana uwezo, *they are finished*. Naomba sana suala hilo liangaliwe upya ili Wizara hii iweze kulifanyia kazi. *Let us have a human face on this*.

Mheshimiwa Spika, la pili, Mkoa wa Singida ni Mkoa ulioachwa katika mgawo wa fedha za *MCC*. Sasa kuna malengo matatu ya fedha hizi za *MCC*. Lengo la kwanza, “*To expand and strengthen the transport infrastructure so as to stimulate economic activities in rich agricultural areas, improve access to the basic services and enhance exploitation of tourism potential something*”.

Mheshimiwa Spika, lengo la pili linasema: “*To improve water infrastructure networks*. La tatu: “*To increase the capacity of supplying power to consumers in both rural and urban areas*”.

Mheshimiwa Spika, lakini Mkoa wa Singida katika takwimu za Serikali umewekwa kuwa ni Mkoa wa mwisho kwa maana ya pato la mtu kwa mwaka. *Actually* kwa maana ya umaskini, wanasesma pato la mtu wa Singida kwa mwaka ni shilingi laki tatu.

Mara nyingi viongozi wanapotutembelea kule basi hutupa dozi hiyo kwamba nyie ndiyo maskini kuliko mkoa mwingine wowote. Lakini cha ajabu katika kupanga matumizi ya hizi fedha za *MCC* sisi tunaambulia vyandarua ili tuzidi kulala zaidi. Kweli mgao umeanza Ruvuma, siuonei vivu Mkoa wowote ule lakini imeanza Ruvuma ikaja Mbeya, Iringa, Dodoma, ilipofika Dodoma ikarukwa Singida ikaenda Shinyanga. Hivi tunatenda haki kweli? Mkoa maskini wa mwisho au mnataka watu wa Singida tumwandikie Rais George Bush aliyetoea hizi fedha kwamba bwana hawakupanga vizuri. Tunaweza kumwandikia au tukamwomba bwana njoo utusaidie kugawana hizi fedha!

SPIKA: Subirini aje Obama.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, ndiyo tunasubiri aje Obama. Naomba Serikali *i-review* kwa sababu hizi fedha zinakuja kwa awamu, basi iwe-reviewed na Mkoa masikini zaidi kuliko Mkoa mwingine uweze kupata, maana tumefikia hatua ya kutukanwa, wanasema ninyi ndiyo wa mwisho, ninyi ni wavivu wa kufikiri. Sasa hali kama hii hatuwezi kuendelea nayo.

Mheshimiwa Spika, namuunga mkono kabisa ndugu yangu mmoja sijui alikuwa Mheshimiwa Zambi au nani, kuhusu mikopo hii kwa watumishi. Mikopo hii ni kweli tulidhani kwamba ingewasaidia wafanyakazi lakini cha ajabu unajua neema huja na matatizo yake. Mvua inaweza kunyesha lakini inaweza kuleta mafuriko. Sasa hizi fedha zimekuja zipo waziwazi, watumishi kwa kutumia dhamana ya kazi zao wanawenza kukopa, lakini tatizo ni kwamba wameingizwa mjini na hizi *financial institutions* kiasi kwamba riba ni kubwa sana, wanakuta hakuna kitu, wamekatwa mishahara yote, wanarudi nyumbani mikono mitupu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kama Mwalimu, atakwendaje darasani, *definitely* ataanza kwenda kukopa, anarudi anaambowi alipe mkopo hana pesa. Matokeo yake nini? Matokeo yake ni kwamba, taaluma inaanguka kwa sababu muda mwingi atatumia kutafuta riziki na muda mwingi wa kuwakimbia hao watu wanaomdai matokeo yake watoto wetu wanafunzi hawafundishwi.

Mheshimiwa Spika, nina mfano mmoja, nisiseme Mwalimu au mtumishi gani, lakini niseme tu mtumishi, kuna sehemu iliandaliwa semina ya wiki mbili hivi ya wajasiriamali, sasa walikuwepo wanaandaa vitafunwa. Vitafunwa vile huandaliwa jioni na kufungiwa kwenye *store* ya hilo jengo la Serikali. Siku ya kwanza asubuhi walipokwenda kufungua ili wavipashe moto wanakuta hakuna. Wakashangaa. Kuuliza *authorities* pale wakasema mbona tuna mlinzi? Basi wakavipika tena maana waliangalia wakakuta hata hakuna dalili ya panya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi jioni wakatengeneza tena wakaweka, saa 4.00 usiku yule mbaya wao akakamatwa, ni mtumishi wa Serikali. Wanamwuliza kulikoni? Akasema jamani, nina siku ya pili sijala, nimekwenda benki sina mshahara, nimekatwa zote na hivi sasa nifanye nini? Wakaenda nyumbani kwake kweli hata punje ya mtama au mahindi hakuna, mama na mtoto wameshaambaa hawapo, ikabidi wamkaribishe hapo ili naye awe mshiriki wa semina hiyo kwa wiki mbili ajikimu. Unaona mambo haya? Lakini sasa maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba hawana kitu!

Mheshimiwa Spika, hii ni sawa na *shylock business*, anataka *a pound of flesh*, yaani anataka pesa zake pamoja na ratili ya nyama yake sasa itawezekana wapi? Tunaomba Serikali *i-review* hawa ni watumishi wao, wasije waka-affect watu wetu, wanafunzi wetu au shughuli za Serikali. Waone kama wanawenza kubeba huo mzigo au wa-investigate hayo Makampuni yasiweze kuwanyonya.

Naomba Benki ya Posta ifikiriwe kuongezewa mtaji angalau shilingi bilioni kumi waweze kufanya kazi. Wanafanya kazi vizuri sana na hawa wanaweza kuwa *solution* kwa maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na nakushukuru kwa kunisikiliza na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa John Lwanji kila mara navutiwa sana na namna unavyochangia. Unachangia kwa dhati na unayajua sana matatizo ya wapiga kura. Mheshimiwa Kilontsi Mporegomyi sasa naona Mheshimiwa Rished Abdallah hayupo, kwa hiyo badala yake msemaji wa mwisho leo atakuwa Mheshimiwa Richard Ndassa kwa mchana huu.

MHE. KILONSTI M. MPOROGOMYI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kunipa nafasi hii. Naomba nianze moja kwa moja niende kwenye hoja ili kusudi nipate majibu kwa mashaka yangu. Naomba na mimi niunge mkono hoja hii. (*Makofi*)

Naunga mkono hoja hii nikiamini ya kwamba yale nitakayozungumza yatapatiwa majibu. Wastaifu wa Afrika Mashariki wamezungumziwa sana katika nyumba hii, ninachokihitaji ni maelezo yanayohusu matatizo gani yaliyowasibu hawa. Hakuna mtu anayefurahia kuhangaika kama hawa Wastaifu wa Afrika Mashariki walivyokuwa wanahangaika, mpaka madai yao ukiwaona wenyewe walivyo hali hii inatia kichefuchefu kabisa. Tunaomba tupatiwe majibu sahihi kwa nini wenzao walilipwa miaka 20 iliyopita, Watanzania mpaka leo hawajalipwa. (*Makofi*)

Lakini la pili ni *pensioners* wa Watanzania. Sisi wote tulioko humu na hawa watumishi wa Serikali waliopo siku moja watakuwa *pensioners* wote. *Pensioners* wanatoka huko mikoani fedha walivokuja nayo Dar es Salaam inakwisha majibu hakuna, mimi wengine nimekaa nao mpaka unawahurumia. Nenda pale Hazina kile Kitengo cha *Pension* ni vurugu hujui mtu anaanza kuhudumiwa wapi? Watu wanapata kiasi kidogo ambacho hawawezi kujikimu badala yake watu waliotumikia Taifa hili waanze kuombaomba hawajui pa kwenda, lakini sheria zipo *ILO Convention 102* inaeleza utaratibu wa kuwalipa watu waliostaifu na namna gani mishahara yao iweze kuletwa katika thamani ya leo, *convention* hiyo ninayo iko hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini sisi tunayo *National Social Security Policy* ya nchi hii Serikali inasemaje juu ya haya. Kwa nini Serikali inaendelea kutowalipa hawa watumishi wa Serikali waliostaifu walioitumikia nchi hii kwa heshima kubwa wanaendelea kuwalipa *peanuts*. Kama hawajui mimi naomba tuwasaidie *formula* iko wazi ambayo imekuwa *set*, *formula* iko wazi. Niliwahi kuandika kwenye gazeti nikasema nguvu ya kodi ya nchi hii haiwezi kuhimili vishindo vyta uchumi tunaotaka kujenga katika Taifa hili. Nikasema even kwa *comparative analysis* tukifanya na wenzetu wa Kenya na Uganda sisi tuko chini sana. Shilingi bilioni 300 ukilinganisha na Kenya sisi tunakusanya 3.75% ya makusanyo ya Kenya. *Difference* ya maendeleo kati ya Tanzania na Kenya haiwezi kuwa ndio kielelezo cha kusema kwamba Kenya wanatupita kiasi

hicho. *I think they are more efficient. We need to be more efficient* katika makusanyo ya kodi ya Taifa hili. Mimi naomba tusifumbie macho rushwa ndani ya makusanyo ya kodi ni nyingi. Maana yake kuna maswali ya kujiuliza kwa nini wafanyabiashara wetu wanapitisha bidhaa zao Mombasa wengi wanakwepa urasimu wanakwepa kuombwa rushwa pale *Port* ya Dar es Salaam na haya yanatokea. (*Makofi*)

La pili, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mimi sikuwepo alipowasilisha hotuba yake ya kwanza lakini kesho atakapokuja na *Finance Bill* ninamtaka atoe maelezo sahihi juu ya kodi ya Serikali inayokuwa *infringed*, moja, mafuta ya kupikia.

Mimi ni Mbunge ambaye nimebahatika kupelekwa na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi nikaenda Malaysia na nimekaa Malaysia, Malaysia pale hakuna malighafi au mafuta ghafi yanayokuja Tanzania, hakuna, 40% ni *charged* kwa mtu yeoyote anayetaka malighafi na hakuna mfanyabiashara unakuta anayelipa 40% *tax on export* kwa sababu Malaysia wana mambo mawili. Moja wanataka kulinda *employment* yao, mbili wanataka *value addition*. Kwa hiyo, kama ni mafuta ghafi wanayopeleka wanapeleka tu kwenye nchi ambayo wana *joint venture partnership* sio nchi nyingine hivi hivi tu ya kudanganya danganya, hakuna mahali ambapo wanapeleka mafuta ghafi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi niko tayari ichaguliwe Tume iende Malaysia *uta-prove* kwamba hakuna mafuta, mfanyabiashara hata huyu wa Tanzania anayoleta kutoka kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, minofu ya samaki. Toka mwaka 1996/1997 minofu ya samaki inauzwa kwa dola 2.5. *International Market* ya samaki *a kilo of fish fillet is about 6 dollars* na tumeachia bado tunaendelea kulipwa *the same profit* walizokuwa wanapata wakati ule. Mafuta ya petroli tuliweka *flow metres* pale bandarini. Bahati nzuri mimi nilikuwa nimetoka Kenya nimetembelea *pipeline* ya Kenya kutoka Mombasa mpaka Eldoret. Mafuta haya ya petroli ni dhambi kubwa kwa Watanzania. Tunatoa misamaha *to the extent of billions and billions* kwa makampuni yanayochimba dhahabu na migodi mingine. Ni kosa kabisa wanatumia mafuta wanayotaka na mengine wanauzza wapendako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam pale tuliweka *flow metres*, zile *flow metres anything you introduce* mahali popote hata kama ni *computer system*, *it can only be as good as the system you introduced* na mtu anai-manage ile *system* itakuwa sawa sawa na huyu ziliuawa baada ya miezi mitatu. Leo hii hakuna mtu hata mmoja anayejua mafuta kiasi gani tunaingiza nchini *and therefore value* ya mafuta mengi ya Tanzania hayajulikani, kodi ya Serikali inapotea, watu wanachukua, rushwa hiyo. Uchumi wa nchi hii utakua tu kama tunaweza tukatoa vipaumbele. Tukitoa vipaumbele yako mambo ya msingi ambayo tunaweza kuyaangalia na huwezi kuyapa vipaumbelee kama huwezi *to emphasize production*. Viko vyombo katika Taifa hili ambavyo vilikuwa vinatusaidia sana kuongeza *production* vyote tumetupilia mbali. Kwa hiyo, suala la kilimo *as a priority* na viwanda *as a priority* tunalichukua *tangentially not seriously as a country*. Uchumi ili ukuwe lazima u-priorities na vyombo vya kutusaidia tu-priorities. (*Makofi*)

SPIKA: Weka neno vipaumbele, *priorities* hata kule Kasulu vigumu hata kukuelewa ukisema *prioritisation*. (*Makofi*)

MHE. KILONSTI M. MPOROGOMYI: Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Tulikuwa na chombo kama *TIRDO, NYUMBU, TEMDO, SIDO, CAMARTEC* kwa upande wa teknolojia, hivi vyombo vyote vina uwezo mkubwa sana na vingetusaidia sana kuweza kutusaidia kama nchi tuweze kupata uwezo wa kuzalisha na kisha tutoze kodi lakini tunahitaji nini hapa. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa maamuzi yake mazuri na hotuba yake nzuri aliyooita hapa Bungeni. Maneno yake ni *well intened*. Lakini tunahitaji kutengeneza *structure* nzuri ya ku-manage pembejeo hii, mbolea hii ili iweze kuwafikia wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kule Kasulu sisi tumekuwa tunatafuta hii mbolea ya msamaha uliosamehe kodi hatuioni, haionekani popote. Wakulima wangu wa kahawa kule Manyovu, Kalinzi hawaioni hii mbolea wanaitafuta. Lakini lazima tutafute utaratibu wote mzuri ambao utaweza kupeleka hii mbolea iwafikie wananchi vizuri na waweze kuifanyia kazi. Lakini kingine ambacho kingetusaidia ni kuangalia hivi vyombo tumeweka kwa ajili ya teknolojia, vitusaidie kuzalisha vyombo. Teknolojia yao iwe ni teknolojia ambayo ni *easily adaptable* kwa watu wetu ndani ya nchi ili waweze kuitumia na kisha iweze kusaidia sana ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, uvezeshaji. Mimi sielewi tulikuja na maneno mazuri sana. Nchi nyingine zote nenda *South East Asia* ambao walikuwa kwenye *level* moja ya *development* sawa sawa na sisi *in the 1960s and 1970s*. Wale wanafanya uvezeshaji wa sawa sawa na wanatoa *resources* kwenda kusaidia watu wao. *Apparently focus* ya uzalishaji wa nchi hii sidhani kama imeelewaka vizuri.

Hivi tumetenga kiasi gani Waziri tueleze? Zimetengwa fedha kiasi gani kusaidia uvezeshaji katika nchi hii Watanzania tumewahamasisha, tunawaambia tuna uvezeshaji, tueleze fedha ngapi zipo? Mwaka jana ziliombwa shilingi bilioni 31 zikatolewa kidogo tu shilingi bilioni mbili. Mwaka huu wameomba shilingi bilioni 70, tuna vyombo kama *National Economic Empowerment Fund* iko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *Planning Commission* hiki ni chombo tunakihitaji na tumekuwa tunakizungumza sana humu ndani. Kitu kimoja ambacho nimekuwa nakizungumzia ni kwamba tumekuwa na *planning organization, planning institution* katika nchi hii lakini ambayo ilikuwa *divorced from finance* na sasa zimeunganishwa. Zikiunganishwa watu wengi wanataka tu *ku-deal* na pesa tu sio kitu kingine na ndicho kinachofanyika. Ukianzisha *Planning Commission of the type* tunayofikiria sidhani kama tunaanzisha *Planning Commission* kama Wabunge wengi wanavyozungumza humu ndani. Kinachofikiriwa ni *think tank*.

Mheshimiwa Spika, *think tank* is enforced from the mainstream ya Serikali, it will have notice, it will do nothing and will just look like a university system, haitatusaidia sana. Lazima tujifunze katika nchi mbalimbali kama China, South Korea, Malaysia na nchi zingine. Hii *think tank* ambayo lazima iwe linked na Serikali ikisema ni *final* hamna maneno ya kuhanja hanja tena. Wakisema ni *final* Wizara yako wakiishambulia bwana

juu kazi huna, maana inafanya kazi ya kweli kweli na hawaendi kufanya kazi ya kubabaisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya maneno ni maneno mazito sana. Nchi haiwezi kwenda kama vyanzo nya mapato havitunzwi na kama vipaumbele haviangaliwi vizuri kama tunavyopenda kufanya katika Taifa hili na uwezo tunao miaka 45 Watanzania wamesoma wanaelewa vitu. Lakini leo bado Bunge tunazungumza mambo ambayo hayana mantiki ndani yake kwa maana ya vipaumbele vinavyoletwa ndani ya Bunge unawaambiwa watu kwamba kodi hii ndiyo sahihi tunayoitoza, lakini kusema kweli sio sahihi. (*Makofi*)

Naomba Waziri wa Fedha aje na maelezo sahihi kuhusu kodi ya mafuta ya kupikia na kodi zingine nilizoziaiinsha hapa leo, hayo yatatupa dira nzuri. Uchumi wa nchi ni kitu muhimu sana sio kitu cha kuchezza chezea. Sisi tunataka hili Bunge ndilo lisaidie Taifa hili kuelekeza tunakotoka na tunakokwenda. Bunge hili tuilinde Katiba tukishalinda Katiba tuwe wasema ukweli ndani ya Taifa hili watu wapate imani na Bunge hili kama ambavyo imekuwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze sana kwa namna ambavyo umekuwa unaongoza Bunge hili, kwa sababu watu hawatambui kwamba unavyotuendesha ndani ya Bunge hili ndivyo tunatakiwa twende ili tuwatetee Watanzania walio maskini mali zetu, *resources* nydingi tunazo, madini mengi tunayo lakini watu wetu hawana thamani ndani ya nchi yao. Lazima tufike mahali Watanzania wawe na thamani ndani ya nchi yetu. Kama ni madini wachimbe, kama ni *resources* wapewe, kama ni uzawa tukubali kwamba wazawa kwanza hawa wengine mnaowapa wanapeleka fedha Canada, Uingereza, *off show banking*. Tunalihitaji na mimi nafikiri tusiwe na mjadala tena wa haya mambo kwamba Watanzania ambaa ndio wenyе rasilimali wako *divorced* na utajiri wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *private sector* inatakiwa iwasaidie Watanzania wa Taifa hili waingie kwenye *mainstream*, wawezeshwe. Leo maneno ya uvezeshwaji yamezungumzwu *tangentially* Mwfrika mwenye ngozi hii kwa kweli sijali nalisema hili kwa dhati kabisa ninavyoamini. Ngozi hii wanafanya maisha yao yawe ya kusononeka kila wakati. Ngozi nyeusi kama ya kwangu hii na hili tusilione aibu, mimi napenda kuwa wazi tusilione aibu. Tumewatajirisha watu ambaa hawana maslahi na Taifa hili. Kwa nini tunaogopa ogopa? Waliotuchagua ni maskini tunakuja humu hatuwasemei, hawana faida na yale tunayokuja kuzungumza humu ndani. Tuwasemee. Juzi tulikuwa tunaonana na wachimbaji wadogo wadogo wa *Tanzanite* wanapigwa vita waondoke pale wasisikilizwe tena waondoke na vile vitalu vifutwe yule bwana anayesema *Tanzanite* anaizalisha *South Africa* nayo ipotee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kitu cha mwisho kimoja, kwamba hawa wanaofanya kazi kwenye madini wanaotoka nje hawatozwi kodi hapa Tanzania, juzi nilikuwa Benki moja nikakutana na mtaalamu mmoja amekuja kuhamasisha fedha zao zote zipelekwe *off show banking* waka-deposit huko. Nikamuuliza zikienda *South Africa* mnafanya nini maana hapa hamlipi kodi, wakasema wakifika kule kama hawakutoa kodi wanatozwa kodi *South Africa*. Kwa nini uchumi wa nchi hii ndio ukaimarishe uchumi wa *South Africa*? Haya yote ni maneno ya masikitiko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga hoja mkono lakini naomba maelezo hayo niliyoyasema, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kilontsi Mpologomyi, tunajua umebobeaa katika masuala hayo, kwa hiyo, nadhani Serikali imekusikia na kwa sasa namwita mchangiaji wa mwisho kwa mchana huu ambaye ni Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa Richard Ndassa. (*Makofi*)

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii mchana huu na mimi nichangie kwenye hotuba hii ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Lakini kama ilivyo kawaida nianze kwa kutamka kwamba naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Lakini pia naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Lakini pia naomba uniruhusu nimpongeze sana *CEO* au Mkuu wa *TRA* Bwana Harry Kitilya kwa kazi nzuri anayoifanya ya kukusanya mapato yetu ambayo kwa sasa imefikia karibu shilingi bilioni 300. Namtakia kila la kheri naomba aendelee hivyo na ikiwezekana wazidi kutukusanya fedha nyingi zaidi ili uchumi wetu uweze kufaa. Nianze kwa kuomba kumshukuru na kumpongeza *CEO* wa *The Gaming Board* Ndugu Abbas Tarimba, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kukusanya mapato mengi zaidi kutoka shilingi bilioni 3 kwenda shilingi bilioni 3.9. Ni kazi nzuri sana naomba waongeze bidii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa kazi moja kubwa mengi yamesemwa lakini mimi nitajikita sana kwenye Halmashauri yangu ya Wilaya ya Kwimba. Nina masikitiko makubwa kwamba kwa mwaka huu Halmashauri yangu ya Wilaya ya Kwimba haikupata fedha za ruzuku kwa sababu ya ukosefu wa wataalamu wa uhasibu. Ni zaidi ya shilingi milioni 800 ambazo zilitakiwa zipatikane kwa ajili ya kuendeleza maendeleo katika Wilaya ya Kwimba kwa maana ya maeneo mawili jimbo la Kwimba na Sumve, lakini tatizo kubwa ni wafanyakazi Idara ya Uhasibu. Hatukuwa na wafanyakazi hao, lakini tatizo sio la kwetu, sisi tumehukumiwa kwa sababu ya ukosefu wa wataalamu wa Uhasibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niiombe sana Serikali kwa sababu tunapeleka fedha nyingi sana huko Wilayani lakini ninavyojua tunavyo vyuo vyetu ambavyo vinazalisha hawa wataalamu kwa maana wataalamu wa Uhasibu. Tunayo *IFM*, *CBE*, Chuo cha Uhasibu Mbeya, Chuo cha Uhasibu Arusha tatizo kubwa ni upungufu wa walimu. (*Makofi*)

Naomba sana kwa sababu ukiangalia fedha ambazo tunazipeleka kwenye Halmashauri zetu, kwenye Majiji yetu, Manispaa zetu bila kuwa na wataalamu wa Uhasibu wa kikweli matatizo haya yataathiri Halmashauri zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini unaangalia kwamba unapeleka kwenye Halmashauri, Manispaa, Jiji kwa mfano kwenye Jiji kuna fedha zinaenda za maendeleo pamoa za

mishahara na *other charges* unakuta karibu shilingi bilioni 40 lakini ukimuuliza Mhasibu (*DT*) wake pale unaambiwa kiwango chake cha elimu labda ni *diploma*, lakini anasimamia mabilioni ya fedha. Ukienda kwenye Halmashauri zingine zinapata kuanzia shilingi bilioni 15 mpaka shilingi bilioni 20, zingine zinapata shilingi bilioni 30 lakini anayesimamia pale kwa maana ya Mhasibu labda hana *CPA* ana *certificate*.

Mimi naomba na kushauri na ndiyo maana utaona kuwa mara nyingi fedha zinazokwenda kwenye Halmashauri zetu haziendi ndiyo maana utakuta kwamba haziendi kufanya kazi ile inayotakiwa kwa sababu mchanganuaji wa mpango hana ule uelewa mkubwa zaidi matokeo yake anashindwa kufanya *reconciliation* lakini mnakuja kupata adhabu Halmashauri husika. (*Makofi*)

Wilaya yetu ya Kwimba mwaka huu tumekosa fedha za ruzuku kwa sababu ya upungufu wa wataalamu. Naiomba Serikali, inawezekana zipo Halmashauri zingine nazo hazikupata fedha za ruzuku, nina uhakika Urambo mmepata lakini mmepata kwa sababu mna wataalamu wanaoweza kufanya *reconciliation* vizuri, kuna ma-auditor wazuri pale ndiyo maana mmepata fedha za ruzuku. Tunaiomba sana Serikali ifanye utaratibu, itupelekee wataalamu wa kwenda kusimamia fedha nyingi zilizokwenda kwenye Halmashauri zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie Chuo cha Mipango kwa maelezo tunaambiwa ni Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini. Nilitegemea chuo hiki sasa ndio kiwe kitovu, kiwe chachu ya Maendeleo Vijijini kwa sababu pale wanafundishwa wengine mpaka ma-*VEO*, ma-*WEO*, Makatibu Tarafa na Maafisa Mipango. Sasa niiombe Serikali ifanye utaratibu kwa kushirikiana na TAMISEMI na Wizara ya Fedha, *VEOs* kwa maana ya watendaji wa vijiji na watendaji wa Kata ili waende wakasimamie mipango ya maendeleo vijijini, lazima wapate elimu kwenye Chuo cha Mipango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, si lazima kuwaleta Dodoma lakini mnaweza mkafanya utaratibu mzuri mkafanya Kikanda. Kanda ya Ziwa mnaweza mkaamua mkawapaleka Mwanza, Shinyanga au Mara wakapata mafunzo ya kuweza kusimamia mipango ya maendeleo vijijini, vinginevyo tutawalaamu kwamba hawa hawasimamii kwa sababu hawana muda, wengine hawakusomea namna ya kutumia hii mipango ya maendeleo vijijini. (*Makofi*)

Naomba na kushauri tufanye utaratibu. Nakumbuka *VEOs* wangu, watendaji wangu wa vijiji na kata hawajapelekwa kwenda kujifunza hata siku moja namna ya kusimamia mipango ya maendeleo vijijini. Inawezekana hata wa Bariadi hawajakwenda, wa Urambo hawajakwenda, naomba na kushauri kwa sababu hawa ndio wasimamizi wa mipango ya maendeleo vijijini waweze kupata elimu ya kutosha ili waweze kusimamia vizuri mipango ya maendeleo vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mmesema kwamba tunavyo vyuo vyetu ambavyo vinafundisha Uhaisibu bila kupata Wahaisibu wa kweli kweli hatuwezi kwenda kusimamia fedha nyingi ambazo leo tunazipitisha hapa. Tumepitisha karibu trilioni saba, lakini

fedha nyingi zinakwenda vijijini, tujiulize nani anakwenda kuzisimamia hizo fedha. Je, wanaokwenda kuzisimamia wanao uelewa wa kihasibu au tunapeleka tu watu ili mradi?

Naomba sana Serikali ifanye utaratibu pale ambapo unapeleka shilingi bilioni 20 unapeleka shilingi bilioni 40 tuwe na uhakika kwamba huyu mtu anayesimamia ikiwezekana kwa mfano kwenye majiji huyu anayesimamia hizo shilingi bilioni 40 ana ujuzi gani, ana *CPA* au ana *diploma*. Lakini unampa mtu mzigo aubebe wakati hana uwezo wa kuubeba na yeye sio Mnyamwezi naambiwa hapa. Usimpe mtu mzigo ambao hawezi kuubeba, mpe mtu mzigo lakini mwenye uelewa mkubwa zaidi, kwa kufanya hivyo tutakuwa tumepata wasimamizi wazuri wa fedha za Halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini niombe kwenye vyuo vyetu nya sasa ilisemwa jana sijui labda ni kwa sababu ni biashara utakuta mrundikano ni mkubwa kweli kweli wa wanafunzi, sina uhakika kama ile elimu wanayoitafuta wanaipata kikweli kweli. Kwa sababu ukiuliza unaambiwa walimu hawatoshi. Sasa kama walimu hawatoshi hivi ni kweli hawa kile kilichowapeleka pale kwenda kusomea wanakipata, jibu hapana. Zamanii tulikuwa tunaambiwa masomo ya Uhasibu yalikuwa ni magumu, lakini siku hizi sisikii watu kulalamika, siku hizi watu wanapeta kwa sababu nafikiri ni soko huria. (*Makofi*)

Naomba na kushauri fedha hizi tunazopitisha hapa ni nyingi. Naomba vyuo vyetu, naomba Waziri mhusika, Waziri wa Fedha lazima tuimarishe vyuo vyetu na lazima wanafunzi wanaosoma lazima wachaguliwe wajue vizuri ili waweze kwenda kusimamia fedha zetu hizo za wapiga kura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo niseme tena kwamba naunga mkono hoja na nakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa mchana huu ndio tumefikia hapo. Mpango wa kazi yetu tutakaporejea saa 11.00 jioni nitamwita Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kama mchangaji wa mwisho. Saa 11.15 jioni nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Jeremiah Sumari, halafu saa 11.30 jioni nitamwita Naibu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee na saa 11.45 jioni nitamwita mtoa hoja kwa saa moja yaani dakika 60 itatufikisha kwenye 12.45 jioni.

Kwa hiyo, tutakuwa na saa moja ya Kamati ya Matumizi. Huo ndio mpangilio wa kazi yetu kwa jioni. Sasa kwa kuwa muda umekaribia sana wa kusitisha shughuli basi nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

(*Saa 06.58 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

HOJA ZA SERIKALI

(*Majadiliano yanaendelea*)

SPIKA: Msemaji wa mwisho katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed , Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni. (*Makofit*)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na kuwa msemaji wa mwisho wa Wizara hii ya Fedha na Uchumi na kwa sababu nina mambo mengi naomba niende kwa haraka kidogo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, tuna taarifa kwamba *flow metre* imeharibika muda mrefu na moja ya madhumuni ya Serikali kuweka *flow metre* ni kuhakikisha kwamba tunakusanya kodi vizuri inayotokana na mafuta. Pengine ni vizuri Mheshimiwa Waziri akatueleza katika kipindi hiki ambacho *flow metre* imeharibika kuna tofauti gani na kile kipindi ambacho *flow metre* ilikuwa inafanya kazi. Kwa sababu hizo taarifa hakuna wakati wowote tumezipata na Serikali imeigharimu fedha nyingi kupata hiyo *flow metre*. Hilo la kwanza. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala la wastaa fu wa Afrika Mashariki. Wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na wakati Waziri Mkuu anajibu swali langu hapa Bungeni alisema kwamba kazi inayofanyika sasa hivi ni kutoa majina ya watu wote ambao wamelipwa na wale ambao bado *cheque* zao zimekuwa ziko tayari lakini hawajachukua fedha zao ili halafu tuweze kufanya uhakiki. Naona Serikali au Wizara mpaka leo imekaa kimya hilo zoezi halijafanyika. Lakini vile vile tulionba katika Bunge lako Tukufu na nilimwomba Waziri Mkuu kwamba wakati umefika kwa Bunge hili sasa kuunda Kamati kuisaidia Serikali. Kwa sababu kwa kweli ni aibu kwa Taifa letu. Kama wenzetu katika kipindi cha miaka 20 wameweza kulipa sisi mpaka leo bado wananchi wetu, raia wetu wanateseka na sisi tumekaa kimya. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri muda umefika wa Bunge kuunda Kamati kuisaidia Serikali kulimaliza tatizo hili *forever*. Hilo lilikuwa ombi langu na naomba unikubalie. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, la tatu Serikali ilikuwa inafanya utafiti kuweka kwenye *register assets* zetu na kwa bahati mbaya kwenye kitabu cha hotuba ya Waziri hakueleza hatua iliyofikia ni kiasi gani kwa sababu wakati fulani tuliambiwa baadhi ya Mikoa wameshaweka takwimu za mali za Serikali na ziko katika *registry*.

Sasa hatukuelezwa katika taarifa yake amesema tu hiyo inaendelea, inaendelea mpaka lini? Ni jambo ambalo Bunge lako limelidai si chini ya miaka mitano mpaka hivi sasa. Bado Serikali haijui mali zake mpaka leo kwa ukamilifu. Tulitaka nalo hili tupate maelezo kutoka kwenye Serikali. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, suala la nne ni suala la manunuzi. Manunuzi tulikubaliana kabisa katika Bunge hili kwamba kutokana na umaskini tulionao kununua kitu kimoja kimoja hakitusaidii. Kwa hiyo, twende kwenye *bulk purchase* na tukakubaliana kabisa na Serikali ikasema kwa kweli inalifikiria jambo hilo, tulitegemea katika hotuba ya Waziri hilo lingeweza kusemwa lakini wamekaa kimya na bado tunaendelea kununua kidogo

kidogo jambo ambalo linasababisha hasara kubwa kwa manunuzi ya Serikali. Tunataka tupate maelezo na hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri wa Maji anawasilisha Bajeti yake kulikuwa na utata juu ya takwimu ya fedha ambazo Waziri amepata. Waziri wa Maji alisema yeye ameomba shilingi bilioni 156. Lakini Waziri wa Fedha akasema kwamba ni shilingi bilioni 230.6, nakumbuka Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya alihoji na Mheshimiwa Naibu Spika, alitoa maelekezo kwamba tupate majibu katika Bunge hili ni zipyi takwimu sahihi. Nategemea Mheshimiwa Waziri hilo atalifanya ili Bunge hili liwe na takwimu sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la Bajeti yenyewe. Mawaziri wote waliokuja hapa wanaleza kwamba fedha nyingi sana zinakwenda kwenye Halmashauri. Ukichukua takwimu sahihi ambazo ninazo ni kwamba Bajeti yetu ya shilingi trilioni 7.4 *only 1.5 trillion* ndiyo zimekwenda kwenye Halmashauri kama asilimia 17 hivi. Katika hizo shilingi trilioni 2.4 ziko kwenye *development* lakini zilizokwenda kwenye Halmashauri ni shilimgi bilioni 356 tu. Sasa mimi nafikiri hapa kuna tatizo la msingi. Ukichukua kwa jumla Halmashauri haipati zaidi ya asilimia 18 au 19 ya pesa zote zinazotoka Serikalini. Pesa nyingi zinabaki Serikali Kuu na huko kwenye Serikali za Mitaa zinazokwenda zinakwenda kwenye *OC* na *employment allowance* na *pay as you earn.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye *development* na mambo mengine hakuna fedha kabisa. Lakini hapa tunaambiwa pesa zimekwenda kwenye Halmashauri tunawajengea matumaini wananchi kumbe kitu chenyewe hakipo. Sasa mimi nina ombi kwamba wewe uagize Kamati yako ya Fedha na Uchumi ikae na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ikae na Waziri wa Fedha tuchambue kwa kina fedha hasa zinazokwenda kwenye Halmashauri badala ya taarifa tunazopewa hapa ndani ambazo si sahihi hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili naliomba kabisa kwako vinginevyo kama kuna asilimia 25 ya fedha hizi zinakwenda kwenye Halmashauri tungeona *impact* ya uchumi, tungeona kabisa. Sasa pesa zote zinazobaki kwenye Serikali Kuu nazo huoni *impact* kwa sababu matumizi yanayotumika hayatumiki vizuri. Chukua *personal emolument*, chukua *employment allowance* angalia na fedha nyingine inayobaki ni kiasi gani. Utakuta fedha nyingi inakwenda kwenye utumishi tu, lakini haiendi katika kazi ambazo zinakwenda kubadilisha taswira ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, shilingi trilioni 7.5 ni fedha nyingi sana kama unaziingiza kwenye uchumi na kama uchumi unasihamiwa vizuri. Sasa hili nasema ni vizuri Kamati yako ya Fedha na Uchumi ikae na Wizara ya Fedha na Wizara ya TAMISEMI tuone ni kiasi gani cha fedha hasa zinakwenda kwenye Halmashauri ili tuondokane na hili tatizo la kuzisingizia Halmashauri kama fedha zinakwenda lakini kwa kweli hakuna kinachokwenda. Ni maneno zaidi tu kuliko *figures* halisi na nasema hilo tumelifanyia utafiti na mimi nafikiri tulifanyie kazi kwa undani kabisa ili tuone Halmashauri zetu ambazo tunazibebesha lawama kubwa tunataka maendeleo wananchi wayaone chini,

hayaonekani kwa sababu pesa zinamalizikia huku juu kwa mambo ambayo pengine si sahihi katika matumizi yake. Hilo ni moja ambalo ningependa kulisema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni takwimu. Inasikitisha sana kwamba huwezi kupanga mipango ya maendeleo kama takwimu za nchi si sahihi. Ukichukua kitabu cha hali ya uchumi cha mwaka unaomalizikia mwaka 2007 na ukachukua kitabu hali ya uchumi cha sasa hivi tulichopewa hapa Bungeni, kuna vitu viwili tofauti. Kwa mfano, katika kitabu cha mwaka jana tunaelezwa kwamba uzalishaji katika kilimo mikopo ya Benki za Biashara katika sekta mbalimbali yaani Benki za Biashara fedha zilizokopesha katika sekta mbalimbali. Uzalishaji katika kilimo mwaka 2006 ilikuwa ni kama asilimia 19.3. Ukichukua kitabu cha sasa wamezichanganya sekta mbalimbali, wamezichanganya pamoja zote ni asilimia 11.6. Sasa hizi *data* unasema zinatokea wapi. Kwa sababu huwezi kujenga *data* kesho asubuhi lazima zitakuwa na mtiririko kutoka huko nyuma. Lakini unafika mahali unaona inakatika, katikati kuna *figure* inakuja juu wala huelezwi inatokea wapi na hapa zimechanganywa hizi hapa. Huku zimebaguliwa sekta zote mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jingine. Kuna sekta ya uuzaaji wa mazao ya kilimo. Kwa mwaka 2002 mpaka 2006 ni zero hakuna kitu. Katika kitabu hiki hakuna habari hizo. Kuna sekta nyingine ya biashara uzalishaji wa mazao ya kilimo yaliyosafirishwa nje. Kwenye kitabu hiki ni zero tupu, kwenye hiki kingine hakuna kitu. Sasa unajiuliza hizi takwimu zinatoka wapi? Tutapangaje maendeleo ya nchi? Kama Benki za Biashara hazikopeshi kwa mazao yaliyotakiwa kusafirishwa nje ya nchi ile *export guarantee scheme* inafanya kazi au data zake zinaonekana wapi katika kitabu hiki? Benki Kuu inatoa *export guarantee scheme* tulitegemea katika data hizo basi itaonyesha kwamba mwaka huu tumesafirisha nje maua kiasi fulani pesa zilizokopesha ni kiasi gani na Mabenki humu katika taarifa hizi za Sekta ya Fedha hakuna. (*Makofi*)

Sasa nasema kama nchi tunafika mahala tunapanga mipango, na takwimu zetu si sahihi hatuwezi kufika mahali popote hata kidogo. Tutakuja hapa, tutapiga maneno, tutaondoka kama takwimu zetu si sahihi na takwimu zetu si endelevu. Tutakuwa na matatizo makubwa ya kupima hata pale ambapo tunafikia katika hali yetu ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, jingine ambalo ni la muhimu sana ni suala la Tume ya Mipango. Nchi yetu imekuwa nchi ya majaribio. Kila wakati tunafanya *experiment* na hizi *experiment are very expensive* na mimi nafikiri tumefika mahala Bunge hili sasa tukae tuandike katika Katiba hivi Rais akiingia madarakani ni Wizara ngapi aunde. Tusipofika hapo itakuwa kila Rais anayekuja atakuwa anaunda vyake na kesho anaunda, kesho kutwa anaunda. Unawahamisha watumishi kutoka mahala pengine unawapeleka huku. Ni gharama. Mtumishi kwenda kujifunza kupata uzoefu mahala pengine inamchukua si chini ya miezi sita. Kwa hiyo *on that time* na *wasting period*, ni kipindi cha kupoteza tu. Sasa umekuja wakati tumeunda Wizara nyingi, tunazivunja, tunazichanganya. Leo Tume ya Uchimi katika nchi yetu imevunjwa sijui mara ngapi? Hivi kweli katika miaka 45 hii hatujaweza kujenga uzoefu wa Tume gani ya Mipango tunaitaka katika nchi hii? Halafu tukaiingiza kwenye Katiba ikawa haichezewi chezewi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi leo tumekaa katika Bajeti hii hatukuweza kumhoji Waziri wa Fedha na Uchumi juu ya Tume ya Mipango maana haikuwa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi anasema hiyo haikuwa kwangu. Tukaambiwa iko chini ya Ofisi ya Rais Utumishi. Hana *background* ya mambo ya uchumi, hajui a, b, c, d ya hali ya uchumi, hajui chochote. Sasa unafika mahali unasema huu mpango kwa mwaka huu unaendaje.

Kwa hiyo zile programu zote za MKUKUTA hazina uratibu ambapo ungetegemea hata Rais anapokuja kulihutubia Bunge jambo la kwanza angetazama ratiba yake ya MKUKUTA inaendaje hasemi hayo kwa sababu hana *reference*. Ungetegemea kabisa anasema jamani MKUKUTA umesema hivi na sisi tulichokifanya ni hiki. Ndiyo programu ya taifa hiyo. Lakini hilo halitokei kwa sababu hatuna tume ya mipango ambayo iko *established* ina watu wanafanya kazi kwa umakini na watu ambao wanajua kabisa tunakwenda wapi katika nchi yetu. Matokeo yake kila wakati katika nchi tunafanya majiribio kila siku. *It's dem expensive experiment* katika nchi yetu. Tunawapa umaskini Watanzania usio na sababu kwa sababu ya majaribio. Tumejaribu kwenye sera nyingi nyingi, hakuna hata moja ambayo imekuwa endelevu kwa sababu hakuna chombo cha kusimamia yale ambayo tunakubaliana.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nashauru Bunge lako Tukufu tufike mahali katika mabadiliko ya Katiba tuseme sasa Katiba yetu lazima iseme wewe Rais tunakuchagua Wizara zetu tunazozitaka Tanzania kwa uchumi wetu ni 13. Tume yetu ya Mipango ni haya, tufike hapo wanafanya wenzetu. Wanafanya Wamarekani, haingii pale Rais akajiundia Wizara tu. Tufike hapo, lakini leo una Wizara 20 kesho 25 kesho kutwa 30 uchumi wenyewe kama huu ambao ni wakubembeleza wa kuombaomba kila siku tunaweza wapi? Hatuwezi Mheshimiwa Spika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuipima *growth* hata ya *human capacity* yetu, hatuwezi kuipima. Kwa sababu leo mtumishi umemweka kwenye Idara hii, kesho unamhamishia kwenye Idara hii, hawezi kujenga uzoefu. Ndiyo maana hata Wabunge humu ndani wa muda mrefu wana uzoefu mkubwa kwa sababu wamekaa ndani ya Bunge kwa muda mrefu. Ni kitu ambacho nakiona halali tu. Anayeingia jana na aliyeingia nyuma atakuwa amejijengea uzoefu kama wewe Mheshimiwa Spika, uzoefu wako ndiyo uliotufikisha hapa. Ingekuwa ni mtu tu tumechukua huko hana uzoefu tungeyumba tu humu ndani ya nyumba hii. Sasa lazima tujenge uzoefu na huwezi kujenga uzoefu kama hatuna utaratibu wa kusema kwa kweli taasisi hii tumeiunda hapa basi tuifanyie kazi na iendelee. Mimi nafikiri hilo tukilifanya itatusaidia. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atupatie ufanuzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ni suala la *Twin Towers* pale Benki Kuu. Benki Kuu imetumia fedha nyingi sana. Pamoja tukitembelea majengo na tunayaona mazuri na kadhalika lakini bado *value for money* pale kuna swali kubwa ambalo halijapata majibu. Tunataka Waziri atujibu. Tumeambiwa kwamba Tume imeundwa ili kuchunguza thamani halisi ya majengo yale, atuambie Waziri ni lini taarifa ya Tume hiyo ataileta katika Bunge hili ili wote tuione kama kweli fedha iliyotumika ya Watanzania

imetumika kwa madhumuni yanayotakiwa. Kuna taasisi chungu nzima Benki Kuu inatoa dhamana hawatuelezi. Dhamana hizo watu wamelipa na kama hawakulipa je, hatua gani zimechukuliwa? Kuna nyingine wanachukua dhamana lakini hakuna *security* inayowekwa. Tunamuuliza maswali yote haya Mheshimiwa Waziri kila akija wakati wa Bunge hatupati majibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mara hii kwa ruhusa yako tunaomba atupatie majibu wakati tunapitisha mafungu nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa mchango mzito. Sasa kama nilivyotangulia kusema tumehitimisha wachangiaji kutoka kwa Wabunge na sasa ni wakati wa majumuisho kutoka kwa Naibu Mawaziri na Waziri. Sasa nitamwita Mheshimiwa Jeremiah Sumari kwa ajili ya kujibu yaliyo chini yake kwa dakika kumi na tano na atafuatiwa na Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee naye kwa dakika kumi na tano. Karibu Mheshimiwa Jeremiah Sumari. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na yenye ufanuzi wa kina na kuhusu Wizara hii.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia.

Pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwanza, napenda kuwapongeza wafanyakazi/watumishi wote wa *TRA* kwa kazi nzuri wanayofanya ya kukusanya mapato na ushuru. Naiomba Serikali iboreshe mazingira ya kufanya kazi ili waweze kukusanya mapato mengi zaidi

Serikali ilikuwa na mpango wa kujenga jengo la *TRA* Wilaya ya Mpwapwa na kiwanja kilitengwa kwa ajili ya ujenzi huo. Je, Serikali ina maelezo gani; kwa nini ofisi hiyo haijajengwa hadi sasa. Kulipa kodi ni suala la kisheria; je, Serikali imewachukulia hatua watu wangapi ambaao walikwepa kulipa kodi 2007/08 na fedha kiasi gani zimekusanywa kwa walipa kodi hao waliokwepa kulipa kodi?

Kwa kuwa Shirika la Bima la Taifa limekumbwa na matatizo mengi ya kukosa fedha za kulipa wateja wake ambaao Bima zao zimeiva, wakiwepo Walimu wa Wilaya ya Mpwapwa. Je, Serikali ina maelezo gani kuhusu Shirika hili na madeni makubwa wanayodaiwa; na je, ni lini madeni hayo yatalipwa kwa wateja hao?

Kwa kuwa Wilaya ya Mpwapwa kuna huduma ya Benki ya NMB na hivi sasa kuna wateja wengi wakiwemo wachimba madini wa Winza; je, ni lini Serikali itafungua huduma ya ATM Mpwapwa?

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Mawaziri, pamoja na Watendaji, kwa kuandaa hotuba hii.

Kuhusu Kodi za Mapato; kwa sasa hivi mnazo *sticker* nyingi sana za mapato zinazobandikwa kwenye magari mfano kodi ya Mapato, Kodi ya Jiji, *Sticker* ya *MOT* (*Road Licence*) ni kwa nini isitumike *sticker* moja kwa malipo yote hayo? Magari yanachafuka na hizi *sticker* mpaka mengine yanabandikwa katika kioo cha nyuma ambapo kunaweza kusababisha ajali.

Mheshimiwa Spika, hoteli kubwa za kigeni huwa zinapata fedha nyingi sana za kigeni na za Kitanzania; je, ni mara ngapi *TRA* wamefanya ukaguzi wa ghafla kwenye hoteli hizo na kuhakikisha wanapata kiasi gani? Sababu wakishatengeneza faida zao wanabadilisha majina, lakini wenyewe hoteli (*Local*) wao utakuta Maafisa wa *TRA* wanaenda asubuhi hata saa kumi na moja na nusu kukagua ni wageni wangapi wamelala katika hoteli husika.

Mheshimiwa Spika, nahitaji maelezo ya kina kama kuna Sheria ya *TRA* inayoruhusu maofisa kuja kwenye hoteli kusumbua wageni na kucheki kama kweli wamelala watu au la? Pia nataka maelezo kama hawa maofisa (*TRA*), huwa wanafanya ukaguzi wa aina hii kwenye hoteli kama VIP Serengeti, Kempisk na Movenpick Dar es Salaam?

Mheshimiwa Spika, ni kitu cha kusikitisha, Watanzania wanaojitahidi kuanzisha hoteli badala ya kupata *support* kutoka Serikalini wao ndio wanawawekea kodi ya 20% kwa wale wafanyabiashara wadogo wadogo wakati hawa wawekezaji wakubwa hawalipi kodi; hii siyo haki kabisa. Pamoja na Shilingi ya Tanzania kupanda thamani, lakini ukweli mtupu hii ni sababu tu American U\$ imeshuka thamani. Cha kusikitisha, sisi wenyewe hatuthamini fedha zetu. Kwa nini malipo yote nchini yasifanyike kwa Shilingi ya Tanzania? Nchi jirani Kenya na Uganda, ukitaka kufanya malipo yoyote hata hotelini, Park Fees na Licences lazima uende bureau-de-change kubadilisha fedha hizo za kigeni kwa aidha Kenyan Shillings au Ugandan Shillings ili uweze kufanya malipo hayo. Hii inaonyesha jinsi wanavyothamini fedha zao.

Mheshimiwa Spika, hapa Tanzania tukikata TALA Licence lazima ulipe kwa U\$. Park fees na hoteli nyingine wanalipa kwa U\$. Kuna haja ya kuleta sheria ya kufanya malipo yote yafanywe kwa Shilingi ya Tanzania.

Ni jambo lililo wazi, kwa sasa hivi hali ya uchumi imepanda sana, maisha yamekuwa ghali hata wastaifu wanaathirika sana na viwango vidogo vya pensheni wanavyopata. Kwa sasa hivi hata kama wazee hawa walitegemea watoto, inakuwa ni vigumu sana ukilinganisha watoto yatima wanatunzwa na wazee hawa. Kuna haja ya Serikali kuzingatia ni jinsi gani pensheni hizi zitalipwa kulingana na hali ya maisha kwa hivi sasa. Kupanda kwa bei ya bidhaa hapa kwetu, kisingizio kimekuwa ni kupanda kwa bei ya mafuta duniani, lakini hili si kweli mbona tunasikia bei ya mafuta imeshuka duniani lakini hapa kwetu badala ya bidhaa kushuka ndio zinazidi kupanda bei?

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninamshukuru Mungu, kwa zawadi ya uhai na utashi wa kujadili hoja hii. Ninaomba

kuunga mkono hoja. Pili, ninatoa pungezi zangu za dhati kabisa kwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kutuletea hotuba iliyosheheni matumaini.

Tatu, ninaomba niorodheshe kero zangu ambazo ninaamini zitajibiwa vizuri, nisilazimike kusimama wakati wa vifungu na kutaka ufanuzi

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali kutoa fedha za uwezeshaji, je, Serikali inayo taarifa kuwa riba ni kubwa sana na inawaumiza wananchi? Kwa kuwa Serikali inaipa benki kwa 10% na wao wanatoa kwa SACCOS ambazo zinawafikishia wananchi kwa 13% - 15% ili kupata hela ya kuendesha ofisi na kulipa mishahara; je, Serikali ipo tayari sasa kukubaliana/kuweka msimamo na hizo *Commercial Banks* zilipe *savings interest* 2% zaidi ya wanazolipwa watendaji wengine ili wamudu kuendesha ofisi zao za SACCOS?

Mheshimiwa Spika, riba inayotolewa na Benki zetu ni ndogo sana ukilinganisha na inayotozwa kwa wakopaji; benki zinalipa 2% na zenyewe zinalipwa 10% - 25%.

Mheshimiwa Spika, hivi ni shughuli gani ambayo Mtanzania wa kawaida, ataifanya aweze kulipa riba kubwa hivyo na bado kuweza kubakiwa na mtaji wa kuendesha biashara na hasa ukizingatia mikopo yote ni ya muda mfupi?

Mheshimiwa Spika, Waziri atueleze mkakati wa kupunguza riba kwenye *Commercial Banks*.

Mheshimiwa Spika, Kodi inayokatwa kwenye gawio. Wananchi wengi wamesusa kuchukua gawio CRDB hasa ukizingatia nauli ya kufuata inazidi gawio. Kwa kuwa Serikali ina nia nzuri kuhamasisha wananchi kununua hisa; kwa nini wale wote wanaolipwa gawio chini ya Sh. 200,000 au chini ya kima cha chini cha mshahara wasisamehewe kodi? Matumaini yanguni kuwa Waziri atalipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero yangu ya mwisho leo ni ile ya Chuo chetu cha IFM; wanafunzi wa mwaka I – III wanateseka sana kupata mahali pa kulala na wanapishana kitanda kwa saa. Wazazi sasa wanalipa hadi laki Sh. 800,000 kinyemela ili watoto wapate kulala chuoni. Je, Serikali ina mpango gani wa kuipanua hosteli na kuondoa kero kwa wanafunzi wanaotoka mikoani?

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, Rais George W. Bush, alitoa ruzuku ya shillingi bilioni 700 mapema mwaka huu, kuisaidia Tanzania kupambana na umaskini kwenye mikoa iliyo nyuma sana kwa miundombinu ya barabara, umeme na maji, mbali na Janga la UKIMWI.

Mkoa wa Singida ambao upo nyuma zaidi kimaendeleo, haukufikiriwa kwenye mgao wa rasilimali kama fedha za kujenga ama kurekebisha miundombinu ya barabara zake za ndani. Barabara inayojengwa ya Dodoma – Singida – Mwanza inapita sehemu ndogo tu ya Mkoa na ni ya Kitaifa.

Kulingana na takwimu za Serikali yenyewe, zinaonyesha kuwa, Mkoa wa Singida ni wa mwisho kwa pato la mtu kwa mwaka nchini (*per capital income*); na mara kadhaa mkoa huo umetolewa mfano na Viongozi Wakuu wa nchi kuwa ndiyo mkoa unaoshika mkia katika mikoa yote kwa umaskini!

(a) Napenda kupata ufanuzi, je, ni vigezo gani vilivyotumika kwenye kugawa fedha za MCC na kuuacha mkoa maskini zaidi wa Singida usipate hata senti moja kurekebisha miundombinu yake ya ndani wakati lengo la fedha hizo ni kupunguza makali ya umaskini?

(b) Je, kwenye mgao huo wa rasilimali fedha, mikoa kwa ujumla ilihuushwa vipi kabla ya kufikiwa kwa maamuzi yaliyotolewa kwamba Mkoa wa Singida usipate na mikoa mingine teule ipate mgao huo?

(c) Napendekeza mgao wa Fedha za MCC uwe *reviewed* (urejewe), ili kuuhusisha Mkoa wa Singida ambao ndio maskini zaidi kwenda sambamba na malengo ya ruzuku hiyo ya Sh. 700 bilioni za Rais Bush; vinginevyo, uamuzi huo wa awali ni wa upendeleo na unaubagua Mkoa wa Singida kwa sababu zisizoleweka. Naomba *fairness* kwa mgao huu wenye utata.

Riba zitozwazo na taasisi za fedha zinazowakopesha watumishi ni za juu sana. Walimu wa Shule ya Sekondari ya Kimadoi ya Mjini Itigi, walikopeshwa Sh. 700,000 kila mtu marejesho ya mikopo huo ni Sh. 2.3m kila mtu. Mzigo huu wa riba za mikopo umewaelemea watumishi kiasi kwamba, wanashindwa kumudu maisha yaliyopanda. Mwisho wa mwezi hawapati mishahara kwa sababu ya makato makubwa yanayofanywa. M/S Bayport ni moja ya taasisi zinazolalamikiwa sana kwa riba kubwa. Taasisi hii inafanya biashara ya mfano wa mfanyakibashara wa Venice Shylock, ambaye anaamua apate *a pound of flesh* kutoka kwa mdaiwa wake kwa kukosa cha kulipa!

Matokeo ya kuathirika kwa watumishi hao wanashindwa kufundisha kwa makini. Muda mwingi hupita kwa kujitafutia riziki kwa njia nyingine na pia muda mwingi huutumia wakopeshaji wengine kutoroka kuepuka kufilisiwa vifaa vyao. Matokeo yake ni Taaluma kuathirika, wanafunzi hukosa walimu kwa muda mrefu kwa sababu nilizozitaja. Mwisho wa yote ni kwamba, tutakuwa na taifa la watu ambao hawakusoma vizuri kwa kukosa taaluma inayostahili. Yasemekana asilimia 60 ya walimu nchini wamekumbwa na tatizo hili la mikopo hii yenyе hila na ghiliba.

Napendekeza Serikali ifanye tathmini ya tatizo hili na kuwa walimu na watumishi wengine wa Serikali basi ifikirie kufuta/kuchukua dhamana ya mikopo hii na pia kuzifungulia mashtaka taasisi zilizodanganya zirejeshe fedha hizo.

Inatia shaka na aibu ni kwa nini hadi leo hii wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki hawajamaliziwa mafao yao. Itigi kulikuwa na karakana kuu ya *East African Road Services* na baada ya Jumuiya kuvunjwa, wafanyakazi wengi walibakia hapo. Wapo, leo wanaendelea kusota kufuatilia na kusubiri mafao yao. Hawa wamekuwa kero kubwa kwa Wabunge na Madiwani kwa kuwa fuata fuata hukumbushia malipo yao. Wafuataao wachache walnikaba koti Jimboni jana Jumapili, tarehe 24 Agosti, 2008 walikumbushia malipo yao.

| Jina | Cheque No | Status |
|---------------------|-----------|--------------------------|
| 1. Idi Hatibu | 801890 | Hajawahi kulipwa |
| 2. Shaban Miraji | 658226 | " |
| 3. Issa Kisaka | 762009 | Anasubiri malipo ya pili |
| 4. Anthony Igonja | 664257 | " |
| 5. Shaban Ilonga | 762938 | " |
| 6. Abdalah Uledi | 742070 | " |
| 7. Jumanne Kisaka | 032573 | " |
| 8. Shiawa Makomelo | 658120 | " |
| 9. Sadiki Abdul | 763881 | " |
| 10. Hamisi Saidi | 814373 | " |
| 11. Ramadhani Omari | 762398 | " |
| 12. Mussa Juma | 740084 J | " |
| 13. Juma Katoto | 792246 | " |

Tume ya Umbrich iliainisha malipo ya mafao kwa nchi zote tatu; na Kenya na Uganda ikalipa mara moja mafao hayo kwa wafanyakazi wao. Tanzania haikuwalipa kwa maagizo kwamba, wanaendelea na kazi watawekewa na kulipwa pale watakapostaifu. Wafanyakazi hawa waliingizwa mjini.

Naishauri Serikali iondokane na aibu hii, ikope fedha au iombe ruzuku nchi marafiki kuimaliza kero hii. Hata Uingereza ikielezwa vizuri matatizo yetu, wanawenza kutusaidia kumaliza kero hii.

Ni dhambi kudhulumu. Tuondokane na madaraja ya watu inapofikia suala la kutoa au kutenda haki.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri na Wizara kwa ujumla, kwa hotuba nzuri na yenye kuonyesha mwelekeo mzuri katika mwaka huu wa fedha 2008/09. Ninayo imani ya kwamba, *implementation* ya *plans* zilizopo kwenye hotuba, zitaongeza maendeleo ambayo yatakuwa majibu ya utekelezaji wa Ilani yetu na kukidhi malengo ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, katika hobuta hii, ninayo mambo machache sana ya kuwasilisha.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza ni lile la Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). Naipongeza kwa dhati mamlaka hii, kwa kazi nzuri inayofanya ya ukusanyaji wa juu wa mapato.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri ya kwamba, mfumo na taratibu za ukusanyaji kodi zimeboreshwa na mamlaka hii na hivi leo tunajivunia ukusanyaji mzuri wa mapato yatokanayo na kodi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudhi hizi za mamlaka hii ni lazima Wizara ijjitahidi katika kubuni mipango bora ya matumizi katika Wizara zetu, ambapo kwa sasa imeonekana Wizara nyingi zina matumizi yasiyo ya msingi mfano: Bei zilizolingana na ununuzi wa magari makubwa (*Landcruisers*) na idadi kubwa ya magari haya kwenye mawizara; Gharama za matengenezo zisizolingana ambapo Wizara nyingine zimeongezeka kuwa na gharama za juu sana za matengenezo ya magari haya; Ubabilishwaji wa samani za maofisi na zile za majumbani za mara kwa mara ambazo hununuliwa ghali sana; Wizara nyingi zimegundulika mara magari yanaponunuliwa huvisiwa *seatcovers* mpya, jambo ambalo si la lazima kwani magari haya hutoka Japan yakiwa na *leather seat covers* ambazo ni *original*; hivyo ununuzi wa zile feki ambapo pengine hununuliwa *two pairs* kitu ambacho ni upotezaji tu wa pesa; na ununuzi wa *Tracksuit* kwenye sherehe kama za Mwenge na nyinginezo ni matumizi mabaya ya fedha.

Mheshimiwa Spika, ipo mifano mingi sana ya matumizi mabaya ya fedha, hapo juu ni mifano michache tu hivyo ni muhimu kudhibiti matumizi haya mabovu ili kazi nzuri ya mamlaka hii, jasho kubwa la mamlaka hii lielekezwe zaidi kwenye maendeleo na si vitu *luxury*.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie suala zima la *seminars/workshops* ambazo pia zimeonekana ni njia mojawapo ya utozaji wa fedha kwenye mawizara yetu.

Mheshimiwa Spika, naelewa umuhimu wa *seminars/workshops*, lakini nazo zikizidi sana kama hali ilivyo sasa kwenye mawizara mengi, inaleta upoteaji mkubwa wa mapato ya Serikali na matumizi makubwa ya fedha za walipa kodi. Namwombwa Waziri atueleze ana mikakati gani ya kuboresha hali hii kwenye mawizara yetu?

Mheshimiwa Spika, suala la mikopo bado ni kitendawili kwa mabenki yetu. Hivi ni wapi watu wenye kipato kama cha Watanzania wameendelea bila ya mikopo? Kwa sasa upatikanaji wa mikopo ni sawa na kupata almasi kwenye machimbo ya dhahabu. Hali imekuwa mbaya zaidi na ya kulalamikiwa na Watanzania wengi kwa Benki ya CRDB, ambapo benki hii inasemekana ni benki inayojali wateja wakubwa tu hasa wenye asili ya Kihindi/Kiasia.

Mheshimiwa Spika, benki hii ni moja ya benki zilizopewa dhamana na Serikali kwa ajili ya kukopesha wajasiriamali wadogowadogo, lakini malalamiko ni mengi sana kwa Watanzania wajasiriamali waliojaribu kutaka kukopa katika benki hii.

Mheshimiwa Spika, namwombwa Waziri atoe tamko juu ya benki hii, kutokana na kujielekeza sana kwa wafanyabiashara wenye asili ya Kiasia na si Watanzania Wazalendo.

Mheshimiwa Spika, yangu ni hayo machache, naomba kuwasilisha.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kuupongeza uamuzi wa Serikali kuunda Tume ya Mipango. Hii

itakuwa *think tank* ya nchi hii, kwani naamini katika maeneo ambayo Serikali imeonyesha udhaifu miaka yote hii ya kujitawala ni eneo la Mipango (*Planning*).

Naamini tuna wataalam wengi sana, ambao ni wasomi wazuri katika kila fani hapa nchini.

Napenda vile vile kuamini kuwa, Tume ya Mipango nzuri ni ile itakayosheheni wataalam wazuri, waliobobeia katika sekta mbalimbali (*Intergrated Planning Team*). Hata hivyo, napenda kukumbusha kuwa, tuna Sheria ya Mazingira ya 2004, inayotawala sheria nyingine zote. Katika sheria hiyo, Serikali inasisitiza kuwa, sheria, mipango na mikakati yote, sharti ifanyiwe Tathmini ya Kimkakati ya Athari za Mazingira (*SEA*). Ili tathmini hizi zizingatiwe wakati wa utayarishaji wa mipango ya nchi ni busara wataalam wa mazingira (hususan *SEA*) wajumuishwe katika Tume hiyo ya Mipango. Kwa hiyo, nashauri Tume ya Mipango ijumuise wataalam waliobobeia kwenye masuala ya Mazingira hususan *SEA*.

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Spika, huko tunakotaka kuelekea kwa maisha bora kwa kila Mtanzania, hatuwezi kufika kama matumizi ya Serikali hayatadhibitiwa na misamaha ya kodi kutazamwa upya.

Lazima kuwe na nidhamu katika matumizi ya fedha za Serikali. Maeneo ya kubana ni yafuatayo:-

(i) Manunuzi ya magari ya kifahari ya Serikali. Hatuwatendei haki Watanzania, wengine wanakula mlo mmoja kwa siku, lakini tunatumia mapesa mengi kununua magari ya kifahari. Magari haya pamoja na kuwa ni ghali sana, lakini pia vipuri ni ghali pia na mafuta ni ghali sana. Naomba Wizara iweaonee huruma Watanzania na kwa kurekebisha tatizo hili. Magari yanunuliwe kwa jumla ili bei yake iwe nzuri kama wanavyofanya Umoja wa Mataifa.

(ii) Eneo lingine ni manunuzi ya fanicha. Nashauri Wizara ipige marufuku Serikali kununua fenicha za Serikali nje. Tuna uwezo wa kutengeneza hapa nchini na kuongeza ajira. Hivi kweli kama tunataka kujitegemea karne hii, tunashindwa kutengeneza fenicha hadi tupeleke fedha za walipa kodi nje ya nchi?

(iii) Lingine ni misamaha ya kodi, naomba suala hili lizingatiwe.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani Serikali iliamua kununua ndege mpya ya Rais mwaka 2005 kwa sababu iliyopo imechakaa na inaweza kuhatarisha usalama wa Rais. Bahati mbaya ndege iliyonunuliwa ni ya anasa sana na inabeba watu 12 tu, wakati huo huo msafara wa Rais *minimum* ni watu 18. Hii ndege mpya sasa hivi imekaa tu na Mheshimiwa Rais bado anatumia ndege ya zamani. Nashauri ndege hii mpya iuzwe kwa matajiri na fedha itakayopatikana inunue ndege ya kumfaa Rais.

MHE. STEPHEN J. GALINOMA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Waziri, Manaibu wake, Katibu Mkuu na timu yao yote, hususan *TRA* na Kamishna Mkuu, kwa kazi nzuri ya mwaka uliokwisha na hotuba ya bajeti ya mwaka mpya.

Pili, pingamizi kubwa la *D by D* ni utaratibu wa *Cash Budget*. Ikizingatiwa kwamba, 70% ya *budget* mwaka huu imelengwa mikoani na ikizingatiwa kwamba, upelekaji fedha kwa kususua unaathiri kwa kiwango cha kutisha utekelezaji wa miradi. Mara nyingi fedha hufika mwishoni mwa mwaka wa fedha. Matokeo yake ni ucheleweshaji maendeleo kwa sababu mara nyingi miradi hucheleva na watekelezaji hukaa bure hadi fedha zipatikanapo.

Ninashauri turudie utaratibu wa zamani wa *Warrant of Funds* au mfumo wowote utakaowezesha Mikoa na Wilaya kupata fedha kwa wakati.

Tatu, mara kadhaa nimelalamikia ushiriki wa kubahatisha wa Wabunge, Kata na Vijiji katika mchakato mzima wa kufanya bajeti kwa sababu ya kutolewa *ceilings* mapema kabla ya vikao mbalimbali; na *lack of synchronization* ya ratiba za vikao katika ngazi mbalimbali.

Kumekuwa na jitihada ya kuelekeza vikao viwe *sychronised* na mwaka juzi Serikali za Mitaa zimeingizwa katika mikataba na Serikali Kuu, lakini usimamizi wa maelekezo hayo ni sawa na hakuna. Nashauri kama ifuatavyo:-

(i) *Budgetary Ceilings* zitolewe mapema baada ya kuzingatia mipango toka Wilayani/Mikoani.

(ii) Serikali ichukue hatua za dhati ili kuhakikisha kwamba, Wabunge, Kata na Vijiji wanashirikishwa kikamilifu katika mchakato wote wa *budgeting*. Ikumbukwe kuwa, bajeti ni mchakato wa kupangilia fedha katika mipango na siyo kama sasa kwamba ni kugawana tu kila kinachopatikana.

(iii) Ingefaa Waziri athibitishe kama Mikataba ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ina tija yoyote kama siyo kuongeza urasimu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii lakini naomba hoja hizi chache zijibiwe au zitekelezwe. Nawatachia kila la kheri.

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. Pamoja na pongozi hizi, nina maoni machache yafuatayo:-

Kutokana na wananchi wengi wa kipato cha chini kutoweza kumudu kukopa katika benki nyingi za biashara hapa nchini, kutokana na benki hizo kuijidesha kibiashara, ingefaa sasa uanzishwe utaratibu wa kuanzisha benki ya ushirika kwa kila mkoa na hatimaye benki hizo za kila mkoa zianzishe Benki ya Ushirika ya Taifa. Benki hii itakuwa mkombozi kwa wananchi wafanyabishara wadogo wadogo na wakulima wa

matunda, mbogamboga na mazao ya muda mfupi. Benki hii pia itasaidia sana kuongeza ajira kwa vijana wetu.

Naipongeza Serikali kwa kuonyesha kwa dhati, nia ya kuanzisha Benki ya Kilimo. Hii pia itasaidia kuongeza ari kwa wakulima kulima mazao mengi ya biashara na chakula kutokana na riba kuwa ndogo na muda wa marejesho uzingatie mavuno ya mazao husika na pia upatikanaji wa mitambo uliosaidia sana kurahisisha kilimo kuwa cha kisasa na chenye tija.

Kitengo kinachohusika na utoaji wa udhamini wa Serikali (*Government Guarantee*) katika Wizara ya Fedha kujaribu kufuatilia kwa ukaribu masuala muhimu yahayohusu maslahi ya umma. Mfano katika ufuatiliaji wa GG ya Jengo la Machinga, *Business Park* ilichukua miezi minane; hali hiyo inachelewesha miradi mingi kuanza na pia bei ya vifaa vya ujenzi kupanda mara kwa mara, hali ambayo husababisha gharama kuwa kubwa sana. Tatizo kubwa ni kutokuwa na maamuzi ya haraka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. GODFRED W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua nafasi hii, kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara, hasa wale waliohusika na maandalizi ya bajeti hii na hatimaye kuiwasilisha vizuri mbele ya Bunge lako Tukufu. Pili, napenda sasa nichangie mambo machache yanayohusiana na Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shamba Na. 208 (*NAFCO*) Magamba, lenye ukubwa wa ekari 12,051 ambalo liko Wilayani Mbozi, lilisimamisha shughuli za uzalishaji mahindi mwanzoni mwa miaka ya 1990. Mnamo mwaka 1996, shamba hilo liliwekwa chini ya *PSRC* (lilikuwa *specified*) ili libinafsishwe. Hadi *PSRC* inamaliza muda wake, shamba hili lilikuwa bado halijabinafsishwa, miaka takriban 12 sasa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Ubunge wangu, nimekuwa nikiiomba sana Serikali, iliuze shamba hilo kwa Wananchi wa Mbozi kupitia Halmashauri yao, lakini Serikali imekuwa ikitoa majibu ya kukatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, Waziri ya Fedha na Uchumi, alipokuwa anawasilisha Bajeti ya Serikali hapo tarehe 12 Juni, 2008 alisema katika ukurasa wa 51 nanukuu: “Hatta muhimu kuliko zote ni kutumia ongezeko la bei ya chakula duniani, kama fursa ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula hapa nchini, kwa kuhimiza kuwekeza katika mashamba makubwa na kuhimiza wananchi walime chakula kwa wingi ili kujipatia chakula na kipato.”

Mheshimiwa Spika, nashawishika kusema, kama kweli Serikali ingedhamiria kufanya hilo, kwa vyovyyote vile Shamba hilo lingekuwa limebinafsishwa muda/siku nyingi sana. Bahati mbaya tunasema na kuandika mambo ambayo hatuwezi kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Waziri awaeleze wana-Mbozi, je, nini kigugumizi cha kulibinafsisha shamba hilo? Je, sasa ni wakati muafaka shamba hili likauziwa Wananchi wa Mbozi kuititia Halmashauri yao ili waweze kuliendeleza kwa madhumuni ya nukuu niliyoifanya hapo juu?

Mheshimiwa Spika, moja ya shabaha ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005 ni kuona kwamba, kila Mtanzania anapata maisha bora. Moja ya njia ya kuwawezesha Watanzania wengi kushiriki vyema kwenye shughuli zao mbalimbali za kiuchumi ni kupata mikopo kutoka kwenye vyombo mbalimbali nya kibenki. Hata hivyo, inasikitisha kuona kwamba, riba za mikopo kutoka benki na taasisi nyingine za fedha, siyo rafiki kwa mteja hata kidogo. Kwa mfano, riba zinazotolewa na benki mbalimbali kwenye amana ni ndogo sana, karibu asilimia 2 – 3 wakati riba za mikopo zinazoambatana na masharti magumu (*Stringent Collateral*) ni kubwa sana kati ya asilimia 15 – 30. Hali hii haiwezi kumtoa Mtanzania kwenye umaskini hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa na la kusikitisha ni jinsi ambavyo Serikali imeziachia taasisi binafsi zinazofanya biashara ya fedha, kuiendeshea biashara hiyo kwa uhuru mkubwa wa ajabu kabisa. Mfano wa taasisi hizo ni Bayport *Financial Services*, *Blue Financial Services* na *Ease Money*.

Mheshimiwa Spika, Taasisi hizo zimetoza riba za ajabu sana na huu ni ubepari mkubwa na ubepari ni unyama. Mfumo tuliofikia ni ule wa *man eat man*, uliwhali kuona wapi mtu anakopa shilingi 500,000 anaurudisha mkopo pamoja na riba Sh. 1,600,000; unakopa Sh. 1,000,000 unarejesha Sh. 3,300,000; unakopa Sh. 1,700,000 unarejesha karibu Sh. 5,000,000; huu kama siyo wizi ni nini?

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anieleze mimi na Watanzania kwa ujumla, riba hizo zinaruhusiwa wapi Duniani? Naomba pia ijulikane kwamba, urejeshaji wa mikopo hiyo ni miaka mitatu au chini ya hapo. Nini wajibu wa Serikali katika kusimamia taasisi hizo za kinyonyaji ili zisiwanyonge wananchi? Je, ni riba asilimia ngapi zinazoruhusiwa kutozwa na taasisi hizo, kwa mikopo inayotolewa sasa riba hufikia hadi asilimia 200; huu ni ubepari na wizi mkubwa sana?

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, juu ya hoja hizo, vinginevyo sitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni baadhi ya wafanyabishara Mkoani Mbeya na hususan Wilaya ya Mbozi, wamekuwa wakikataa kupokea sarafu za Sh. 5, 10, 20, 50 na 100 kwa madai kwamba, zimeondolewa kwenye mzunguko. Hali hiyo imesababisha vitu vidogo vidogo ambavyo vilikuwa vikinunuliwa kwa sarafu hizo, sasa viuzwe kwa bei kubwa (*inflation*) ya kujipangia.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe tamko rasmi kuhusu matumizi ya sarafu hizo.

MHE. MUHAMMAD A. CHOMBOH: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wangu katika hoja ya Waziri wa Fedha na Uchumi kama ifuatavyo:-

Katika mchango wangu kwenye Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Muungano, nilisema kwamba, moja kati ya kero zinazotaka kuchukuliwa hatua za dharura ni tatizo kubwa lililoanza hivi karibuni katika Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Nyerere Dar es Salaam, kuwataka au kuwalazimisha wasafiri wanaotoka nje ya Tanzania ambao wanapita kwenda Zanzibar, walipie ushuru wa mali zao hapo hapo Dar es Salaam wakati mwisho wa safari yao ni Zanzibar, ambako kuna ofisi na maafisa kamili wa *TRA*!

Mheshimiwa Spika, jambo hili linawasumbua sana wasafiri kutoka Zanzibar hasa ukizingatia kwamba, wanakuwa hawana pesa za kulipa ushuru wa Forodha mpaka watakapofika kule kwao Zanzibar ambako ndiko kwenye shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Wanafanya kazi nzuri, ambapo wakiendelea na kasi hii, ifikapo mwaka 2010 uchumi wa nchi yetu utakua kwa kasi nzuri na pia maendeleo yatawafikia Watanzania wote hata wale wanaoishi vijijini.

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu hasa wale wanaozalisha mbegu za mafuta wa Mikoa ya Singida, Dodoma, Manyara, Arusha, Iringa, Shinyanga, Tabora, Kigoma, Morogoro na kadhaika, sasa hivi wanafanya kazi nzuri ya kuongeza uzalishaji wa mbegu na hatimaye mafuta na kusambaza hapa nchini na hata nje ya Tanzania. Uzalishaji huu umeongezeka sana, baada ya Serikali kuweka 10% ya mafuta yanayotoka nje. Sasa hivi hakuna Mtanzania anayelia kwamba, kuna upungufu wa mafuta. Mafuta yanatosha tena ya uhakika ambayo hayaleti madhara kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, ulikuwepo kwenye mkutano uliofanyika hapa Dodoma, uliowashirikisha wadau wote wa mafuta Tanzania, wenye viwanda na ninyi Wawakilishi wa Serikali; kwa masikio yako, ulisikia wadau wote walisema ushuru wa 10% urudishwe haraka sana. Wahenga walisema sauti ya wengi ni Sauti ya Mungu. Nashauri Serikali isianzishe msuguano usio na maana na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilisema kwamba, hayo ya kuweka asilimia kumi ni makubaliano ya nchi zote za Afrika Mashariki. Nashauri mfahamu ya kwamba, Serikali iliingia kwenye makubaliano hayo, ilifanya hivyo bila kuwashirikisha wananchi kupitia kwa wawakilishi wao ambao ni Wabunge.

Mheshimiwa Spika, wenye viwanda vya kutengeneza mafuta hakuna wanaoingiza *crude oil*, bali kuleta *semirifined* na kusamehewa kodi kwa bidhaa ambayo si halali hata kwenye kikao tulichofanya Dodoma wenyewe kwa wenyewe walipingana. Kuruhusu mafuta mengi yatoke nje, maana yake mtaua soko la wakulima wetu. Mafuta yanayotoka nje yanauzwa kwa bei ndogo sana na haileleweki yanatengenezwa na malighafi ipi.

Tumeacha kutumia Kimbo, Cowboy na kadhalika, tunataka tutumie mafuta ya alizeti, mawese, pamba, karanga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu mpendwa, kwa uamuzi mzuri alioufanya wa kupeleka fedha za *EPA* kwenye Benki yetu ya Rasilimali (*TIB*), kwa kuwasaidia wakulima wa nchi hii wapate mikopo yenye riba nafuu. Ungozi wa *TIB* uifanya kazi hii kwa uaminifu mkubwa ili wananchi wengi wapate mikopo kwa ajili ya kuendeleza kilimo na hatimaye kukuza vipato vyao na pia kuongeza ukuaji wa Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, nirudie kukupongeza wewe, kwa usimamizi wako mahiri na pia niwapongeza sana Wafanyakazi wa *TRA*, chini ya Uongozi wa Bwana Kitillya na Bwana Lauwo, kwa kazi nzuri wanayoifanya kuongeza mapato kwa faida ya nchi hii. Nawaomba waongweze jitihada zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba misaada yote ya kodi ifufuliwe maana Serikali inapoteza fedha nyingi sana kwa kupitia misamaha ya kodi. Naomba walipa kodi wengi zaidi wasajiliwe na kodi kwa wafanyabiashara wa kat iipunguzwe ili wasiendelee kukwepa bali walipie kwa hiari yao.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kupitia *TRA*, ianze kukusanya kodi kwa ajili ya Halmashauri zetu za Wilaya. Naomba hili liende kwa Halmashauri zote. Naunga mkono hoja

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa suala la wastaafu wa *EAC* limeendelea kuleta utata na kwa kuwa majibu tofauti yameendelea kutolewa hapa Bungeni na hata nje ya Bunge, kwa nini Serikali inaendelea kulipotosha suala hili? Hakuna ubishi kuwa baadhi ya wastaafu walilipwa. Swali ambalo nataka leo Waziri ajibu bila kigugumizi, ni kwa nini wamelipwa tu jumla ya shilingi bilioni 117 kati ya shilingi bilioni 450 zilizoahidiwa na kutamkwa ndani ya Bunge hili kuwa kiwango hicho kitalipwa kwa awamu?

Serikali iko tayari kutoa hapa Bungeni “*deed*” iliyosainiwa kati ya wastaafu, jambo ambalo sasa ndio msingi wa mabishano? Lakini wazee wetu wanaendelea kupata adha, kufa na kuhangaika kupiga kambi Ikulu, Hazina na sasa hata kwenda kutafuta haki zao kwa Balozi za nje jambo ambalo ni aibu kwa Taifa letu.

Iwapo Serikali haikuwa tayari kutoa taarifa kamili Bungeni na kutoa nyaraka zote husika ili Wabunge wajiridhishe, Serikali iko tayari kuunda kamati ya Serikali, ikishirikisha Wabunge kuchunguza kiini cha matatizo na kupata ufumbuzi wa kudumu wa wazee wetu hawa au mpaka iundwe Kamati Teule ya Bunge?

Je, ni fedha kiasi gani, baada ya *EAC* kuvunjika zililipwa na Serikali ya Uingereza kwa ajili ya Kenya, Uganda na Tanzania na ziliwu *pound* za Uingereza ngapi kwa kila

nchi na wakati Kenya na Uganda walilipa wastaaafu wao mara moja, kwa nini Tanzania ilishindwa kuwalipa wastaaafu wake hadi miaka 30 au zaidi baada ya kustaaafu?

Mheshimiwa Spika, kipindi chote hicho, fedha hizo za wastaaafu zilizolipwa na Serikali ya Uingereza zilikuwa wapi na zikifanya nini, kwa kipindi chote hicho? Fedha hizo zilizaa *interest* ya kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, Kenya na Uganda walilipa wastaaafu wao kwa dolla za Marekani au kiwango cha dolla kwa siku ya malipo. Tanzania ilipatwa na shida gani kutolipa kama wenzao wa Kenya na Uganda kama ilivyokuwa imependekezwa na kukubalika kutokana na Ripoti ya “*Umbricht*”?

Mheshimiwa Spika, nisipopata majibu ya kuridhisha, natoa taarifa kwa mujibu wa kanuni kuomba kuunda Kamati Teule ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, wizara hii ni nyeti sana kwa maendeleo ya nchi kwani fedha ndio msingi wa maendeleo na ndio maana kwa nchi zinazotumia fedha zake kwa utaratibu mzuri, basi na uchumi hukua vizuri. Wizara hii ndio yenye chombo cha kukusanya mapato *TRA*. *TRA* imefanya kazi kubwa sana ya kukusanya mapato ambayo ndiyo nguzo kuu ya maendeleo ya wananchi wetu. Pamoja na ukusanyaji mzuri wa *TRA* bado Serikali ina jukumu la kuona ni jinsi gani ya kutumia fedha hizo vizuri. Kamwe isiwe kutumia vibaya fedha kwa kisingizio cha mapato makubwa pamoja na *TRA*, bado tuna *BOT* ambayo kazi yake kubwa ni kuhakikisha inasimamia uchumi wa nchi kwa kudhibiti na kuratibu hasa mfumko wa bei na kulinda thamani ya fedha yetu.

Ni vyema benki kuu ifanye kazi ya ziada katika kuhakikisha fedha yetu haishuki mara kwa mara. Mwaka jana tulihoji matumizi mabovu ya fedha zilizotumika katika ujenzi wa majengo pacha ya benki kuu kwani ilionekana wazi kuwa gharama zake ni kubwa sana. Bado naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwanini gharama zilipanda kiasi hicho na kwa manufaa ya nani?

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Manunuzi cha Serikali kina umuhimu mkubwa sana kwani zaidi ya asilimia 75 ya fedha katika bajeti huishia katika manunuzi na hivyo ni muhimu sana fedha hizi au manunuzi hayo yafanywe kwa umakini na utaratibu na utaalamu wa hali ya juu. Pamoja na sheria ya manunuzi, bado baadhi ya maafisa wamekuwa wakinunua vifaa bila kufuata utaratibu hususan katika Halmashauri zetu. Lakini hata katika Serikali kuu tumeshuhudia Wizara zikiagiza magari katika kampuni moja kwa wakala tofauti na hii imeliongezea Taifa hasara. Ni ukweli wa wazi kwamba kama Wizara fulani inaagiza *Toyota GX 10*, kwa nini isishirikiane na Wizara nyingine zinazoagiza aina hiyo ya magari na kuagiza kwa pamoja ili kupata punguzo? Lakini pia kama Waziri ana *VX* ni kwanini Manaibu wawe pia na *VX* na sio *GX* au *Prado*? Ni ajabu kuona hakuna *Uniformity* katika Serikali kuu. Tofauti ya gharama za *VX* na *GX* ni zaidi

ya shilingi milioni 30. Hivyo ni lazima Serikali ione ni jinsi gani inaweza kutumia fedha kwa utaratibu mzuri na siku zote tuangalie (*value for money*).

National Microfinance Bank (NMB), napenda kuipongeza sana *bank* hii kwa mafanikio yake. Lakini kubwa ni uuzaji wake wa hisa kwa wananchi. Hii ni hatua nzuri ya kuletea wananchi maendeleo. Hisa imekuwa hatua nzuri sana ya kumkomboa Mtanzania. Lakini nadhani muda wa ununuzi ni mfupi sana. Nadhani muda uongezwe ili wengi waweze kununua hisa nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu deni la Taifa, ni wazi kwamba nchi nyingi huwa zina madeni, lakini inategemea mifumo ya fedha/*budget* ya nchi husika. Mfumo wetu wa bajeti ni *cash budget*. Lakini cha ajabu tuna deni la Sh. 1,832,420,666,865/= kama deni la ndani. Hii inahitaji maelezo ya kina, kwani mimi kwa uelewa wangu *cash budget* maana yake ni kutumia kile ulichonacho, kilicho ndani ya bajeti. Sasa deni linatoka wapi? Au nielimishwe maana ya *Cash budget* na faida au hasara zake.

Mheshimiwa Spika, nimeshtushwa sana na maelezo ya Kambi ya Upinzani kwamba *BoT* imetumia shilingi milioni 551 kwa ajili ya ununuzi wa picha za Marehemu Daudi Balali ili ziwekwe katika benki hiyo. Swali la kujiuliza, kwanini awekwe ukutani wakati hata utumishi wake una ukomo? Yaani ultengeliwa kwa sababu ya ubadhifuru! Je, picha za magavana wengine waliopita akiwemo, Edwin Mtey, Charles Nyirabu, Rutahinda, Idrisa zimetundikwa? Thamani zake ni kiasi gani? Au Daud Balaki ana historia ipi kwa *BoT*? pamoja na kumuenzi, lakini kama kweli fedha zilizotumika kununua picha yake ni shilingi milioni 551 huu ni ufisadi kwa maana na tafsiri yoyote ile.

Mwisho, nawatakia kila la kheri katika kuhakikisha matumizi bora ya fedha zetu ili wananchi wapate maendeleo na hivyo dhana ya maisha bora kwa kila Mtanzania ione kane wazi.

MHE. AMEIR ALI AMEIR: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uzima na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu kwa kazi nzuri ya kusimamia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapongeza watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao na Wakuu wao kwa kufanikisha hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa wakati, hotuba ambayo imetoa ufanuzi mzuri na dira ya maendeleo na utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2005 – 2010. Nina mchango mdogo sana unaohusu mabenki.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeruhusu mabenki mengi ili kuondoa msongamano kwa wananchi na wananchi wamekuwa huru kuchagua wapi akajiwekee akiba yake. Hili ni jambo zuri na linafaa kupongezwa na halina budi kuungwa mkono kwa wananchi kutumia fursa hii kwa kuweka fedha zao badala ya kuziweka sehemu sizizo salama. Mabenki nayo yanafanya kazi hiyo kwa ushindani kwa kutoa vishawishi

na vivutio vingi ili kumrahisishia mteja kupata huduma kwa urahisi na kumsevu pamoja na kuwapatia mkopo.

Mheshimiwa Spika, panapo mazuri na mabaya hayakosi. Mabenki yametoea *ATM Card* pamoja na *Visa Card* kwa nia nzuri tu ya kupunguzia wateja wake matatizo. Lakini kumejitokeza matatizo kwa watumiaji wa *Visa Card* wakati wanapotoa fedha katika benki tofauti na fedha zisipatikane na kwenye benki husika inaeleza fedha zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia hilo, mteja anaambwa acae kwa muda wa siku 40 Mabenki yawasiliane. Muda huo ni mrefu sana hasa ukizingatia watu wote hawapo katika hali moja. Wengine wanacho na wengine kile unachomwambia asubiri siku arobaini ndio chote alichonacho. Je, Mheshimiwa Waziri mtu huyo umemsaidia au unamtesa?

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimwa Waziri aliangalie suala hili na kulipatia ufumbuzi wa haraka kwani utaratibu huu haujengi bali unabomoa malengo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mchango huo mdogo naunga mkono hoja hii.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, tofauti za takwimu hili ni tatizo kubwa sana ambalo limejitokeza hasa katika kipindi hiki cha bajeti.

Wakati wa hotuba ya fedha na uchumi Juni 12, 2008 Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema sekta ya maji imetengewa shilingi bilioni 230.6 kwa mwaka 2008/2009 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2007/2008 ambapo sekta ya Maji ilitegewa shilingi bilioni 309.1 baada ya mradi wa Kahama (maji kutoka ziwa *Victoria*) kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kinachoshangaza, Mheshimiwa Waziri wa Maji wakati akiwasilisha hotuba ya bajeti yake, aliomba Bunge lipitishe Sh.156,243,079,700/=. Hapa kuna tofauti kati ya maombi ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na yale ya Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa zaidi ya shilingi bilioni 74. Naomba ufanuzi, kwa nini hali hii imetokea? Iweje tofauti iwe kwa kiasi hicho chote?

Mheshimiwa Spika, naona kuna umuhimu wa Serikali kufanya Ofisi ya *CAG* (Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa taasisi huru na hivyo *CAG* atawezza kutimiza vyema kazi yake kwa uhuru kama vile ilivyo katika nchi wanachama wa *INTOSAI* na *AFROSA – E*. Hivyo Serikali ione umuhimu wa mabadiliko ya baadhi ya vifungu vya katiba yetu ili uhuru huo upatikane.

Mheshimiwa Spika, Mfumuko wa Bei, sasa mfumuko wa bei umefikia asilimia 9.7 hali hii inatisha na yawezekana kabisa hali ikazidi kuwa mbaya. Sababu zinazotolewa za bei ya mafuta kwenye soko la dunia ni sahihi, lakini sio nchi zote zinazozalisha mafuta, lakini mfumko wa bei umedhibitiwa. Wiki mbili zilizopita niliuliza swali lenye ushauri ndani yake kwa Waziri Mkuu kuwa hatuna uwezo wa kupanga au *ku-control* bei ya mafuta lakini tunao uwezo wa kurekebisha sera zetu za kodi hasa

kuziondoa kabisa au kurekebisha sera zinazotoa *tax holiday* kwa wawekezaji wa mahotel, madini na wawekezaji wengine. Inasikitisha mfano Zanzibar ilikusanya shilingi bilioni 20 na kusamehe shilingi bilioni 19.1.

Mheshimiwa Spika, tutakopobadili sera na sheria zinazowapa *tax holiday* wawekezaji pesa inayopatikana itaweza kutumika kama ruzuku kwenye mafuta ili kusaidia wananchi kupunguza ukali wa maisha, kwani maisha nayapanda kutokana na bei ya mafuta kupanda. Serikali iharakishe sheria hizo, ziletwe Bungeni tufanye marekebisho haraka ili nchi ipate mapato zaidi na haya yanayokusanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Public Procurement Act*, sheria hii ni nzuri, lakini yahitaji kufanyiwa marekebisho. Manunuzi bado ni tatizo kwa nchi yetu na ndiyo yanayotawala bajeti yetu. Mimi naona kuna umuhimu wa chombo kusimamia manunuzi ya Serikali kuliko ilivyo sasa kila Wizara kujinunulia magari yake kwa bei na aina ambayo wanaitaka.

Ili kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, Serikali iamue ku-standardise aina ya magari nchi nzima yawe ya aina gani na bei *i-arrange amount* fulani ili kuzuia Wizara kununua magari ya kifahari. Vile vile nashauri mawaziri wakopeshwe magari ya kazi ili waweze kuyatunza. Tuige mfano mzuri wa nchi ya Rwanda, wanatumia mtindo huo wa kuwakopesha magari Mawaziri ili wayatunze. Inashangaza kuona katika nchi yetu ilivyo maskini, Waziri anakopeshwa gari ya Ubunge, bado anapewa gari la Uwaziri ambalo linamilikiwa na Serikali. Haina haja! Hayo ni matumizi mabaya, kwani magari wanayonunua ni ya kifahari sana.

Suala lingine ni samani za maofisini. Hakuna utaratibu mzuri wa manunuzi, wanabadili samani na mapazia ya baadhi ya Wizara na Ofisi za Serikali wanabadilisha kila baada ya mwaka na wengine wanapobadilishwa kutoka Wizara moja kwenda nyingine hutaka wababilishiwe samani, kapeti na pazia kulingana na matakwa yake. Kwa upande wa samani za majumbani za mawaziri, nashauri wawe wanazilipia/wanakopeshwa ili wazitunze. Kitu kikishakuwa cha Serikali/cha umma utunzaji wake unakuwa sio mzuri.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza Serikali iangalie vyanzo vingine vya mapato na vile vile izingatie matumizi bora.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Hali ya uchumi wetu bado sio nzuri sana. Kwa maana hiyo, Serikali lazima ibane matumizi hasa kwenye magari ya kifahari, eg. *GX & Toyota*. Ninafahamu kuwa *GX* za kawaida hazitengenezwi tena, lakini na mashangingi ambayo hata miaka mitano haijatimiza, iweje leo wanapewa *GX8*? Ingeelekeza pesa hizo kwenye huduma nyingine. Serikali sasa itoe dhamana kwa Halmashauri zinazokuwa na uwezo kwenye miradi ya miundombinu.

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake kwa kazi nzuri ya kuandaa mpango wa bajeti ya mwaka 2008/2009.

Wafugaji wamekuwa wakibaguliwa kwa madawa ya mifugo, kudaiwa kulipia asilimia 10 yanapoingizwa nchini. Pembejeo za kilimo hazitozwi chochote na sio vyema kutoza dawa za mifugo kodi ya aina yoyote. Hivyo ninaomba Wizara iondoe hili tozo mapema iwezekanavyo.

Muundo (*structure*) wa bajeti zetu kwa ujumla ina upungufu, kwani gharama za uendeshaji (*recurrent*) ni kubwa kuliko bajeti za Maendeleo (*development*). Napendekeza Wizara iweke mkakati maalum ili kwa siku za usoni *budget structure* ibadilike na hatimaye *development budget* iwe ni kubwa kuliko *recurrent budget*.

Mfumko wa bei (*inflation*) ni tishio kwa manufaa ya Watanzania wengi. Kwa kipindi kirefu mfumko wa bei umeongezeka sana na hii imepunguza sana “*purchasing power*” ya watu wengi wa kawaida. Naomba Wizara ijitahidi kuwa na mkakati maalum wa Kudhibiti *inflation*.

MHE. MARGARETH AGNES MKANGA: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa wahusika wa Wizara kuanzia Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Manaibu Katibu Wakuu, Wakurugenzi wa Wizara na Taasisi zilizoko chini ya Wizara, Wahasibu na kadhalika kwa kazi nzuri wanayofanya kupitia maeleo yaliyomo ndani ya hotuba ya Wizara.

Napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Naipongeza Wizara kwa kuwa siku katika maeneo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge walitoa ushauri kadhaa wakati wakichangia bajeti kuu ya nchi kwa mfano kupitia upya misamaha ya kodi ambayo kwa kweli Serikali inapoteza mapato kwa sababu wasamehewa wengine ni matapeli kwa kutumia taasisi za mifuko tu. Kimsingi, ni muhimu sana kwa Wizara kutoa taarifa za mara kwa mara juu ya utekelezaji huo ili umma ufahamu.

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya *TRA* inajitahidi sana katika kutekeleza majukumu yake lakini kwa kutumia kodi ya mapato kuwa ndiyo chanzo kikuu, kwa kweli wanatoa mapato hayo, wanapunguziwa uwezo wa kifedha sana (wafanyakazi) hivyo napongeza kwa sababu naelezwa kuwa kwa mwaka 2008/2009 *TRA* itapanua wigo wa walipa kodi. Nashauri kodi zipangwe kwa kampuni zinazoshughulikia upambaji katika sherehe na tafrija mbalimbali, mama lishe wakubwa wanaopika kwenye sherehe kubwa kubwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa vile *Twiga Corp. Ltd* ndiyo benki pekee ya Serikali, nashauri kwamba inapaswa sasa kuwa na mkakati wa kujitanua katika Mikoa mingine hatua kwa hatua badala ya kubakia Dar es Salaam tu.

Mheshimiwa Spika, elimu ya kuuza na kununua hisa kwenye soko la Dar es Salaam bado haijawafikia wananchi walio wengi hasa vijijini. Hivyo nashauri mamlaka ya Masoko na Mitaji na Dhamana (*CMSA*) na soko la Hisa la Dar es Salaam wajitahidi

kueneza elimu hiyo hasa vijiji ambako kutokana na mgao wa hisa wananchi wanawea kuendeleza shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika kutambua kwamba shughuli za Bodi ya Michezo ya kubahatisha zinakwenda vizuri na kwa faida. Hata hivyo, ndani ya sheria iliyoanzisha uendeshaji wa michezo “*The Gaming Act*” kuna kipengele kilifafanua wazi kuwa katika faida itakayopatikana zitatumika kuendeleza michezo ya watu wenye ulemavu, kwa msingi huo naomba ufanuzi ni kiasi gani cha fedha kimetumiwa “so far” kwa shughuli za michezo hiyo. Je, ni vigezo gani vimewekwa ili kuweza kupata fedha hizo za kuendeleza michezo ya wenye ulemavu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafao ya wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, bado ni tatizo katika mlolongo wa kushughulikiwa kwake hasa kwa wafanyakazi ambao kwa sasa wamefariki. Wengi wao bado hawajui taratibu za kufuata hasa ikizingatiwa kwa hatua nyingi hizo huanzia na kuishia Dar es Salaam na kwamba huduma hizo hazipo Mikoa mingine. Nashauri kwamba ingawa Serikali zinaeleza kuwa wengi wa wastaafu, hao wamekwishalipwa, lakini wagine bado hawajalipwa na wengine wanalamika kuwa wamepunjwa. Yafaa suala hili limalizike haraka iwezekanavyo, kwa sababu wengi wa wastaafu hao sasa ni wazee ambao hawana uwezo wa kuzalisha mali na kujikimu kimaisha.

Mheshimiwa Spika, napongeza idara ya *TAKWIMU* kwa kuanza utafiti wa idadi, hali zao za kichumi, aina za ulemavu mbalimbali nchini. Ninaamini mwisho wa utafiti huu idadi na kadhalika ya watu wenye ulemavu itafahamika na kuiwezesha Serikali na taasisi zake kupanga raslimali za kutosha na mipango thabiti kwa kundi la jamii ambalo kwa muda mrefu linasahaulika ndani ya jamii.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

MHE. BASIL P. MRAMBA : Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Mipango ivalie njuga suala ya utawala bora wa vyombo vidogo vidogo vya fedha (*small scale financial intermediaries*). Kwa sasa tuna sheria inayomiliki vyombo hivyo na ushirika (*saccos*), hatuna utaratibu wa kumiliki/kusimamia vyombo vya aina hiyo visivyo vya ushirika. Naamini kuwa Wizara ilianza mchakato wa kushughulikia suala hilo tangu mwaka 2004/2005 kwa ushauri wa Benki Kuu. Hadi sasa bado uamuzi haujafanywa. Matokeo tunayoona vijijini na mijini, hasa baada ya wimbi la “mapesa ya JK” yanayolenga ushirika (*SACCOS*) na kuzusha mlipuko mkubwa wa hizo *SACCOS*, ni hatari ya kuikumba sekta hiyo ndogo.

Kwa maoni na uzoefu wangu wa muda mrefu, watu wengi hawapendi ushirika. Baadhi wameingia tu kwa kufaidika na mapesa ya JK, hawana dhamira ya kweli ya kuendeleza ushirika. Wasiopenda ushirika hawana utaratibu mzuri wa kisheria wa kujiandikisha, kujitawala na kusimamiwa. Kwa taasisi hizo (za ushirika au visivyo vya ushirika) hakuna nafasi ya kisheria kwa ulezi au uongozi wa Halmashauri za Wilaya, hasa kwa vikundi visivyo vya ushirika, wala hakuna sheria inayomwongoza Mkurugenzi

mtendaji namna ya kulea na kuingilia kati pale matatizo yanapotokea kama vile wizi, ubadhirifu na kadhalika mionganoni mwa wanachama na viongozi wao.

Naomba wizara ikamilishe mchakato uliokwishaanza, ikibidi ulete Muswada ili Waheshimiwa Wabunge tuamue mwaka huu wa fedha.

MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake na wafanyakazi wote wa Wizara hii na taasisi zake kwa hotuba nzuri sana. Naomba kutoa ushauri na kuomba ufanuzi katika maeneo machache.

Kwanza nashauri Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu aongezewe uwezo wa Wakaguzi kutosheleza hitaji la dharura la kuwa na *Resident Auditor* katika kila Halmashauri ya Mji na Wilaya kusimamia vizuri fedha nyingi za Serikali na michango ya wananchi ngazi ya Wilaya, Kata na Vijiji.

Pili, nashauri Serikali ikubali kwa msingi wa haki na usawa (*equity*) kwamba viwango vya malipo ya pensheni wanayolipwa wastaaful wote wa ngazi ile ile walio hai kwa mfano Makatibu Wakuu viwe *current* kwa maana ya kurekebishwa vilingane kwa wastaaful wote wa ngazi ile ile kwani hali ya sasa inawapendelea wastaaful wa leo na kuwadidimiza waliowatangulia.

Tatu, bei ya mafuta inaathiri sana sekta zote za uchumi wa Taifa letu *negative multiples effect*. Nashauri Serikali ianzishe mchakato wa vyanzo mbadala vya kodi hatimaye tuweze kufuta kodi zote za mafuta kuleta nafuu ya bei ya mafuta kwa manufaa ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FELIX N. KIJKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza mchango wangu huu, naomba kusema kuwa naunga hoja mkono hotuba ya Waziri mwenye dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuunga mkono hoja, napenda kutoa mchango katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu wastaaful. Fedha ya pensheni kwa wataafu ni kidogo mno. Lakini hata hiyo fedha wanaipata baada ya kusota. Utaratibu uliokuwepo ulikuwa ni kulipwa Sh.120,000/= kwa kila baada ya miezi sita. Sasa hivi utaratibu umebadilika, wastaaful wanalipwa kila mwezi shilingi 20,000/=. Ni kwa maana hiyo sasa ingefaa wastaaful waongezwe kidogo kama shukrani kwa kazi nzuri waliyoifanyia nchi hii katika utumishi wao. Mtu kulipwa Sh. 20,000/= kwa mwezi ni kiasi ambacho kinatia uchungu kwa wastaaful wote. Ninaombwa Wizara ipeleke mapendekezo yake Serikalini ili kuwakwamua wastaaful hao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu magari makubwa, miundo mbinu ya barabara hapa nchini bado siyo mizuri hata kidogo. Kutokana na sababu hiyo, ninapingana kabisa na hoja kuwa Serikali ipige marufuku matumizi ya magari makubwa ya aina ya *Land Cruiser* na badala yake yatumike magari madogo. Utendaji wa kuyafikia maeneo waliko wananchi itashindikana. Nchi zinazotumia magari madogo ni zile zenye barabara nzuri na siyo kama Tanzania ilivyo.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba Chuo cha Mipango Dodoma kipewe kipaumbele kwa kukipatia miundo mbinu inayostahili. Chuo hakina usafiri wa kuaminika kwa ajili ya wanachuo. Gari lililopo mara nyingi linakuwa bovu. Aidha hadhi ya mabweni siyo ya kuaminika. Majengo yaimarishwe.

MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS: Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kazi nzuri chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Waziri Mustafa Mkullo na Manaibu wake Mheshimiwa Jeremia na Mheshimiwa Omari Yussuf Mzee kwa ushirikiano mzuri pamoja na watendaji wake wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pensheni au fedha za wastaifu bado zina usumbufu, kwa hiyo, naiomba Serikali kurekebisha vizuri kupitia bajeti hii kusiwe na malalamiko hata ya urithi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji wengi kuwa na marekebisho ya fedha na mambo mengine kuondokana na utumiaji ovyo wa fedha pia kuwajibika kwa nchi yao na kuondoa mabaya yote iwe Serikali inayokwenda na wakati wa awamu ya nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TRA*, hivi kwa nini kusiwe na mpango mzuri? Kwani Zanzibar na Tanzania Bara kuhusu kupokea mapato ya ushuru kunakuwa na usumbufu mwangi, kwa hiyo, ifahamike. Naiomba Serikali irekebishe yale madhara na usumbufu kwa wananchi. *TRA* iwe na mkakati mzuri kwa kupitia mtandao mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba serikali kusimamia benki kutoa mikopo kwa wananchi ili waweze kujikimu katika mambo ya kilimo, biashara, ufugaji na uwekezaji wa mambo mengine katika maisha yao ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumaini hoja hii itaungwa mkono na mimi naiunga mkono hoja ila asilimia za kodi ziangaliwe, zipunguwe kwa wananchi hapa Tanzania. Ahsante.

MHE. HEMED MOHAMED HEMED: Mheshimiwa Spika, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuamka hali nikiwa mzima. “*Allamdullilah!*”! Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake inayoonyesha mwelekeo wa uchumi nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sasa natoa mchango wangu katika hotuba husika. Kwa kuzingatia hali ya uchumi wa nchi yetu Serikali inapaswa kuimarisha sekta ya fedha kwa kuimarisha Benki Kuu ya Tanzania ili kuipa uwezo wa

kusimamia na kuboresha benki na asasi za fedha nchini. Hatua hii itasaidia kushughulikia suala la riba katika mabenki kwa mtazamo wa kupunguza tofauti kubwa baina ya riba za kukopesha na riba ya kukopea.

Mheshimiwa Spika, benki zetu ni vyema ziwatendee haki wananchi wetu. Utashangaa mkopaji benki hulazimika kutoa riba kwa asilimia 12 mpaka 16, lakini ukiweka fedha wewe unapewa riba asilimia mbili mpaka tatu. Sijui kwa nini utaratibu huu ukawa na umbile hili.

Mheshimiwa Spika, wastaafu wetu mara nyingi huingizwa katika dimbwi la unyonge pale mfumko wa bei unavyopanda na kusababisha kupanda kwa gharama za maisha. Kwa kweli viwango vya pensheni vimezidi kuwa vidogo siku hadi siku. Ni vyema Serikali itoe mwelekeo wa maisha ya mfanyakazi awe na mategemeo ya maisha yake pale anapofikia kustaafu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TRA*, chombo hiki kiko chini ya mamlaka ya Serikali ya Muungano katika kukusanya mapato katika nchi yetu. Maumbile ni Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Je, inakuaje chombo hiki kiwe na utofauti wa mpango mzima na wajibu wake, ndani ya nchi moja?

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iandae mpango maalum wa katuondolea malipo yenye utofauti kwa *TRA* ndani ya Serikali zetu mbili.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na manaibu wake. Nasema Ahsante.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi.

Napenda kuzungumzia mafanikio ya mabenki yetu kama *NMB*. Benki hii ni moja kati ya mabenki yanayotoa huduma katika maeneo mengi sana. Matatizo katika baadhi ya Wilaya ambazo hazina mabenki kwenye Wilaya hizo ni shida sana kupata namna ya kufanya shughuli zao kwani kuwa na huduma mbali na Makao Makuu ya Halmashauri ni shida kuu. Naomba Wilaya ya Longido wapatiwe benki ya *NMB* ili watumishi na Halmashauri kwa ujumla wasiende tena Mkoani Arusha.

Jambo lingine kuhusu fedha za mikopo ya JK Wilaya ya Longido hawakupata fedha za mikopo kana kwamba hawako kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Waziri, kitendo kingine ni kucheleta kwa fedha za miradi kwenye Halmashauri, jambo ambalo linaathiri kupanda gharama kutohana na muda wa mradi ulivyopangwa.

Mheshimiwa Waziri katika maeneo ya wafugaji imeshindikana kuwa na shule za kutwa kutohana na makazi yao kuwa mbali na shule ndiyo maana Serikali wameshindwa kuacha shule hizo bila ya kuwa na mabweni. Naomba shule hizo wapewe fedha za chakula ili wanafunzi waweze kusoma kwenye shule hizo.

Napenda kuipongeza *TRA* kwa makusanyo mazuri sana ambayo ndiyo mafanikio ya miradi mingi na maendeleo ya kujivunia yameonekana kwa ajili yao. Napenda kuipongeza *TRA* Mkoani Arusha kwa ajili ya kuandaa mazingira mazuri ya uelewano na wananchi ambao wanalipa kodi bila uwoga. Uhusiano wa watumishi wa *TRA* na wafanyabiashara Arusha ni nzuri tofauti na miaka mingine.

Mwisho, naiomba Wizara wanapotoa fedha za Halmashauri ya Longido wasipeleke tena Halmashauri ya Monduli. Wakumbuke kwamba Wilaya zimegawanywa. Nawaomba sana kwani kutuma fedha Monduli ni kuchelewesha maendeleo ya Halmashauri ya Longido. Naomba mkumbuke kwamba kuna Halmashauri mpya, wanahitaji huruma na kupewa bajeti yao mapema.

Mheshimiwa Spika, nategemea hayo niliyoyasema yatazingatiwa. Naunga mkono hoja.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia Ofisi ya Msajili wa Hazina. Nikiwa mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, ninafanya kazi kwa karibu sana na ofisi ya *TR*. Mimi nimesoma sheria ya *TR*. Ofisi hii yapaswa kuwa *Corporation Sole*. *TR Office* yapaswa kuwa ni chombo kama wakala wa Serikali ili kiweze kuendesha mashirika na pia kusimamia mitaji na hisa za Serikali katika mashirika kadhaa. Hivi, iko Serikali imewekeza *TR* 4.4 trillioni. (\$4.4bn) katika mashirika mbalimbali. Ofisi ya *TR* yapaswa kuwezeshe na kujengewa uwezo ili kufanya kazi hii ya kusimamia mali za Watanzania. Mawaziri wanateua Bodi za Wakurugenzi bila kushauriana na Msajili wa Hazina, wateule hawajali *CV* wala uwezo. Matokeo yake Wajumbe wa Bodi wanahudhuria vikao kwa ajili ya posho tu za vikao. Ninalaani tabia hii. Ofisi ya Msajili wa Hazina ndio tunaipa jukumu la kuangalia mali zetu katika mashirika, ndio mratibu wa mashirika, lazima apewe nguvu zinazostahili. Ninapenda kupata “*timeline*” ni lini Serikali italeta Muswada wa marekebisho ya sheria ya “*Treasury Registrar*”? Suala hili ni la muhimu sana. Tunataka sheria bora ya *Treasury Registrar*.

Kuhusu Soko la Hisa, Serikali ina mashirika mbali mbali ambayo inamiliki hisa. Mashirika mengine yanapata faida inayoridhisha, sina sababu yoyote kama Mtanzania kuelezea ni kwa nini Serikali inashindwa kuongeza “*Capitalisation*” katika soko la hisa. Soko la hisa ni kipimo kimojawapo cha ukuaji wa uchumi au kuporomoka kwa uchumi. Ni vyema kuwe na wakati maalum “*fast track*” kuhakikisha kuwa soko la hisa la Dar es Salaam linapata makampuni mengi. Tujiwekee lengo kwamba ifikapo mwaka 2010 tuwe na makampuni japo 20 katika *DSE*. Nitawasaidia katika hili kwa kuanzia hebu tuhakikishe hisa kadhaa katika mashirika ya Serikali zinaorodheshwa katika soko la hisa.

(1) *Zain (Celtel)* - Serikali iwe na hisa zake 25% kwa wananchi;

(2) *Twiga Bankcorp* – Asilimia 45%;

(3) *Tanzania Standard (TSN)*;

(4) NBC;

(5) CRDB (hisa 30% zilizokuwa DANIDA, 10% wabaki nazo na 20% ziuzwe kwa wananchi kupitia DSE;

(6) ATC, utaratibu ufanyike ili ATCL iwe katika ‘*alternative market*’ na baadae wawe ‘fully’ katika soko; na

(7) Kilombero Sugar 25% za Serikali zifanyiwe utaratibu kuuzwa katika soko la hisa.

Makampuni binafsi yahamasishwe kujisajili katika soko la hisa ili kuongeza makampuni, ‘*Standard Charter some mining companies IPP Media VODACOM, TIGO*’, na kadhalika, hawa wote wahamasishwe ili soko letu la DSE liwe ni chachu ya kupima uchumi wetu.

Napongeza sana uanzishwaji wa *Enterprise Growth Market (EGM)*, itasaidia sana makampuni mengi ya Watanzania kuingia katika ‘*formal economy*’ na kupata mitaji ya kuendesha shughuli zao. Hata hivyo, kumekuwa na tatizo la mahusiano ya kiutendaji kati ya CMSA na DSE katika kufanya maamuzi muhimu kuhusu soko la mitaji. Kwa mfano, kuna fedha inatoka Benki Kuu kwa ajili ya utendelezaji wa soko la mitaji, fedha hizi DSE wanapata? Tafadhali naomba kuwe na utaratibu wa kusaidiana kati ya DSE na CMSA.

DSE waliomba nyumba iliyokuwa inatumiwa na BOT, tafadhali naomba DSE wapewe jengo hili kwani duniani kote soko la hisa ndio kioo cha “*corperate governance financial street*” ya Tanzania ipo wapi? Ninaomba Benki Kuu waruhusu jengo hili wapewe DSE.

Hivi sasa Serikali inatunga sheria ili kutenganisha biashara na siasa. Hii maana yake ni kwamba Wabunge hawataruhusiwa kuendesha makampuni wala kukaa kwenye Bodi.

Hii inatokana na “*conflict of interest code*” inayoandaliwa. Maana yake ni kuwa hata Wabunge hawataruhusiwa kuwa katika Bodi za Mashirika kwani sheria haitabagua sekta binafsi peke yake.

Hivyo, ni bora Wabunge wazoe mabadiliko anayoyataka Rais Kikwete ni makubwa sana “*conflict of interest*” sio Wabunge tu wanaomiliki makampuni, hata Wabunge walio Wakurugenzi katika mashirika ya umma. “*This is a fact which the government must insist. Those who wish to be MPs let them be, those who wish to serve in parastatals let them. But not both, it is against “conflict of interest principles”.*

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, Napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Fedha na Uchumi - Mheshimiwa Prof. Mustafa Mkullo, Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi - Mheshimiwa Yusuph Omary

Mzee, Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi - Mheshimiwa Jeremia Sumari, Katibu Mkoo pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye mwelekeo wa kuboresha huduma katika Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu napenda kutamka rasmi kuwa naunga mkono hoja hii na ninawaombea kheri kwa Mwenyezi Mungu ili awape nguvu, afya na mshikamano ili waweze kutekeleza malengo yao barabara.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza sana Serikali kwa kuboresha huduma katika Chuo cha Mipango cha Dodoma pamoja na kuongeza mafunzo kwa kada mbalimbali. Ukweli, taaluma inayotolewa hapo ni nzuri, kwani kila kada wanachuo wanafaulu vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kushauri katika chuo hiki ni Mkoo wa Chuo kukaimu kwa miaka mingi wakati tayari ameonesha uwezo wa juu katika kuongoza chuo hiki cha mipango cha Dodoma. Ninaomba Waziri wakati wa majumuisho alieze Bunge, huyu Kaimu Mkoo wa Chuo hiki lini atateuliwa kuwa Mkoo wa Chuo hicho? Kwani kuendelea kuwa Kaimu ni kumvunja moyo sana.

Mheshimiwa Spika, nadhani Serikali imesikia hoja hii imeongelewa na Wabunge wengi sana. Hii imetokana na umuhimu wa tatizo lenyewe. Hivyo sasa ninaomba Serikali baada ya kusikiliza hoja hii mara nyingi sana ndani ya Bunge hili kupitia maswali ya Wabunge na kupitia hotuba mbalimbali pamoja na michango mingi kupitia hotuba hii, ninaomba Serikali itoe majibu kiwango cha pensheni kima cha chini kitakuwa kiasi gani? Kwani kiwango wanachopata wastaafu ni kidogo sana. Kinaishia kwenye nauli, malazi na chakula wakati wakifuata malipo haya benki kwani wengi wao hukaa vijiji vya mbali sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Wabunge wenzangu ambao wameishauri Serikali kuwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkoo wa fedha za Serikali sasa ajitegemee asiendelee kuwa chini ya Wizara hii ya Fedha na Uchumi kwani kunampunguzia uwezo wa kufanya kazi zake vyema hasa kukagua mahesabu ya Wizara hii kwani atapata uwoga kumkagua mwajiri wake. Hivyo ninategemea Waziri atatoa ufanuzi kwa hoja yangu hii.

Mheshimiwa Spika, ninapongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kuitishia malipo ya wastaafu katika benki jambo ambalo wastaafu wengi wamefurahia, lakini tatizo ambalo nimelibaini ni wastaafu wengi hawana habari kuwa walitakiwa kujaza fomu ili malipo yao yaanze kupitia benki.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali itoe tangazo hili upya hadi vijijini ili wastaafu ambao hawajaingizwa benki wajaze fomu ili wasiendelee kupata usumbufu wa kukosa malipo yao ya pensheni kwani wapo ambao malipo yao hurudi Hazina kwa kutokuwepo akaanti ya mwenye malipo hayo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa *TRA* kukusanya kodi za majengo ni mzuri sana. Hivyo basi, ninaishauri Serikali kuitumia *TRA* kukusanya vyanzo vingine vya mapato vya Halmashauri zetu.

Hii itasaidia kukusanya mapato makubwa ya Halmashauri kwani Halmashauri nygingi hazina wataalam wa kutosha. Vile vile nawapongeza watendaji wa *TRA* kwani kazi wanayofanya ya kukusanya mapato kila mwaka wanavuka lengo. Ninaionba Serikali iendelee kuwapa motisha wenyewe kuwatia moyo.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuamua fedha za *EPA* kuwekwa kwenye benki hii ili fedha hizo sasa waanze kukopeshwa wakulima ambao sasa hivi ni wengi sana ambao wameamua kuwekeza kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali mpango huu uanze mara moja tuachane na maneno kwani kama Mkuu wa Nchi ametoa maelekezo bado nini sasa utekelezaji uanze ili wakulima waweze kukopa kwa lengo la kuimua kilimo ambacho kitaongeza pato la familia zao na taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoshauri juu ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Fedha za Serikali, vile vile hata wakaguzi wa ndani kuajiriwa na Halmashauri ni kuwanyima uhuru wa kufanya kazi zao vyema kwani lazima kutakuwa na hali ya kumlinda mwajiri wake.

Hivyo basi, ni vyema wakaguzi wa ndani wawe chini ya Serikali Kuu ama kuwa chini ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali. Itasaidia sana kuwa huru kukagua mahesabu ya Halmashauri zetu.

MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI: Mheshimiwa Spika, nami naungana na wenzangu kwa kuunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustapha Mkulo na Naibu Mawaziri wake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mengi mazuri yanayofanywa na Wizara ya Fedha kwa kuongeza mapato na naomba Wizara ya Fedha iweke jitihada zaidi katika kusimamia matumizi ya Serikali. Mheshimiwa Waziri, wakati wa majumuisho yako naomba kukukumbusha suala la shamba la Bugwema, lililokuwa linamilikiwa na J.K.T. nilizungumza nawe na nikakupatia vielelezo vyote vya barua husika.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri awape majibu watu wetu wa Mkoa wa Mara wanaolisubiri kwa hamu J.K.T wanasema suala la shamba hilo kibali kimekwama ofisini kwako.

Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kuunga mkono hoja.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuunga mkono hoja na kuipongeza Serikali yetu kwa juhudhi inazozichukua. Pamoja na pongezi hizo nina jambo ambalo ni lazima Wizara, watendaji pamoja na Serikali

liangaliwe kwa upeo wake ili lisije likaleta maafa baadae. Suala la mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ni jambo la kusikitisha sana kwa watendaji kutowajua waliowakopesha, wanaowadai, idadi yao na mengine hili ni jambo la hatari sana.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo inaonekana imeshindwa kabisa kufuatilia fedha hizi kwa kina na badala yake wanasubiri mwanafunzi aliyekopeshwa ama atangazwe anakofanya kazi au wasikie tu kuwa mwanafunzi huyo yuko sehemu fulani ndio wampelekee barua ya madai, hii inaonyesha dhahiri kuwa bodi ya wanafunzi wa elimu ya juu hawafanyi kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna maelezo kuwa hata baadhi ya fomu za wanafunzi waliokopa pia hazijulikani zilipo, huo ni upotevu mkubwa wa fedha. Bodi imeng'ang'ania Dar es Salaam peke yake badala ya kufungua ofisi zao hadi mikoani kwani wanafunzi waliokopa na kuajiriwa wametawanyika Tanzania, wengine wapo hata Zanzibar lakini bodi haina habari.

Mheshimiwa Spika, baya zaidi kuna mtindo unaofanywa na bodi hii ni kule kumkabidhi mtendaji mmoja fedha nyingi kiasi cha shilingi milioni arobaini ili akawakabidhi wanafunzi wanaosoma nje ili waweze kujikimu, huu si mtindo mzuri na ni wa hatari sana, lakini lingine ni lile la kumpelekea fedha nyingi mwanafunzi mmoja kwenye akaunti yake binafsi ili awagawiye wenzie wanaosoma nje, je, wote wawili hawa wakitoweka katika mazingira ya ajabu Wizara itasemaje.

Mheshimiwa Spika, Wizara isisahau kwamba fedha hizi ni za wananchi kupitia mifuko mbalimbali ya wananchi, fedha hizi zisiporejeshwa fedha za wananchi wanaowekeza zitakuwa hatarini. Kwa mfano, Ubalozi wa Tanzania nchini Urusi kiasi cha shilingi 1,023,094,746/= na Ubalozi wa Tanzania nchini India ni shilingi 526,616,352/= .

Mheshimiwa Spika, hii ni afadhali kidogo japokuwa marejesho yake hayajulikani lakini angalau zimepitia katika balozi zetu, lakini kuna fedha wanazopewa watu mkononi tena fedha taslimu. Wizara lazima ichukue hatua madhubuti. Ahsante.

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA: Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mustapha Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi na Naibu Mawaziri wake kwa kazi nzuri wanaoifanya na hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia. Baada ya kuunga mkono hoja napenda kuchangia machache yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunayo mifuko ya pensheni kama vile *NSSF*, *PPF*, mifuko hii inakusanya pesa nyingi ya kuziwekeza katika miradi mingi na kupata fedha nyingi kama faida. Tatizo ni kuwa wafanyakazi wanalipa fedha katika mifuko hii lakini hawapati gawio au faida yoyote. Hii imefanya wastaa fu wengi kupata fedha kidogo sana

wakati wa kustaa fu kuto kana na mfumko wa bei na kupungua thamani kwa shilingi. Mifuko hii inatakiwa kuwapatia *dividend* (gawio) wanao changia mifuko hii kama Mfuko wa Umoja unavyofanya. Lakini mifuko hii inafanya wizi wa wazi wazi. Tunaomba hali hii irekebishiwe.

Mheshimiwa Spika, fedha nyingi hutolewa kwa ajili ya maendeleo. Fedha hizi hupelekwa kwenye Wizara na halmashauri za wilaya na manispaa. Baada ya kuzitumia mkaguzi huenda kukagua wanachokaguliwa ni makaratasi au risiti na sio kazi zilizofanyika. Huu ni mtindo wa karne ya 18 au 19. Kuna haja ya kubadilisha mfumo na mkazo uwe wa kukagua kazi iliyofanyika hii itasaidia kujua kama kazi iliyofanyika inakidhi *value for money*. *Value for money* ndio muhimu na sio kukagua makaratasi ofisini bila kuona kazi gani imefanyika. Badilisha mfumo wa ukaguzi uwe kila miezi sita na sio miaka miwili. Sasa hivi kompyuta zipo huhitaji muda wa miaka miwili kukagua mahesabu.

Mheshimiwa Spika, hii nchi watu wanalipa kodi kikamilifu ni wafanyakazi tu. Watu wengine hawalipi kodi inayotakiwa kwani utaratibu unaotumia ni hafifu. Tunataka watu wajaze *tax return form* hii ndio itafanya wakwepa kodi wabainike na kuchukuliwa hatua za kisheria. Tunaomba mtindo wa kujaza *tax return form*. Makusanyo ya kodi yataongezeka asilimia mia tatu.

Mheshimiwa Spika, Wabunge huitumikia nchi lakini wakinika hapa baada ya miezi sita maisha yao yanaathirika sana. Tunaomba Wabunge wanaotumikia zaidi ya vipindi viwili walipwe pensheni ya 80% ya Mbunge wa wakati huo.

MHE. MWINCHOUM A. MSOMI: Mheshimiwa Spika, kwanza naupongeza uongozi wa Wizara ya Fedha kuanzia Waziri na Naibu Mawaziri kwa uandaaji wao mzuri na wenye ushirikiano bila ya kumsahau Katibu Mkuu na Wakurugenzi pamoja na Makamishna wa Wizara hii kwa jinsi wanavyowasaidia kiutendaji Waziri na Naibu Mawaziri wake kufanikisha utelekezaji na malengo ya Wizara na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo sugu la aliyekuwa mtumishi wa Shirika la Bima Ndugu Simon ambae kwa takriban miaka kumi sasa amesimamishwa kazi kwa kosa ambalo limejibowi kwa maandishi na kwa risiti juu ya fedha ambazo ametumia na kufanya ubadhirifu. Nimelifikisha tatizo hili kwa Waziri wa Fedha ili kulitolea maamuzi ya mwisho na kumnusuru mtumishi huyu na maafa makubwa ya maisha yanayomkabili. Ni vyema likaamuliwa na kujulikana mwisho wake, inavyoonekana kwa mtu au kikundi cha watu kimeamua kumtesa kwa makusudi. Liangalieni kisheria lifikie hatima yake. Mtu huyu amefikisha malalamiko kwangu kwa kuwa ni mpiga kura wangu hivyo naomba lipewe msukumo unaostahili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa taratibu za ujenzi wa daraja la Kigamboni zimeanza, naishauri Wizara ya Fedha kuitumia Kigamboni kiuchumi hasa katika kuwekeza kwenye fukwe kwa kujenga hoteli za kisasa na vile vile ujenzi wa viwanda. Wizara ya Fedha ndio pekee inayoweza kushawishi wawekezaji duniani kuwekeza

nchini. Tuiwahi Kigamboni kujenga kisasa na pia kuliwezesha daraja la Kigamboni kutumika vyema kiuchumi.

Aidha, naiomba Wizara ya Fedha kuzishawishi benki zilizopo nchini kufungua matawi ya benki zao Kigamboni au angalau kwa kuanzia kufungua huduma za *ATM* huku wakijiandaa kwa hatua za kufungua matawi ya benki. Naipongeza Benki ya *NBC* na *Exim Bank* kwa kufungua *ATM* Kigamboni. Benki za *CRDB* na *NMB* zina wateja wengi sana Kigamboni hivyo washawishiwe kufungua kwa haraka huduma za *ATM* Kigamboni na baadae kufungua matawi ya benki zao.

Vile vile tunaomba Wizara kutafuta wawekezaji wa kuweza kujenga viwanda vya kusindika samaki katika fukwe za tarafa ya Kigamboni kwa nia ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka, 2005 – 2010, ambayo katika ukurasa wa 32(d) inasema; “Kuvutia wawekezaji katika kuanzisha viwanda vya kusindika samaki hasa katika ukanda wa mwambao wa Bahari ya Hindi na Visiwa vya Unguja, Pemba, Mafia” (Kigamboni ni mwambao wa bahari ya Hindi pia). Tumeinadi sana kwenye mikutano ya hadhara lishughulikiwe kwa umuhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wote wawili kwa kuwasilisha hotuba yao ya matumizi ya fedha kwa ajili ya kazi zao za kila siku kwa umakini kabisa.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwapongeza Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wataalamu wao wote kwa kushirikiana vizuri na viongozi wao wakuu katika kuhakikisha uwasilishaji wao unakidhi matarajio ya Watanzania walio wengi ili wafaidike na kodi zao wanazotoa kwa kupata maisha bora.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kila siku zinavyoendelea kusonga mbele tujue wastaifu ndipo wanapozidi kuongezeka kwani kila siku zinapoongezeka ujue na umri unapanda kwa hiyo, ongezeko lazima la wastaifu nalo litaongezeka kwa kasi kabisa.

Mheshimiwa Spika, ningewaomba sana viongozi wakuu wa Wizara hii wakabuni mbinu madhubuti kabisa ya kuweza kuwasaidia wastaifu wetu ili wapate malipo yenye kuridhisha kutokana na hali yenye kuridhisha kutokana na hali halisi ya maisha ilivyo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, penye wengi pana mengi, naelewa msukumo wa watu tofauti ni lazima uwe na maelezo tofauti kati ya hayo ni tofauti ya malipo ya kila mwezi na malipo ya miezi sita. Kwa muda huu mchache yalipoanza mabadiliko ya malipo kwa wastaifu manung’unko mengi yameanza kujitokeza kwani walio wengi bado wanapendelea urudi mpango wa miezi sita, kutokana na umbali wa kufuata fedha zao kila mwezi umeongeza kwa kiasi kikubwa gharama za maisha hasa kutokana na kukosa kulipwa fedha za nauli ambazo zinatumika bila ya kupata marejesho katika fedha hizo

hasa ukiangalia suala la kupata fedha ikiwa za mshahara au pensheni ni vizuri zikakufikia ulipo ili uondokane na hasara zisizokuwa za lazima.

Mheshimiwa Spika, baada haya machache napenda niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante naunga mkono.

MHE. SIRAJU J. KABOYANGA: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote katika mashirikiano na taasisi zote chini ya Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri ya utayarishaji wa hotuba hii ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, deni la Serikali, pongezi kwa usimamizi mzuri. Lakini maelezo yaliyo katika ukurasa wa 39 hayatoshi kutoa picha ya hali ya deni la Taifa siku zijazo hususan kwa kukosa maelezo kuhusu ratiba ya utekelezaji wa mpango wa Serikali kuhusu *sovereign bonds*. Ratiba hii ni muhimu kutuwezesha kujua lini na ni kiasi gani kitakachopatikana chini ya utaratibu huu. Aidha, tufahamishwe vile vile miradi inayokusudiwa kutafutiwa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Soko la Hisa la Dar es Salaam (*Dar es Salaam Stock Exchange - DSE*), utekelezaji wa sheria ya kubinafsisha *NMB* unaendelea chini ya ubinafsishaji huu Serikali imeamua kutoa upendeleo wa kipekee kwa wafanyakazi wa Benki hii kwa kuwapa 5% ya hisa zinazouzwa.

Hawa ni wafanyakazi takribani 2000! Na kubakiza 16% ya hisa zinazouzwa kwa Watanzania wengine pamoja na Mashirika kama *NSSF, PPF, LAPF, PSPF* na kadhalika. Hiki ni kiasi kidogo kwa nini Serikali isiwapo wafanyakazi hisa za upendeleo toka kwenye hisa zake zilizosalia za 30%?

Mheshimiwa Spika, ikopo toka kwenye vyombo vyao fedha kwa ajili ya kununulia hisa, katazo la Benki Kuu kuhusu kutokukopa kwenye mabenki kwa ajili ya kununulia hisa benki linahitaji kutazamwa upya. Tukizingatia kwamba sheria ya makampuni inakataza kampuni yoyote kuongeza mtaji wake kwa njia ya kuwakopesha wana hisa wake watarajiwa. Wanahisa kukopa toka sehemu nyingine ili kununua hisa za kampuni inayotaka kuongeza mtaji wake. Kwa mantiki hii, nadhani wananchi wasikope toka mabenki na taasisi nyingine za fedha ili kununua hisa za *NMB*. Naomba Waziri anipe ufanuzi wa katazo hili.

Kuhusu udhibiti wa fedha haramu, naishauri Serikali iongeze kasi ya kujenga uwezo wa kukabiliana na tatizo la fedha haramu. Yaliyotokea katika eneo la *EPA* ni sawa sawa na kengele inayoashiria hatari. Kama Benki Kuu pamoja na kitengo cha hazina cha kudhibiti fedha haramu vingekuwa makini tatizo hili lingeweza kudhibitiwa mapema. Ndiyo maana nasisitiza umuhimu wa kuvijengea uwezo wa rasilimali watu na vitendea kazi taasisi zetu za kupambana na tatizo hili la fedha haramu.

Mheshimiwa Spika, Twiga Benki, naunga mkono hoja ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu haja ya kuongeza mtaji wa benki hii. Lakini nasisitiza kiwango cha mtaji utakaoongezwa uwe kati ya shilingi bilioni 4.0 na shilingi bilioni 5.0 ili kuunusuru

mtaji wa benki hii usiwe chini ya kiwango cha shilingi bilioni 5.0 ikiwa benki hii itapata hasara ya kiwango chochote kutokana na mikopo mibovu iliyotolewa siku za nyuma.

Kuhusu muundo wa Tume ya Mipango, napendekeza muundo wa tume hii urekebishwe kulingana na mfumo wa India na kama pendekazo hili litakubalika, nadhani Mheshimiwa Rais atahitaji kuwa na Waziri wa Nchi Mipango badala ya mfumo wa sasa ambao mmoja wa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Rais waliopo ndiyo wanaomsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, kuhusu pengo la riba, Amana *vs* Mikopo, pengo la riba za amana na mikopo ni kubwa sana. Aidha, riba za amana ziko chini sana na zinapolinganishwa na ukubwa wa mfumuko wa bei nchini, watanza fedha katika amana za mabenki mwisho wa siku wanapata riba hizi! Serikali/Benki Kuu iendelee na juhudzi za kuirekebisha hali hii mbaya.

Mheshimiwa Spika, fedha za barabara ya Manyoni – Tabora – Kigoma, naomba uthibitisho wa Hazina kama shilingi bilioni 10 zilizoahidiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ajili ya barabara hii kama zimekwisha tengwa na kupelekwa Wizara ya Miundombinu.

Kuhusu pensheni za watumishi wa Mashirika ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika, hili ni tatizo kubwa. Wizara ya Fedha itoe kauli thabiti kuhusu mustakabali wa malipo ya wastaafu hawa.

MHE. ESTERINA J. KILASI: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kutika yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kina kazi inayofanywa na *Consolidated Holding Corporation* ni nzuri sana lakini tatizo ni kukwamisha na ugumu wa wadaiwa kutokulipa hisa walizorithiwa kutoka *PSRC, LART* na hata waliobinafsishiwa makampuni/mashirika mbalimbali kutotimiza malipo yao kufuatana na mikataba yao. Kutokana na sababu hizo gharama za uendeshaji zinakuwa kubwa sana kulinganisha na mapato yanayopatikana. Je, Serikali au Wizara imeweka mkakati gani ili kupunguza gharama za *CHC* katika kufuutilia madeni hayo hasa kwa kesi zilizoko mahakamani? Je, katika kesi hizo 236 ni ngapi zimetegemewa kuleta mafanikio?

Kwa kuwa ofisi ya *CAG* imeonyesha umakini wa kazi nzuri katika utendaji wake na kazi kwa sasa, napendekeza kuwa mashirika yote ambayo yanafanya kazi nzuri kwa sasa, taasisi na wakala wa Serikali, ukaguzi wake ufanywe na ofisi hiyo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali badala ya kuwapa au kuteua makampuni binafsi ya ukaguzi ili kuwa na ufuutiliaji wa karibu na utoaji taarifa endelevu.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kuwa na benki akaunti nyingi ni kubwa sana kama Waziri wa Fedha alivyoliona na hii ni kuanzia Serikali Kuu kwa maana ya wizara zote, taasisi na mashirika ya umma na mpaka halmashauri na zingine hazina pesa kabisa zinatumika vinginevyo. Mkakati unaowekwa au kupendekezwa na wizara ni mzuri sana

hasa baada ya kufunga akaunti zote ambazo hazihitajiki. Wasi wasi wangu kwa utaratibu wa kulipa kutumia mtandao Wizara ya Fedha imejipanga vipi kuzuia wizi wa njia ya mtandao usuluhishi wa malipo utakuwaje, uwezekano wa kumlipa asiyehusika tayari kiuaminifu kuruhusu ulipaji wa mtandao huu utumike?

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya mdhibiti na ununuzi wa umma, kazi yao ni nzuri wanatimiza wajibu wao vizuri. Lakini bado elimu inatakiwa kwa wadau mbalimbali, napendekeza ukaguzi ufanyike maeneo yote ili kujuia sheria ya manunuzi inafuatwa. Watendaji wengi hasa kwenye Mashirika ya Umma, Wakurugenzi wa Bodi za Mashirika na taasisi mbalimbali za umma wanaonekana haweko tayari kufuata sheria za fedha na manunuzi? Wengi wamekuwa wakilalamika kuwa sheria inachelewesha utendaji wao hasa kwenye ujenzi mbalimbali, ununuzi wa vifaa mbalimbali, kwa hiyo, elimu inatakiwa na ufuatiliaji wa karibu.

Mheshimiwa Spika, tathimini na uhakiki wa mali za Serikali kasi yake ni ndogo, Mhakiki Mali wa Serikali aongezewe uwezo wa kuweza kuhakiki mali za Serikali katika maeneo mengi kwa mwaka, kwa sasa nguvu zao ni ndogohaziendani na taarifa ya CAG.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya *PPF* iangaliwe upya ikiwa ni pamoja na kuona uwezekano wa kubadili jina la *PPF* kwa sababu jina hili lililenga Mashirika ya Umma tu ambayo hayapo kwa sasa, inajumuisha na taasisi zingine zaidi ya Mashirika ya Umma peke yake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mustapha Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, Waheshimiwa Naibu Mawaziri na wasaidizi wao kwa hotuba nzuri na utendaji wao wa kuridhisha. Nami naiunga mkono hotuba ya Wizara asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, mapato ya ndani ya Serikali yanaonyesha kwamba Serikali iliweka malengo ya kukusanya shilingi bilioni 3,502.58 kati ya hizo mapato yaliyotokana na kodi ni shilingi bilioni 3,189.27 na yasiyo ya kodi ni shilingi bilioni 313.31. Mapato halisi yaliyokusanywa yalikuwa shilingi bilioni 3634.58.

Mheshimiwa Spika, nataka kufahamu, je, tuna wigo mkubwa kiasi gani (*tax base*) au tunayo *potential* kiasi gani ya *tax base* yetu nchini?

Mheshimiwa Spika, mauzo yetu ya nje (*export*) hayaridhishi. Mkakati mmojawapo wa Serikali ni kupunguza thamani ya shilingi yetu. Je, Serikali imewahi kufanya hivyo na imesa diaje katika kukuza mauzo yetu ye nje?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki Kuu, suala la *Twin-Towers* limekuwa likijitokeza mara kwa mara likihojiwa. Naamini kuna wahandisi walibobea katika ujenzi ambao wanaweza kuelezea. *Twin Towers* kuwa aghali kunaweza kutokana na aina ya makusudi na matumizi ya jengo, uimara unahitajika, *materials* zinazotumika kukabiliana

na mazingira fulani kama ya chumvi, mfano *cement* inayoweza kukabiliana na chumvi, inayoimarika upesi chini ya maji (*rapid hardening cement*). Yote haya yanaweza kuwa sababu. Kwa nini Serikali isitoe angalau maelezo ya kina kutoa majibu ya kudumu ili yaishe?

Mheshimiwa Spika, suala la *pensioners* na mirathi ni kero ya kudumu. Wizara ione changamoto hiyo inafikia tamati. Naunga mkono hoja.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, kuhusu misamaha ya kodi, sehemu kubwa ya misamaha ya kodi inayotolewa na Serikali inawanufaisha wafanyabiashara na wawekezaji na huku Serikali ikiendelea kukosa mapato na wananchi kuendelea kukosa huduma muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha, Waziri anasema Serikali itaendelea kuzingatia misamaha hiyo kila leo Wabunge tanalisema hili lakini hakuna utekelezaji. Serikali itaendelea kuzingatia hadi lini? Mbona kila kitu kiko wazi?

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi kwa makampuni ya madini ni aibu tupu. Makubaliano ya mikataba ya kukusanya 0.3% huku 97% ikiachwa kwa wawekezaji hao/makampuni hayo yaendelee kuvuna hivi kweli *are we serious?* Hapa Serikali inaangalia nini?

Mheshimiwa Spika, msamaha wa kodi kwa mahotelii makubwa (kodi ya thamani) ni kuwapa wenye hoteli hizo ulaji tu. Ikiwa wafanyabiashara wadogo wadogo hata wauza chumvi wanalipa kodi tena kwa wakati, na wakichelewa tu wanafuatiliwa hawa wakubwa kwa nini wasilipe kodi?

Kuhusu fedha za *EPA*, wote waliohusika na utoaji wa fedha kutoka kwenye akaunti ya *EPA* ni wezi kama wezi wengine wanaoiba popote. Sheria ile ile ambayo inawabana wezi iwabane wote! Ni kwa nini wezi hawa wa *EPA* wanabembelezwa na kupewa muda walipe? Na wale wote waliorudisha kiasi hicho kidogo kwa sasa wapo wapi? Japo wanarudisha na kukiri waligushi vielelezo wakaiba sheria inasemaje? Ikiwa mwananchi wa kawaida ameiba kitu, anawekwa ndani na analipa akiwa *lock-up*. Hawa kwa nini wanatesa mitaani na wengine ni watumishi wa Serikali bado wapo kwenye kazi yao wanaendelea?

Mheshimiwa Spika, hii inatoa picha kuwa Serikali inaogopa baadhi ya watu, wakubwa wenye pesa hawaguswi. Huu ni udhaifu mkubwa katika uongozi.

Kuhusu *pension* kwa wastaafuli, Serikali ione sasa kutoa kero hii ya malalamiko ya wastaafuli wetu. Ni aibu wazee waliotumikia Taifa hili kwa muda mrefu tena kwa uaminifu mkubwa wanaweka kambi Ikulu kwa sababu ya kufuatilia haki zao. Serikali inajisikiaje inapowaona pale? Tulio mbali tunajisikia vibaya nyie wenzetu mnawaona pale mnaona sawa tu.

Mheshimiwa Spika, pia kiasi cha pensheni hizo ziongezwe ili kuweza kuwasaidia kukidhi mahitaji yao ukizingatia gharama za maisha zimepanda. Ni vizuri Serikali

ikachukua jukumu la kumaliza kero hii ili Wabunge na wananchi waweze kuwa na imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kitengo cha manunuzi ya umma, kati ya maeneo ambayo fedha ya Serikali/fedha ya wananchi inaliwa ni kupidia manunuzi ya umma. Tatizo hili lipo kila mahali, kila Wizara, kila Idara na huko Wilayani ndiyo kabisa hali ni ngumu sana. Ni lini kitengo hiki kitaboreshwa ili kuweza kufanya kazi yake kwa ufanisi na hiyo fedha ya wananchi iweze kufanya kazi ya kusaidia maendeleo yao na siyo kuishia kwenye matumbo/mifuko ya wachache. Sheria za manunuzi zilizopo hazifanyi kazi ipasavyo na mahali pengine hazitumiwi kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezeshaji wa wahasibu wa wilaya. Kwa mfumo tunaotumia hapa kwetu Tanzania *decentration* fedha zaidi ya 80% zinakwenda kwenye wilaya zetu na fedha hizo zinasimamiwa na wahasibu hao. Ikiwa hawatejengewa uwezo wa kutosha na kupewa maadili ya kazi hatutaweza kupiga hatua. Tatizo la kuwahamisha wahasibu wanapotafuna fedha za wananchi (*misuse*) wanatolewa kwenye kituo kimoja wanapelekwa kituo kingine kwa utaratibu wa kuleana, ni kuhujumu fedha za wananchi na kulea matatizo na kuendeleza ufisadi.

MHE. YONO S. KEVELA: Mheshimiwa Spika, kuhusu rasilimali ya nchi, ni vizuri kwa Wizara hii iweze kuyatazama maeneo yaliyo nyuma kimaendeleo kuliko ilivyo sasa maeneo yaliyoendelea bado fedha za miradi ya maendeleo bado yanapelekewa fedha na iangalie idadi ya watu. Maeneo yaliyo nyuma ni kama vile ya Kigoma, Lindi, Mtwara, Rukwa na maeneo mengine ambayo bado hata umeme na barabara zimechelewa kufika.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Njombe Magharibi liko pembezoni, lipo mpakani mwa Mbeya. Fedha za wajasiriamali hasa fedha za mabiloni ya Mheshimiwa Kikwete ziliishia Makambako (Njombe Kaskazini) na Njombe Mjini (Njombe Kusini) nao walipata fedha kidogo. Maeneo ya Illembula (Njombe Magharibi) walikosa kabisa. Ombi langu, tunaomba tupatiwe benki ya *NMB* au *CRDB* sasa tuna kituo kikubwa cha polisi pale Illembula. Wenzetu walipata fedha hizi za Mheshimiwa Kikwete kwa vile kulikuwa na *NMB* na *CRDB* kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni michango ya wananchi iliyopelekwa wilayani haina usimamizi mzuri na yafaa fedha hizi wananchi kuwa na ukaguzi kuliko ilivyo sasa fedha za wananchi zinatumika vibaya na zinaliwa sana na baadhi ya viongozi wa wilaya wasiowaaminifu. Mfano fedha za *harambee* za michango ya elimu kuna malalamiko sana. Hata hivyo wilaya zingine zinafanya vizuri sana juu ya fedha za *harambee*.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, *BOT*. Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze mgao wa faida kwa Serikali ya Jamhuri na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar mwaka uliopita ulikuwa kiasi gani? Ni lini Wizara italeta taarifa ya matumizi mabaya ya ujenzi wa *Twin Tower* kama ilivyoahidiwa hapa Bungeni?

Mheshimiwa Spika, wakala wa mpango *SAP-IMF* iliitaka Serikali, riba kwa mabenki isiwe chini ya *inflation rate* ya wakati huo, je, ni nini sera ya sasa juu ya riba na maelekezo ya *IMF*? Ni lini Wizara italeta Bungeni taarifa kamili ya Meremeta na *Mwadui Gold Co.* na gharama iliyopata Serikali kwa kuzichukulia dhamana kampuni mbalimbali, ambazo hatimae zimeshindwa kulipa?

Mheshimiwa Spika, Wizara inachukua hatua gani ya kuhakikisha kuwa watumishi wa ngazi za juu za *BOT, TRA* zinaonyesha sura ya Kimuungano? Kwa mfano *BOT* hakuna Mkurugenzi hata mmoja kutoka Zanzibar na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliahidi kuipandisha daraja Bandari ya Mkoani Pemba, ahadi ilitolewa miaka mitano iliopita.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ilivoletwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Napenda kuleta mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza fedha za JK au mabillioni ya JK. Napenda kumpongeza Rais kwa kuliona jambo hilo la kuwasaidia wajasiriamali wa nchi hii. Nachukua fursa hii kuipongeza benki ya *CRDB* na *NMB* matawi ya Mbeya kwa ujasiri na ubunifu mkubwa walioufanya katika fedha zile. Kiasi kilichotolewa ni kile kile walichopewa mikoa mingine lakini matawi ya Mbeya yaliamua kuongeza kiasi cha kutoa kutohana na mipango mizuri iliyowekwa ya kuzisimamia fedha hizo. Pia marejesho mazuri yalisaidia benki kuongeza fedha hii katika mzunguko. Si fedha ya ziada toka Serikalini bali ubunifu wa matawi ya Mbeya. Wajasiriamali walikuwa *very positive and aggressive* katika biashara. Pia ikumbukwe kuwa Mbeya, ilikuwa mkoa wa kwanza kuanzisha benki kata na zilifanikiwa sana na zilipokuja asasi kama *SACCOS*, Mbeya ilikutwa imekamilika sana katika miundombinu hiyo ya kifedha. *Motto* ya mkoa wa Mbeya ilikuwa kuachana na *docility* ya aina yoyote katika kuzitumia fursa tunayopewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mbeya wanastahili kupongezwa kwa kufanikisha mpango wa mabilion ya JK.

Mheshimiwa Spika, eneo langu la pili ni kuhusu *Bayport Financial Services*. Tunaomba Serikali itoe tamko juu ya asasi hii ambayo imekuwa kero kwa walimu nchini. Riba yao ni zaidi ya asilimia 200. Pia nitaomba nipate maelezo, juu ya Chama cha Walimu (CWT) au *Teachers Trade Union*, hawa wana nafasi gani katika asasi hii ya *Bayport*? Ni kwa nini nakala ya mikopo ya wahanga wa asasi hawapewi. Serikali itoe tamko juu ya hili.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, kwa juhudhi kubwa anazofanya katika kusimamia na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005.

Nawapongeza pia Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Naibu Mawaziri, pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kazi kubwa wanazozifanya katika kusimamia mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi kama ifuatavyo, katika nchi nyingi duniani mgeni katika nchi au mwenyeji wa nchi hawezi kununua au kuuza pasipo kutumia *local currency* mfano mzuri ni baadhi ya nchi nilizozitembelea Afrika Kusini, Msumbiji, Dernmark na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, *CHC* ililirithi shughuli zilizokuwa zikifanywa na *PSRC* na *LART*, chini ya usimamizi wa *PSRC* Mashirika mengi ya umma yalibinafsishwa. Mashirika yaliyobinafsishwa yapo mengine yasiyozaalisha, yapo yaliyobadilisha matumizi na yapo mengine ambayo hayajaanza uzalishaji mpaka sasa. Je, Serikali inasema nini kwa makampuni ambayo hayajaanza uzalishaji na yale yaliyobadilisha matumizi? Katika nchi zingine mgeni kutoka nje (asiye raia) haruhusiwi kuwekeza pasipo ubia na raia wa nchi, je, kwa makampuni yaliyobinafsishwa ni mangapi yana ubia na Watanzania na mangapi ni ya wageni kwa asilimia mia?

Mheshimiwa Spika, uvezeshaji wananchi kiuchumi haujafanikiwa na Mheshimiwa Waziri hajalieleza Bunge lako Tukufu changamoto zilizojitokeza. Kuna changamoto nyingi sana katika suala la uvezeshaji wananchi kiuchumi. Sera hii haitafanikiwa iwapo wananchi hawapati elimu ya ujasiriamali. Ninachotaka kujua ni je, kwa nini baadhi ya nchi duniani haziruhusu kununua au kuuza ndani ya nchi zao kwa kutumia fedha za nje? Na kwa nini nchi yetu hili siyo tatizo (*dollarization*).

Mheshimiwa Spika, Shirika la Bima ya Taifa ina hali mbaya kifedha na madeni mengi hayalipwi tena kwa muda mrefu. Shirika linadaiwa zaidi ya shilingi bilioni 21.46 madai mengi katika shirika hili ni ya wafanyakazi wa kawaada, Serikali na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu mikakati madhubuti iliyojiwekea kulikwamua Shirika la Bima.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mheshimiwa Mustapha Mkulo na Naibu Mawaziri wake kwa hotuba nzuri pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 62 kifungu Na.109 Waziri anaelezea suala la mafao ya waliokuwa wafanyakazi wa Jumuia ya Afrika Mashariki. Maelezo hayatoshelezi, suala hili linaiabisha sana Serikali yetu wananchi wanasumbuliwa siku hadi siku kama vile sio wananchi wa nchi hii. Aibu, walilipwa ni fedha za mizigo na nauli ya shilingi 2,000,000/= kwenda makwao, wapi fedha za pensheni za wahusika. Naomba maelezo ya kutosha vinginevyo sitaunga mkono hoja hii.

Kuhusu pensheni kwa wastaafu wa Serikali, nashauri zilipwe kila mwezi au kama haiwezekani walipwe kila baada ya miezi mitatu. Mimi sikubaliani na suala la malipo kwa muda wa miezi sita tatarudi nyuma hasa kwa kuwa nia ya Serikali ni kuiboresha pensheni ya kima cha chini.

Mheshimiwa Spika, narudia kuipongeza Serikali kwa kuliokoa Shirika la Posta na kuamua kuchukua madeni na pensheni ya wafanyakazi wa *East Africa Posts and Telecommunication*. Swali langu ni lini utekelezaji utafanyika ili shirika hili liweze kujikwamua na kuboresha huduma zake. Aidha, ni lini posta watapatiwa mtaji (*capital*) kama vile sheria Na. 19 ya 1993 inayohitaji Waziri wa Fedha na wa Miundombinu kukutana kuamua kuhusu mtaji. Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, bado ulipaji wa pensheni ya watumishi ni tatizo na vile vile ulipaji mirathi bado tatizo. Wafiwa wanansumbuka sana hata baada ya kukamilisha taratibu zao na za mahakama.

MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, kwanza nampongeza Waziri na Naibu Mawaziri pamoja na watendaji wake wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kuhusu masuala ya ucheleweshwaji wa utolewaji wa fedha ambazo tayari zimeshapangiwa kwa ajili ya kufanyiwa kazi, sijui ugonjwa huu utapatiwa dawa lini na kukomeshwa kwani unarudisha nyuma maendeleo ya nchi na inakatisha tamaa kwa wananchi mfano hai kwa daraja la Kigamboni lilikuwa liwe tayari limeshamalizika na wafadhili walipatikana lakini likayumbishwa mpaka sasa limekuwa na gharama kubwa na wafadhili hawapo tena. Ipo na miradi mingi tu inayoyumbishwa sijui hao wahusika na usimamizi wa kutoa fedha sijui huwa hawaipendi au hawaitaki? Kwa hiyo watu kama hao bora waondolewe maana wanasababisha upandaji wa gharama za kila siku.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kiinua mgongo na pensheni, litiliwe mkazo na utekelezaji mzuri kwani wananchi wanatumikia Taifa lao kwa moyo wote, leo wanatelekezwa.

Napongeza Wizara kwa kuja kuanzisha Tume ya Mipango ila tu nasisitiza Tume hiyo wajumbe wake wawe wenye ujuzi na uzoefu wa kutosha na wawezeshwe vizuri ili waweze kupanga mipango bora ya kuikomboa nchi yetu kijamii, kimaendeleo na kiuchumi. Na masuala ya mambo ya kijamii, Wizara iyape uzito na wayaendeleze kwani bila ya kuendeleza jamii na maendeleo hayatopatikana.

Mheshimiwa Spika, pia naomba vifaa vya watu wenye ulemavu wanavyotumia vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi visamehewe ushuru kutokana na hali zao, wengi hawamudu. Kuhusu vyanzo vya uchumi navyo vichunguzwe upya na vifikiriwe vingine zaidi ili kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, masuala ya kununuliwa magari ya gharama, samani za gharama nayo yapunguzwe, kwani fedha zinatumika bila mipango wakati huo huo fedha hizo zingetumika kwa mambo mengine kuliko ufahari huo. Naitakia kila la kheri Wizara hii na mipango mema.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu sana kwa muda huu aliotupa. Nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii, nikupongeze vile vile kwa jinsi ambavyo umeendesha Mkutano huu wa Bunge wa Bajeti ya mwaka 2008/2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Naibu Spika na Wenyeiti wa Bunge letu. Nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na wajumbe wote wa Kamati yake kwa kadri ambavyo wametusimamia na kutufikisha hapa tulipo, tunashukuru kwa ushauri wao na maelekezo mbalimbali ambayo tumeyaingiza kwenye majumuisho yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda niungane na Waziri wa Fedha na Uchumi kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa jinsi ambavyo wamechangia kwenye hoja zenu na kwenye Bajeti za Wizara mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nianze kujibu baadhi ya hoja ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza nitaanza na hoja ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kama ilivuosomwa na Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji na hoja yake ni kwamba kuna maduhuli yanayofikia shilingi bilioni 7.9 ambayo yanatokana na ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma ambayo hayajakusanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la *Consolidated Holding* linaendelea na juhudi za kufuutilia madeni haya kwa nguvu na kasi ya kuridhisha na katika kipindi cha kati ya Julai, 2007 mpaka sasa jumla ya shilingi bilioni 3.2 zimekusanya na kiasi ambacho kimebakı kukusanya na ambacho tunaendelea kukfuutilia ni shilingi bilioni 4.6. Matumaini yetu ni kwamba kwa kasi yetu ambayo tumefikia na kuamua tuchukue hata haya madeni ambayo bado hayajakusanya yatakusanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa George Lubeleje, anaomba ajengewe Ofisi ya Mamlaka ya Mapato Wilayani Mpwapwa. Nina mhakikishia kwamba kutokana na mipango ambayo ipo kwenye Mamlaka yetu ya Kodi tunategemea kwamba pale tutakopata kiwanja cha ukubwa wa kutosha basi Ofisi hiyo itajengwa katika kipindi cha awamu hii ya nne na katika mwaka wa fedha wa 2010/2011. (*Makofi*)

Mheshimiwa Shally Raymond anasema pamoja na nia nzuri ya Serikali kuanzisha mpango wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kwa kutoa mikopo yenyenye masharti nafuu, bado riba ni kubwa sana na inawaumiza wananchi. Serikali ilibuni mpango huu wa uwezeshaji na kukuza ajira kwa kutambua kwamba wananchi wengi wanashindwa kupata mikopo kutoka kwenye Mabenki ya Biashara kwa shughuli za kuichumi lakini la msingi na kwa sababu hawana dhamana. Wananchi hao wanashindwa kupata mikopo kwa sababu ya riba kubwa kutoka kwenye Mabenki haya ya Biashara na kwa hiyo, baada ya majadiliano ya muda mrefu Benki mbili za CRDB na NMB zikakubaliana na Serikali kwamba wangeweza kutoa mikopo mara tatu ya dhamana ambayo Serikali ingewekeza kwenye Benki hizi kwa riba ya asilimia 10. Lakini kwa sababu Serikali tulihamasisha

mikopo hii itolewe kuitia *SACCOS* za wananchi. Serikali ikakubali vile vile kwamba ingekuwa sahihi kama hivi vyama vingetoza wanachama asilimia mbili zaidi ya ile kumi maana yake 12%. Sasa hiyo ndiyo inayosemekana kuwa ni kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niseme kwamba ukweli ulio sahihi ni kwamba ukichukua kiasi cha riba ambacho wananchi wangetozwa na Mabenki ya Biashara hata hii asilimia 12 wala si robo tatu ya riba yenye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, wiki iliyopita riba ambayo inatozwa na Benki Kuu kwenye hati fungani za mwaka mmoja ambao ndiyo msingi wa Mabenki ilikuwa ni asilimia 11.50. Sasa kama ukiongeza kwa mfano *basis point* 500 ambayo Benki za Biashara ni lazima ziongeze kwenye ile riba ya Benki Kuu tayari umeshafikia 17 ukiongeza zaidi ya tano basi unaelekea 20. Kwa hiyo, ingawa asilimia 10 kwa tarakimu ni kubwa lakini kwenye soko la fedha la sasa hivi na tangu mpango huu ulipobuniwa Serikali tunasema kwamba kwa kweli ni kiasi cha riba ambacho kwa vyovyote vile tusingewenza kupata chini ya hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dr. Zainab Gama anasema ni wakulima wangapi wamepata mkopo kutoka katika mpango wa mabilioni ya JK. Mpango huu wa uwezeshaji katika awamu ya kwanza kama tunavyofahamu wote ulihusisha *CRBD* na *NMB*. Hadi kufikia Julai, 2008 mwezi uliopita mikopo yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 37.92 ambayo ni zaidi ya asilimia 100 kulinganisha na shilingi 31.50 ambazo zilitarajiwa kutolewa. Kati ya hizo *NMB* imekopesha shilingi bilioni 16.23 na *CRDB* shilingi 21.69 na niseme hapa kwamba Benki hizo bado zinaendelea na mpango huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa mipango hii mpaka sasa hivi imefaidisha watu 48,221 kati ya hao wanawake ni 13,782 na wanaume ni 34,439. Tunakiri kwamba zoezi la kuchanganua kwa sekta bado halijakamilika. Kwa hiyo, kutoa takwimu hapa kwamba ni wakulima wangapi wamefaidi na mpango huu bado ni mapema lakini sisi tunaahidi kwamba hapo zoezi hili litakapokamilika tutatoa taarifa kwa wakati muafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda anasema kitengo cha Iitelejensia ya fedha kuyachunguze Mashirika ya Umma yasiyotoa gawio kwa Serikali kulingana na faida yanayopata. Kitengo hiki cha udhibiti wa fedha haramu kimeanzishwa chini ya Sheria maalum ya Udhibiti wa Biashara ya Fedha haramu sura 423 na majukumu ya kitengo hiki ni kupokea kutoka kwenye Mabenki, Taasisi za Fedha na vyombo vingine taarifa zenye muelekeo wa mashaka kuhusu biashara ya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi na baada ya kuzipokea taarifa hizo basi kitengo hiki kinatakiwa chini ya sheria hii kuwasilisha taarifa hizo kwenye vyombo vya dola. Kwa hiyo, kwa msingi huo kitengo hiki hakina mamlaka ya kushughulikia masuala ya Mashirika ya Umma yanayoshindwa kuwasilisha gawio kwa Serikali kutokana na mapato halisi kama inavyopendekezwa na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda. (*Makofi*)

Lakini niseme hapa kwamba *issue* kubwa hapa sio hiki kitengo kitoe taarifa, *issue* ni taarifa ifike Serikalini na gawio lipatikane ili liende kwenye mfuko mkuu wa Serikali na hapa nieleze kwamba kuna utaratibu mwingine wa kufuatilia gawio hizi

Msajili wa Hazina anafanya kazi hiyo baada ya mahesabu yale ya mwisho wa mwaka yanapokuwa tayari basi Msajili wa Hazina anakaa na kuangalia kama ni kweli kuna gawio ambalo linastahili kuletwa kule Hazina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ijielimishe kuhusu sababu za ucheleweshaji wa fedha za wafadhili na kuchukua hatua za kupunguza athari zake. Tunakiri kwamba mara nyingine kweli hizi fedha zinachelewa pamoja na kwamba wafadhili wanakuwa wameshaahidi. Lakini kuna sababu ambazo nyingi zinaeleweca na itaendelea kutokea. Kwa mfano, hizi fedha zinatoka kwenye nchi mbalimbali kunapotekea mabadiliko ya Serikali Chama kimoja kinaunda Serikali wanaweza kubadilisha utaratibu wa kutoa misaada, masharti yenye ya misaada inaweza kubadilika, uongozi katika vyombo vya Mataifa mfano *ADB*, *World Bank* au *IMF* kubadilisha utaratibu wa kutoa mikopo au misaada, urasimu ni sehemu moja ya kuchelewesha. Lakini vile vile kutokana na ucheleweshaji unaotakana na wakandarasi. Kwa hiyo, jawabu ni nini? (*Makofi*)

Kwanza jawabu ni kutoingiza kwenye Bajeti ya Serikali. Ahadi ambazo tunabaini dhahiri kwamba pamoja na kwamba tumeahidiwa uwezekano ni mkubwa kwamba zile fedha hazitafika kwa wakati, maana yake pale unapofanya hivyo unatoa pitcha kwamba Bajeti yako ni kubwa lakini kwa kweli si kubwa kwa sababu hazitafika fedha zile. Ni kuongeza umakini katika uteuzi wa makandarasi ili waweze kufanya kazi ambazo wanashinda zile zabuni ili zile pesa ambazo zinakuja ziweze kutumika kulipia. Lakini la msingi na kubwa kuliko lote ni nchi kujitegemea na kuacha kutegemea hawa wahisani ambao wanatusaidia. Haiwezekani tukasema kwamba tutawafuta moja kwa moja au tutaacha kuomba misaada, hapana. Lakini tukiweza kushusha utegemezi wetu kwa kiwango ambacho tutafikia sio lazima tupige magoti basi hata fedha hizi zikichelewa mipango yetu ya maendeleo haitaathirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed vile vile anasema baadhi ya wafanyakazi wa kigeni hawalipi *PAYE*. Taarifa tulizonazo ni kwamba kwanza sheria inawataka walipe. Miaka ya nyuma ni kweli kuna ambao walikuwa wanakwepa kwepa na hapa niipongeze *TRA* sasa hawakwepi na katika miaka mitatu iliyopita zaidi ya dola milioni 14 zimekusanywa ambazo zilikuwa hazikufika kwenye vitabu vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Uchumi iongeze kasi ya maamuzi kuhusu maombi ya dhamana. Naomba niseme hapa kwa kweli jitihada ni kubwa katika kila wakati ambao tunapata maombi haya. Lakini kuna taratibu ambazo huwezi kuzikwepa. Kwa mfano ni lazima maombi haya yakidhi matakwa ya Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile ni lazima Kamati ambayo inashauri utoaji wa dhamana hizi ni lazima ikae, ni lazima ifanye mchanganuo na kabla haijamshauri Waziri wa Fedha na kwa hiyo, muda huo unaweza kuonekana kwamba unachelewesha maamuzi, lakini ni hatua ambazo ni lazima zichukuliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed tena anasema kwamba *CAG* afanye *surprise cash audit* yaani aende akafanye uchunguzi wa vitabu kwa kushitukiza. Naomba niseme kwamba kuanzia mwaka 2007/2008 Halmashauri zote 132 zilishitukizwa kwenye ukaguzi na pamoja na Wizara na Ofisi za Balozi zote za Nje ya nchi. Matokeo ya zoezi hili yatapatikana katika taarifa za mwaka za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotumika kuchangia miradi ya kujumuishwa katika mpango wa uwezeshaji unaofadhiliwa na *MCC*. Mheshimiwa John Lwanji, alichangia vizuri sana na naomba nimwambie kwamba kazi ya kuandaa miradi hii ilikuwa ni jukumu letu pamoja na wenzetu wa Marekani na katika kufanya hivyo, kulikuwa kuna vigezo maalum ambavyo viliwekwa lakini kwa ujumla wake ilielekezwa pale ambapo matokeo ya uwekezaji ule yangetchangia kwenye uchumi wa Taifa kwa ujumla wake. Uchaguzi wa ni wapi fedha zile zielekezwe hazikwenda kimkoa ama kiwilaya.

Kwa hiyo, zilipangwa vile vile kutokana na matakwa ya MKUKUTA na MKUZA na kwa hiyo, Mheshimiwa John Lwanji, pamoja na kwamba Mkoaa wa Singida unawezekana haukupata moja kwa moja, lakini tegemeo letu ni kwamba matokeo ya matumizi ya ule msaada kwenye uchumi wa nchi kwa ujumla wake, basi na Mkoaa wetu wa Singida utakuwa umefaidika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ambayo ulikuwa umenipa. Naomba niunge mkono hoja! (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Jerry Solomon Sumari. Sasa Naibu Waziri wa pili katika Wizara hiyo, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, unazo dakika zako 15. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Spika, na mimi nataka nikupongeze wewe binafsi pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya katika kuendesha Bunge letu hili. Lakini vile vile nataka nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi pamoja na Wajumbe wake kwa miongozo yao wanayotupa wakati wote ule tukiendelea na shughuli zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka nimpongeze na nimshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa Mustapha Mkulo, kwa kutulea mimi na Naibu mwenzangu. Anatulea vizuri sana na anatupa miongozo na tunamshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka vile vile nimshukuru sana mke wangu Bi. Narman Yussuf, kwa kweli kwa kunivumilia muda wote wa miezi mitatu kuwepo hapa Dodoma. Nawapongeza vile vile wanangu na vile vile nawapongeza wapiga kura wangu wa Jimbo la Kiembesamaki, nawaambia baada ya kumaliza shughuli hii, tutakuwa pamoja huko Jimboni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo na shukrani, sasa na mimi naomba na kabla sijajibu au sijasaidia kujibu hoja, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha siku ya Ijumaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ni nyingi, lakini kama nilivyoeleza awali kwamba kwa miongozo ya Mheshimiwa Waziri na mimi nimepewa baadhi ya hoja nisaidie kuzitolea ufanuzi. Kwanza, nitataka nitoe ufanuzi juu ya hoja ya Wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba sisi sote tuliomo humu ndani pamoja na Serikali ya Chama cha Mapinduzi hakuna hata mmoja ambaye hataki hawa wafanyakazi walipwe. Sote tunataka wafanyakazi hawa walipwe na suala hili liishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nieleze kwa kifupi, wakati Serikali ilipoamua kuwalipa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Hazina ilipokea mafaili zaidi ya 41,000. Wafanyakazi mafaili yao yalikuwa zaidi ya 41,000 ambayo ndiyo ilipokea Hazina. Kwa kifupi tu ni kwamba watu zaidi ya 41,000 wanajaza viwanja viwili vya Amani na wengine wanabakia nje. Lakini Serikali imeweza kuwalipa watu zaidi ya 30,000, hawa ndio ambao walijitokeza na wakalipwa cheki zao na wakaondoka, zaidi ya watu 30,000! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nimekuwa nikieleza Bunge lako Tukufu kwamba zaidi ya cheki 6,332 zimetayarishwa, lakini wenye hawajajitokeza kuzichukua. Tumewalipa vipi, ndilo la msingi ambalo likulizwa sana na Waheshimiwa Wabunge. Nataka niseme na Waheshimiwa Wabunge mko wazi kuchukua fomu za malipo, tumewalipa *on the basis* za mishahara yao ya mwisho. Lakini tumewalipa *with compound interest* ya 17.53%. Kwa wale wenzangu ambao wamesoma mahesabu wanaelewa jinsi ya *compound interest* inavyofanya kazi. Ili kukidhi kwamba toka mwaka 1977 kama hujalipwa, unalipwa leo *with interest*, tumewalipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile, lazima ulimwengu, Watanzania waelewe, Rais wa Awamu ya Tatu alitoa agizo akasema hawa wafanyakazi wote walipwe shilingi milioni mbili *on top* kwa kila mfanyakazi kwa ajili ya ile nenda rudi, nenda rudi na tumelipa *on top* ya hizo pesa shilingi milioni mbili tumelipa. Lakini nataka tuijulize tatizo liko wapi? Ndilo hili ambalo nataka nilisema. Tatizo kubwa lililopo kwanza kuna wafanyakazi wa *East Africa* walikuwa ni vibarua, hawa hawaingii kwenye pensheni, nao wameingia katika huu mkumbo na wao wanataka kulipwa. Tunawaambia ninyi hamuingii kwenye pensheni, kwa hiyo, hamuwezi mkalipwa kwa sababu ninyi mlikuwa ni vibarua. (*Makofi*)

Lakini la pili kuna baadhi ya wafanyakazi wanasema wana mapunjo, tumewauliza mapunjo yako wapi? Punjo linaweza likatokea katika maeneo mawili tu, eneo la kwanza, kama mshahara wako uliofanyiwa malipo ni mdogo kuliko *pay slip* yako ya mwisho, pale punjo litaonekana. Nimewaomba wote ambao wana mapunjo ya aina hiyo wawasilishe na kweli kuitia kwenye Mashirika yao baadhi yao wameonekana na Hazina sasa hivi inakokotoa malipo yao wale ambao wameonekana wana mapunjo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande wa pili, punjo lingine linaloonekana ni kwamba kama kuna mtu amechukua pesa, amelipwa pesa kwenye shirika lake, katika fomu ya mwisho ya malipo amekatwa wakati hakuchukua pesa, Hazina hawataweza kuthibitisha hilo isipokuwa shirika lake liweze kuthibitisha kwamba huyu kweli hakuchukua pesa hizi lakini kwenye fomu yake kakatwa. Kuna baadhi imethibitishwa na Mashirika yao tumetayarisha, sasa hivi tunatayarisha malipo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niseme kwamba kazi ya kuwalipa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki imefanywa na Serikali na kilichofanywa ni kikubwa sana, lazima tuipongeze Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu, sisi tunaposema kwamba mwenye tatizo aje amuone Waziri, katika *high rack* ya uongozi ndani ya Wizara, mtu yeoyote anapokwenda kwa watumishi, watendaji akaona anazungushwa zungushwa, *appeal* aipeleke wapi, lazima *appeal* aipeleke kwa mwanasiasa ambaye ni Waziri. Waziri katika Wizara ni *political commissar* lazima alinde sera na lazima awasadie wale ambao wanazungushwa zungushwa na watendaji. Lazima Waziri awasadie, kwa hiyo ndio maana tukasema kwamba lazima waje ili tuweze kusaidiana nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spia, sisi ni watumishi wa umma na sisi tumewekwa na wananchi. Mimi sikubaliani na Wabunge wanaposema kwamba utamwona saa ngapi Waziri! Mbona wanania mimi wanaotaka kuja kuniona! Wakati wowote tu Waziri yupo! Waziri lazima aonekane! Waziri ambaye hataki kuonekana na wananchi, basi huyo mimi nasema hajajua nini maana ya *political commissar*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niseme kwamba suala la wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, atakapokuja mwenyewe Mheshimiwa Waziri anaweza akalimalizia, lakini Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi kubwa na mahangaiko ya shilingi milioni mbili kwa kila mtumishi aangalie ile *statement* yake ya malipo ipo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo nataka niifafanue ambayo imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi tu ni suala la ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma ambayo tulieleza wiki iliyopita. Tuna Mashirika kama 37 hivi ambayo yako katika michakato mbalimbali, hatujabinafsisha bado. Wazo la kuyabinafsisha haya Mashirika ni wazo zuri tunakubaliana nalo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Joseph Mungai amezungumza hili, Mheshimiwa Susan Lyimo amezungumza hili, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na Mheshimiwa Raymond amelizungumza hili. Tunasema nia ya Serikali ndiyo kama ile nia walionayo Waheshimiwa Wabunge. Lakini tukianza kuyapeleka leo kwenye *Stock Exchange* haya Mashirika, hali yake ni mbaya, unamfanya mwananchi aende akanunue shirika ambalo hali yake ni mbaya. Tunachokisema sisi Serikali kwanza, tunatengenezea utaratibu haya Mashirika ili yaweze kuimarka. Tunataka tutafute *Strategic Investors* kama tulivyofanya kwa *NMB*, kama tulivyofanya *NBC*, kama tulivyofanya kwa *TBL*, baadaye tutayapeleka kwenye *Stock Exchange* wakati yameshakidhi ile haja ili

tuweze kuwasaidia wananchi wetu waweze kununua *shares* katika Mashirika hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lengo na nia ya Serikali ni nzuri, ni kuhakikisha kwamba tunawawezesha wananchi wetu. Lakini vile vile Waheshimiwa Wabunge wengine wameelezea haja ya kutoa elimu ya hisa.

Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana na Wabunge wote walioelezea haja hiyo na nataka niwahakikishieni kwamba kwa kushirikiana na wenzetu wa *Dar es Salaam Stock Exchange* na Mashirika yenye we tutafanya hivyo kwa kutoa elimu ya hisa ili kila mwananchi ajue uzuri na ubaya wa kununua hisa na wakati gani anatakiwa yeye mwenyewe anaweza akaiza hisa zake na wakati gani anaweza akanunua hisa katika shirika lingine. Hili tunalifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini hoja nyingine ambayo imeulizwa na Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamaed, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia na wengine, suala la *Tanzania Investment Bank (TIB)*, iongezewe uwezo ili iweze kukidhi majukumu yake. Nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna haja kubwa sana ya kuongezea uwezo Benki hii hasa kwa utendaji kwa sababu Benki hii tunaiongezea majukumu ni dhahiri kwamba kuna haja ya kuongezea uwezo kiutendaji, kuna haja vile vile ya kuongezea uwezo wa vifaa. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tutalifanya hilo ili Benki hii iweze kutekeleza majukumu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo lilzungumziwa ni suala zima la takwimu. Nataka nieleze tu kwamba ni kweli kuna haja ya kuwa na takwimu sahihi kabisa katika suala zima la kutumia katika kupanga mipango yetu ya maendeleo. Lakini nataka nieleze kwamba siyo kila takwimu ambayo ipo hapa Tanzania utaweza kuiona kwenye kitabu kimoja. Vitabu vya takwimu vipo vingi sana. Kuna takwimu nyingine unaiona katika vitabu vinavyofanya *House of Budget Survey*, takwimu za Kaya, takwimu za familia, takwimu za kilimo, kuna takwimu za biashara. Hivi vitabu viko vingi kabisa, inawezekana katika kitabu kimoja usiione, ukaiona katika kitabu kingine. (*Makofi*)

Lakini nakubaliana naye kwamba kuna haja ya kuwa na takwimu sahihi sana katika kupanga mipango yetu ya kimaendeleo na hili tutaliangalia na tutaangalia kwamba takwimu zetu za kiuchumi basi zote ziwe katika kitabu ambacho Wabunge au Waheshimiwa wengine wanaweza kuzipata kwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limezungumziwa ni suala la kutumia *RITA* katika suala zima la uandikishaji wa vitambulisho au utayarishaji wa vitambulisho vya Taifa. Nataka niseme kwa kifupi tu kwamba nina li-respect *RITA* very much kwa sababu linazalisha takwimu za vizazi na vifo na tunazitumia. Kitengo chetu cha takwimu, *agency* wetu wa takwimu za Taifa anatumia takwimu za *RITA*. (*Makofi*)

Lakini hatuwezi tukaitumia *RITA* kwa ajili ya vitambulisho vya Utaifa kwa sababu hiki chombo si cha Muungano na suala la vitambulisho vya Utaifa ni suala la

Muungano, hatuwezi tukatumia *RITA*. Maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kuanzisha chombo cha Muungano ni sahihi kabisa na hicho chombo kimeshaanzishwa, kwa hiyo, chombo hicho ndicho kitakachopewa dhamana ya kuanzisha vitambulisho vya Muungano. Lakini huko siku za baadaye basi, kuunganisha chombo hiki na *RITA* nadhani litakuwa ni wazo zuri, nacho vile vile kiweze kutekeleza majukumu ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie ni suala la *ATM*. Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamelielezea suala la *ATM*. Wengine wamesema *ATM* zina kero, wengine wamesema *ATM* katika maeneo yao hakuna. Mheshimiwa George Lubeleje anasema Mpwapwa kule hakuna *ATM*. Nataka niseme nia ya Benki zetu na lengo, kila kwenye matawi yao, wana nia nzuri tu wanataka kuanzisha *ATM*. Lakini uanzishwaji wa *ATM* utategemeana na Bajeti zao. *NMB* wamejipanga vizuri tu sasa hivi, nadhani Mheshimiwa George Lubeleje akirudi Jimboni kwake anawea akaona *progress* nzuri za kuanzishwa *ATM* katika Jimbo lake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwamba na maeneo mengine vile vile tutaweza kuangalia jinsi gani benki zetu zinaweza kufungua *ATM* katika matawi yao. Lakini hizi kero ambazo zimeelezwa za *ATM*, nataka kuwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba tukimaliza tu, tutakaa na Menejimenti za Benki hizi ili waweze kuyapatia ufumbuzi haya matatizo ambayo yana-*associate* katika *ATM* zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nieleze vile vile hali ya Chuo cha Mipango, Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema kwamba hali ya Chuo cha Mipango ni mbaya. Nataka niseme kwamba tutaboresha hali ya Chuo kile, tutaboresha majengo, tutawapatia walimu wa kutosha na vile vile nataka niseme kwamba huyu Mkuu wa Chuo kuanzia Desemba tayari ameshathibitishwa, hakaimu tena. Kwa hiyo, huyu Mkuu wa Chuo kuanzia Desemba, 2007, hakaimu tena, sasa hivi ameshathibitishwa na nimejaribu kutafuta ukweli halisi kutoka kwake mwenyewe na tumeweza kuupata kwamba amethabitishwa kuanzia mwezi Desemba, 2007, kwa hiyo, sasa hivi hakaimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie, nimeulizwa hapa, kwa nini deni la ndani linakua wakati tuna matumizi ya *cash budget!* Nataka niseme kwamba hivyo ni vitu viwili tofauti. La msingi tunalosema sisi hapa kwamba hatutakopa kutoka katika Benki zetu za ndani kwa sababu ukikopa katika Benki zetu za ndani, wenzetu wale wanaoendesha Benki watakuwa na uhakika wa mteja, kwa hiyo, wao suala la kushusha riba litakuwa halipo kwa sababu wana uhakika wa mteja ambaye ni Serikali. Lakini la pili watakuwa hawana *liquidity* ya kuweza kuwasaidia wananchi wetu ambao tunataka wakope. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Serikali tumesema hatutakopa kutoka kwenye Benki zetu za ndani. Lakini kama kuna *issue* ambayo ni muhimu sana, tunaweza tukakopa kutoka kwenye mifuko. Nataka nitoe mfano tu, Bunge hili tumekopa kutoka kwenye mifuko, limeongeza deni letu la ndani, nyumba za wanajeshi na polisi tumekopa kwenye mifuko, limeongeza deni letu la ndani, Chuo Kikuu tumekopa kutoka kwenye mifuko, limeongeza deni letu la ndani. Lakini la msingi Waheshimiwa Wabunge ni uhakika wa kuweza kulipa deni letu la

ndani na la nje. Sasa hivi Serikali tuna uhakika tunalipa kwa viwango ambavyo tumejipangia deni letu la ndani na la nje.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana! (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Nadhani imeeleweka tu, aliunga hoja mkono alipoanza kusema, kwa hiyo kwangu mimi inatosheleza na ikitosheleza kwangu humu ndani, ndio imetosha tena! Kwa hiyo, nafurahi sasa kumwita Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, mtoa hoja wa hoja hii. Anazo dakika zisizozidi 60. (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyevit wa Bunge kwa kazi kubwa na nzuri mliyofanya ya kuongoza majadiliano ya Mkutano huu wa Bajeti kwa mwaka 2008/2009 ambao umehusisha Bajeti ya Serikali kwa ujumla na za Wizara mbalimbali na ambao leo tunahitimisha kwa mjadala huu kuhusu mpango wa kazi na mapendekezo ya mapato na matumizi ya Wizara yangu ya Fedha na Uchumi kwa mwaka 2008/2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni kwa jinsi alivyowasilisha maoni ya Kamati yake ambayo kwa sehemu kubwa ni ushauri kwa Serikali kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu majukumu ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Napenda pia kutoa shukrani zangu kwa Kiongozi na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed pamoja na Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, aliyewasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kwa ushauri wao kuhusu Bajeti hii ya Wizara ya Fedha na Uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuitumia fursa hii pia kuwashukuru kwa dhati kabisa Naibu Mawaziri wa Wizara yangu, Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee kwa ushauri wao ambao wamekuwa wakiutoa kwangu na kuwezesha kufanikisha kwa utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Uchumi. (*Makofi*)

Aidha, napenda kuwashukuru Katibu Mkuu, Bwana Grey Shaibu Mgonja, Naibu Makatibu Wakuu, Bwana Ramadhan Kija, Bwana John Haule na Bwana Raston Msongole, Makamishina wa Wizara ya Fedha, Wakurugenzi na watumishi wote ndani ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa ushauri na utekelezaji wa maelekezo mbalimbali yanayoelekezwa kwenye Wizara yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kadhalika, napenda nitambue na kuwashukuru Gavana wa Benki Kuu, Profesa Benno Ndulu, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Harry Kitilya, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Ludovick Uttoh, Watendaji Wakuu wa Taasisi zote chini ya Wizara kwa ushauri na ushirikiano wanaonipatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika mjadala huu kwa kuzungumza hapa Bungeni na kwa maandishi.

Aidha, naamini kwamba hata wale Waheshimiwa Wabunge ambao hawakupata nafasi ya kuchangia wataunga mkono hoja hii ya Wizara ya Fedha na Uchumi ili tupate uwezo wa kutekeleza yale ambayo wananchi wa Tanzania na Waheshimiwa Wabunge wanatutaka tuyafanye. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, napenda niwataje Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni na ni hawa wafuataao, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Magalle Shibuda, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Kabuzi Rwiomba, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Joseph Mungai, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Fred Tungu, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Kilontsi Mpologomyi, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuataao, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Mohamed Rajab Moahmed Soud, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Damas Nakei na Mheshimiwa Mohamed Missanga. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwataja waliochangia, sasa naomba niende kwenye hoja moja moja jinsi zilivyojitekeza. Naibu Mawaziri wangu wamejaribu kujibu chache, mimi nitajaribu kujibu zile nitakazoweza kabla muda haujaisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ilitoka kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi na vile vile Mheshimiwa

Dr. Zainab Gama. Wao wasema mwongozo wa Bajeti za Halmashauri, unachelewa kutolewa.

Mheshimiwa Spika, mwongozo wa mapato na Bajeti wa Serikali za Mitaa hutolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa baada ya kuzingatia maelekezo yaliyo katika mwongozo wa mpango wa Bajeti wa Serikali Kuu. Kama walivyoeleza wachangiaji katika hoja hii, mwongozo wa Bajeti mwaka huu ultolewa mwezi Machi badala ya lengo la kuutoa mwezi Januari. Hali hii ilitokana na mabadiliko ya muundo wa Serikali pamoja na mgawanyo wa majukumu baina ya Wizara mbalimbali. Hali hii itarekebishwa katika mwongozo wa mwaka ujao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ilikuwa ubinafsishaji wa Mashirika yaliyosalia kufanywa kwa kuuza hisa zake katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (*DSE*) ili kumarisha soko la hisa na liende kwa haraka. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Joseph Mungai, Mbuge wa Mufindi Kaskazini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Uchumi inakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Joseph Mungai. Makampuni yatakayoendelea kubinafsishwa yatapitia Soko la Hisa la Dar es Salaam endapo watakuwa wamekidhi masharti ya kuandikishwa sokoni chini ya utaratibu wa *SMA* na *DSE*. Aidha, kwa Mashirika ambayo Serikali bado ina hisa chache, uuzaaji wake utapitia Soko la Hisa pale ambapo Mashirika hayo yatakuwa yamefuzu masharti ya soko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ya tatu, ilikuwa ni mauzo ya hisa za *NMB*. Tumepokea hoja ya Wabunge wengi kuhusu Serikali kutenga sehemu ya hisa zake 30% katika *NMB* kwa wafanyakazi wa *NMB*. Serikali itaangalia uwezekano huo katika toleo yaani *IPO* la sasa, vinginevyo mchakato wa kuuza 30% zinazosalia utaharakishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini Benki Kuu imekataza wananchi wasikope kwenye benki ili kununua asilimia 20 ya hisa za Serikali katika Benki ya *NMB*, hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sheria ilivyo sasa hivi inazuia mtaji wa benki yoyote, kwa maana nyingine ni kwamba huwezi kukopa ili ununue hisa katika benki, hii ni kuhakikisha kuwa akiba za wateja kwenye mabenki zinakuwa salama, kwa kuzingatia masharti haya ya kisheria Benki Kuu imezikumbusha benki kutotoa mikopo kwa kutumia hisa za *NMB* zinazolengwa kama dhamana ya mikopo hiyo. Kabla ya hisa hizo kugawiwa na kuthibitishwa kwa kila mwenye hisa kwa mtu mwenye dhamana tofauti na hiyo inawezekana kupata mikopo na kutumia fedha hizo kununua hisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii inawezekana kwa kuwa fedha hizo zinalipwa kwa Serikali kama mwanahisa anayeuzza hisa zake na si sehemu ya mtaji wa kampuni.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba ni marufuku kwenda kwenye *NBC* uka-*pledge* hisa za *NMB* unazokusudia kuzinunua ili *NBC* ikupe mkopo, lakini ukikopa mahali pengine Benki Kuu haijakataza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kama Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Msemaji Mkuu wa Wizara ya Fedha alikuwa na hoja nyingine kwamba pamoja na mafanikio ya mamlaka ya mapato Tanzania bado hajafanya vizuri kwani ingefanya vizuri tungejitosheleza kwa Bajeti yetu bila kutegemea wahisani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kuboresha makusanyo ya mapato ya ndani ili kuongeza uwezo wetu wa kugharamia mahitaji yetu. Mapato yaliyokusanywa na *TRA* yameongezeka kutoka wastani wa shilingi bilioni 25 kwa mwezi mwaka 1996 hadi shilingi bilioni 346 ilipofika tarehe 30 Juni, 2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka huu *TRA* inatarajiwa kukusanya wastani wa shilingi bilioni 374 kwa mwezi, haya ni mafanikio makubwa kutoka milioni 25 mpaka bilioni 374. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mpango mkakati wa tatu wa *TRA* unalenga kuongeza ukusanyaji kutoka asilimia 17.2 ya Pato la Taifa hivi sasa hadi kufikia asilimia 20.3 ifikapo mwaka 2012 hadi 2013 sawa na shilingi triliuni tisa na hamsini na nne bilioni.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuhusu wafanyakazi wa kigeni walioajiriwa na makampuni mbalimbali ya Kimataifa ya *Multinationals* kutolipa kodi ya mapato kwenye mishahara yao, hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kama kiongozi wa upinzani na vile vile kama Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria ya kodi ya mapato, mwajiri anatakiwa kukata kodi ya *employee* kutoka kwenye mshahara wa mfanyakazi na kuwasilisha makato *TRA*, *TRA* imekuwa ikikagua kuhakikisha kwamba kodi hiyo inalipwa, kwa wafanyakazi ambayo waajiri wao wako nje ya nchi, hao hutakiwa kujaza taarifa za mapato na kulipa kodi zao kwa mujibu wa sheria ambapo mamlaka ya mapato hufanya ukaguzi wa mikataba yao ya ajira ili kuhakiki kuwa wamelipa kodi sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kama zipo kampuni ambazo Waheshimiwa Wabunge na hasa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, wanahakika kuwa hazilipi *PAYE* Serikali kuititia *TRA* itaomba tuzipate hizo na tutazifanyia kazi mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihu Wizara kurejea maeneo ya misamaha ya kodi na kupunguza zile sehemu ambazo hazina ulazima sana wa kupata msamaha, hoja hii ilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Margreth Agness Mkanga, Mheshimiwa Mhonga Ruhanywa, Mheshimiwa Damas Nakei na Mheshimiwa Magdalena Sakaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa katika hotuba yangu Wizara imezingatia ushauri huo na kwamba inapitia upya misamaha ya kodi na kwa lengo la kuipunguza,

kwa kuanzia hatua za kukidhi misamaha kwa *NGO'S* na wawekezaji zimependekezwa katika Muswada wa Fedha wa mwaka huu ambao tutajadili nahisi itakuwa kesho, tutajadiliana na wahisani kuhusu misamaha ya kodi kwa miradi inayofadhiliwa, hatua zaidi zinaandalila na zitawasilishwa Bungeni baada ya uchambuzi kukamilika. Tunategemea kwamba hatua hizi huenda zikawasilishwa kwenye Bunge la mwezi Novemba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kuhusu ushuru wa mafuta ya kula, hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Mgana Msindai na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, wakati nikiwasilisha hotuba ya Bajeti ya Serikali, Serikali ilipendekeza kuondolewa kwa ushuru wa forodha wa asilimia 10 unaotozwa na mafuta ghafi ya kula, napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mkutano wa wadau ulioshirikisha wakulima wa mbegu za mafuta na wenyewe viwanda vya kusindika mafuta ya kula ulifanyika hapa Dodoma tarehe 25 Julai, 2008 na mimi nilihudhuria mkutano huo, kutokana na mashauriano hayo Serikali imeamua yafuatayo:-

Kwanza, Tanzania itaendelea kutoza asilimia 10 kwa mafuta ghafi yanayotoka nje, pili, Serikali itafanya utafiti kubaini mahitaji halisi ya mafuta ya kula na mazingira ya kuzalisha mbegu zaidi na tatu, Serikali itaangalia maeneo yote ya changamoto ambayo yalipendekezwa katika kongamano lile lililoitishwa kati ya wakulima wa mbegu na wazalishaji wa mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihu Wizara ya Fedha na Uchumi iboreshe sera ya kodi kwenye kilimo kwa kutoza vivutio zaidi, hii ilitoka kwa Mheshimiwa Joseph Mungai, sekta ya kilimo ikijumuisha mazao, mifugo na misitu ni sekta ya kipaumbele katika mfumo wetu wa kodi, vivutio vinavyotolewa na pamoja na vifuatavyo:-

Kwanza, kutotoza ushuru wa forodha kwa pembejeo za kilimo, kusamehe VAT kwenye pembejeo za kilimo, kutoza punguzo la asilimia 100 la gharama za uwekezaji katika kilimo katika mwaka wa uwekezaji (*capital expensing*) na kutoa msamaha wa ada ya mafunzo kwa watumishi wa mashambani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na vivutio hivi sekta ya kilimo imeendelea kupata upendeleo katika sera za matumizi pia kwa kupata ruzuku kwa mikopo ya pembejeo. Serikali iko tayari kupokea mapendekezo ya vivutio zaidi vinavyoweza kutolewa ili kuvutia uwekezaji katika kilimo cha kisasa. Tungependa kupata mapendekezo haya mapema ili yaweze kujumuishwa katika Bajeti ya mwaka ujao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kwa nini Serikali inadhamini mikopo ya makampuni binafsi, hoja hii ilizungumzwa kwa nguvu sana na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na vile vile na Mheshimiwa Halima Mdee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba Serikali imetoa, *NSSF* imetoa mkopo wa shilingi milioni 100 kwa kampuni ya sukari ya Kagera na vile vile siyo kwa shinikizo la Serikali, wala siyo kutokana na dhamana ya Serikali. Taarifa sahihi ni kwamba *NSSF* ni mojawapo ya taasisi za fedha zinazounda jopo yaani *syndicate* ambayo ni zaidi ya mabenki saba zilizotoa mkopo wa shilingi bilioni 74.8 ya kampuni hiyo. Mfuko huo

ukiwa umechangia takribani asilimia 16 ya mkopo huo kwa maana kuwa NSSF ilichangia asilimia 16 ya bilioni 74.8 na siyo bilioni 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jopo hilo la wakopeshaji linaloongozwa na *Stanbic Bank* na linajumuisha benki na taasisi kadhaa nyingine, Serikali kupitia mfuko wa dhamana wa mikopo ya maendeleo ya *DFES* ilitoa dhamana ya asilimia 80 ya mkopo wenyeve yaani *principle only* na si asilimia mia moja, kutokana na sababu mbalimbali na hasa kuchelewa kuwasili kwa mashine ya umwagiliaji yaani *irrigation equipment*, utekelezaji wa mradi haukwenda kama ilivyotarajiwa na hivi sasa wakopeshaji wameshakubaliana na mteja wao namna ya kurekebisha masharti ya mkopo na kuwezesha mradi huo kuendelea kutekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inafuatilia majadiliano hayo kwa kuwa imedhamini mkopo lakini pia isingependa fursa za ajira zinazotokana na mradi huo zipotee, nataka kuwashakikishia Wabunge hao kwamba kama nilivyosema awali kwamba Serikali inatazama upya dhana nzima ya dhamana, kwa maana ya kuipunguza au kutoa dhamana tu ya Mashirika ya Umma na si makampuni binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kupitia mfuko maalumu wa Serikali wa kuendeleza kilimo, *TIB* ilitoa mkopo ili kuibua sekta ya maua na mboga mboga kwa makampuni sita huko Arusha pamoja na kiwanda cha nyama cha Saafi cha Sumbawanga ili kuongeza mapato ya nje na ajira. Miradi hiyo ilifanyiwa uchambuzi na kuonekana inafaa, *TIB* iliteuliwa kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo na urejeshwaji wa mikopo hiyo, dhamana ya mikopo hii ni mali zisizohamishika na zinazohamishika za miradi hiyo kama ilivyo katika utoaji mikopo mingine ya kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa miradi hiyo kumetokea uchelewashaji wa kufika vifaa vilivyoagizwa kutoka nje ambapo umesababisha uchelewashaji wa kumalizika baadhi ya miradi hiyo. Pia kuongezeka kwa bei ya pembejeo na mahitaji mengine kama mbolea, dawa, gharama za kusafirisha maua nje na kadhalika katika uzalishaji, umeathiri urejeshwaji wa mikopo, hali hii imesharekebishwa kwa kuzingatia hali halisi na mikopo imeanza kurejeshwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TIB* na Benki Kuu imeendelea kufuatilia kwa karibu sana maendeleo ya miradi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa inahusu hoja ya *EPA* ambayo iliibuliwa na Kambi ya Upinzani na hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Kabwe Zitto na Mheshimiwa Suzan Lyimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, madai kuwa hoja hii iliibuliwa na Kambi ya Upinzani siyo sahihi, suala hili liliibuliwa na wakaguzi wa *Deloitte and Tosh*, Serikali baada ya kugundulika ilimwagiza *Controller and Auditor General* afanye ukaguzi wakati inazungumzwa Bungeni, *Controller and Auditor General* alishaanza kutekeleza agizo la Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua za dhati kulingana na taarifa za ukaguzi na si taarifa za upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matumizi ya fedha za *EPA*, hii ilitolewa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Suzan Lyimo na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, nashukuru asubuhi ulisaidia kutoa ufanuzi, Serikali imeamua kutumia fedha hizi kuongeza mtaji wa *TIB* na ruzuku ya pembejeo za kilimo, mifugo na uvuvi ili kuongeza fedha kwa sekta ya kilimo ambayo ni sekta kiongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongeza mtaji wa Benki ya Posta na *Twiga Bankcorp*, Serikali itaangalia uwezekano wa kupata fedha za kufanikisha azma hii, suala kwamba Rais angengoja Bunge ligawe kama Mheshimiwa Spika alivyosema, Bunge huidhinisha anayepanga pesa ni Rais na Serikali yake kwa hiyo sasa Rais ameagiza. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nataka nieleze sahihi kwamba nimepanga fedha ni mhimili wa *executive*, ndiyo maana natafuta fedha na kuzipanga, lakini kwa sababu ni matumizi ya Serikali inabidi ziletwe Bungeni ili Bunge liidhinishe, kwa hiyo, alichofanya Rais hajakosea kama mkuu wa *executive branch* ametekeleza na anatakiwa kuyatekeleza na wakati muafaka, nitawaambia kuna pesa zingine ambazo tumezipata hivi majuzi, sasa tumezipata baada ya Bajeti kupita hatuwezi kuja tu hapa kama Waziri nikasema kwamba kuna milioni 200 tumezipata mahali mpaka zipitie mlolongo unaotakiwa ndipo tuje Bungeni kuwaambia kwamba tumepata shilingi milioni 200 kutoka mahali fulani na tunazi-*allocate* zifanye kazi fulani kwa hivyo alichofanya Mheshimiwa Rais ni sahihi kabisa hakuna popote alipokosea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyininge ilikuwa mamlaka ya mapato ichukuliwe hatua za nidhamu Afisa wa Mapato wa Kibaha ambao anawanyanyasa wananchi kwa kuwatolea makadirio makubwa ya kodi yasiyolingana na mapato yao, hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Kibaha, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hilo Wizarani tunalifahamu na tunalifanyia kazi na tunashukuru kwa kutukumbusha, tutahakikisha kwamba tunalifanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyininge iliyofuata ilikuwa ni ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kutumia majengo ya wateja wao ni jambo linaloathiri utendaji wa wakaguzi, hii ilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, ingawa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inaendelea kutumia majengo ya wateja wao, kuna juhudu zinazoendelea za kutatua tatizo hili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuititia Bajeti ya Serikali Ofisi imeweza kujenga au kununua majengo ya Ofisi katika Mikoa ya Mara, Iringa Manyara na Dodoma, pili, kwa kuititia ufadhili wa *SIDA* na Ofisi wa ukaguzi wa hesabu ya Serikali ya Sweden, tatu, ofisi imeweza kununua jengo la Ofisi Mkoani Arusha na kujenga majengo mawili katika mikoa ya Mbeya na Singida, nne, Serikali itaendelea kusaidia shirika ofisi hii kuweza kupata ofisi katika mikoa mingine na tano, Serikali pia imeazimia kutenga fedha katika

Bajeti yake ya maendeleo kwa ajili ya kujenga majengo angalau mawili kila mwaka katika mwaka wa fedha 2008/2009 kiasi cha shilingi bilioni 2.8 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa ofisi katika mikoa ya Lindi na Morogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Serikali huwajibika kwa Bunge badala ya Rais, hoja hii ilitolewa na kiongozi wa Kambi ya Upinzani ambaye pia ni Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kimsingi utaratibu ulivyo sasa kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kwa Rais, wakati wa mchakato wa kutunga sheria mpya ya ukaguzi wa umma namba 11 ya mwaka 2008 suala hili lilijadiliwa kwa kina na kuonekana kwamba litahusisha mabadiliko ya Katiba, hivyo ilikubalika kuwa utaratibu unaotumika hivi sasa uendelee yaani Mkaguzi na Mdhhibit Mkuu wa Serikali atawajibika kwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ijitegemee kiutendaji badala ya kuwa chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inajitegemea *hundred percent* isipokuwa katika kuwasilisha Bajeti yake Bungeni inatumia Wizara ya Fedha na Uchumi kama mhimili wa kuwasilisha Bajeti yake Bungeni kwa sababu yenye haina *locus stand* ya kuweza kuwasilisha Bajeti Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupewa uwezo wa kutoa adhabu kwa watendaji anaowakagua, hoja hii pia ililetwa na Kambi ya Upinzani, kufuatana na kanuni za utendaji bora yaani *best practices* siyo sahihi kwa Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua, kushtaki na kuadhibu, jukumu lake linabaki kukagua, kutoa taarifa na ushauri kwa Serikali na Bunge na kuwaachia mamlaka husika Mahakama kuendelea na taratibu nyingine za kisheria au za kinidhamu pale inapobidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali irekebishe sheria ili Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aweze kufanya ukaguzi kwa makampuni ambayo Serikali inamiliki chini ya asilimia 50 ya hisa, hoja hii pia ilitolewa na Kambi ya Upinzani, Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali ana mamlaka ya kisheria ya kukagua taasisi zote za umma ambayo Serikali inamiliki hisa zaidi ya asilimia 50, kwa taasisi nyinginezo ambayo Serikali ina hisa chini ya asilimia 50 utaratibu wa ukaguzi unasimamiwa na bodi za kampuni au shirika husika ambazo huteua Mkaguzi kwa mujibu wa sheria ya makampuni, hata hivyo utaratibu wa kushirikishwa kwa Serikali pamoja na Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa makampuni ya aina hiyo umewekwa bayana katika sheria mpya ya ukaguzi wa umma namba 11 mwaka 2008 kifungu cha 30(4) iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Juni, 2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile wakaguzi wanaokagua ofisi hizi ni lazima wawe wameandikishwa na bodi ya uhasibu na wakaguzi wa NBAA na wanatakiwa kufuata taratibu zote za ukaguzi, kwa jinsi hii bado Serikali inapata taarifa sahihi za hali ya

kifedha ya mashirika ambayo ina hisa chini ya kiwango cha kulazimisha ukaguzi kufanywa na *KGB*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu kutozingatiwa kwa sheria ya ununuzi na kanuni zake unalisababishia Taifa upotevu mkubwa wa fedha, hoja pia ilitolewa na Kambi ya Upinzani, Wizara yangu kupitia *PPRA* inaendelea kutekeleza mikakati ambayo ina lengo la kuongeza ufanisi na tija katika manunuzi yanayofanywa na taasisi za umma, baadhi ya mikakati hiyo ni kujenga uwezo wa wataalamu wa fani ya ununuzi na ugavi, kuboresha vitengo vya ununuzi na ugavi, kuboresha vitengo vya manunuzi ya taasisi vya taasisi za umma na kuhakikisha kuwa ina wafanyakazi na vitendea kazi vya kutosha. Ili kufanikisha hivi Wizara imeanzisha kitengo cha ununuzi ambacho kitasimamia sera ya manunuzi na uamuzi na uamuzi umeshafanywa na Serikali kuihamisha kada ya ununuzi na ugavi, kuihamishia Wizara ya Fedha na Uchumi, kuongeza ukaguzi wa manunuzi unaofanywa na taasisi za umma na kuwachukulia hatua wale wanaokiuka sheria na kutekeleza mfumo wa kusimamia na kudhibiti manunuzi ya taasisi za umma na wa kukusanya na kusambaza taarifa muhimu ya ununuzi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo *PPRA* iko katika hatua za mwisho za kuandaa utaratibu utakaotumiwa kufanya manunuzi yanayotumiwa na taasisi nyingi za umma na iko katika hatua za mwanzo za kuainisha njia bora ya utekelezaji wa utaratibu wa manunuzi kupitia njia ya mtandao uitwao *E-Procurement*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka kuliarifu Bunge lako Tukufu pia kwamba kutokana na mapendekezo ya Wabunge, sheria ya *PPRA* inafanyiwa marekebisho na Muswada wa marekebisho hayo utaletwa katika kipindi cha kikao cha mwezi Novemba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ihakikishe kukamilisha ajira ya Mkurugenzi wa Kitengo cha Ununuzi yaani *PPU* na kukamilisha kada ya ugavi na bodi ya wataalamu wa ugavi kutoka Wizara ya Miundombinu kwenda Wizara ya Fedha na Uchumi, hoja hii imetolewa ililetwa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Wizara imepokea maoni ya Mheshimiwa Mbunge na itaharakisha zoezi zima la kukiwezesha kitengo cha ununuzi na uhamishaji wa kada ya ugavi na bodi ya wataalamu wa ununuzi na ugavi kama ilivyopendekezwa na Mheshimiwa Mbunge sambamba na hilo Wizara chini ya programu ya maboresho ya usimamizi wa fedha katika sekta ya umma inatekeleza mkakati wa kujenga uwezo wa taasisi za umma kufanya ununuzi kwa ufanisi na tija na kwa kuzingatia sheria ya ununuzi na kanuni zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii itajumuisha kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wataalamu wa ununuzi, kuhakikisha kuwa kila taasisi hasa Halmashauri za Serikali za Mitaa zinawataalamu na vitendea kazi vya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu marekebisho yaliyopendekezwa ya sheria ya ununuzi yazingatie kwa undani na kuweka wazi mahusiano kati ya kitengo cha ununuzi kilichoanzishwa, *PPRA* na *PPPA*, hoja hii pia ililetwa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Wizara imepokea ushauri wa Mheshimiwa Victor Mwambalaswa na

itaufanya kazi kwa nia ya kuhakikisha kuwa vyombo hivyo vinatekeleza majukumu yake bila mwingiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihu msamaha wa VAT kwa wafanyabiashara wakubwa unawapa wafanyabiashara hao kutolipa kodi ambayo kimsingi wanapaswa kulipa na kiwango cha asilimia 20 ni kikubwa na hakizingatii gharama za uendeshaji, hoja hii pia ililetwa na upande wa Upinzani, sheria ya ushuru wa hoteli inamtaka mmiliki wa hoteli au nyumba ya kulala wageni ambaye hajasajiliwa na VAT kulipa ushuru wa asilimia 20 kwa huduma ya malazi, kwa mujibu wa sheria hii ushuru unaotozwa kwa nyumba ya kulala wageni unapaswa kulipwa kwa Halmashauri ambapo hoteli inayotoa huduma za chakula kulipwa kwa Serikali Kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sheria ya ushuru wa hoteli imemsamehe mfanyabiashara aliyesajiliwa na VAT ili kumpunguzia mzigo wa gharama anazopata kutokana na ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu za VAT, kwa vile wafanyabiashara wakubwa wamesajiliwa na VAT hawalazimiki kisheria kulipa ushuru wa hoteli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu malalamiko ya kiwango cha asilimia 20 kwa kuwa ni kikubwa tunapenda kuwashauri wenye hoteli na nyumba za kulala wageni kupitia chama chao kuwasilisha mapendekezo yao rasmi ili yafanyiwe kazi marekebisho ya kodi na hivyo yaweze kuingizwa kwenye Bajeti ya mwaka ujao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe kuwa Wabunge, Kata na Vijiji wanashirikishwa katika mchakato wa Bajeti, hoja hii ililetwa na Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mbunge wa Kalenga, utaratibu wa kuanda Bajeti ya Taifa unazingatia malengo yaliyoainishwa katika dira ya Taifa ya Maendeleo hadi mwaka 2025, MKUKUTA na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala, maandalizi ya dira ya maendeleo na MKUKUTA yalipitia mchakato shirikishi sana. Aidha, Ilani ya Uchaguzi ni msingi wa kura za kishindo ambazo wananchi walikipigia Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo, miongozo mikuu ya Bajeti ya Taifa ni nyaraka ambazo zimenufaika na maoni ya wananchi wengi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikishirikisha wadau mbalimbali katika maandalizi ya Bajeti ya kila mwaka, kama tulivyowahi kueleza Serikali inahusisha wadau kupitia mchakato wa *Public Expenditure Review* unaowashirikisha Serikali, watalaa mbalimbali, asasi zisizo za Serikali na wawakilishi wa wahisani wetu, utaratibu huu pia huwashirikisha Waheshimiwa Wabunge katika vikao vya ngazi husika.

Aidha, kuanzia mwaka jana Serikali imeanza utaratibu wa kuwasilisha kwa Wabunge mwongozo wa mpango wa Bajeti ya Serikali kwa ajili ya kupata ushauri kuhusu mwelekeo wa Bajeti ya Serikali kabla ya kukamilisha maandalizi ya Bajeti yenye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia njia hizi tunaamini kuwa fursa za kutosha za Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuchangia katika maandalizi ya Bajeti ya Taifa ni nyingi na za wazi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilisema inafaa Serikali ianzishe Benki ya Ushirika ya Taifa na benki ya kilimo, hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Janeth Massaburi, kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais wakati akihitubia Bunge hivi karibuni Serikali inadhamiria kuanzisha Benki ya Kilimo kwa kuanzia Benki ya Rasilimali imeelekezwa kuwa na dirisha la mikopo ya kilimo ili baadaye huduma hiyo ihamishiwe katika Benki ya Kilimo kwa wakati muafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mpango huo hivi sasa Serikali inapitia mpango wa awamu ya pili ya mageuzi katika sekta ya fedha inaandaa mkakati maalumu wa kufikisha huduma za fedha vijijini (*Rural Financing Strategy*) pamoja na mambo mengine. Mkakati huo unalenga kusogeza huduma za fedha karibu na wananchi waishio vijijini ili kukidhi mahitaji ya uendeshaji wa shughuli zao za kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu ubinafsishwaji wa shamba la mahindi Mbozi na kwa nini umechelewa sana na aliomba Waziri lazima atoe maelezo vinginevyo Mheshimiwa Godfrey Zambi atamtafuna Waziri. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Godfrey Zambi kwa ufuatiliaji wake wa karibu kuhusu ubinafsishwaji wa shamba la mahindi la Mbozi ambalo lilikuwa likiendeshwa na *NAFCO*, ni kweli kwamba mchakato wa kubinafsishwa shamba hili umechukua muda mrefu, katika kubinafsisha shamba hili Serikali imekuwa makini sana ili kuhakikisha anapatikana mwekezaji mahiri mwenye uwezo kifedha na kitalaamu ili kulifufua na kuliendesha shamba hili kibiashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumuarifu Mheshimiwa Godfrey Zambi kwamba mchakato wa ubinafsishaji wa shamba hili umefikia hatua nzuri na kwamba tunategemea kumpata mwekezaji hivi karibuni na ninamkaribisha ofisini kwangu ili aweze kukaa na wataalamu wa Ofisi ya Hazina wampe hali halisi ya pale tulipofikia katika kubinafsisha shamba hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, viwango vya waliositishwa pensheni zao walipwe riba hii ilitoka kwa Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma unalipa mafao kwa wastaa fu wake kulingana na *PPF Act 14* ya mwaka 1978 pamoja na marekebisho mbalimbali yaliyofanyika. Mfuko huu ni wa kuchangia kwa hiyo, mafao au pensheni yanayolipwa yanategemea michango iliyokusanywa na mapato yanayotokana na vitega uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafao ya pesheni hulipwa kwa kuzingatia kanuni yaani *formula* kama sheria inavyoelekeza, kanuni hizo huzingatia mambo makuu mawili yafuatayo katika kukokotoa mafao ya pensheni ya kila mstaa fu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, moja, wastani wa mishahara ya miezi sitini iliyokuwa mikubwa katika kipindi cha wanachama wake, jambo la pili ni muda aliochangia, kanuni hizi ndizo hutumika katika mifuko mingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukubwa wa kiasi cha pensheni anacholipwa mstaafu, hutegemea ukubwa wa mshahara wake na urefu wa muda wake aliochangia katika Mfuko. Kwa hiyo, pensheni za wastaa fu hutofautiana. Kwa kutumia kanuni hizi mbili, wapo wastaa fu wanaolipwa kima cha chini cha shilingi 21,000 kwa mwezi, lakini pia wapo wastaa fu wanaolipwa zaidi ya shilingi milioni moja kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa *PPF*, kwa kuzingatia hali halisi ya uchumi, umejiwekea utaratibu wa kupandisha pensheni na kima cha chini. Kima hiki kimekuwa kikipanda kutoka shilingi 8,000, 10,000, 15,000 na sasa shilingi 20,000. Mfuko utaendelea kupandisha pensheni kwa wastaa fu wake kulingana na uwezo wake na hali ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu muundo (*structure*) wa bajeti zetu kwa ujumla, ina upungufu kwani uendeshaji (*recurrent*) ni kubwa kuliko bajeti ya maendeleo (*development*). Wamependekeza kwamba, kwa siku za usoni, *budget structure* ibadilike na hatimaye *development budget* iwe kubwa kuliko *the current budget*. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mbunge wa Kiteto.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la Mheshimiwa Mbunge ni zuri. Hata hivyo, ni vyema kuelewa kwamba, wakati wote gharama za uendeshaji ni kubwa. Mgawanyo wa *recurrent* ni kama ifuatavyo: Deni la Taifa (*Consolidate Fund Services*); Mishahara ya Watumishi; na Matumizi Mengine (*Other Charges*).

Mabadiliko ambayo yamekuwepo katika uendeshaji wa Serikali, yamefanya gharama za uendeshaji ziendelee kupanda. Hata hivyo, tukiwa na bajeti kubwa ya maendeleo na hivyo kuwa na miradi mingi ambayo hatimaye itakamilika au kukamilishwa, bado tutahitaji fedha nyingi tena za uendeshaji. Kwa mfano, Mradi wa Ujenzi wa Hospitali au Shule tunahitaji wafanyakazi, vifaa, vitendea kazi, miundombinu inayozunguka eneo hilo na kadhalika. Hivyo basi, mradi wowote unaokamilika unaongeza mahitaji ya fedha za uendeshaji.

Hoja nyingine ilikuwa kwamba, faida ya mwaka 2004/2005 ya Benki Kuu iliyopatikana, Serikali ilipata asilimia 3.9 tu ya faida. Gawio hilo likiwa ni shilingi bilioni tano kati ya shilingi bilioni 127.5 na kwamba, gawio hilo la Serikali ni dogo mno likilinganishwa na faida iliyopatikana. Hoja hii ilitolewa na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya msingi ya Benki Kuu si kutengeneza faida, bali kuhakikisha uchumi wa nchi unakua na kuimarika. Kadiri thamani ya shilingi inavyoimarika, ndivyo uwezo wa Benki Kuu kutengeneza faida unavyopungua kama ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu, malipo ya gawio hufanyika kutokana na faida baada ya kutenga fungu kwa ajili *general funds*, kiasi

kingine cha faida hutengwa kwa ajili ya mafungu mengine kama vile *foreign exchange re-evaluation reserve* na *special project reserve* kabla ya kutoa gawio kwa Serikali. Hivyo, si faida yote inayopatikana hutolewa kama gawio kwa Serikali.

Halafu kuundwa Tume Huru ya Bunge kuchunguza gharama za ujenzi wa majengo pacha ya Benki Kuu. Hoja hii ilitolewa na Kambi ya Upinzani, ilitolewa pia na Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu ilikwishaanza mchakato wa kutafuta kampuni huru ya wataalam watakaofanya ukaguzi unaolenga katika kuhakiki gharama halisi ya uendelezaji wa majengo pacha ya Benki Kuu (*Value for Money Audit*). Uamuzi huu ulichukuliwa kwa kuzingatia kwamba, tathmini ya gharama za ujenzi wa majengo hayo pacha ni suala linalohitaji utaalam katika fani mbalimbali zihusozo ujenzi, hususan majengo yenye kiwango cha majengo pacha. Mchakato wa kupata kampuni huru na wataalam unakaribia mwisho na inatarajiwa kwamba, kazi ya uhakiki inaweza kuanza kabla ya mwisho wa mwezi Oktoba mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni fafanuzi kuhusu Benki Kuu kwamba, imeyazuia mabenki; nadhani hii nimeshaelezea.

Hoja nyingine ilihu Serikali iuze sehemu ya hisa zake asilimia 40 kwenye *Celtel* au Zain. Ni kweli kwamba, Serikali ina hisa asilimia 40 kwenye iliyokuwa *Celtel* na sasa Zain. Serikali imepokea ushauri tutautazama na tutafanya *cost benefit analysis*, tuone kama tutapata faida zaidi kwa kubakia kule kama *shareholders* au tuziuze zile *share* ama tungojee tufanye *IPO* halafu *shares* ziuzwe kwa wananchi kuitia soko la hisa. Kwa hiyo, tunachukua ushauri kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihu riba kubwa itozwayo na Benki Kuu kwa Mabenki ya Biashara, inapelekea mabenki hayo kutoza riba kubwa kwa wakopaji. Hoja hii ilitoka pia Kambi ya Upinzani na kwa Mheshimiwa Shally Raymond.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu haipendelei Mabenki ya Biashara kukopa kutoka kwake, kwani ukopaji wa mabenki uliokithiri kutoka kwenye Benki Kuu unaongeza mfumko wa bei na pia itapunguza haja ya kasi ya mabenki kupanua huduma zake mijini na vijijini, kwa nia ya kukusanya amana kutoka kwa wananchi. Kwa hiyo, nia ya Benki Kuu ni kuona Mabenki ya Biashara yakitumia njia kuu za kupata fedha za kukopesha ikiwemo kukusanya amana kutoka kwa wananchi na kukopeshana wenyewe kwa wenyewe (*Inter Bank Rending*). Lengo kubwa lililopo kati ya riba za mikopo na pia riba za amana kuwa chini sana. Hili lilitolewa na Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora na Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, Serikali pamoja na Benki Kuu, zinafanya jitihada mbalimbali za kurekebisha mifumo mbalimbali, ambayo husababisha ongezeko la gharama za mabenki katika utoaji wa mikopo, ikiwa ni pamoja na sheria za uboreshaji na utendaji katika mahakama, uboreshaji wa ofisi zihusozo usajili wa hati na usajili wa ardhi na uhamishaji wake, pamoja na uandikishaji wake. Pia uanzishwaji wa mfumo wa

kumbukumbu za wakopaji (*Credit Reference System*), inategemewa kwamba, maboresha haya yatapelekea kupungua kwa gharama za ukopeshaji na hivyo kupunguza riba za mikopo itolewayo na mabenki ya biashara na vile vile kupunguza pengo lililopo kati ya riba za amana na riba za mikopo.

Kwa mfano, riba za mikopo katika kipindi cha mpaka Juni, 2008 ilishuka kufikia asilimia 14.7 kutoka asilimia 16.36 zilizokuwa zinatozwa katika kipindi cha Desemba, 2006. Katika kipindi hicho hicho, riba za kuweka amana zilipanda hadi kufikia asilimia 2.79 kutoka asilimia 2.56.

Gharama kubwa za riba zitozwazo na taasisi za fedha za asili na athari zake kwa wananchi wakiwemo walimu. Hili lilitoka kwa Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa Paul Lwanji. Riba za mikopo hazipangwi na Serikali, bali huzingatia hali halisi ya masoko ya fedha na gharama za utoaji wa mikopo. Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mabenki ya mwaka 1996, taasisi hizi za fedha kama *Bayport Financial Services*, *Blue Financial Services* na *Easy Finance*, hazisimamiwi na Benki Kuu, kwa kuwa hazipokei amana za wateja. Hata hivyo, kuongezeka kwa malalamiko ya wananchi kuhusu riba zitozwazo na makampuni haya, Serikali kwa kushirikiana na Benki Kuu, imeanza mchakato wa kutathmini shughuli za makampuni haya ili kuhakiki kama yanaweza kusimamiwa chini ya Sheria za Mabenki. Hata hivyo, kwa sasa wananchi wanashauriwa kuwa waangalifu wanapotaka kukopa kutoka kwa taasisi za fedha zitoazo huduma za mikopo, hususan taasisi za fedha ambazo hazipo chini ya usimamizi wa Benki Kuu.

Wananchi wanashauriwa kuangalia kwa undani, masharti ya taasisi hizi ili kuepuka gharama kubwa zitokanazo na riba zinazotozwa. Pale ambapo wananchi wana wasiwasi, tungewashauri waende kwenye benki iliyo karibu na wao ili waweze kupata ushauri wa kitaalam kabla hawajajiingiza kukopa kwenye vyombo hivi ambavyo havisimamiwi na Benki Kuu.

Baadhi ya wafanyabiashara Mkoani Mbeya kukataa kupokea sarafu; hili lilitoka kwa Mheshimiwa Gofrey Zambi. Sarafu za shilingi 5, 10, 20, 50 na 100 ni fedha halali na bado hazijaondolewa kwenye mzunguko. Tunawashauri wale wote wenye fedha hizo, wanapokataliwa na wenye maduka, waziwasilishe kwenye benki iliyo karibu. Benki itazipokea fedha hizo na kuna utaratibu wa benki kuziwasilisha Benki Kuu na wao wanajua nini cha kuzifanya noti ambazo zimeisha matumizi yake.

Hoja nyingine ilihusu kuboresha mazingira, ambayo ilichangiwa na Mheshimiwa Profesa Mwalyosi. Tunaupokea ushauri wake wa kitaalam sana kuhusu kuzingatia mazingira katika mipango yetu ya maendeleo na tunamhakikishia kwamba, tutafanya hivyo katika mipango yote mingine itakayokuja huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Beatus Lyamba, ameshauri tozo la dhati kwenye kilimo cha miwa liondolewe. Hoja hii ililetwa hapa Bungeni wakati wa majadiliano ya Bajeti Kuu ya Serikali. Kwa kuzingatia mazingira ya kilimo cha miwa, Serikali iliama kufanya utafiti wa kina na baadaye kufanya mashauriano na wakulima wa miwa mnamo tarehe 15

mwezi huu. Baada ya mashauriano, Serikali imeamua kutoa msamaha wa dhati kwa huduma za kuandaa mashamba, kukata miwa, kupakia miwa, kupakua na kusafirisha miwa, kutoka shambani hadi viwandani. Huduma hizi zitasamehewa endapo zitatolewa na chama cha wakulima wa miwa kilichosajiliwa kwa wanachama wake. Uamuzi huu ni wa mara moja. (*Makofi*)

Lingine kuhusu wastaa fu wasamehewe kulipa kodi ya majengo. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Esther Nyawazwa. Sheria ya Kodi ya Majengo (*Urban Authority Renting*), imeainisha majengo ambayo yanastahili kusamehewe kodi. Katika msamaha huu, majengo ya wastaa fu hayakutajwa bayana. Hata hivyo, Halmashauri za Miji zimepewa uwezo wa kusamehe kodi na majengo ambayo hayakubainishwa wazi endapo itadhihirika kuwa kuna sababu za msingi za kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kodi hii itakusanywa na *TRA* kwa niaba ya Halmashauri, mimi na mwenzangu Waziri wa TAMISEMI, tutashauriana jinsi ya kuwasaidia hawa wasio na uwezo. Kwa kuwa uhusiano wetu na Jumuiya ya Ulaya, unapitia *cotton agreement* na unasimamiwa na Kitengo cha *PSU* kilichopo Wizara ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa anaomba Wizara ihakikishe shughuli za kitengo hicho hazisitishwi. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mbunge wa Kigoma Kaskazini. Kitengo cha *PSU* katika Wizara ya Fedha, kilianzishwa mwaka 1964 kwa makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya, kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa miradi inayotekelizwa kwa ufadhili wa misaada ya mikopo kutoka Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwake, kitengo hicho kimesaidia sana kuimarisha utekelezaji wa miradi na *program* mbalimbali zinazotekelizwa kwa ufadhili wa Jumuiya hiyo, kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kutoa taarifa za utekelezaji kwa wakati kwa mujibu wa makubaliano yetu na Jumuiya hiyo. Aidha, kazi nyingine za kitengo hicho imekuwa ni kuratibu ushiriki wetu katika mazungumzo kuhusu ushirikiano kati yetu na Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha uhai wa kitengo hiki, majukumu yake pia yameongezeka kutohana na kuongezeka kwa msaada wa *EU* kwa Tanzania kutoka *Euro* milioni 55 wakati wa EDF 7 hadi *Euro* 555 katika kipindi cha EDF 10, ambacho kinaanza mwaka huu wa 2008/2013. Kuongezeka huku kwa majukumu pia kumeongeza umuhimu wa kuwepo kwa kitengo hiki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu huu, taratibu zinafanywa ili kuangalia upya muundo wa kitengo hiki ili kuweza kubaini muundo unaokidhi mahitaji ya sasa. Ili kufanikisha hili, Serikali inafanya taratibu za kumpata mshauri (*consultant*), ambaye atafanya upembuzi yakinifu na kushauri Serikali muundo unaofaa. Kwa kifupi, Serikali na *EU* tunaamini kwamba, kitengo hiki ni muhimu na bado tunakihitaji. Kwa msingi huo, katika mpango mpya wa ushirikiano wa EDF 10 tumetenga fedha za kuendesha shughuli za kitengo hiki kwa miaka sita ijayo. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, asiwe na wasiwasi kwamba kitengo hiki kitafutwa.

Hoja nyingine ilihu *flow meters* katika Bandari ya Dar es Salaam kwamba, zimekuwa na hivyo hakuna anayejua ni kiasi gani cha mafuta yanayoingia nchini na hivyo kusababisha upotevu wa mapato. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi. Vile vile hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ili kupima kwa usahihi kiasi cha mafuta ya petroli kinachoingia nchini na *TRA* waweze kukadiria kodi kwa usahihi. Mamlaka ya Bandari (*TPA*), inafunga mita 14 pale KOJ. Mita hizi zilifanya kazi kwa muda zikaharibika. *TPA* waliagiza vipuli nchini America na kuvifunga kwenye mita hizo mwisho wa mwezi Julai mwaka huu.

Hivi sasa zinafanya kazi ya uhakiki (*testing*), kubaini kama zimetengamaa ili zianze kutumika tena kupima mafuta. Kutokana na tatizo hili, *TRA* ilibidi itumie hatua mbadala za kuhakiki usahihi wa mafuta yanayoingia nchini, ambazo ni pamoja na kufanya *dipping* kulinganisha kiasi kwenye nyaraka za *slip, master* na zile za *dipping*, kulinganisha kiasi kilichoonyeshwa kwenye nyaraka za *insurance* na *dipping* na kulinganisha kiasi kilichobainishwa na *surveyors, certificate* na *dipping*. Hatua hizi zinaiwezesha *TRA* kujua kiasi cha mafuta kilichoingia nchini, japo si kwa usahihi mkubwa kama *flow meters* kwa ajili ya ukadiriaji kwa kodi ya mafuta. Uwezeshaji unasemwa tu, lakini hakuna kinachofanyika. Mfuko wa uwezeshaji mwaka huu umetengewa shilingi ngapi? Hii pia ilikuwa hoja ya Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi.

Hoja nyingine, Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, ulizinduliwa rasmi mwezi Januari, 2008 kwa kianzio cha shilingi milioni 400. Kwa mwaka 2008/2009, Mfuko huo haukuweza kutengewa fedha kutokana na ufinyu wa bajeti. Hata hivyo, jitihada zinafanyika ili kuweza kutafuta vyanzo vingine vya kutunisha Mfuko huu, ikiwa ni pamoja na kushirikisha makampuni binafsi. Pia mpango wa mabilioni ya JK, Mbeya ilipata milioni sita, Dar es Salaam ilipata milioni mbili, Singida 500,000,000; hili liliulizwa na Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda. Tathmini iliyofanyika ilionyesha Wilaya ya Chunya ilipata mkopo wenye jumla ya shilingi milioni 112,720 za *NMB* katika awamu ya kwanza, *CRDB* haikutoa mkopo katika awamu ya pili. Wilaya hii imepata mkopo wenye thamani ya shilingi milioni 50 kupitia *SACCOS* 10 na *SCCULT, SACCOS of Part* ni pamoja na Winome, Kambi Katoto, Chalangwa, Wakibi, Ukuna, Umako, Makongorosi, Imanagula, Sungusungu na Kanga. Mheshimiwa alisema kwamba, kwake hajapata chochote lakini tumetafuta taarifa tumekuta kwamba, kuna Kata ambazo zinaweza kupata. Namshauri akaangalie kama hizi hazikupata basi tuwasiliane ili tuweze kujua fedha hizi zilipelekwa wapi. (*Makofi*)

Hoja nyingine kwamba, Serikali inaweka uwiano gani wa kugawana fedha za JK; ameuliza Mheshimiwa Halima Mdee. Mpango wa uwezeshaji kwa mabilioni ya JK ulianzishwa kuwanufaisha wajasiriamali nchini kote. Shilingi bilioni 21 zilitengwa ili kila Mkoa upate wastani wa bilioni moja. Mpango huu siyo wa kugawa fedha kwa uwiano sawa kimkoa, bali kule kwenye wajasiriamali, vikundi na mtu mmoja, wanaopenda kujikwamua kiuchumi. Mpango huu wa awamu ya kwanza ulitumia Benki za Biashara za *NMB* na *CRBD* kwa kigezo cha mpango. Tunakubali kwamba, kwa awamu ya kwanza kulikuwa na matatizo, lakini kwa sasa tumeongeza vyombo 13 zaidi ya *NMB* na *CRBD*, kuna benki nyingine ndogo ndogo 13 ambazo tumezipa jukumu la

kutoa fedha hizi, tunategemea kwamba kwa awamu ya pili hali itakuwa nzuri zaidi kuliko ilivyokuwa hapo mwanzo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, aliliuliza Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, kuhusu *sovereign bonds* na kwamba, kwa nini hazimo kwenye bajeti hii. Hapo tulipofikia, tunatafuta kampuni ya kufanya *sovereign rating*. Kabla hatujaenda kwenye *international bond market*, lazima tufanyiwe tathmini kama nchi. Hili kwa Tanzania ni kwa mara ya kwanza. Hivi karibuni, Benki Kuu itateua mtu wa kufanya *sovereign rating*, baada ya hapo tutapata wale ambao watakuja kufanya hiyo kazi inayohusika ili tuweze kujiona Tanzania tupo wapi. Wenzetu wa Ghana, wamefanyiwa *frame rating* walipata B na wameweza kukopa kwenye *international Market* dola bilioni 750. *Gabon* wamefanyiwa *rating* wameweza kukopa dola bilioni moja. Tunategemea kwamba, sisi tunaweza tukapat *rate* ambayo ni nzuri kuliko hiyo waliyopata wenzetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kusahihisha waliochangia; Mheshimiwa Tungu Mpendazoe siyo Jungu Mpendazoe. Kwa hiyo, napenda kusahihisha.

Mheshimiwa Spika, tutakapofika mwezi wa 11 hapa, naweza kuahidi kwamba, Serikali inaweza kuja angalau na taa ya awali kuhusu *sovereign rating* tumefikia wapi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kutoa hoja.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)
KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 21 – Hazina

Kif. 2001 - *Government Budget Division* Sh. 570,809,339,300

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nilikuwa naomba tupate mwongozo wako, kwa sababu kifungu hiki kina *sub-vote* ya *Treasury Registrar* ambapo kuna maswali Waheshimiwa Wabunge tuliuliza na hatujapata ufanuzi wa Serikali. Hiki ni cha *treasury* na halafu huku kuna *vote* 50. Sasa nilikuwa naomba kufahamu ni eneo gani hasa ambalo naweza nikauliza kuhusiana na fungu la *Treasury Registrar* tuweze kupata maelezo ya Serikali?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, kuhusu *Bill* ukurasa wa 29 kuna *sub-vote* 2003 *Treasury Registrar* siyo hapa uliposimama.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2002 – *Policy and Research Division* Sh. 138,015,028,300

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2003 – *Treasury Registrar* Sh. 17,254,412,200

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, ni *sub-vote 2003 - Treasury Registrar*. Nakushukuru sana kwa jinsi ulivyonipa maelekezo. Katika eneo hili Waheshimiwa Wabunge, tulihoji kuhusiana na jinsi gani ambavyo Serikali inachukua hatua za kuiimarisha Ofisi ya Msajili wa Hazina ili ifanye kazi kuendana na sheria iliyoienda kwamba ni *corporation sole*, mpaka sasa hivi inafanya kazi kama idara tu yoyote ndani ya Hazina. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tupate ufanuzi katika eneo hilo ili tuweze kujiridhisha kwamba, kuna hatua za uimarishaji wa ofisi hii ili iweze kufanya kazi inavyopaswa kuwa ya kulinda mali ambazo Serikali inazo. Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, unaweza kusaidia mjadala kwa sababu una dakika tano umeachia hailengi kitu unasema tu kuimarisha; unakusudia nini ili Waziri ajibu mahususi?

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa mwongozo, kwa sababu tulilizungumza hili ndani ya Bunge mimi pamoja na Mheshimiwa Kilasi, lakini Waziri hajalijibu kabisa. Kwa hiyo, maelezo ambayo tuliyatoa wakati wa mchango ndiyo haya tunahitaji Waziri aweze kutolea majibu.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kutokana na muda, utaona kwamba kuna hoja nyingi za Wabunge zilitolewa lakini tumeshindwa kuzijibu zote licha ya kwamba tupo watatu. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Kabwe Zitto kwamba, suala la *Treasury Registrar* na idara nyingine pale Hazina, ambazo zina hadhi fulani fulani na kuna wazo kwamba, ama zifanywe *agency* au vinginevyo. Hilo limeshafanyiwa kazi na taarifa zipo kwa *Chief Secretary*.

Sasa kwa sababu ni taarifa za Kiserikali, nafikiri niachie hapo tu kwamba, Serikali imeliona na imeshalifanyia kazi si; *Treasury Registrar* peke yake, zipo pia idara nyingine ambazo zimefanyiwa kazi na Bunge litajulishwa baada ya *Chief Secretary* na sekretarieti kufanyia kazi na Baraza la Mawaziri kufanya uamuzi. (*Makofi*)

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *sub-vote* hiyo 2003, kifungu cha 280200, ningependa kukichanganya na kifungu cha 280500; naomba ufanuzi tu kama katika vifungu hivi ndipo zitakakopatikana fedha za kuongeza mtaji wa twiga *Bancorp*.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *book* hili hakuna bajeti yoyote kwa *Twiga Bancorp*. Kutokana na Kamati ya Fedha na Uchumi na Wabunge walivyozungumza, tumelichukua pendekezo tutalifanyia kazi fedha hizo zitatafutwa. Zitawekwa wapi? Tutawajulisha, lakini katika *book* hili hutazipata mahali popote.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya

Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 4001 – *External Finance Division* Sh. 5,895,418,800
Kif. 7001 – *Poverty Eradication and Eco
Empowerment* Sh. 1,735,326,200

*(Vifungu vilivyotajwa hapo vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali

Kif. 3001 – *Public Debt Management* Sh. 2,114,713,200
Kif. 3002 – *Expenditure Management* Sh. 655,963,000
Kif. 3003 - *Financial Management* Sh. 83,033,485,400
Kif. 3004 – *Systems and Internal Audit* Sh. 5, 774,150,700
Kif. 3005 – *Sub Treasury Arusha* Sh. 247,410,700
Kif. 3006 – *Sub Treasury Coast* Sh. 216,860,000
Kif. 3007 – *Sub Treasury Dodoma* Sh. 265,100,000
Kif. 3008 – *Sub Treasury Iringa* Sh. 216,152,000
Kif. 3009 – *Sub Treasury Kagera* Sh. 213,800,000
Kif. 3010 – *Sub Treasury Kigoma* Sh. 221,822,000
Kif. 3011 – *Sub Treasury Kilimanjaro* Sh. 229,328,000
Kif. 3012 – *Sub Treasury Lindi* Sh. 235,400,000
Kif. 3013 – *Sub Treasury Mara* Sh. 226,500,000
Kif. 3014 – *Sub Treasury Mbeya* Sh. 235,430,000
Kif. 3015 – *Sub Treasury Morogoro* Sh. 262,626,000
Kif. 3016 – *Sub Treasury Mtwara* Sh. 225,680,000
Kif. 3017 – *Sub Treasury Mwanza* Sh. 236,400,000
Kif. 3018 – *Sub Treasury Rukwa* Sh. 244,768,000
Kif. 3019 – *Sub Treasury Ruvuma* Sh. 219,437,000
Kif. 3020 – *Sub Treasury Shinyanga* Sh. 230,240,000
Kif. 3021 – *Sub Treasury Singida* Sh. 233,180,000
Kif. 3022 – *Sub Treasury Tabora* Sh. 241,114,000
Kif. 3023 – *Sub Treasury Tanga* Sh. 220,492,000
Kif. 3024 – *Sub Treasury Manyara* Sh. 223,690,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 7001 – *Pension and Gratuity* Sh. 818,314,000

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. *Sub-Vote* ndogo 260700 – *Rental Expenses*. Naomba nipate ufanuzi; kwa miaka miwili ya nyuma walikuwa wanalipa hizi *rental* lakini mwaka huu hakuna; je, wamejenga Ofisi au ni kwa sababu gani?

MWENYEKITI: Hebu rudia hicho, samahani kidogo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Kifungu kidogo cha 260700 - *Rental Expenses*; nilikuwa naomba tu kujua kama wamepata makazi mapya, kuna Ofisi au ni kwa sababu gani?

MWENYEKITI: Kuna sifuri pale. Mheshimiwa Waziri, kwa ufanuzi, kulikuwa na *rental* inalipwa halafu sasa hakuna tena.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunakodisha nyumba sasa tumepata nyumba yetu wenye. Ndiyo maana hakuna *rent* tena. Pale Hazina kuna majengo mapya yamejengwa. Kwa hiyo, kile Kitengo ambacho kilikuwa kina majengo ya kukodisha kilihamishiwa kwenye jengo letu.

MWENYEKITI: Umesema kwa lugha ya unyonge kabisa.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema ukifika pale Hazina, kuna majengo matatu mapya. Sasa miaka ya nyuma walikuwa wakikodisha lakini mwaka huu yale majengo yamefunguliwa, kwa hiyo, vitengo vyetu vingine vinahamia kwenye yale majengo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Hivyo ndiyo unatakiwa ujibu Waziri ambaye una-*control* trilioni saba. (*Kicheko*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Kif. 1001 – *Administration and General* Sh. 12,280,798,000

MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba ufanuzi kidogo tu; nilikuwa nimetoa ushauri kwamba, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu iongezewe uwezo iwe na Wakaguzi Wakazi (*Resident Auditors*) ngazi ya Wilaya na Halmashauri. Mheshimiwa Waziri, anasemaje juu ya ushauri huo?

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri tunaupokea na bahati nzuri mchakato huo umeshaanza. Ahsante.

MHE. JOHN M. CHEYO: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Wakati Mheshimiwa Waziri akijibu hoja ya Kambi ya Upinzani kuhusu kuwajibika kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, ameliambia Bunge kwamba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anawajibika kwa Rais. Jambo hili naona kidogo labda linahitaji ufanuzi, kwa sababu ukiangalia katika Katiba, *Section 143* na *Section* ndogo ya 4 inasema wazi kabisa kwamba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atalaeta Ripoti yake Bungeni na *product* ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ni Ripoti. Sasa kama

angelikuwa anawajibika kwa Rais, basi angepeleka Ripoti hiyo kwa Rais. Halafu ile *Public Finance Act* pamoja na Sheria ambayo tumeitunga juzi, inasema wazi kabisa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, atakagua mahesabu ya Serikali kwa niaba ya Bunge. (*Makofi*)

Sasa kama wewe unakagua kwa niaba ya Bunge; itakuwaje tena usiwajibike kwa Bunge? Hata ukienda kwenye *section* ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anaondolewa au kabla ya hapo; ukiona ile *section* ya nne na kifungu kidogo cha sita kinasema wazi; katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu na masharti ya ibara ndogo 2, 3 na 4 na ibara hii; Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, hatalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu mwingine yeyote au Idara yoyote ya Serikali. Maelezo hayo ya ibara hii ndogo hayataizua Mahakama. Anaendelea, huo tena ni ushahidi mwingine kwamba, hawajibiki kwa Rais, anachaguliwa na Rais, lakini kuchaguliwa na Rais haina maana kwamba kazi zake ...

MWENYEKITI: Anateuliwa.

MHE. JOHN M. CHEYO: Anateuliwa, haina maana kwamba, kazi zake anawajibika kwake. Si hivyo tu, mwisho kabisa hata akitaka kumwondoa Mheshimiwa Rais, anapaswa kwenda kwa Tume Maalum. Kuna utaratibu ambao umewekwa kwenye kifungu cha 144(3). Hata akimaliza kazi zake, mtu ambaye ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu aliyewahi kuwa Mdhibiti Mkuu wa Hesabu, hawezi kuteuliwa kushika au kushikilia madaraka ya kazi nyingine yoyote katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo, vyote hivi vinaashiria wazi kabisa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali hawajibiki kwa Rais anateuliwa na Rais. Kwa kuwa kazi ya Bunge ni kudhibiti matumizi ya Serikali, hawezi tena huyu akawajibika kwa *Executive*. Naomba ufanuzi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Niseme tu, Waziri huna haja; hili ni eneo moja ambalo bado tunalifanya kazi na Utawala. Kilichopo sasa siyo *best practice*. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa John Cheyo, tutaendelea kujadiliana ili jambo hili likae vizuri, kusiwe na utata tena. (*Makofi*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*
Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Uchumi

Kif. 1001 – *Administration and General* Sh. 9,491,457,900

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Hausikiki.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza. Mimi nilitaka nipaye ufanuzi mdogo tu kuhusu eneo la misamaha ya kodi. Katika eneo hili, kuna malalamiko makubwa kwamba, Serikali

inapoteza pesa nyingi kutokana na kusamehe watu ambao hawapaswi kusamehewa. Kuna maeneo kama Sekta ya Madini na Sekta mbalimbali za uwekezaji, ambako Serikali inapoteza hela nyingi sana kwa kusamehe hawa wawekezaji. Kuna mifano ya watu ambao wanajifanya wawekezaji, wanamiliki zana mbalimbali za kazi, lakini wana msamaha mkubwa sana wa mafuta. Je, Serikali ina mpango gani wa kurudia utafiti kwa wawekezaji kama hawa ili kuona kama wanastahili au hawastahili kusamehewa kodi hizo. Ahsante.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Mbunge. Niligusia kwenye majumuisho yangu kwamba, tuna-review hiyo misamaha, pamoja na misamaha ya mafuta na mambo mengine. Hata kwenye Kamati ya Mheshimiwa Jaji Bomani, kuna pendektezo kule ambalo wamependekeza kwamba, hiyo iwe *reviewed* na ilipelekwa kwenye Kamati ya Fedha. Nilisema kwamba, tuna-review maeneo mengine, nadhani tumeshapata mahali ambapo tunataka kwenda kwenye *Cabinet*, lakini maeneo mengine inabidi kufanya *cross-reference* ya mapendektezo ya Kamati ya Jaji Bomani na mikataba ambayo yale makampuni inayo ili tutakopokuja kufanya *review* isiwe *review* ambayo tunaweza tukapelekwa Mahakamani.

Kwa hiyo, tunakubali kwamba inawezekana ni pesa nyingi sana ambazo zinasamehewa mafuta, lakini tunaomba tupewe muda tuifanyie kazi kwa makini, ili tutakopokuja kuleta mapendektezo Bungeni, yawe ni mapendektezo ambayo yanatekelezeka. Ahsante.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Mheshimiwa Waziri mtoa hoja ni rafiki yangu sana na sina haja ya kutoa au kushika mshahara wake. Vipengele ninavyovihoji hapa ni katika kumjenga yeye mwenyewe ili ajipange sawa sawa. Nilipokuwa nachangia kwa kuongea, nilihoji kama Serikali ina Sera ya Magari na mtoa hoja hajalitolea ufanuzi hilo. Utaona kwa mfano, Serikali ya Uingereza, Malkia anatumia *Rolls-Royce* ndiyo Sera yao hiyo; Waziri Mkuu, anatumia *Jagwa* na Mawaziri wengine wote wanatumia *Ford*. Kwa hiyo, huko chini Wakurugenzi nao wanatumia magari madogo madogo. Chukua Serikali ya India, wao wameamua wote wanatumia magari yanayoitwa Mohinda. Sasa hapa kwetu utakuta Waziri anatumia *VX* na Naibu Waziri anatumia *VX*. Mkurugenzi huyu anatumia *Lexas* na yule anatumia *Range Rover*. Sera ya magari ni nini? Hiyo ya kwanza. (*Makofii*)

Ya pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nikitoa mchango wa maandishi, nilisema kwa nia nzuri kabisa, Serikali ilimnunulia Mheshimiwa Rais mpendwa wetu, ndege kwa ajili ya kufanya kazi. Bahati mbaya hiyo ndege inabeba abiria 12, wakati msafara wa Rais; *minimum* iwe *regional* au *international* ni watu 18. Sasa jana mtoa hoja alisema, haujafika wakati wa kuiiza ndege hiyo kwa mabepari ambao wanataka kuitumia *individually*, waweze kumnunulia Mheshimiwa Rais ndege ya kufanya kazi. Naomba ufanuzi. (*Makofii*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali kwamba, Mheshimiwa Mwambalaswa ni rafiki yangu sana kabla hata hatujawa

Wabunge. Tatizo ni muda wa saa moja na hoja ambazo Wabunge wengi walizitoa ni nyingi kweli kweli hata kama ningepewa saa mbili, bado nisingeweza kujibu. Kwa hiyo, tulichofanya ni kujaribu kujibu pale tulipoweza na pale nilipoishia ikabidi niachie hapo.

Serikali inalifanyia kazi suala la Sera ya magari. *Actually*, Wizara inayohusika hasa na Sera hii ni Wizara ya Miundombinu, pamoja na Utumishi na Mkuu wa Utumishi Serikalini. Kwa hiyo, kuna ofisi tatu; Miundombinu, Utumishi na Ofisi ya Rais (*Chief Secretary*). Katibu Mkuu wangu bahati nzuri amehusishwa, nadhani kwa vile ndiyo tunaotoa pesa. Kwa hiyo, nafahamu kinachoendelea lakini ile *review* haijamalizika. Napendekeza tu kwamba, tuachiwe Serikali tuikamilishe, nadhani tutakuja na hiyo Sera wakati muafaka baada ya kukamilisha hii. (*Makofi*)

Kuhusu Ndege ya Rais, ningeomba tulichukue. Sina jibu la moja kwa moja; mimi kama Waziri wa Fedha, siyo mtaalam sana. Utaalam wangu ni ku-value shilingi, mambo ya *inflation* na ku-stabilize uchumi. Haya ndiyo ya kwangu. Hili naomba nilichukue, tutalizungumza Serikalini na kuleta taarifa kwa wakati muafaka. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, mtakapokuwa mnapanga haya mambo ya magari msiingilie mihimili mingine; tuachieni Mahakama na Bunge, maana ninyi kujilinganisha kila saa haiwezekani. Msije mkasema Mahindra hapa na Spika apande Mahindra, hapana. (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Sawa Mheshimiwa Mwenyekiti.

MHE. JOHN P. LWANJI: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Mimi katika mchango wangu, nilieleza bayana kwamba, kuna tatizo na nina watu sehemu yangu ya Itigi na Manyoni, ambao bado wanadai mafao ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sasa nisingependa kuonekana kwamba nashabikia sana suala hili, lakini tatizo bado lipo. Wanadai; wengine hawajalipwa kabissa na wengine wamelipwa nusu. Sasa wanansumbua mara kwa mara. Ningeliomba Serikali iwe *serious* kwa hili. Waziri ametoa ofa kwamba, waende ofisini. Sasa je, Serikali ipo tayari kuwalipa nauli, posho ya njiani na malazi mpaka hapo watakaozungumza na Mheshimiwa Waziri aweze kuwatatulia tatizo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kwamba, Mkoo wa Singida nadhani kiutaalamu kwa upande wa uchumi, hawajaelewa vizuri. Mkoo huu umekaa kama kiatu vile, hapo unapoingizia ndiyo unatoka; sehemu za Kintinku unakwenda Manyoni halafu unapinda kulia unakwenda Singida, Iramba unatoka. Kusini mwa reli karibu asilimia 60 ya mkoo ndiyo umekaa; asilimia 58 ya Mkoo wa Singida ipo Kusini. Huwa wanauangalia juu juu tu. Sasa kutuambia kwamba, katika hizi fedha za MCC, wale waliopewa mpaka waboreke na ndiyo tutaona sisi tutanufaika na matunda ya hao haileweki.

Mimi ningeisihi sana Serikali, kwa sababu fedha hizi zinakuja kwa awamu, basi wajaribu kuangalia kama wanaweza kufanya *re-allocation* ili kuweza kuihusisha miundombinu ya ndani ya Mkoo. Nadhani inaonekana kwamba, hiyo barabara

inayojengwa sasa hivi ni sehemu ndogo sana; inapita pembeni mwa Mkoa wa Singida halafu ni *National Road*, wakati wenzetu wapewa himo pesa lakini wana barabara za lami miaka nenda rudi. Mimi ningelipenda nipate ufanuzi; kwa kuwa inaonekana kwamba wataalamu wa uchumi hawauelewi vizuri mkoaa huu; je, wapo tayari kuleta wataalamu hao ili waweze kutathmini na kuulewa vizuri Mkoa wa Singida? Ahsante.

MWENYEKITI: Kwa lile la kwanza, hakuna jipyaa. Nadhani utawasaidia sana wapiga kura wako, kwa sababu ulionyesha makaratasii hapa. Pengine ni vizuri sasa ili kwenda jina kwa jina, wale unaosema wanakusumbua; wewe upo hapa shirikiana na Naibu Waziri, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, naona ndiyo amekabidhiwa hili; tuone linafika wapi, halafu basi kama Novemba litakuwa bado lipo, tutaona namna ya kusaidia tufike wapi. Najua watajibu hivyo hivyo na itatupotezea muda, ila hili la pili sasa la Singida kuwa kama kiatu. (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida siyo kiatu ni mkoaa kama ilivyo mikoa mingine. Pesa za *MCC*, tulikubaliana baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Wamarekani kwamba ni miradi gani, tuliwapelekeea miradi mingi tu mikoa yote ilikuwa inafikia karibu bilioni nne. Baada ya kuichambua ile miradi, wakatuelekeza kwamba, kwa awamu ya kwanza tunataka tusaidie miradi hii. Kwa hiyo, wakaja kwenye elimu, umeme, barabara, maji; miradi ambayo wao walifikiri kwamba, kwa kusaidia miradi hiyo, wanaweza wakaisaidia jumuiya kubwa zaidi na pana yale maeneo ambayo miradi hiyo ipo. Dola milioni 698 au 700 milioni ni ya awamu ya kwanza.

Sasa awamu ya pili nafikiri tuanze kuipokea hiyo miradi sasa, ili tutakapokuja kuzungumza nao kwenye mwezi Novemba, tuwe tumeshapa ile miradi mingine kwa mfano ya Singida. Si kweli kwamba, ningetaka kuondoa hiyo dhana kwamba, Singida ni Mkoa ambao wengi hatuufahamu au ni kiatu; hapana. Hata kama siyo wote ambao tunaishi kule, lakini kijiografia tunaufahamu vizuri. Kuna uchumi kule mzuri, hata kama hakuna viwanda, lakini yapo maeneo mengine ambayo ninyi ni *better* kuliko mikoa mingine.

Kwa hiyo, tuchukue kwamba, awamu ya kwanza Singida haikuwemo, lakini Ruvuma ipo. Awamu ya kwanza Kigoma ipo, Malagarasi kule, Sumbawanga ipo kutegemea jinsi tulivyokubaliana na pesa zilizokuwepo. Sisi kwetu milioni *700 dollars* ni pesa nyingi sana, kwa Bush ni pesa ndogo. Yeye anasema *I will give you this*.

Mimi nafikiri kama ile miradi ambayo tayari unafikiri kwamba ni muhimu sana kwako ianzie sasa, tuletee hiyo mapema na tutahakikisha kwamba, tunaiweka kwenye orodha yetu. Bahati nzuri, ofisi imeshaanzishwa. Mkuu wa ile ofisi ni Mtanzania, Ndugu Benard Mchomvu, aliyekuwa Katibu Mkuu, Viwanda na Biashara, ambaye ni mchumi mzuri sana.

Anafahamu kuchambua miradi na Wamarekani wenyewe wametuletea watu karibu watano wa kutusaidia kuchambua hiyo miradi. Tulichochukua awamu ya kwanza, awamu ya pili inakuja; kama ipo sawa sawa tuletee tutaichambua.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lwanji, naona bado hujaridhika?

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ningependa kufafanua tu kwamba, sikusema Mkoo wa Singida ni kiatu. Nimesema unafanana, yaani ilivyokaa; kwa hiyo, hapa isije ikaeleweka vibaya. Nimeridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri na kwa hiyo naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana na mfano wa kiatu wala usiuogope. Kwa mfano, leo Spika amevaa kiatu cha *bally cha* Switzerland. Kwa hiyo, lazima kiatu kiwe ni cha ovyo ovyo. (*Kicheko*)

MHE. SIJARU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuomba ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kuhusiana na kauli ya Waziri Mkuu, baada ya Wabunge wa Tabora kuomba sana ile Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora – Kigoma itengewe fedha. Ilipendekezwa kwamba, zitatengwa bilioni kumi kwa kuanzia. Sasa nataka kufahamu tu kutoka kwa Waziri wa Fedha, kama hizi bilioni kumi tayari keshazitenga na kama amezitenga atazipitishia moja kwa moja *TANROAD* au Wizara ya Miundombinu?

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Waziri, nashukuru kwa swali. Kwanza, uamuzi wa Waziri Mkuu tumeutekeleza, shilingi bilioni kumi zimetengwa. Kwa sababu zimetafutwa na kutengwa baada ya Bajeti Kuu kupitishwa, tutaitela hapa kwa wakati muafaka kwa ajili ya kibali cha Bunge kuonyesha zimetoka wapi na kwa nini tunazipeleka Tabora.

MHE. SIJARU J. KABOYONGA: Nimeridhika nusu, lakini nusu inanichanganya kwa maana kwamba, zitaletwa hapa habari zake. Sasa je, matumizi yake yatasubiri mpaka ziletwe hapa habari hizo au tutaanza kutumia halafu mtaleta kwa taarifa?

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno mengine huwa tunauma uma, kwa sababu yanaandikwa kwenye magazeti. Kuna utaratibu wa matumizi wa Serikali, tukipata *extra cash* mahali fulani, kifungu fulani cha sheria kinampa Rais madaraka ya kuweza kumwagiza Waziri atumie na halafu uamuzi huo wa Rais uende kwenye *Cabinet* na baadaye ufikishwe Bungeni. Kwa hiyo ni utaratibu, lakini ninapokwambia hivi sasa mimi pesa ninazo ila siwezi kukueleza nimezipata wapi.

Kwa hiyo, nataka kukuhakikishia kwamba, Waziri Mkuu ni bosi wangu, ameahidi ndani ya Bunge; ni wajibu wangu mimi kuzitafuta. Nimeshazitafuta na pesa hizo zitapatikana. Sasa tutaangalia kama zipelekwe kwenye Barabara ya *TANROADS* au Barabara ya Kitaifa. Hilo litakuwa ni utekelezaji, lakini pesa zitapatikana na tutafanya ule utaratibu unaotakiwa ili baadaye muelewe kwamba pesa zilitoka wapi na kwa nini zimepelekwa Tabora. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri; sijui kwa nini unazungukazunguka, hizi si ndiyo zile za kuweka lami Tabora - Urambo au siyo hizo; ya nini kuzungukazunguka mambo mepesi kama hivi? (*Makofi/Kicheko*)

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Nilikuwa naomba ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kuhusiana na Waraka uliotoka Ikulu miaka ya 80. Waraka huo ulikuwa hauruhusu Wabunge ambao ni wasimamizi, kuingia kwenye Bodi na kuwa Wakurugenzi katika hizo Bodi mbalimbali za Mashirika, kwa sababu ya kuondoa mgongano wa kimaslahi. Sasa nataka kujua Waraka huu unatekelezwa vipi?

Suala lingine, nataka kujua kwa nini kuna tofauti ya takwimu, Juni 12 wakati akiwasilisha hotuba yake hapa alituambia kwamba, Sekta ya Maji imetengewa shilingi bilioni 230, lakini siku ya Wizara ya Maji yenye Waziri aliomba shilingi bilioni 156; sasa nataka kujua hapa kwa nini kuna tofauti ya bilioni 74? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri au labda nimwombe, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi kuhusu *circular*. Mheshimiwa Waziri wa Fedha haya.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *circular* nadhani dada yangu Mheshimiwa Hawa Ghasia atanisaidia. Kuhusu bajeti ya Wizara ya Maji ni kweli tulipoangalia tulikuta *correct* ile milioni 156.

Nilichosema mimi, kwa mfano, ukizungumza bajeti ya elimu trilioni moja bilioni mia nne sitini na tatu, ukienda kwenye Wizara ya Elimu huwezi kuzikuta hizo zote kwa sababu ni Sekta ya Elimu. Sasa bilioni 230 ni kwa sekta ya maji, ambayo ni pamoja na maji yanayokwenda kwenye Halmashauri za Wilaya na mahali pengine. 156,000,000 alizokuwa nazo Mheshimiwa Waziri wa Maji ni za kwake yeye Wizara ya Maji na Umwagiliaji na hizo dada yangu Mhonga ni *correct*, nimecheki na hizo *figures* zipo sawa, 156 ni sawa na 230, nyingine atajibu mwenzangu. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kutoa ufanuzi wa Mheshimiwa Mhonga Said Ruhanywa kama ifuatavyo:-

Kwa kawaida, nyaraka huwa zinafutwa na nyingine zinahuishwa na kurekebishwa. Hivi sasa si kweli kwamba, Wabunge wanakataliwa kuingia katika Bodi, inategemea ni aina gani ya Bodi. Bodi nyingi Waheshimiwa Wabunge wanaruhusiwa na hatujawa na Waraka ambao unawakataza kuingia. (*Makofi*)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, nilizungumzia hapa suala la matatizo ambayo yapo katika bajeti yetu kutoka Serikali Kuu na kwenda kwenye Serikali za Mitaa. Bahati mbaya Waziri hakufafanua lolote, lakini moja ambalo hata hilo alilolisema sasa hivi la Wizara ya Maji

na takwimu ambazo Waziri wa Maji amezitoa, bado Wabunge watakuwa wanakanganyika na bado utaratibu wetu wa bajeti utakuwa na matatizo.

Je, Waziri haoni kwamba bado kuna matatizo ya msingi juu ya kujua kima halisi ambacho kinakwenda kwenye kila Wizara kutokana na tatizo mtambuka lililojitekeza hivi sasa na kwa maana hiyo Wabunge hawapati takwimu sahihi ambazo zinakwenda kwenye fedha; je, anakubaliana na ule ushauri nilioutoa kwamba ni wakati muafaka sasa tukae na Kamati ya Fedha na Uchumi tupitie vifungu kwa vifungu tuone kweli hizo pesa zimekwenda, kwa sababu hizo anazozisema nina hakika kabisa kwenye Halmashauri itakuwa hazipo ila katika vitabu hapa inaonekana kama zipo, fedha yenyewe *actually* hakuna? Sasa Je, Waziri anakubali ule ushauri niliompa wa kwanza? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la pensheni ya watu ukiacha ile ya Afrika Mashariki. Waziri hapa amesema kwamba, watu wakienda wanaweza kupata na kadhalika. Mimi mwenyewe nimeshakwenda na mdai mara sita Wizarani, nimeshaandika barua sita Wizarani, lakini hata barua moja bado haijajibwa. Mimi Mbunge, watu wangapi wana nafasi ya kwenda huko Wizarani na Wabunge kwenda kudai? Lipo tatizo la msingi la kulipwa pensheni watu wetu na hasa warithi.

Hivi sasa mimi ninazo zaidi ya kesi kumi unazipeleka Wizarani hakuna anayeshughulika. Bado Serikali haijatoa utaratibu mzuri na hasa warathi kuweza kupata pensheni za watu wao na haki za watu wao. Waziri atueleze ni utaratibu gani mzuri; sio wa kumuata Wizarani, Wizarani mimi nimeshakwenda mara chungu nzima. Nimeonana na Waziri Meghji, nimeonana na Naibu Waziri, nimeonana na Waziri Mwenyewe, nimeandika barua, nimekwenda kwa Katibu Mkuu, nimekwenda kwa watu wote wa Utumishi, bado majibu hayapatikani kwa watu wa mirathi, hebu tuambieni ni utaratibu gani wananchi hasa warithi utawawezesha kupata haki zao? Ahsante sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hili la mirathi nitamwachia Mheshimiwa Omar, maana ndio mtaalamu wa mambo hayo pale Wizarani. Hili la bajeti kutofautiana kati ya Bajeti Kuu na bajeti za Halmashauri, hatuna tatizo kukaa na Kamati. Kwa mfano, lilitotokea hili la Wizara ya Maji, mimi mwenyewe nilishtuka siku ile, lakini baada ya kwenda kucheki nikakuta tarakimu zipo sahihi kabisa hazina hata matatizo; zinaonyesha ngapi zinakwenda Halmashauri, ngapi zinakwenda huku na ngapi zinakwenda kwenye ile Wizara.

Tatizo tulilonalo ni kwamba, kuna pesa ambazo Wizara inahusika na TAMISEMI; kwa hiyo, jumla kuu inakwenda TAMISEMI. Sasa TAMISEMI pale ndio unawenza kupata kiasi gani kimekwenda Kilosa, kiasi gani kimekwenda Urambo, kiasi gani kimekwenda wapi na kiasi gani kwa bajeti nyingine kimekwenda mkoani. Sasa mimi sina tatizo kabisa, kwa wale Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, nafikiri tumekubaliana kwamba, kwa mwaka ujao wa fedha, tutakaa mapema sana kupitia kila *figure* ambayo tunayo. Mimi nakubali kabisa kwamba, wakati wowote bajeti yetu ikiwa tayari, tutakaa kati ya Wizara, Wataalamu na Kamati, mimi mwenyewe na Kamati ili tutakapokuja hapa Bungeni kila mmoja angalau ajue anaweza aka-*trace* kwamba 230,000,000 ngapi zinakwenda Wilayani na ngapi zinakwenda kwenye Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kabisa ambalo ninaweza kukwambia ni ugomvi na Waziri wa Elimu kwamba, mle Bungeni umeniambia mimi napata trilioni moja bilioni mia nne sitini na tatu, mbona bajeti yangu ni *less than 600,000,000?* Baada ya kumwonesha *figures* tumeshaelewana hakuna matatizo. Kwa hiyo, mimi nakubali Kamati tutakapofika, tutakubaliana tu ni muda gani ili iwe mapema kidogo kabla ya Kamati ya Bunge Zima, hatujaenda kwenye mipango.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. OMAR YUSSUF MZEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba nitoe ufanuzi juu ya suala zima la mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa mirathi; nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kweli kuna matatizo ya ucheleweshaji lakini nataka nieleze tu kwamba, mchakato wa mirathi nao ni mrefu sana. Hii ni kutokana na kwamba, tunaogopa tusije kuwalipa watu amba si wahusika. Kwanza, mchakato unaanza kwa kikao cha familia; familia yenyewe inakaa wanakubaliana mpaka wateue msimamizi wa mirathi na wao vilevile wanachukua muda. Wanavutana, nani awe msimamizi; mke wa marehemu au mtoto wa marehemu. Vilevile wakishamaliza hapo wanatakiwa waupeleke Mahakamani ule mchakato wa kumteua msimamizi wa mirathi ili Mahakama itoe kwamba huyu ndiyе aliyeuleliwa kuwa msimamizi wa mirathi. Hata hivyo, ikimalizika hapo ile haitakiwi kuja moja kwa moja Wizara ya Fedha, inapitia katika taasisi yake; taasisi yake ndio inayoweka zile *documents* zote pamoja na faili lake analileta Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukishamaliza sisi Hazina kupitia zile nyaraka zote na vielelezo vyote ambavyo vinatakiwa kuwemo mle ndani, tukishaona *the file is complete* tunaandika cheque, kiutaratibu ile cheque inatakiwa tena irejeshwe kulekule Mahakamani walikofungua hiyo mirathi. Kwa hiyo, tatizo hapa linaweza likatokea, mimi binafsi nimeshakumbana nalo; wanakuwa hawaweki hata namba za simu, cheque ile ikishafika inakaa pale Mahakamani. Mimi binafsi nimegundua hilo, wamekuja watu pale ofisini wamelalamika, wamesema cheque zao hawajazipata, nilipofutilia Mahakamani zilikuwepo lakini hakukuwa na anuani zao au namba zao za simu za kuweza kuwaita.

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, hayo matatizo yapo lakini nataka nimhakikishie kwamba, tutayaangalia ili tuweze kuyarekebisha, tupunguze hizi kelele au hii nenda rudi; hizi ni kero. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutalifanyia kazi na *Inshallah* Mwenyezi Mungu, atatusaidia tuweze kupunguza hizi kelele. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, zikiwa zimebakia dakika tisa tu, naomba nitumie Kanuni ya 104(1) kuongeza muda baada ya saa 1:45; dakika zisizozidi 30. Tunaendelea, Mheshimiwa Dr. Slaa.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi ninazungumzia suala ambalo nililieza kwa kirefu kwenye mchango wa maandishi; nilieza kwamba, iwapo sitapata majibu ya kuridhisha ninaweza kwenda kwenye kifungu cha kutoa shilingi, hatimaye kuomba hata kuunda Kamati Teule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikia hapo kwa sababu leo ni karibu mara ya saba ndani ya Bunge hili, tangu Bunge lililopita, ninahoji juu ya suala la Wastaifu wa Afrika Mashariki sipati majibu. Waziri amejibu hapa, ametupa takwimu za waliolipwa na ambao hawajalipwa. Ametueleza tofauti ambazo hawajalipwa na cheque za watu 6000 zipo tayari, sina ubishi na hawa. Leo kidogo Waziri ameenda mbele zaidi, kwa mara ya kwanza amejibu kwamba, wamelipwa *compound interest* ya 17%, leo hii inasemwa mara ya kwanza katika muda wote huo; sasa *compound interest* kwa nini; si ajabu Wabunge wengi hatujui?

Nimefanya utafiti wa suala hili, fedha hizi zimetoka na zimelipwa na Waingereza. Nilimwambia Waziri anijibu kama si kweli, kwa sababu taarifa tulizonazo zinaonyesha kwamba, zimetokana na mtiririko wa nyuma tangu *East African Common Services*, ndio maana Mwingereza akalipa. Kwa sababu zimetoka kule, zilikubalika zilipwe kwa fedha za kigeni za dola, wao walileta kwa *British Pound*. Nchi zote tatu zilikubali zilipwe kwa fedha za kigeni, kuepuka badiliko la viwango vya dola kwenda kwenye fedha za Tanzania, za Kenya au za Uganda. Wenzetu wa Kenya na Uganda, walilipa mara moja palepale, sisi Tanzania niliuliza kwenye hoja yangu, kwanza Waziri aniambie zilikaa wapi na zilifanya nini muda wote? Sijapata jibu. Ya pili, *rate of exchange*, yaani kiwango cha kubadilisha fedha za kigeni wakati ule na leo, tofauti ni kiwango gani? Je, ni kweli hizo 17% ambazo zimelipwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linanifikisha hapa kwa sababu wale wazee ni wetu, wanatoka nchi nzima waliopo Dar es Salaam ni wachache tu, wengine wametapaka nchi nzima hawawezi kusafiri kwenda kudai. Wapo waliokufa hawajapata haki zao, waliolipwa hizo 17% inawezekana wamelipwa kweli lakini ndani ya Bunge hili, kuna ahadi iliyotolewa kwanza na Rais Mstaifu nje ya Ukumbi ya kuwalipa wastaifu bilioni 450 na wakaandika kitu kinachoitwa *deal of settlement* nadhani. Kwenye taarifa niliyoipata, Serikali ikalipa bilioni 117, tofauti iliyobaki kati ya 450 na 117 italipwa lini? Je, kiwango hiki kinafanana na alichosema Mheshimiwa Waziri kwamba ni sawa na 17% ya *compound interest*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa hili suala lina utata, leo ningependa kujua Waziri anipe uhakika; hatuwezi kama Taifa kuona aibu ya wazee wetu kila siku wanaandamana, mara ya mwisho wamekwendwa Ikulu na hatuwezi kuwaambia kwamba hawawezi kuwadai mmoja mmoja kwa sababu alizozieleza Waziri.

MWENYEKITI: Dakika zako zimeisha.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba Kamati ya Bunge ishughulikie suala hili pamoja na Kamati ya Serikali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. OMAR YUSSUF MZEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nataka nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba, kila ambaye hajalipwa atalipwa, hakuna ambaye hatutamlipa. Nataka nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba, nilisema pale kwamba, wenzangu wanafahamu hesabu,

wanaelewa nini maana ya *compound interest*, nataka nifafanue tu kidogo ili kuweka mambo sawa.

Compound interest maana yake ni nini? Maana yake una kitu unadai nakuongezea 17.53% juu yake, halafu *plus* ile *interest* kinakuwa kitu kizima. Mwaka wa pili nakiongezea tena 17.53%, mwaka wa tatu kinakuwa kitu kizima, hiyo ndiyo *compound interest*, kila mwaka naipiga na *interest* ya 17%, sio mara moja tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niseme kwamba, suala la Mheshimiwa Dr. Slaa tumelipokea na kwa sababu linahitaji takwimu za uhakika, twende nyuma zaidi, namwomba atupe muda tulifanyie kazi ili tuweze kutoa majibu sahihi hasa. Kwa sababu anaponiuliza mimi kwamba kilicholetwa na kilichoahidiwa na Rais, lazima na mimi nirudi nyuma kabisa nikaangalie hicho kilicholetwa na kimeletwa mwaka gani? Lazima tukubali kwamba, kama kimeletwa katika miaka ambayo nchi hii Watanzania hawaruhusiwi kulipwa kwa dola, inawezekana ndio sababu Serikali haikuweza kuwalipa wakati ule *foreign currency*. Kulikuwa na sheria ambayo haiwaruhusu Watanzania kumiliki. Kwa hiyo, atupe muda twende nyuma na mimi niangalie muda na *amount* ilioletwa, ili tukija kumjibu tumjibu kwa maelezo sahihi kabisa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nadhani Dokta, inasaidia hii au? Hebu kwa kifupi basi.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi na nilisema nitakwenda kwenye kutoa shilingi. Kwanza, kwa sababu moja kubwa, suala la *compound* mimi ninalielewa lakini halikuwepo kwenye mkataba. Kwa hiyo, hata wale wahusika kama hawakuelezwu ndio maana wanataka wakae pamoja na Serikali.

La pili, Waziri anihakikishie sasa hili jibu alilolitoa leo kwenye *Hansard* nadhani ya mwezi wa nne, lilijibiwa hivyo hivyo. Nataka uhakika sasa, hili jibu la uhakika analosema atalileta; atalileta lini ili Bunge hili liweze kujihakikishia? Hatuwezi kuwa na majibu ya aina hii kila siku halafu wazee wetu wanaendelea kuhanganya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri? Novemba ni karibu mno au?

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wastaifu wa Afrika Mashariki; kwanza, lina mkataba, walikuwa na wawakilishi wao, wakakaa na Serikali. Malipo yote yanayofanywa, yanafanywa kwa kutumia mkataba ule. Tunachosema, tumefanya mashauriano hapa kwamba, maadam umezungumzia kwamba si wengi ambaao wanaelewa *compound interest* na wewe umezungumzia pia kwamba, inawezekana kuna pesa zimetoka Uingereza kuwalipa watu hawa. Sasa vitu hivi kama Waziri, siwezi nikasimama hapa nikasema kweli Waingereza walileta pauni 2,000,000 au walileta pauni 50 halafu kweshokutwa useme *no*, walileta pauni 20; kwa kweli hakuna Waziri ambaye anaweza akaja Bungeni akasema uwongo.

Sasa ndio nasema, kwa sababu yanajitokeza mambo ambayo hayakuwemo katika ile hotuba yangu wala jibu langu nililokuwa nimelitoa, basi wewe tupe muda tukalifanyie

kazi. Ila la 17% la *compound interest* hilo tunalifahamu. La kwamba kuna fedha Uingereza, hatuna uhakika asilimia mia moja, kwa hiyo, hayo yote yafanyiwe kazi halafu Mheshimiwa Spika, ataamua lini anataka sisi tulete. Tunaweza tukalitoa kwa njia mbili; ama kuleta katika kikao kijacho kuja kulizungumzia au kulileta kama Kauli ya Serikali, tunaweza tukatoa katika njia mojawapo kati ya hizi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Sawa, itasaidia hasa ikiwa ni Novemba hii inayokuja. Serikali ya kasi mpya, lazima sasa miezi miwili na mitatu, takriban karibu mitatu nadhani mtaweza. Mheshimiwa Kabwe Zitto.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Wakati nachangia kwa maandishi na nilipochangia kwa kuzunguma, nilizungumzia tatizo ambalo lipo hivi sasa kwenye Mashirika ya Umma la watu wanaoteuliwa kuingia kwenye Bodi za Mashirika ya Umma kwenda kushiriki kwenye kazi za Bodi bila kufanya mawasiliano yoyote na mwenye mali, yaani Wizara ya Fedha kupitia kwa Msajili wa Hazina.

Tumekutana na hali hiyo kwenye mashirika mengi sana, ambayo tunafanya nayo kazi; anatoka mtu nyumbani kwake huko anakurupuka anakwenda kwenye kikao cha bodi anarudi mwenye mali hajui chochote kinachoendelea. Matokeo yake ni kwamba, kuna mali nyingi sana za Serikali ambazo zinapotea na wale amba wanapaswa kuzilinda kama Wakurugenzi kwenye hizo Bodi hawafanyi kazi ambayo inastahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa napenda kufahamu Waziri anasema nini kwa utaratibu huu? Kumetokea baadhi ya Wakurugenzi; Msajili wa Hazina anapotaka wapeleke maelezo yao Wizara ya Fedha, wanasema kwamba wao wanapeleka kwa Wizara Mama. Kwa hiyo, kuna tatizo pia kati ya Wizara, yaani wale amba wanateuliwa na Hazina kwa maana ya Wizara ya Fedha, lakini mwenye mali ni Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, nilikuwa naomba mwenye mali atoe kauli leo ya kiserikali kwamba, anasema nini kwa hawa watu amba wanateuliwa kuingia kwenye Bodi kwenda kulinda mali zetu kama Watanzania lakini hakuna *any reporting mechanism* ambayo wanaifanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilikuwa napenda tu Serikali ifahamu kwamba, tulipokuwa tunazungumzia mashirika ya kuyaongeza kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam, tulikuwa hatuna maana ya mashirika ambayo yapo sasa chini ya *Consolidated Holdings*, ambayo yapo *specified*. Kuna mashirika ambayo tayari yapo nje ya *specification*, kwa sababu yameshabinafsishwa. Tilitolea mfano na Waziri ameuelezee vizuri wa Celtel/Zain na ninashukuru kwa maelezo ambayo Waziri ameyatoa. Tumetolea mfano wa NBC, tumetolea mfano wa Twiga, ambayo Serikali inamiliki 100% na mashirika mengine mengi tu ambayo Serikali inafahamu kwamba, hivi sasa yanafanya faida na tunaweza tukayapeleka kwenye soko la hisa tukasema kwamba, tuweke *target* angalau tufikie mashirika 20 itakapofika mwaka 2010. Serikali bado haijatoa maelezo kuhusiana na hili na vilevile haijatoa maelezo kuhusiana na ombi la *Dar es Salaam Stock of Exchange* kuchukua Jengo la Benki Kuu ili kuweza kuimarisha *financial distribution* yetu. Nilikuwa naomba maelezo kutoka Wizara ya Fedha.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda nimshukuru Mheshimiwa Zitto Kabwe, ndio kwanza amekuwa Mwenyekiti wa *POAC*, kwa hiyo, Wizara ya Fedha inaanza kupata faida ya Uenyekiti wake. Kama kweli wapo Wajumbe wa Bodi ambao wanakwenda kuhudhuria kikao, inakuwa kama amehudhuria yeche mwenyewe na haleti taarifa kwa mwenye hisa, hilo *definately* ni kosa. Kwa hiyo, tutalisahihisha hilo na ninadhani tutamwagiza *Treasury Registrar* aweze kuhakikisha kwamba wanaleta.

Mimi mwenyewe nimewahi kuwa *Treasury Registrar* kwa miaka minne pale Hazina na kwa hiyo, naifahamu sana idara ile. Ninadhani tutamsaidia *Treasury Registrar* kuweza kuhakikisha kwamba, kunakuwa na usimamaizi wa kutosha ili tuweze kupata taarifa na tuweze kuchukua maamuzi yanayostahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mashirika.

MWENYEKITI: Lakini Waziri, unapolijibu hilo ndio maana mara nyingine wanakuja tena; unajua wanapenyeza kitu, ukikikubali kinaleta shida. Mimi sioni wajibu wa kila Mkurugenzi katika Bodi wakishakutana mihutasari inaandaliwa na Katibu wa Bodi hiyo. Sasa wajibu wa kupeleka huko hauwezi ukawa wa *Board Members* ni wajibu wa Katibu wa Bodi hiyo na hao Makatibu mnawenza kuwadhibiti. (*Makofii*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana umenisaidia. Sasa kuhusu mashirika ya kuongezwa kwenye *DSE*, hilo tumelifanya kazi, sitayataja kwa sababu hayafikishwa, lakini kuna mashirika matano ambayo wakati wowote yanaingia kwenye *DSE*, ikiwa ni pamoja na *NMB* ambayo tayari ipo kwenye soko. Kuhusu Jengo la Benki Kuu, nafikiri hilo tutamwambia *Treasury Registrar* azungumze na Benki Kuu kuona kama uamuzi unaweza kufanyika. Nashukuru. (*Makofii*)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ubinafsishaji ni pamoja hizi shughuli za Wizara hii. Hivi karibuni tumesikia *Air Tanzania* ambayo imekuwa na ubinafsishaji mbovu na watu wa *South Africa*, hatujakaa sawasawa tunasikia sasa inabinafsishwa China. Sasa tunataka kujua hivi Sera ni nini juu ya *Air Tanzania* kwa sababu kila mmoja sasa anakaa na wasiwasi; wafanyakazi wana wasiwasi, hata sisi tunaopanda ndege tuna wasiwasi kama kutakuwa na maendeleo ya aina yoyote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nataka kuulizia juu ya Watanzania kununua hisa. Kama unavyofahamu, sasa hivi ulimwengu ni mdogo kwa sababu ya mawasiliano ya *internet* na vitu kama hivyo na pia kuna makampuni mengi ambayo yanatumia rasilimali zetu hapa Tanzania kama vile madini, Kahama Minning, inakuwa *registered* hapa lakini inakuwa na *shares* zake Toronto, Watanzania hawawezi kununua hizo hisa Toronto. Sababu gani inayofanya sisi tuweze kukataliwa kununua hisa za makampuni ambayo yapo hapahapa, yanatumia rasilimali zetu na sisi angalau tuwe na chochote katika makampuni hayo?

Si hivyo tu, kuna makampuni mengine ambayo yapo *East Africa*, hakuna utaratibu ambao umewekwa bayana sisi kuweza kununua hisa kama hizo. Shilingi inaimarika, tuna *exchange control regulation*, ambayo mimi naona ni nzuri kwa sasa hivi; ni viyi Mheshimiwa sisi hatupati fursa ya kuweza kutumia hayo masoko na kujitajirisha?

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nitajibu kuhusu suala la ATC, la hisa nitamwachia Naibu wangu atalielekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza si kweli kwamba, *ATCL* sasa hivi inabinafsishwa ni kwamba, juzi tu tumetoka kuichukua kutoka *South African Airways* na kurudisha kwetu. Kilichofanyika sasa hivi ni kwamba, *ATCL* kama kampuni wame-*approach investors* wakapata *investor* mmoja ambaye anawakopesha.

Kwa hiyo, kilichotokea ni kwamba, hii Kampuni ya Kichina inawakopesha *ATCL* na Serikali imetoa *guarantee* kwa mkopo mmoja wa zile ndege ambazo zipo pale. *ATCL* walikuwa hawana uwezo wa kuweza kuzinunua kwa *cash*, kilichofanyika ni kwamba, wamekodishwa. Sasa yule mkodishwaji hakuiamini *ATCL* na *balance sheet* yake wakataka Serikali iweke *guarantee*.

Kwa hiyo, kilichofanyika ni kwamba, mkopo umetoka kwa Kampuni ya Kichina inayoitwa *SONAGO* na kwa hiyo si mwenye hisa. Serikali inachokusudia kukifanya ni kama tulivyofanya *NMB* kwamba, kui-strengthen *ATCL* ifike mahali ambapo ukitaka kuuza *shares* zake nchi inaweza kupata pesa za maana. Kwa hiyo, kwanza nataka kuondoa hiyo kwamba, *ATCL* inataka kubinafsishwa; hapana hatujafikia hatua hiyo, lakini kwa sababu kuna mtu amejitokeza yuko tayari kuikopesha ilimradi tu Serikali iweke *guarantee*, tumeruhusu hilo kufanyika na wamekopesha. Ndege nyininge zile zimenunuliwa kwa pesa na ni deni, lakini ndege moja ile *Air Bus A320*, imetolewa kama kwa kukodisha. Sasa wale wamekodisha *Air Tanzania* wanalipa kila mwezi, lakini Serikali tumeweka *guarantee* ili kuiwezesha *ATCL* kupata hiyo *assistance*. Nashukuru.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. JEREMIAH S. SUMARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nimjibu Mheshimiwa Cheyo, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, Watanzania bado hawaruhusiwi kununua hisa nje ya nchi, kwa sababu bado *capital account* pale Benki Kuu, haijafunguliwa kwa maana ya kufanya malipo nje bila ya idhini maalum. Tutakumbuka kesi ya *Safaricom Kenya*, ambayo nampongeza sana Gavana kwa msimamo wake, maana hatimaye *Safaricom* ina matatizo chungunzima na thamani ya zile hisa imeporomoka. Hiyo ndiyo sababu ya msingi kwamba, bado *capital account* yetu haijafunguliwa, itakapofunguliwa basi Watanzania watakuwa na ruhusa ya kufanya hivyo. Pamoja na hilo, nafikiri inaweza kuchukua muda kidogo kwa sababu hivi ni Watanzania gani tunaowazungumzia kwamba wanunue hisa nje? Ahsante.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ningependa kujuani lini hiyo *capital account* itafunguliwa? Pili, kusema kwamba hakuna Watanzania walio na uwezo wa kununua, mimi naona ni kuwadhalilisha. Kuna Watanzania wengi tu ambao wanatafuta fedha sehemu mbalimbali, kama kungefunguliwa dirisha lile wangeweza kufanya hivyo.

MWENYEKITI: Sijui, kwa sera unaweza kuweka tarehe kweli? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. JEREMIA S. SUMARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niseme kwamba, hii *capital account* inasimamiwa na Benki Kuu na kwa utaratibu wao ndio watakaoamua ni lini kwa kushirikiana na Hazina. Tunaelewa kutoa tarehe nafikiri ni jambo ambalo haliwezekani, kuna mambo mengi ya kutazama. Haikuwa nia yangu kumdhaililisha Mtanzania yeoyote kwamba hatuna uwezo wa kununua hisa. Kwa hiyo, kama nimeeleweka hivyo basi haikuwa nia yetu.

MWENYEKITI: Wapo lakini wachache sana, ndiyo *point* yenyewe. Uende ukulanunue *share* za Barrick unatoka Bariadi labda Mbunge tu huyu. (*Kicheko*)

Sasa Waheshimiwa tutakwenda kwenye hoja moja moja tu, hoja mbili nimeshazifuta; sasa ni moja kwa Mbunge mmoja. Mheshimiwa Beatrice Shellukindo.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kwa nini imeanzia kwangu na nilikuwa na mawili ya moto lakini basi nitasema moja. Pamoja na kwamba, Mheshimiwa Waziri amesema hakuweza kujibu hoja zote, lakini kwa sababu naelekeea Jimboni na suala ambalo linazungumzwa sana sasa hivi ni suala la ujenzi wa Halmashauri ya Wilaya, ambayo imeshafika kwenye lenta, tunahitaji bilioni moja kukamilisha. Vitu vinapanda bei na mvua zinakaribia kwetu. Sasa sijui Mheshimiwa atasemaje kuhusu hili, anirahisishie hata mimi kule kwenye Kamati ya Fedha wamekwishasikia kauli ya Serikali. Ahsante.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Serikali kuna utaratibu wa *Sector Ministries*. Kwa kweli mtu ambaye angeweza kujibu hilo ni Waziri wa TAMISEMI. Hata hivyo, sijazungumza naye kama anaweza kulijibu hilo. Nadhani mimi ningeshauri tu kwamba, Halmashauri ya Wilaya iandike rasmi kwa Wizara ya TAMISEMI, wakiomba hizo pesa na kusisitiza umuhimu wa fedha hizo zitolewe mapema. Sasa Waziri wa Fedha na Waziri wa TAMISEMI, tunaweza tukakaa chini tukazungumza na kuona kama inawezekana au namna gani. Lakini ni vigumu sana, kwa mimi kuahidi hapa baada ya Bajeti Kuu kupita, naweza nikapata shilingi bilioni moja kwa ajili ya Kilindi peke yake.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOANA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu inategemea *cash budget* na sote tunategemea huko huko Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, fedha zikitoka sisi tutazipeleka kwenye Wilaya, huwa mara nyingi zinaendea huko. Kwa hiyo, sasa hivi hatuwezi tkumpa jibu kwa sababu ni fedha kidogo sana zilizopatikana mwezi uliopita,

ndio zimetoka kama *OC* kwenye Wilaya mbalimbali. Mpaka hapo wenzetu Wizara ya Fedha, watakapopata makusanyo vizuri ili watuletee Wilayani na zikitoka sisi hatuna matatizo, zinaenda moja kwa moja kwenye Wilaya.

MWENYEKITI: Nadhani mkalimalize nje ya Ukumbi kwa sababu ni suala la hesabu na kulinganisha Bajeti. Mheshimiwa Hafidh Ali.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipochangia kwa maandishi, nilimwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kufanya majumuisho basi anieleze kuhusu fedha za elimu ya juu, ambazo huwa zinapelekwa nje ya Tanzania kwa wanafunzi wetu. Utaratibu ambao ulikuwa unafanyika katika kupeleka fedha hizo na katika maelezo yangu nilitoa mfano kwamba, si mtindo mzuri wa kumpa fedha mtu milioni 200 au 300 *cash*, asafiri nazo hadi waliko wanafunzi, jambo ambalo ni hatari sana na limeshafanyika.

Lingine ambalo nimelisema katika mchango wangu ni pale ambapo Wizara inachukua fedha kupeleka kwenye akaunti ya mwanafunzi mmoja nje ili awagawie wenzake. Nilitaka Mheshimiwa Waziri, atuambie Serikali inashindwa nini katika kuhakikisha wanafunzi hawa wanapata fedha katika njia sahihi zisizokuwa za hatari na ambazo mtu anaweza kutoweka bila kujua? Alipokuwa anatoa majumuisho hakusema kitu. Sasa naomba Serikali iniambie imefanya mpango gani katika suala hili?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI - MHE. JEREMIAH S. SUMARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sisi tunashangaa; kama kuna aliyepewa shilingi milioni 200 *cash* kwenda nazo na sijui atakuwa alifikafikaje kule, maana kwa hali ya sasa ni vigumu. Kama ilitokea, nataka kusema huo si utaratibu. Kuna utaratibu ambao unaeleweka wa kutuma fedha kwa wahusika na mara nyingine zinakwenda kuititia kwenye Balozi zetu, zikifika kule kuna utaratibu wa kuwfikishia wale walengwa. Kwa hiyo, utaratibu upo, mara nyingine labda haufuatwi kama anavyosema Mheshimiwa Hafidh.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hafidh, mimi nashauri hizo nyaraka zinazoonyesha hayo ziweze kufikishwa Wizarani wazifanyie kazi. Inatisha sana, kwanza itakuwa ni jambo la ajabu mtu kuchukua Shilingi ya Tanzania ukaenda nje ya nchi. Sasa utaitumiaje huko, kwa sababu inabadilishwa ili iwe dola hapa hapa, labda mtu anakwenda nayo. Sasa ukienda nayo Shilingi ya Tanzania mathalani Uingereza, utarudi hivyo hivyo haiwezi hata kutumika.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa maelezo zaidi. Hivyo, nilivyosema ni sahihi na niliposema shilingi milioni 300 si kwamba, zilikuwa ni shilingi za Tanzania. Nadhamiria kwamba, zile Dola alizoondoka nazo hapa ni sawa na hizo fedha nilizozitaja. Kwa hiyo, hilo limeshatokea lipo kwenye taratibu na lipo kwenye mahesabu.

La pili, alilolisema Mheshimiwa Naibu Waziri sasa hivi kwamba, anazitumia Balozi zetu za Tanzania nalo lina matatizo. Nitakupa mfano; fedha zilizopelekwa Ofisi za Ubalozi wa Tanzania nchini Urusi, kiasi cha shilingi bilioni 1.023, hazikutolewa kwa

uhakika kwa wanafunzi wote na hazina mchanganuo. Hali kadhalika, fedha zilizotolewa huko shilingi milioni 526. Sasa naomba Wizara iwe makini sana katika masuala haya ya fedha na wawe makini katika kufuatilia utekelezaji wa masuala mbalimbali hasa wanafunzi walioko nje, kwa sababu wanapata matatizo kwenye masuala ya fedha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hafidh, una taarifa muhimu sana inaelekea, isije ikawa tumeibiwa kama nchi. Nashauri Waheshimiwa Wabunge, mkiwa na vitu kama hivi msisubiri Kamati ya Matumizi ni moja kwa moja. Mambo haya yanaweza kuwa ni jinai. Nashangaa kabisa. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA): Mheshimiwa Mwenyekiti, si kweli kwamba, pesa zilizokwenda Urusi kwa ajili ya wanafunzi hawakupewa, isipokuwa kuna matatizo yanayojitekeza ya ku-*transfer* hizi pesa kutoka kwenye akaunti ya Wizara ya Elimu ya Juu wakati ule na kwenda kwenye Balozi zetu. Mara nyingine unakuta hizi fedha zinakosa thamani kwa sababu muda umekuwa umepita wakati wa fedha hizi zinakuwa transferred.

Tatizo analolizungumza mara nyingine ni matatizo ya kawaida ya kifedha na mimi mwenyewe nimekwenda Urusi wakati huo wa matatizo na kulikuwa na *Audit Query*; kwa hiyo, ilishajibowi na matatizo yalishatatuliwa.

Kwa hiyo, si kwamba tatizo lile lilikuwa limesababishwa kwa makusudi ni matatizo madogo madogo yanashughulikiwa yanapojitekeza na ni kweli pesa hizi zinapitia katika Balozi zetu na wanafunzi wanapewa kikamilifu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwa kanuni zetu na taratibu za Bunge, sasa zimebaki dakika kumi, muda ambao hatuwezi kuendelea kubaki humu. Kwa hiyo, tunakwenda kwenye kipindi cha *guillotine*, hakipo rasmi kwenye kanuni lakini ni kawaida ambayo imekwishatumika inaitwa *precedent*. Katibu atatuchukua kwa mafungu kamili tumalize. Nawaomba radhi wale wenzetu wengine basi imekuwa bahati mbaya.

Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Uchumi

| | |
|---|-------------------|
| Kif. 1002 - <i>Administration and General</i> | Sh. 9,491,457,900 |
| Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i> | Sh. 8,161,482,200 |
| Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i> | Sh. 1,161,651,900 |
| Kif. 1004 - <i>Legal Services</i> | Sh. 1,111,774,500 |
| Kif. 1005 - <i>Information Education and Communication</i> | Sh. 1,023,165,400 |
| Kif. 1006 - <i>Internal Audit Unit</i> | Sh. 235,296,000 |
| Kif. 1007 - <i>MCC Tanzania</i> | Sh. 364,892,400 |
| Kif. 1008 - <i>Procurement Management Unit</i> | Sh. 993,725,700 |

| | |
|---|-------------------|
| Kif. 2001 - <i>Government Budget</i> | Sh. 0 |
| Kif. 2001 - <i>Policy and Research</i> | Sh. 0 |
| Kif. 2003 - <i>Treasury Registrar</i> | Sh. 0 |
| Kif. 4001 - <i>External Finance</i> | Sh. 0 |
| Kif. 5001 - <i>Stock Verification</i> | Sh. 3,863,592,800 |
| Kif. 6001 - <i>Computer Services</i> | Sh. 1,638,492,400 |
| Kif. 6002 - <i>Tax Revenue Appeals Board</i> | Sh. 773,539,000 |
| Kif. 6003 - <i>Technical Audit Unit</i> | Sh. 419,103,500 |
| Kif. 6004 - <i>Tax Revenue Appeals Tribunal</i> | Sh. 449,163,300 |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 21 – Hazina

| | |
|---|--------------------|
| Kif. 2001 - <i>Government Budget Division</i> | Sh. 7,200,000,000 |
| Kif. 2002 - <i>Policy and Research Division</i> | Sh. 7,448,901,000 |
| Kif. 2003 - <i>Treasury Registry</i> | Sh. 2,650,900,000 |
| Kif. 4001 - <i>External Finance Division</i> | Sh. 1,135,000,000 |
| Kif. 7001 - <i>Poverty Eradication and Eco. Empowerment</i> | Sh. 11,648,998,000 |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali

| | |
|---|-------------------|
| Kif. 3003 - <i>Financial Management</i> | Sh. 8,237,469,000 |
|---|-------------------|

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

| | |
|---|-------------------|
| Kif. 1001 - <i>Administration and General</i> | Sh. 5,600,000,000 |
|---|-------------------|

Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Uchumi

| | |
|---|--------------------|
| Kif. 1001 - <i>Administration and General</i> | Sh. 1,179,750,000 |
| Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i> | Sh. 5,427,650,000 |
| Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i> | Sh. 591,900,000 |
| Kif. 1004 - <i>Legal Services</i> | Sh. 0 |
| Kif. 1005 - <i>Information, Education and Communication</i> | Sh. 650,000,000 |
| Kif. 1007 - <i>MCC Tanzania</i> | Sh. 68,511,000,000 |
| Kif. 2001 - <i>Government Budget</i> | Sh. 0 |
| Kif. 2002 - <i>Policy and Research</i> | Sh. 0 |

| | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|-------|-------|-------|-------|-------|-------|-------|-------|-------|-------|-------|-------|-------|-------|----------------|
| Kif. 2003 - <i>Treasury Registrar</i> | | | | | | | | | | | | | | | Sh. 0 |
| Kif. 4001 - <i>External Finance</i> | | | | | | | | | | | | | | | Sh. 0 |
| Kif. 5001 - <i>Stock Verification</i> | | | | | | | | | | | | | | | Sh. 0 |
| Kif. 6001 - <i>Computer Services</i> | | | | | | | | | | | | | | | Sh. 55,500,000 |
| Kif. 6002 - <i>Tax Revenue Appeals Boards</i> | | | | | | | | | | | | | | | Sh. 0 |
| Kif. 6003 - <i>Technical Audit Unit</i> | | | | | | | | | | | | | | | Sh. 0 |
| Kif. 6004 - <i>Tax Revenue Appeals Tribunal</i> | | | | | | | | | | | | | | | Sh. 0 |

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

T A A R I F A

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Uchumi na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2008/2009, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote.

Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mwaka 2008/2009
yalipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, tunapoyapitisha natumaini mtakumbuka ahadi milizozitoa na kwamba, zitafanyiwa kazi ili katika vikao vyetu vingine na mikutano yetu ijayo, tuwe tunaona maendeleo ya utekelezaji wa dhati wa ahadi za Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kufika hapo, muda umepita tunakaribia dakika nne kufika muda wa mwisho kabisa kutoka humu. Kwa hiyo, kwa haraka haraka tu niseme kwamba, sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi hapo saa tatu asubuhi kesho.

*(Saa 02.12 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,
Tarehe 27 Agosti, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*

